

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 12 Mei, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu

**NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 190

**Malipo ya Wafanyakazi wa Kiwanda cha Chumvi – Uvinza**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inawaeleza nini wafanyakazi wa Kiwanda cha Chumvi ambao walistaafishwa bila malipo ya kiinua mgongo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwabana wamiliki wa kiwanda hicho ili waboreshe mazingira ya kiwanda pamoja na mazingira ya wafanyakazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wafanyakazi wa Kiwanda cha Chumvi ambao walistaafishwa bila malipo ya kiinua mgongo lilishashughulikiwa, ambapo wafanyakazi husika walilipwa mafao yao kwa mujibu wa sheria ikiwemo kiinua mgongo. Aidha, kwa kuzingatia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya mwaka 2016 yaliyopitishwa na Bunge lako Tukufu wakati wa Kikao cha Bajeti, kama kuna mfanyakazi au wafanyakazi wanaoona kuwa hawakulipwa stahiki zao za kupunguzwa kazi ipasavyo, wanayo fursa ya kuwasilisha moja kwa moja madai yao kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi pasipo kupitishia kwa Kamishna wa Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kuimarisha mikakati na huduma za usimamizi na

ukaguzi kazi kwa kuchukua hatua stahiki kwa waajiri wanokiuka sheria ili kuboresha mazingira ya kiwanda na mazingira ya wafanyakazi. Aidha, kupitia Marekebisho ya Sheria za Kazi ya mwaka 2016, Maafisa Kazi wamepewa mamlaka ya kuwatoza faini za papo kwa papo waajiri wanaokiuka sheria. Kanuni kwa sasa zinaandaliwa ili kuweka mwongozo na utaratibu mzuri wa utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nivisih vyama vya wafanyakazi nchini, navyo vitimize wajibu wao wa kutetea na kusimamia haki za wafanyakazi pamoja na kukuza tija na uzalishaji sehemu za kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasna Mwilima, swali la nyongeza.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nina masikitiko makubwa sana, itabidi Naibu Waziri anipe uhakika wa hao wafanyakazi 389 walilipwa lini na wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoongea hivi nina ushahidi, suala hili hata Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali analifahamu. Lilifanyiwa uhakiki, watu walitumwa kutoka Hazina wakaja Uvinza wakafanya uhakiki, wakaona kweli wafanyakazi hawa wana haki hawakulipwa mshahara wao wa mwisho na hawakulipwa nauli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumefanyiwa uhakiki Mwanasheria Mkuu wa Serikali analifahamu bahati mbaya leo hayupo hapa, lakini analifahamu, alihakikisha na akatoa ushauri kwamba hawa wafanyakazi walipwe, wanadai zaidi ya shilingi milioni 320.9; je, Waziri yupo tayari kuniletea ushahidi kwamba walilipwa lini na nani, kwa sababu ninavyofahamu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anayo haya madai juu ya meza yake?

Swali langu la pili, Kiwanda cha Chumvi hivi tunavyoongea wamiliki wameuza kila kitu, wameuza vifaa vyote, wameuza vyuma, wameuza magari, wameuza

matofali, kila kitu. Tunajua kabisa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuimarisha viwanda, vilivyopo na kufufua vingine na kuhamasisha vingine ili viweze kujengwa. Swali langu ni kwa nini, kama dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuendeleza viwanda, leo tunaachia kiwanda kama kile cha chumvi ambacho wananchi wa Uvinza akina mama..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba umalize tafadhali.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu kwa nini wanaachia wamiliki wanaoendesha kiwanda hiki kufunga kiwanda kinyume na utaratibu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu kuleta orodha, jambo ambalo linaweza kufanyika hapa ambalo ni rahisi la kuweza kuwasaidia wafanyakazi wetu, katika majibu yangu ya msingi nilisema kama wako wale ambao wanahisi kwamba madai yao hayakulipwa ipasavyo na bado wana malalamiko, mimi na Mheshimiwa Mbunge tunaweza kuchukua hizi taarifa zote mbili tukazioanisha ili tupate muafaka wa kuweza kuwasaidia wafanyakazi hawa wa Kiwanda cha Chumvi.

Kwa hiyo, nimuondoe hofu tu Dada yangu Mheshimiwa Mwilima kwamba nalichukua jambo lako kwa uzito mkubwa sana, na kwa namna alivyozungumza kwa masikitiko makubwa, na mimi niungane nae kwamba tutakwenda pamoja wote kuangalia arodha hii ili kama bado kuna mapungufu tutafanya kazi ya kushughulikia pamoja na taasisi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusu kufunga viwanda na wakati tunasema nchi yetu ni ya uchumi na viwanda. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hata hili nalo pia linahitaji kuweza kufahamu hasa changamoto ambazo

zimepelekea jambo hili kutokea, lakini nimuahidi tu kwamba chini ya Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tunashughulikia masuala ya kazi na ajira na mategemeo yetu na matazamia yetu makubwa ni kuona kwamba viwanda vingi vinakuwepo, uwepo wa viwanda ndipo ajira zinatengenezwa.

Mheshimiwa Mbunge hata katika taarifa ya *ILO* ya mwaka 2014 ya *The Global Employment Trend* inasema ya kwamba ili kuendelea kuongeza nafasi za ajira hasa kwa vijana ni vema tuwe na viwanda vingi zaidi. Ninakachokisema hapa ni kwamba, nakwenda kufuatilia kufahamu changamoto na tatizo ambalo limepelekea kiwanda hiki kufungwa ili tuweze kupata suluhisho la kudumu, vijana wa Kigoma waweze kupata ajira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhary swali la nyongeza.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa suala la Kigoma – Uvinza lipo sawa la Kiwanda cha Magunia Moshi na Kiwanda cha Kiritimba ambapo nimeshauliza swali la msingi hapa Bungeni na Serikali ikajibu kwamba ipo tayari kwenda kuonana na wale wafanyakazi ambao hawakulipwa mafao yao ili waweze kuwaeleza, kwa nini hawakuwalipa na kama wamewalipa, waliwalipa kwa vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inipe *commitment* kama ni lini itakwenda kuonana na wafanyakazi wa magunia waliostaafishwa na wafanyakazi wa Kiritimba wa Mkoa wa Kilimanjaro. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anahitaji *commitment* ya Serikali ya lini tutakwenda kuwaona na kusikiliza matatizo ambayo yanayowakabili wafanyakazi hawa, nimuahidi tu kwanza kwa kuanzia Jumatatu

nitamuagiza Afisa Kazi aliopo pale Moshi aende kukutana na Wafanyakazi hao na baada ya hapo akishanipatia taarifa kama kuna haja ya Naibu Waziri ama Waziri kwenda kufanya kazi hiyo basi nimtoe hofu Mbunge kwamba tutakwenda kuonana nao na tutatatia matatizo ambayo yanawakabili wafanyakazi hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kumekuwa na changamoto kubwa ya vijana ambao wanaajiriwa kwa mikataba ya muda mfupi kuzungushwa pale wanapoenda kwenye Mifuko ya Pensheni kudai mafao yao ili waweze kuyatumia kama mitaji ya kujiajiri. Kwa mfano, kule Karagwe Kampuni ya Ujenzi ya Chico iliajiri vijana kwa utaratibu wa mikataba ya vibarua, mpaka hivi sasa wanazungushwa vijana hawa.

Je, Serikali inawasaidiaje vijana hawa kudai mafao yao ili waweze kutumia hela hii kama mitaji ya kujiajiri? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi ya pekee sana kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu amekuwa mstari wa mbele sana kufuatilia haki za wananchi katika Jimbo lake na hilo ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumekuwa na malalamiko ya namna moja ama nyingine ya wafanyakazi wa namna hiyo ambao wamekuwa wakiajiriwa kwa mikataba, mikataba yao

inapoisha walizoea kuwa na fao ambalo si fao sahihi lakini lililokuwa linaitwa fao la kujitoa. Baada ya kupitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 11, lakini kupitia Sera ya Hifadhi ya Jamii katika nchi yetu na sheria tulizonazo, Serikali pamoja na wafanyakazi wenyewe na vyama vya wafanyakazi, tumekubaliana sasa kuna haja ya kuangalia namna nzuri ya kuwasaidia wafanyakazi wote ambao wamekuwa wakikumbwa na jambo hilo kwa kuanzisha fao lingine ambalo litaitwa ni Bima ya kukosa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo tumeshaanza kuifanya vizuri kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi, niwaombe wafanyakazi wote nchini ambao walikuwa wanaelekea katika fao hilo wavute subira ili matakwa ya kisheria yafanyiwe kazi na ndipo fao hilo litaanza kutolewa kwa mujibu wa sheria ambayo itakuwa imetungwa na Bunge.

Pia ni maagizo ya Mheshimiwa Rais siku ya Mei Mosi alipokuwa pale Moshi ameendelea kusisitiza kwamba sasa tushughulikie suala hilo na liweze kufungwa kisheria na Wafanyakazi waweze kupata haki zao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Almasi Athumani Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 191

### **Kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** aliuliza:-

Hivi karibuni wakati Mheshimiwa Rais akifungua majengo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *PPF* aliongelea wazo la kuunganisha Mifuko ya Jamii iliyopo sasa *NSSF*, *PPF*, *GEPF* na *LAPF* na kufanya ama mifuko miwili au hata mmoja tu kama ilivyo katika nchi nyingine.

(a) Je, mchakato huu sasa umefikia wapi?

(b) Je, Serikali ina malengo ya kuunda mifuko mingapi baada ya muungano huo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athumani Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina jumla ya Mifuko Saba ya Hifadhi ya Jamii. Kati ya mifuko hiyo, mitano ni ya pensheni ambayo ni *NSSF, LAPF, PSPF, GEPF* na *PPF*, mmoja ni wa fidia kwa wafanyakazi na mmoja ni wa bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa mifuko mitano ya pensheni hapa nchini kumetokana na historia ya mfumo wa kiuchumi ambayo nchi yetu imepitia tangu uhuru mpaka sasa. Mifuko hii ilipokuwa inaanzishwa illenga kutoa huduma za hifadhi ya jamii katika sekta mbalimbali kama vile watumishi wa umma, mashirika ya umma, polisi na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuunganisha Mifuko ya Jamii umefikia hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa tathmini na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*actuarial evaluation*) ambayo pamoja na mambo mengine imetoa mapendekezo kuhusu namna bora na mambo muhimu ya kuzingatwa katika zoezi la kuunganisha mifuko. Aidha, wadau mbalimbali wameshirikishwa wakiwemo vyama vya waajiri na wafanyakazi ili kutoa maoni na mapendekezo Serikalini kwa maamuzi. Kimsingi Serikali imefikia hatua nzuri ya mchakato huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Serikali haijafanya uamuzi rasmi wa idadi ya mifuko itakayobaki baada ya kuiunganisha mifuko iliyopo hivi sasa. Hata hivyo,



Serikali itazingatia maoni na ushauri wa wadau ili kufanya uamuzi muafaka wa idadi na aina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inayotakiwa kuwepo kwa kuzingatia uwepo na mahitaji ya sekta binafsi na sekta ya umma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige swali la nyongeza.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ninaomba Bunge lako Tukufu litambue kwamba nina maslahi katika mifuko yote hii ya hifadhi ya jamii.

Swali langu la kwanza ni kwamba mifuko hii inatofautiana katika kukokotoa mafao ya wafanyakazi wanaoacha kazi au wanaostaafu. Kwanza mifuko inakokotoa kutokana na *gross salary* mapato yote ya mfanyakazi; pili inakokotoa kutokana na *basic salary*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini msimamo wa Serikali, ni kuhusu *basic salary* au *gross income* ya mfanyakazi?

Swali la pili, fao la kujitoa baadhi ya mifuko hii saba iliyotajwa inaitangaza kama ni fao kwa wafanyakazi wanaoacha kazi na mifuko mingine ni marufuku kabisa kulipa mafao kabla ya miaka 60. Je, ni nini msimamo wa Serikali? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nitayajibu yote kwa ujumla kwa sababu yanaingiliana. Kuhusu kukokotoa, kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa mwaka 2014 ambao ulianza kufanya kazi tarehe 1 Julai wenye vipengele 15 umeainisha namna ya ukokotoaji wa mafao kwa wafanyakazi ambao wamestaafu. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba mfumo uliowekwa kupitia *SSRA* ndiyo ambao unatumika na ndiyo ambao umeridhiwa

mpaka hivi sasa, lakini kama kuna mapendekezo ya namna bora ya kuboresha, Serikali bado tupo tayari kuweza kusikiliza na kuona namna bora ya kuweza kuwasaidia wafanyakazi wetu ili wapate mafao ambayo wataweza kuwafanya wamudu maisha ya dunia ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu sana kwamba Mheshimiwa Mbunge ni mdau mkubwa na ana mchango mkubwa sana katika eneo hili na nimpongeze kwa kazi kubwa ambayo amefanya, naamini kabisa kwamba anayo nafasi kama Mwenyekiti wa *ATE* kushirikiana kwa pamoja wakaleta mapendekezo yao ili tuone namna bora ya kuweza kufanya. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitaka mifuko kusitisha fao la wafanyakazi ambao wanataka kuchukua mafao yao mpaka wafikishe miaka 60. Ningependa tu kufahamu kwa sababu kwa hivi sasa sakata la wale wafanyakazi waliopatwa na vyeti *fake* ni dhahiri kabisa watapenda kuchukua mafao yao ili wajingize katika shughuli nyingine.

Nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha kwamba wafanyakazi hao na wale wengine ambao wana ajira fupi wanachukua mafao yao ili waweze kuendelea na shughuli nyingine? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kuhusiana na mafao ya waliokumbwa na kadhia ya vyeti vya kughushi, kwa sasa niseme ni suala ambalo hatuwezi kulitolea maelekezo hapa, pindi taratibu

zote zitakapokamilika basi taarifa itaweza kutolewa na watajua hatima yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Serikali imekuwa ikidaiwa fedha nyingi sana na mifuko ya hifadhi, mfano, *PSPF* ilikuwa inaidai Serikali zaidi ya shilingi 2,671,000,000,000 pia *LAPF* ilikuwa inaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 47 kwa ajili ya asilimia 15 ya makato kwa ajili ya wafanyakazi. Je, Serikali imelipa kiasi gani na hali ikoje kwa wastaafu hawa mpaka sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Serikali ilikuwa ikidaiwa kama hiyo asilimia 15, shilingi trilioni 1.4 mpaka sasa tumeshalipa trilioni 1.1, bado shilingi bilioni tatu, ambayo mwezi huu Mei, tunakamilisha kulipa hiyo iliyobaki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mbunge wa Ole, sasa aulize swali lake na kwa niaba yake Mheshimiwa Mtolea.

Na. 192

### Utaratibu Wakulipa Mafao ya Wastaafu

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y MHE. JUMA HAMAD OMAR)** aliuliza:-

Kumekuwa na utaratibu wa muda wa kulipa malipo ya pensheni kwa wastaafu kama vile kila mwezi, kila baada

ya miezi sita na kila baada ya miezi mitatu.

(a) Je, ni utaratibu gani kati ya hizo zilizotajwa hauwasumbui wastaafu?

(b) Je, ni *formula* gani inayotumika katika kuwaongezea wastaafu pesheni zao ili angalau kwa kiasi fulani ziweze kusaidia kukidhi maisha yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu mzuri wa kulipa mafao ya pensheni ni malipo ya kila mwezi. Aidha, malipo ya pensheni yanaweza kutafsiriwa kama malipo mbadala ya mshahara wa kila mwezi kwa mfanyakazi aliyestaafu. Ni wazi kwamba malipo haya yanakuwa na mahusiano makubwa na maisha ya kila siku ya mstaafu kama ilivyo kwa mshahara ama kipatao kingine kinachotokana na maisha ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kutokana na hali halisi ya mazingira ya nchi yetu kijiografia na gharama za kufuatilia pensheni husika, baadhi ya mifuko ya pensheni iliweka utaratibu wa kulipa kwa mafungu ya miezi mitatu au sita ili kupunguza gharama kwa wastaafu. Aidha, kutokana na maendeleo ya teknolojia natoa rai kwa mifuko yote kuendelea kuboresha mifumo yao ili kuendelea kutoa mafao kwa wakati kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utataratibu wa kuhuisha pensheni, *indexation* umebainishwa katika kifungu cha 32 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135, kikisomwa pamoja na kifungu cha 25 cha sheria hiyo ambacho kinaitaka mamlaka kufanya

tathmini ya mifuko husika kabla ya kutoa viwango vya mafao, kwa mfano, kufuatia tathmini ya mifuko yote iliyofanywa katika kipindi cha mwaka 2015/2016 mamlaka ilikwishatoa maelekezo ya viwango vipya vya malipo ya kima cha chini cha pensheni ya kila mwezi kwa mifuko yote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea majibu ya Serikali yaende mbali zaidi, kwamba mbali ya kuelezea huu utaratibu lakini ijiridhishe kama kweli huo utaratibu unafuatwa. Wastaafu wa Zanzibar wamekuwa wakilipwa kwa mikupuo mitatu, maana yake ni miezi minne badala ya miezi mitatu, mitatu kama utaratibu unavyosema.

Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa kwa miezi mitatu badala ya miezi minne kama utaratibu unataka?

Swali la pili, Bunge la Kumi lilipandisha viwango vya pensheni vya kima cha chini kutoka shilingi 50,000 kwenda shilingi 100,000, mpaka leo baadhi wastaafu hawa baadhi ya wastaafu hawajawahi kulipwa hicho kiwango kipya. Tuliwahi kuuliza hapa na Naibu Waziri wa Fedha akasema kwamba kufika Februari, 2016 wangeanza kulipwa viwango hivyo vipya pamoja na *arrears* zao. Nataka kujua kwa wale wastaafu wote ambao hawalipwi kupitia Hazina ni lini wataanza kulipwa viwango vipya vya shilingi 100,000? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza kwamba wastaafu wa Zanzibar wanalipwa miezi minne, minne, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba hata wastaafu wa Bara waliokuwa wakilipwa na Hazina walikuwa wakilipwa

miezi mitatu mitatu na sasa hivi kuanzia Oktoba 2016, wanalipwa mwezi mmoja, mmoja na tulipokuwa tunafanya uhakiki wa wastaafu wetu, zoezi ambalo linaendeshwa na Wizara ya Fedha tumekuwa tukikusanya mawazo yao kwamba nini wanapendelea na tutakapokuwa tumekamilisha utafiti huo tutakaa chini na kuweza kutoa maelekezo ya Serikali kwamba watalipwaje. Hivyo, hii inakwenda kwa wastaafu wa Zanzibar kwamba na wao tutachukua maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba Serikali imekuwa ikifuata sheria katika kulipa mafao haya, lakini pia kuweza kuchukua mawazo ya wastaafu hawa kwa sababu wao ndiyo wafaidika. Kwa mfano, hii ya sasa hivi hii ya kwenda mwezi mmoja, mmoja kwa wastaafu wa Bara wamekuwa wakilalamika kwamba ile miezi mitatu, mitatu japo kuwa ni wao ndiyo walipendekeza na sheria yetu ikaruhusu lakini wanalalamika kwamba wanakosa kupata mikopo kwa sababu *cash flow* haiko vizuri. Serikali imewasikiliza na kuanza kulipa mwezi mmoja mmoja na hao wa Zanzibar pia tutasikiliza tutaangalia na sheria zetu wataweza kulipwa kwa vile ambavyo wao wanapendelea na sheria yetu inaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalli la nyongeza ya shilingi 50,000 nakumbuka nilijibu hapa katika hapa katika Bunge lako Tukufu, kwamba wale wastaafu wote wanaolipwa na Hazina nyongeza yao walianza kulipwa na wote wanalipwa shilingi 100,000 kwa sasa. Kwa wale wanaolipwa na mifuko nililiambia Bunge lako Tukufu kwamba baada ya kutolewa agizo lile la Serikali, Bodi ya Wakurugenzi wa Mifuko husika, walitakiwa kukaa na kuweza kukubaliana ni lini wanaanza kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwaambie wastaafu wote nchini, kwamba hii tuliyoisema shilingi 50,000 kwenda shilingi 100,000, moja kwa moja ilikuwa ni wale wastaafu wanaolipwa na Hazina. Wale wa mifuko, Bodi zao za Wakurugenzi watafanya tathmini na wataanza kuwalipa kama ambavyo mfuko wetu wa *PPF* wameshafanya tathmini

na sasa tangu Januari 2017, wameanza kulipa shilingi 100,000 kwa wastaafu wote wa kima cha chini. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANAM AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kwanza niwapongeze Naibu Mawaziri wote wawili kwa majibu mazuri ya nyongeza.

Naomba niongeze jambo moja tu dogo nilialifu Bunge lako Tukufu kwamba *SSRA* wameshamaliza kufanya tathmini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yote katika nchi yetu ya Tanzania pamoja na *PPF* kuanza kulipa kima cha chini cha pensheni cha shilingi 100,000 pia Mfuko wa *NSSF* na *LAPF* wameshakamilisha tathmini hiyo na wao wameshaanza kuendelea na mchakato huo wa kupandisha kima cha chini. Kwa hiyo, Serikali imeshatekeleza agizo hilo kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa malipo hayo sasa umeanza kufanyika hata kwenye Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi au makundi katika jamii ambayo yanaajiriwa ajira za mkataba. Kwa mfano, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wabunge wanakuwa na ajira ya miaka mitano na mkataba wao baada ya hapo unakuwa umekwisha. Kama alivyo Mheshimiwa Rais, nembo ya Taifa hili ndivyo alivyo Mbunge nembo ya Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwaacha Wabunge baada ya kustaafu bila kuwapa pensheni na tunajua maisha yalivyo, hamuoni kwamba Wabunge wanadhaliika na makundi ya aina hiyo kiasi ambacho wanashindwa kumudu maisha. Je, ni lini Serikali itafikiria kuliona hili ili Wabunge

wanapostaafu nao waweze kupatiwa pesheni? Ahsante.  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, malipo yote ambayo yamekuwa yakifanywa kwa Waheshimiwa Wabunge yanalipwa kwa mujibu wa sheria, yanalipwa pia kwa kuzingatia masharti ya kazi ya Mbunge ambayo yanakuwa yameandaliwa pia kwa kufuata sheria za nchi tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wana ushauri, wana jambo linalohusu masuala ya kisheria ya haki na mafao yao Tume ya Huduma za Bunge inafanya kazi kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuone namna ya kuwasiliana na tume ya huduma ya Bunge ili kuangalia ni kwa kiasi gani yale yanayohusu Wabunge yaweze kushughulikiwa ipasavyo na Tume ya Huduma ya Bunge, ambayo tumeiweka kwa mujibu wa sheria. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya watumishi ambao fedha zao hazijapelekwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Hapa nina barua ya mtumishi ambaye anatarajia kustaafu tarehe 15 Juni; mpaka leo makato yake ya miezi 18 hayajapelekwa jambo ambalo litaathiri pensheni yake.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kuwa na takwimu ya watumishi ambao wanatarajia kustaafu ili kusudi makato yao yaweze kupelekwa kwenye mifuko na watakapostaafu wapate kile kinachostahili kwa wakati? (Makofi)



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma na matakwa ya Serikali yetu kuhakikisha kwamba watumishi wote ambao wamekuwa wakichangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kulipwa mafao yao ya pensheni kwa wakati. Hivyo, tumekuwa tukitoa maelekezo na maagizo mbalimbali ili taasisi zote zinazoshughulikia malipo ya pensheni kwa wafanyakazi wa Serikali pia kwa wafanyakazi wa *private sector* wahakikishe kwamba watumishi wanalipwa mafao yao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukichua hatua pale mafao ya watumishi yanapochelewesha. Ninamuomba Mheshimiwa Chumi atulettee taarifa za mtumishi huyo ambaye amecheleweshewa nasi tutachukua hatua. Niendeleo kuwaagiza wale wote wenye jukumu la kusimamia malipo ya pensheni kwa wastaafu, watekeleze wajibu wao na wastaafu waweze kupata mafao yao kwa wakati unaotakiwa bila kucheleweshwa na tukizingati kwamba hata Mheshimiwa Rais amesisitiza na ameagiza sana suala hilo lisimamiwe vizuri na sisi tutaendelea kulisimamia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa nchi ya Tanzania imejengwa na tabaka zote hasa wakulima na wafanyakazi; na kwa kuwa Serikali ya awamu iliyopita kwenye bajeti ya mwaka 2013/2014 - 2014/2015 walitoa ahadi kwenye Bunge hili kwamba watalipa wastaafu wote (wazee wote wenye miaka 60) bila upendeleo wa aina yoyote, wawe wafanyakazi au wakulima.

Nataka kupata kauli ya Serikali ni lini watatekeleza ahadi yao hii ya kuwalipa wazee wote nchi nzima ambao wana zaidi ya miaka 60? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa James Mbatia, mzee mtarajiwa swali lake ambalo ameliuza kwa niaba ya wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imetoa ahadi ya kushughulikia suala zima la ulipaji wa pensheni kwa wazee katika nchi yetu ya Tanzania. Naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu mchakato huo umeshaanza na tayari tathmini na *study* zimeshafanyika za kuona ni utaratibu gani utafanyika wa kuweza kuwalipa pensheni wazee hao, michakato hiyo yote ikishakamilika basi Bunge lako Tukufu litaarifiwa ni lini utaratibu huo wa malipo ya pensheni utaanza. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na.193

### **Hitaji la Hospitali ya Wilaya ya Wanging'ombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali katika Wilaya mpya ya Wanging'ombe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya

Wanging'ombe imeanza maandalizi ya awali ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa kutenga eneo la ekari 60 katika kijiji cha Igwachanya ambalo limetolewa na wananchi bila kuhitaji fidia. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 35 kwa ajili ya kupima eneo hilo na kuliweka mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 24 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya maandalizi ya awali ili kuanza ujenzi. Serikali itaendelea kushirikiana na Halmashauri katika kusukuma vipaumbele vilivyoinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe sambamba na kutafuta fedha ili kufanikisha huduma ya afya kwa wananchi wa Wanging'ombe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wanging'ombe wametumia nguvu kubwa sana kujenga zahanati na vituo vya afya vilivyopo kule Mdandu, Saja, Ilembula na maeneo mengine. Je, Serikali itapeleka lini pesa ili vituo hivyo vya afya na zahanati viweze kumalizika ujenzi?

Swali langu la pili, kule Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Jimbo la Lupembe wananchi wamejitolea ekari 52 za kuweza kujenga hospitali; je, Serikali pia inafikiria lini itaanza ujenzi wa hospitali ndani ya Halmashauri ya Njombe?  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kwanza naomba nimpongeze Mbunge kwa *initiative* kubwa sana ya

Mkoa wake wa Njombe. Nafahamu kwamba Wanging'ombe tunatumia Hospitali ya Ilebura kama *DDH* kwa ajili ya Wananchi kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha mnafahamu kwamba zile fedha ambazo nyuma zilikuwa hazipatikani za *Local Government Development Grants* ambazo zilikuwa zinaenda kusaidia hii miradi ya mabomba na ujenzi ulioanza, mwaka huu sasa zimeweza kutoka. Ninashukuru sana Halmashauri mbalimbali wameelekeza fedha hizo hasa katika kumalizia viporo vya zahanati, vituo vya afya, sehemu zingine na madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba nimuagize Mkurugenzi wa Wanging'ombe na Baraza la Madiwani kwamba mpaka mwezi wa sita tutaendelea kutoa fedha zingine mpaka ziweze kukamilika katika bajeti yetu ya mwaka huu, zikija kule lazima zingine wazielekeze katika kuhakikisha hizi zahanati na vituo vya afya katika eneo la Wanging'ombe zimefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo katika Halmashauri ya Njombe kama ulivyosema ni kweli jambo hilo limejitokeza mara kadhaa hapa katika Bunge hili na eneo limeshatengwa. Naomba niwahakikishe kwamba Halmashauri kwa kadri itakavyoibua katika bajeti yake mpango wa bajeti wa Serikali katika Halmashauri husika na Ofisi ya TAMISEMI tutashirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu kubwa ni kwamba kila Halmashauri kuwe na hospitali ya Wilaya ili wananchi waweze kuhudumiwa katika eneo hilo. Kwa hiyo, Serikali iko tayari kushirikiana na wananchi wa Njombe kuhakikisha katika mipango yetu hii tunafanikisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Njombe ili wananchi waweze kupata huduma vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya mpya nyingi hazina Hospitali za Wilaya ikiwemo na Wilaya yangu ya Tanganyika; ni nini mkakati wa Serikali wa kuweza kujenga hospitali sambamba na kuimarisha vituo vya afya wakati inajipanga kujenga hospitali hizo za Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Moshi pale kwake wanahudumiwa na Hospitali ya Halmashauri ya Mpanda iko Mpanda Mjini na Makao Makuu ya Wilaya ya Tanganyika Majarila na eneo lingine lote mpaka unaenda ziwani, wananchi wanapata shida kubwa sana. Mheshimiwa Mbunge unakumbuka tulivyokuwa Jimboni kwako tumeenda mpaka katika Makao Makuu ya Halmashauri yako ambayo inatarajiwa kujengwa hivi sasa na miongoni mwa jambo ulilolipendekeza ni kwamba tufanye utaratibu wa kuboresha kile kituo cha afya cha Majarila.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kwamba, Serikali sasa imetenga takribani shilingi milioni 700 kupeleka katika eneo lako, lengo kubwa ni kuwasaidia wananchi wako ambao wanachangamoto kubwa ya kiafya. Serikali imesikia sana kilio cha wananchi wa Tanganyika na Serikali iko tayari nadhani katika kipindi hiki kuanzia mwezi huu wa Mei mpaka tutakapofika mwezi wa Julai ni imani yangu kubwa tutapeleka nguvu kubwa sana kujenga *theatre* na kuweka vifaa vyote vya wazazi ili tupunguze vifo vya mama na watoto tuweze kuvipunguza katika eneo lako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime ina Hospitali ambayo ni Hospitali ya Mji, lakini inahudumia Wilaya nzima, ningetaka kujua ni lini Serikali itajenga Hospitali kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tarime wakati inasubiria kujenga, iipe ile hadhi kama Hospitali ya Wilaya na kuweza kuleta mahitaji kama inavyotakiwa kwa idadi wa watu wa Tarime nzima na siyo Halmashauri ya Mji tu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kesi anayoizungumzia Mheshimiwa Esther hapa inafanana na ya ndugu yangu Mheshimiwa Chumi, tuna Halmashauri zile za Mji na Halmashauri za Wilaya, kwa bahati mbaya ukiangalia Tarime Halmashauri ya Mji ndiyo ina hospitali, Halmashauri ya Wilaya haina hospitali na bajeti mnayopata ni ndogo, hali kadhalika ukiangalia Mufindi na Mafinga, Mafinga kuna Hospitali ya Wilaya bajeti ikienda inakuwa ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepita maeneo mbalimbali niliwapa maelekezo watu, kwa nini maeneo ambayo hakuna Hospitali ya Wilaya kama kuna hospitali zingine zile za *mission* tunaweka *DDH* na tunapeleka *funas* pale kwa nini kunapokuwa kwa mfano katika Halmashauri ya Tarime kuna Hospitali ya Wilaya, kwa nini watu wa Halmashauri ya Wilaya pale, fedha tunazozipeleka ambao wana bajeti kubwa sana wasielekeze fedha zingine kwa ajili ya kununua dawa na vifaatiba katika Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo nadhani hasa Wakurugenzi wetu katika maeneo husika na viongozi mliopo huko tuangalie haja ya wananchi wetu kuweza kuwahudumia, hili ni jambo kubwa na shirikishi. Kwa hiyo, naomba niagize, katika maeneo ambayo yana *scenario*

kama hii, lazima viongozi mkae muangalie ni jinsi gani tutafanya tuweze kuhudumia eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nakuunga mkono Mheshimiwa Esther Matiko ni jambo lenye mantiki na lina busara zaidi, naomba maagizo haya yachukuliwe sehemu zote kama ni jambo la kujifunza, nini tufanye tuwasaidie wananchi wetu katika suala la afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mchemba swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kituo cha afya cha Manonga jengo lake la upasuaji limekamilika; na kwa kuwa mpaka sasa hakifanyi kazi, je, Serikali ni lini, itapeleka vifaa vya upasuaji katika kituo hicho cha afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna tatizo katika kituo cha afya cha Manonga, pia tulikuwa na tatizo hili katika vituo vya afya mbalimbali ambapo tulivijenga kupitia mradi wa *ADB*, bahati nzuri tumepata mafanikio katika Mkoa wako katika kituo cha afya cha Itobo na Bukene vimeshaanza kufanya kazi, Manonga pale vifaa vilikuwa bado havijakamilika. Hivi sasa tunaendelea kuangalia ni jinsi gani tufanye kwa sababu pale kulikuwa na mapungufu ambayo yalijitokeza huku, katika suala zima mchakato wa ujenzi ule kuna mambo mengine hayakwenda sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalichukua hili tuangalie nini tufanye ili kituo cha afya cha Manonga kiweze kukamilika vizuri kuwa na vifaa pale na wananchi wa eneo lile wajisikie kwamba wana viongozi wao Mbunge wao Mheshimiwa Mwanne Mchemba na Mheshimiwa Gulamali

wanawawakilisha huku. Sasa Serikali tumelichukua hili kwa ajili ya kulifanyia kazi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, sasa aulize swali lake.

Na. 194

### **Upimaji wa Ardhi Kibamba**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Serikali inapaswa kuharakisha upimaji wa ardhi na utoaji wa hati za viwanja katika Jimbo la Kibamba ili kuepusha makazi holela.

(a) Je, ni maeneo gani ambayo hayajapimwa na lini yatapimwa?

(b) Je, kuna mpango gani wa kupunguza gharama na muda wa upimaji na utoaji wa hati ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa huduma tajwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Kibamba, maeneo ambayo bado hayajapimwa yapo katika kata za Manzese, Mabibo na baadhi ya sehemu katika Kata za Ubungo, Mburahati, Kimara, Saranga, Goba, Mbezi, Kibamba, Kwembe na Makuburi. Tayari upimaji unaendelea katika Kata ya Kimara ambapo viwanja 3,196 vimepimwa. Taratibu zinakamilishwa ili kuwapimia wananchi 186 waliolipia gharama katika kata ya Kibamba ambao



unahusisha upimaji wa maeneo ya huduma za umma 123 katika Manispaa ya Ubungo. Aidha, upimaji umepangwa kufanyika katika Kata za Mbezi, Msigani, Goba na Kwembe kupitia kampuni binafsi zilizoidhinishwa na Serikali ili kuharakisha zoezi hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya gharama za upimaji vinavyotumika sasa vipo kwa mujibu wa sheria ambavyo vilipangwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali na kwa kuzingatia matumizi ya zana za kisasa za upimaji ikiwemo mifumo ya kijiografia na kompyuta (*Geographical Information System*). Matumizi ya mifumo hiyo imerahisha zaidi upimaji ambapo ramani za hati (*deed plan*) katika Manispaa ya Ubungo zimeongezeka na kufikia hati 1,000 kwa mwezi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika swali la nyongeza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, haijui mipaka ya Jimbo la Kibamba, kwa sababu kati ya kata alizozitaja kwamba ni za Jimbo Kibamba, kata zifuatazo ni za Jimbo la Ubungo. Kata ya Ubungo, kata ya Mburahati, kata ya Kimara na kata ya Makuburi. Kwa hiyo, maana yake Kata tano alizozitaja kwenye jibu siyo za Jimbo la Kibamba na siyo sehemu ya swali nililouliza. Ni aibu zaidi kwamba kasi ya upimaji ni viwanja 186 tu, kwa upande wa kata ya Kibamba. Sasa nina maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu swali la msingi halijajibiwa, je, Serikali iko tayari sasa kuainisha kata kwa kata, mtaa kwa mtaa, kwa upande wa Jimbo la Kibamba, ratiba ya kuharakisha upimaji ili kuepusha sehemu hii ambayo ni Jimbo jipya kabisa nalo kuwa na makazi holela na maeneo mengi yasiyopimwa? (*Makofi*)

Swali la pili, matatizo haya ya kuchelewa upimaji, na udhaifu katika upimaji yamekwisha leta madhara sasa hivi

tunavyozungumza ambapo Serikali imetoa *notice* na Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwa wananchi kutoka *Stop Over*mpaka maeneo ya Kiluvya mita 121 kutoka katikati ya barabara kwa maana ya mita 240 ukijumlisha pande zote mbili za barabara, wananchi wote hawa wanatakiwa kubomoa nyumba zao hivi sasa tunavyozungumza, lakini ninayo hukumu ya Mahakama ya mwaka 2013 yenye kuonesha kwamba wananchi hao walihalalishwa na hati za vijiji kwenye Kijiji cha Kimara, kijiji cha Mbezi na Kijiji cha Kibamba.

Je, Serikali iko tayari maana hili jambo tumeishauriana muda mrefu, kwa sababu sasa hivi ni dharura hili jambo, kutoa kauli ya kusitisha *notice* hii ya *TANROADS* kwanza ili majadiliano yafanyike kuhusu utata huu wa upana wa barabara, maana maeneo mengine yote ni mita 60 lakini hapa peke yake ni mita 121.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya Serikali.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mnyika, siyo aibu kwa sababu tunajua nini tunachokifanya. Hapa tulikuwa tunazungumzia matatizo ya Watanzania kama Ofisi ya Rais – TAMISEMI na unafahamu Jimbo lako limegawanywa juzi tu.

Mheshimiwa Mnyika, ukisema aibu na wakati wewe ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani na taarifa tunazipata mwaka mzima toka Baraza halijaanza, ndiyo maana mambo mengine ya msingi unashindwa kuyasimamia kwa wananchi wako, hilo ndio jambo la msingi lazima tukubaliane nalo.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo hoja ya msingi kwanza, mipango ya Serikali tumesema nimezungumza

maeneo mbalimbali na jinsi Serikali inavyochukua hatua mbalimbali na ndiyo nimekuambia Mheshimiwa Mnyika hii ni *politics*, haya ni mambo rahisi hata hayataki nguvu haya. Kikubwa zaidi naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge, katika mipango hii ya upimaji katika maeneo yetu tunapaswa wenyewe tuwe karibu jinsi gani tutafanya ili maeneo yetu yapimwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema katika jibu letu la msingi, leo hii ukiaangalia maeneo mengine wamefanya vizuri kwa kutumia wataalam wao mipango shirikishi zaidi na kutumia makampuni mbalimbali, kufanya mipango shirikishi ambayo mwisho wa siku inaweza kujibu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kwamba Serikali imesikia kilio chako Mheshimiwa Mbunge, wala usiwe na hofu, itajitahidi kufanya kila liwezekanalo eneo la Jimbo la Kibamba kama nilivyosema, nashukuru sana, kwa sababu timu sasa iko *site* na Wizara ya Ardhi siku moja ilikuwa inajibu kijumla yake swali la ardhi katika Wilaya ya Ubungo kwa ujumla wake. Naomba nikutoe hofu kwamba, Serikali itashirikiana vema na Baraza la Madiwani kwa kuangalia jinsi tutakavyofanya ili tuweze kupima, ambayo itakuwa ni manufaa makubwa kwa wananchi wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la upana wa barabara. Upana wa barabara upo kwa mujibu wa sheria, bahati nzuri wenzetu wa Wizara ya Ujenzi hapa ndiyo wanajua sheria ukianza ile sanamu pale Posta mpaka unafika Ubungo kuna upana maalum ambao umezungumzwa kisheria, na ukitoka pale mpaka ukija pale Kimara Temboni kuna sheria inaelekeza. Ukitoka pale mpaka unafika maeneo ya karibu na Mto Ruvu sheria inazungumza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kuna *notice* nadhani wenzetu wa Wizara ya Ujenzi wanajua nini wanachokifanya katika eneo lao hilo watatoa maelekezo kwa kadri wanavyoona kwamba inafaa, kutokana na *notice* iliyotolewa na utaratibu wa kisheria jinsi ulivyo katika eneo lao la kazi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea swali la nyongeza.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, majibu ya Serikali yameonesha kwamba eneo pekee lililopimwa katika Jimbo la Ubungo ni eneo la Kimara ambalo kumepimwa viwanja 3,196 au nyumba 3,196; Je, Serikali inasemaje katika maeneo yaliyobaki ya Makuburi, Manzese, Ubungo na maeneo mengine ya Jimbo la Ubungo?

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri amejibu vizuri. Maswali haya yanapaswa kuwa ndani ya mipango ya Halmashauri husika, kama tunavyopanga mipango juu ya shughuli nyingine za maendeleo ndani ya Wilaya basi tujipangie mipango ya namna ya kupima na kupanga miji yetu ndani ya Wilaya zetu, haiwezi kuanzia hapa. Nataka niwaambie wote wawili hata huo mnaosema Mheshimiwa yangu Kubenea tulikuwa wote hapa Kimara, hatupimi pale tunarasimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam ni moja ya miji ambayo imejengwa siku nyingi, imejengwa vibaya ni makazi holela. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa ni kurasimisha angalau wananchi waweze kupata barabara za kupitisha huduma zao, waweze kupata hati kidogo ili angalau nyumba zao thamani zile zisipotee, angalau thamani ya mali waliyowekeza pale na zile hati zivasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imekuja na mpango mbadala wa kuwawezesha hawa maskini kurasimisha mali zao ili angalau zivasaidie katika kujitegemea. Kwa hiyo, tunafanya zoezi la urasimishaji, hapa unaposema ndugu yangu Kubenea tulienda wote Kimara tunafanya zoezi la urasimishaji na haya anayosema ndugu

yangu tunafanya zoezi la urasimishaji, upimaji mpya utafanywa Dar es Salaam baada ya kumaliza *master plan*, tuliyonayo ni ya mwaka 1979, sasa hivi tunaandaa *master plan* tume-engage wataalam, tukishamaliza *master plan* ambayo itashirikisha viongozi wote wa Dar es Salaam na wananchi wa Dar es Salaam, Dar es Salaam itapangwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ni zoezi la urasimishaji kuwawezesha wananchi kutoka kwenye hadhi ile ya makazi holela angalau waitwe nao wanaishi kwenye makazi rasmi. Hilo ni zoezi ambalo linaendelea sasa na zoezi hili ni shirikishi, wananchi kwenye mitaa wanashiriki wenyewe, wanachangia gharama wenyewe, kupanga maeneo yao katika mitaa yao. Kwa hiyo naomba zoezi hili tushirikiane na ninyi tuanzie kwenye mitaa kujadili halafu Wizara hizi mbili tushirikiane na mipango yenu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Aida, Joseph Khenan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 195

### **Changamoto ya kupata Hati Miliki - Sumbawanga**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Wananchi wengi Sumbawanga hawana hati miliki; aidha, kumekuwa na changamoto nyingi katika kupata hati hiyo hali inayowafanya wananchi kukata tamaa.-

Je, ni gharama kiasi gani zinazohitajika ili kupata hati miliki?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali

Ia Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida hati miliki za ardhi hutolewa kwa utaratibu wa mwombaji kuchangia gharamaza upatikanaji wa hati husika. Utaratibu huu umetokana na matakwa ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 95 ambayo inaelekeza kuwa ardhi ina thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kupata hati miliki hutofautiana kutokana na thamani ya ardhi katika eneo linaloombewa hati, ukubwa wa eneo na matumizi yanayokusudiwa katika eneo husika. Kwa mantiki hiyo, gharama za kupata hati miliki hutofautiana kwa kuzingatia vigezo hivyo. Gharama zinazotakiwa kulipwa wakati wa umilikishaji ardhi ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ada ya upimaji;
- (ii) Ada ya uandaaji wa hati ambayo ni shilingi 50,000 ni *fixed*;
- (iii) Ada ya usajili wa hati;
- (iv) Ushuru wa stempu;
- (v) Gharama za upatikanaji ardhi;
- (vi) Ada ya mbele (*premium*) ambayo ni asilimia 7.5 ya thamani ya ardhi; na
- (vii) Ada ya ramani ndogo (*Deed Plan*) ambayo ni shilingi 20,000 nayo ni *fixed*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ada ya upimaji, usajili wa hati, ushuru wa stempu na gharama za upatikanaji ardhi hutegemea ukubwa na thamani ya ardhi katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na uwiano wa gharama za umilikishaji wa ardhi nchini, Wizara imeandaa na kusambaza mwongozo wa ukadiriaji wa bei za viwanja kwa Halmashauri zote nchini. Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini hazina budi kuzingatia mwongozo wa bei elekezi za viwanja uliotolewa ili kuwawezesha wananchi kupata hati miliki kwa gharama nafuu zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pia nashukuru kwa ufafanuzi alioutoa Naibu Waziri ambao utaleta mwanga kidogo kwa wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga wameamua sasa kufuata utaratibu ili wapate hati, shida yao siyo kumiliki tu hati, zivasaidie kwenye taasisi pia za kifedha, lakini hati zimekuwa zinachelewa sana. Hamuoni kwamba kuendelea kuchelewa kwa hati hizo mnawanyima fursa wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa masuala ya maendeleo kwa sababu wanakosa mambo muhimu hasa katika taasisi za fedha?

Swali la pili, Maafisa Ardhi wa Manispaa ya Sumbawanga wanajitahidi sana kwa jitihada zao kuwafuata wananchi kwenda kupima maeneo, lakini wanakabiliiana na changamoto za usafiri, pamoja na vitendea kazi vingine kwenda kupima ardhi.

Je, Serikali hamuoni kuna umuhimu zaidi wa kuwapa kipaumbele ili wale wakafanye kazi kwa mujibu wa sheria ili wasipate malalamiko kama yanayoendelea kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza amezungumzia ucheleweshaji utaratibu wa kupata hizo hati pengine unakuwa ni mrefu na ni kinyume na utaratibu. Pengine Mheshimiwa Aida bado yuko na mawazo yale ya zamani, kwa sababu sasa hivi kama ambavyo tulieleza kwenye bajeti iliyopita ndani ya mwezi mmoja kama umekamilisha malipo yako vizuri, unapata hati yako, hakuna tena usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda zetu zote Nane zinatoa hati hizo tumeishaweka wataalam kule wako wanafanya kazi hiyo. Kama huko kwake bado hilo linafanyika, nadhani siyo sahihi, na mimi siamini kama linafanyika hivyo kwa sababu utendaji wa Wizara kupitia Kanda zake unakwenda kwa utaratibu na mujibu wa sheria ambavyo tumewawekea, hivyo hakuna tena suala la ucheleweshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Maafisa Ardhi kukosa usafiri na vitendea kazi, naomba tu nitumie fursa hii watendaji hawa ambao wako katika Halmashauri ni jukumu la Halmashauri kuweza kuona ni jinsi gani watu hawa watafanya kazi. Wizara tuna-*support* yale ambayo yako nje ya uwezo wa Halmashauri. Hii ni Idara kama Idara zingine, kama Idara ya Elimu, Idara ya Afya wanakuwa na usafiri, wanawekewa bajeti zao kila mnapopanga. Mnashindwa nini kufanya hilo kwa Idara ya Ardhi, kwa sababu sehemu nyingi kila unapoenda unakuta Idara ya Ardhi ile ni ombaomba, wakitaka kwenda *field* mpaka wabembeleze gari sijui la Elimu, lakini ni jukumu la Halmashauri husika kui-*treat* Idara hii sawa na Idara zingine. Kwa sababu ndiyo kwanza wanaofanya zile kazi ambazo inawezesha Idara zingine kuweza kufanya kazi zao kwa ukamilifu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe kwamba mbali na Wizara kusaidia, ni jukumu la kila Halmashauri kuhakikisha kwamba tunapoweka bajeti zetu, katika kupanga vitendea kazi pamoja na kwamba vina gharama lakini lazima tukadirie. Wizara pia inakwenda kuweka utaratibu kwenye maeneo ya Kanda zetu kutakuwa na vifaa vya upimaji kule ambavyo vitasaidia katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, tusaidiane Halmashauri na Wizara ili tuwarahisishie kazi hii na wao waweze kufanya kazi zao kwa ukamilifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri



amejibu vizuri sana, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge niwape *experience* kidogo kwa swali la nyongeza hili kwamba hati hazitayarishwi na Wizara, hati zinatayarishwa pale kwenye Halmashauri. Sasa nawaombeni ninyi Waheshimiwa Wabunge mkirudi majumbani kwenye Halmashauri zenu mfanye tu ujanja ambao nimegundua wanafanya.

Meshimiwa Naibu Spika, nimekuta Kibaha pale hati zinaanza kuandaliwa pale Wilayani makaratasi, hata lile jalada la hati linatengenezwa pale sisi tunakuja kusaini tu huku mwisho. Mkienda kwenye Masjala za Hati kwenye Wilaya zenu zote, mtakuta hati zile zimetayarishwa ziko kwenye mafaili haziendi kokote.

Waheshimiwa Wabunge, hebu kila mmoja aende kwenye Masjala ya Ardhi ya Halmashauri yake, utakuta hati zimeshaandikiwa, watu wameshalipa wametengenezewa na yale majalada ya kaki halafu zimewekwa pale miaka miwili mitatu. Hazifiki kwa Makamishna wa Wizara ya Ardhi kusaini kwa nini? Ndiyo kazi tunayofanya sisi wenzenu kuja kwenye Majimbo yenu kuja kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sasa wote muwe ma-*auditor* muende kwanye masjala za ardhi mkaziondoe zile hati ambazo zimekaa mle, watu wanataka zikae muda mrefu wasahau halafu waweze kubadilisha wampe mtu mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naomba mtusaidie kwenda kwenye masjala, mfanye ukaguzi watu wote ambao majalada yameshaandikwa yafike kwa Makamishna wapewe hati zao, tunataka mwezi mmoja tangu mtu amelipia apate hati yake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, sasa aulize swali lake.

Na. 196

**Uimarishaji wa Huduma za Maji Nchini**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa hotuba ya bajeti 2016/2017 Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilionesha kuwa Serikali ya India imesaidia kiwango kikubwa cha fedha kwa ajili ya uimarishaji wa huduma ya maji nchini.

Je, Serikali inaweza kutueleza juu ya utekelezaji wa jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Jimbo la Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu ilitoa taarifa ya mchango mkubwa inaoupata kutoka Serikali ya India ili kuboresha huduma ya maji nchini. Kwa kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India, awamu ya kwanza Serikali ya Tanzania ilipata dola za Kimarekani milioni 178.125.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizotekelezwa katika awamu ya kwanza ni mradi mkubwa wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu, ujenzi wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara, ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa mradi wa Chalinze-Wami awamu ya tatu. Utekelezaji wa kazi ya upanuzi wa ruvu juu na ulazaji wa bomba kutoka Mlandizi hadi Kimara umekamilika na miradi ya ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji kwa Jiji la Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa mradi wa Chalinze-Wami awamu ya tatu inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya pili, Serikali

ya India itatoa fedha dola za Marekani milioni 268.35 kwa ajili ya mradi mkubwa wa kutoa maji katika mradi wa *KASHWASA* kutoka kijiji cha Solwa kwenda katika miji ya Tabora, Igunga, Nzega, Tinde na Uyui pamoja na vijiji 89 vinavyopitiwa na bomba kuu umbali wa kilometa 12 kila upande, wakandarasi wa kutekeleza mradi huo wamepatikana na wapo katika hatua ya maandalizi ya utekelezaji (*mobilization*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya tatu Serikali ya India imeahidi kutoa fedha kiasi cha dola milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji 16 ya Tanzania Bara pamoja na miradi ya maji upande wa Zanzibar. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kufanya manunuzi ya Mhandisi Mshauri atakayefanya mapitio ya usanifu wa miradi na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi, kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Othman Hija swali la nyongeza.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri npenda kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa upande wa Tanzania Bara maeneo yatakayohusika ameyataja, je, kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni maeneo gani yatakayohusika na mradi huu?  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama unavyofahamu fedha zile zimetolewa dola milioni 31 kwa ajili ya Zanzibar, lakini atakayeamua kwa upande wa Zanzibar fedha zile zinaenda kipande gani cha nchi ya Zanzibar ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hiyo, tumeshawasiliana nao wamesema wanafanya majadiliano na Serikali kwa ngazi za juu ili kuweza kuamua kwamba fedha hizi zitakwenda kuhudumia sehemu gani ya Zanzibara. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 197

**Fidia Kidogo Waliyolipwa Wananchi Waliopisha Mradi wa Bwawa la Kidunda**

**MHE. PROSPER J. MBENA** aliuliza:-

Ujenzi wa Bwawa la Maji Kidunda lililopo katika kata ya Serembala, Morogoro Kusini umesababisha matatizo makubwa kwa wananchi wa kata ya Serembala, Magogoni na vijiji jirani kutokana na fidia kidogo kwa kupisha ujenzi wa mradi huo ikilinganishwa na mali walizoziachia yaani mashamba, nyumba zao na mali nyingine zilizo kwenye maeneo makubwa ya ardhi iliyochukuliwa kwa ajili ya mradi huo.

(a) Je, Serikali iko tayari kurudia zoezi la tathmini ya mali za wanavijiji wote walioathirika kwa kutoa nyumba na mashamba yao ili kupisha mradi wa bwawa la Kidunda na kuwalipa fidia wanayostahili?

(b) Je, Serikali iko tayari kwenye bajeti hii kumalizia malipo ya takribani shilingi bilioni 3.7 kuwafidia wananchi hao kulingana na tathmini iliyofanyika?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuwawekea miundombinu ya uanzishwaji wa mashamba ya umwagiliaji na viwanda vidogo vidogo kwenye kata ya Serembala kwa ajili ya kutoa ajira kwa wananchi Serembala Magogoni, Mvuna na Kkata za jirani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaandaa malipo ya fidia kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ambayo inaelekeza pia kuwa endapo malipo ya fidia yatachelewa kulipwa kwa zaidi ya miezi sita tangu kupitishwa, mlipaji anapaswa kufanya mapitio na kulipa nyongeza kutokana na muda uliozidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 7.4 kwa familia 2,603 kama fidia ya kupisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kwa ajili ya fidia kulingana na tathmini iliyofanyika. Malipo yamekuwa yanafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Kidunda linajengwa mahsusi kwa ajili ya kuhifadhi maji ya matumizi ya majumbani kwa wakazi wa Kibaha, Bagamoyo na Dar es Salaam. Bwawa hilo halitahusu kilimo kikubwa cha umwagiliaji. Serikali itaangalia uwezekano mwingine wa kuweka miundombinu wezeshi ya kilimo cha umwagiliaji kulingana na maeneo husika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prosper Mbena swali la nyongeza.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa fidia kamili kwa wale waliohusishwa na kuchukuliwa maeneo yao haijalipwa kama alivyozungumza

Mheshimiwa Waziri kwamba kuna bakaa ya shilingi bilioni mbili ambayo wametenga kwa ajili ya kulipwa; na kwa kuwa, ninayo taarifa kwamba *DAWASCO* wameshapeleka mabango ili yawekwe kwenye maeneo yote ya sehemu hizo kuzuia wananchi wasifanye shughuli zozote za maendeleo, kwa maana kwamba tayari wameshakabidhiwa maeneo hayo.

Je, sasa Serikali iko tayari kusitisha uwekaji wa mabango hayo hadi wananchi watakapolipwa fidia yao kamili? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa maeneo ya Bwakila Chini, Kiganila na Magogoni katika kata hii ya Serembala imekumbwa na mafuriko makubwa sana na wananchi wako kwenye maji kwa wiki tatu sasa.

Je, Serikali itapeleka msaada wa chakula na madawa ya dharura? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni kweli tayari tumeshalipa zaidi ya shilingi bilioni saba katika hilo eneo na kilichojitokeza ni kwamba baada ya *DAWASCO* kulipa ile fedha yale maeneo kwa taarifa ambazo tulizipata wananchi walianza kuwauzia watu maeneo yale ambao hawajui kwamba maeneo yale yameshalipwa fidia. Baada ya taarifa hiyo kupatikana, Mkurugenzi wa Halmashauri yako Mheshimiwa Mbunge ndiye aliyeamua kuweka vibao ili kuweza kuwapa tahadhari wananchi kwamba lile eneo wasiuziwe kwa sababu lilishalipwa fidia vinginevyo tutapata matatizo zaidi katika Serikali. Kwa hiyo mabao yale niseme kwamba hayajawekwa na *DAWASCO* yamewekwa na Mkurugenzi wa Halmashauri yako.

Swala la mafuriko, kwanza nikupe pole kweli nami ninayo taarifa kwamba kuna baadhi ya vijiji ambavyo

vimeingiliwa na maji, kwa vile taarifa hii uliyoitoa ya mafuriko na kuomba msaada Serikali imesikia na iko Idara husika inayohusika na jinsi ya kusaidia maeneo ya maafa basi nafikiri naomba ulifikishe huko ili liweze kushughulikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 198

### **Huduma zinazofanywa na Mawakala wa Pembejeo**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu mawakala wanaosambaza pembejeo wamekuwa wakihujumu wakulima kwa kutowafikishia kabisa au kuwaletea pembejeo ambazo siyo sahihi na kinyume na maelekezo ya Wizara husika:-

(a) Je, Serikali ilishughulikiaje malalamiko ya wakulima wa Wilaya ya Simanjiro?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa mawakala wasio waaminifu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2013/2014 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara ilipokea malalamiko kutoka kwa wakulima wa kijiji cha Narakauo kuhusu hujuma ya matumizi mabaya ya vocha za pembejeo za kilimo. Halmashauri ya Wilaya iliunda Kamati ya ufuatiliaji na uchunguzi ili kushughulikia malalamiko hayo. Baada ya uchunguzi ilibaini kuwa kijiji cha Narakauo

hakikupelekewa mbolea za kupandia na kukuzia na kasoro zingine za utendaji zilizofanywa na Mwenyekiti wa Kamati ya Vocha na Afisa Mtendaji wa Kijiji. Hatua zilizochukuliwa baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Kamati Teule ni pamoja na watendaji wa zoezi hilo kufikishwa katika vyombo vya sheria, katika maana ya Polisi na TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi, hadi sasa vyombo hivyo vya dola havijatoa taarifa ya matokeo ya uchunguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali ya Wilaya iliamua kuwa mawakala walioonekana kushiriki katika ubadhilifu huo hawataruhusiwa kutoa huduma ya kusambaza pembejeo za ruzuku katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro imezuia malipo ya mawakala hao pamoja na kuwaondoa katika orodha za mawakala wanaosambaza pembejeo Wilayani humo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Umbulla swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, wakulima hasa wa jamii ya wafugaji wanapopelekewa pembejeo kwa maana ya mbegu, mbolea na madawa, pale ambapo hawana maelekezo mazuri ya uelewa wanazikataa pembejeo hizo na hivyo kuwanufaisha wale mawakala kwa kujinufaisha kuziua tena.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba wanapowapelekea pembejeo wakulima wa jamii ya wafugaji na wengineo ambao hawana uelewa mzuri wanawaelekeza vizuri ili waweze kunufaisha kilimo chao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Tarafa ya



Dongobesh katika Wilaya ya Mbulu kwa msimu uliopita hawakupielekewa kabisa mbolea na mbegu na dawa kwa ajili ya pembejeo za kilimo kwa msimu uliopita. Nini kauli ya Serikali pale ambapo inatokea tatizo kama hilo hasa tukiwa katika harakati za kuboresha kilimo tunakoelekea kwenye Tanzania ya viwanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba jamii za wafugaji lakini vilevile Watanzania walio wengi/wakulima hawana ufahamu mzuri kuhusu umuhimu na namna ya kutumia mbolea kwa ajili ya kuendeleza kilimo chao. Katika kushughulikia changamoto hii Serikali imekuwa ikiimarisha huduma za ugani ili wananchi waweze kupata elimu na ufahamu mzuri ili waendee kutumia mbolea kwa namna inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa - Halmashauri zetu, tunaendelea kutoa miongozo ile vile kutoa elimu kwa Maafisa Ugani ili waweze kutoa taarifa sahihi na elimu inavyotakiwa kwa ajili ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile katika kuhakikisha kwamba huduma za ugani zinaendelea kuboreshwa, Wizara yangu imebuni Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*ASDP/II*) ambao utekelezaji wake unaanza katika mwaka wa fedha na moja kati ya masuala yanayotiliwa mkazo sana ni masuala ya ugani na tunategemea kuendelea kuimarisha vituo vya rasilimali za kata (*World Resource Centre*) ili ziendee kutoa teknolojia muhimu ya kilimo na elimu ili wananchi waweze kuweza kutumia mbolea na kufanya kilimo ambacho kinakuwa na tija zaidi.

Pia Wizara kwa sasa imejipanga kutumia huduma za ugani mtandao (*E-extension services*) ili iwe rahisi hata kwa

kutumia tu simu za mikononi wananchi waweze kupata taarifa muhimu kuhusiana na namna ya kutumia mbolea lakini vile vile kuhusiana na taarifa zingine muhimu za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la nyongeza la pili kuhusiana na kata ya Dongobesh kutopata pembejeo katika msimu uliopita, nimueleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika msimu uliopita siyo maeneo yote nchini yalipata pembejeo za kilimo zile za ruzuku, kwa sasa Wizara imejipanga ili makosa kama haya na upungufu kama huu usitokee tena, kuhakikisha kwamba mbolea inapatikana dukani kama CocaCola.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnakumbuka kauli maarufu ambayo Waheshimiwa Wabunge najua mnaipenda sana ya Mheshimiwa Mwigulu alipokuwa Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi, hilo alilokuwa anasema limetima kuanzia msimu unaokuja mbolea ya *DAP* na *UREA* itapatikana nchi nzima kwa bei ambayo itakuwa na dira ili kuhakikisha kwamba hatutakuwa tena na upungufu na bughudha zingine ambazo zimekuwa zikitupata katika kusambaza pembejeo za kilimo. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepata dharura kidogo Mheshimiwa Chenge atakuja kunipokea.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la nyongeza, Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa pembejeo nyingi mwaka huu mawakala wengi walipewa muda wa kupeleka kwa wakulima na hazikufika kwa wakulima mwaka huu, mawakala wameshapewa na Kamati ile ya pembejeo za Wilaya na sasa pembejeo hazijafika.

Je, Serikali inatuambia nini kwa pembejeo hizi ambazo hazijafika wakulima bado wanasubiri na msimu umeshapita?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi ili tuende mbele.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpungeze sana Mheshimiwa Flatei kwa sababu suala alilolileta kwenye swali la nyongeza limekuwa ni suala ambalo amelifuatilia mara nyingi sana Wizarani. Kimsingi amekuwa ni Mbunge mzalendo kama mlivyo wengi humu ndani. Ameniletea orodha ya Mawakala ambao walichelewa kuleta pembejeo Jimboni kwake lakini bado wanataka kulipwa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wakala ambaye hakuweza kuleta pembejeo kwa wakati hatalipwa. Kimsingi Wizara na Serikali haiwezi kulipa kwa huduma ambayo haijatolewa.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea. Swali letu la mwisho linaulizwa na Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, Mbunge wa Kahama Mjini, kwa niaba yake Dkt. Chegeni.

Na. 199

### **Mfumo wa Elimu Nchini Kuchangia Matatizo**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. JUMANNE K. KISHIMBA)** aliuliza:-

Mfumo wetu wa elimu unaonekana kuchangia mfumuko wa matatizo ikiwemo kujenga mazingira ya udanganyifu na wizi wa mitihani hali inayopelekea baadhi ya wanafunzi kufutiwa matokeo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kumpima mwanafunzi kwa kutathmini tangu shule ya msingi na kuoanisha na mtihani wake wa mwisho ili kupata uhalisia na uwezo badala ya kumpima mwanafunzi kwa kigezo cha mtihani wa siku moja?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, Mbunge wa Kahama Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa tathmini unaotumika kwa sasa unajumuisha alama za upimaji wa mwanafunzi awapo shuleni yaani alama za upimaji endelevu pamoja na mtihani wake wa mwisho. Mfano, katika matokeo ya mtihani wa mwisho wa kidato cha nne, kidato cha sita na ualimu yaani cheti na diploma, alama za upimaji wa mwanafunzi awapo shuleni zinachangia asilimia 30 na mtihani wa mwisho unachangia asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya utafiti zaidi kwenye mifumo ya utahini inayotumika katika nchi mbalimbali duniani kwa lengo la kuboresha mfumo wa utahini kwa kadri inavyoweza na inavyoonekana inafaa na kwa kuzingatia mazingira ya utoaji wa elimu bora nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, hoja ya swali la Mheshimiwa Kishimba ni kwamba kumekua na utaratibu wa kumtahini mwanafunzi kwa mtihani wa mwisho na wakati mwingine unakuta mwanafunzi pengine zile siku za mwisho anakuwa na matatizo ambayo yanamfanya ashindwe kufaulu vizuri.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuangalia maendeleo ya mwanafunzi huyu ili kusudi maendeleo yake yawe ni sehemu ya mtihani wake wa mwisho ili kuondoa mchanganyiko huu?

Swali la pili, kwa vile kumekuwa na wizi wa mitihani mara kwa mara na hii inachangiwa kwa sababu wanafunzi wanajiandaa kwenda kushinda mtihani badala ya kujua namna ya kujibu mtihani.

Je, Serikali inatafuta mbinu gani mbadala za kuwasaidia vijana badala ya kukariri kufanya mtihani, wafanye mtihani kwa kuelewa namna ya kushinda mtihani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, Serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa kutumia matokeo endelevu yaani mwanafunzi amekuwa akipimwa katika muda wake anaokuwa darasani, vilevile hata wale wanaofanya shughuli za vitendo, kwa mfano wale wanaosoma masomo ya ufundi wamekuwa wakienda kwenye mazoezi wanafuatiliwa na pia shughuli za vitendo zimekuwa zikichangia asilimia 30 niliyosema katika mitihani ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mtihani wa mwisho ni kweli ndiyo unakuwa na nafasi kubwa zaidi kwa ajili ya hiyo asilimia 70; endapo mwanafunzi amepata tatizo siku ya mwisho ya mtihani, taarifa huwa zinatolewa na kuweza kuangalia kwamba alikuwa kwenye mazingira gani. Wakati mwingine mwanafunzi anashauriwa asifanye mtihani kama hali yake kwa mfano itakuwa ni ya ugonjwa ili aweze kurudia na kufanya mtihani wakati mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wizi kwa kiwango kikubwa Serikali imeweza kudhibiti tatizo hilo, nanyi mtakuwa mashahidi katika kipindi hiki, hasa toka tumeingia halijawahi kutokea tatizo la wizi wa mitihani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ningependa kuweka msisitizo kwenye suala la wizi wa mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kulihakikishia Bunge lako kwamba Serikali imedhibiti suala la wizi wa mitihani na kinachotokea ni udanganyifu katika mitihani, ambapo baadhi ya Walimu ama huwa baada ya kufungua zile karatasi za mitihani wanaenda pembeni wanawaandalia wanafunzi majibu na kuyapeleka katika chumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Serikali imekuwa pia makini katika kuhakikisha kwamba inaangalia kwa karibu usimamizi wa mitihani na wote ambao wanakuwa wanajihusisha na udanganyifu katika mitihani hatua zimekuwa zikichukuliwa na zitaendelea kuwa zinachukuliwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Doto Biteko swali la nyongeza.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi mzuri wa mitihani ni pamoja na kuwalipa stahiki zao wasimamizi wa mitihani wakiwemo walimu pamoja na askari, lakini mwaka 2015 walimu walisimamia mitihani ya kidato cha nne wakakopwa fedha zao, fedha hizo mpaka sasa hawajalipwa. Mnaomba kujua ni lini walimu hao watalipwa fedha zao walizokopwa wakati wanasimamia mitihani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, lini watalipwa walimu wetu hawa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka 2015 tulikuwa na deni ambalo walimu walisimamia mitihani

walikuwa hawajalipwa na deni lile baada ya uhakiki lilikuwa karibuni shilingi bilioni 6.4. Ninapenda kuzipongeza baadhi ya Halmashauri hasa kuna Halmashauri maalum zingine zilifanya *initiative* ya kulipa zile fedha karibu shilingi bilioni tatu ziliweza kulipwa, hivi sasa tuna deni ambalo ni *outstanding* karibuni shilingi bilioni 3.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba deni lile tulipeleka Hazina na liko katika hatua ya mwisho kwa wale watu ambao hawajalipwa watalipwa pesa zao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa swali la Mheshimiwa Kishimba linafanana kabisa na changamoto ya udanganyifu wa mitihani yaani *thesis and dissertation* kwa wanafunzi wa shule ya Uzamili na Uzamivu elimu ya juu.

Je, Serikali imejipangaje kuwa na mfumo mahsus katika kudhibiti ubadhilifu wa mitihani kwa maana ya kuwa na mfumo mathalani *central system plagiarism test?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika masuala haya ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wanafanya mtihani na wanapimwa kwa kiwango wanachostahili kwa kadri ya kuwapima uelewa wao, Serikali tumeendelea kufanya hivyo. Kwa upande wa vyo vikiu hasa kwa upande wa wanapofanya maandishi yao, niseme *thesis* kwa mfano, kweli kumekuwa kunajitokeza udanganyifu wa watu kuomba ama kufanyiwa na watu, wakati mwingine kunakili maandiko ya watu wengine waliopita kiasi kwamba mtu anakuwa hajafanya kazi yake na kupimwa kwa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeshaliona

hilo na tumeshaandaa mfumo kiasi kwamba kila mtu akishamaliza andiko lake litakuwa linapitishwa humo kiasi kwamba likioanishwa litajulikana kwamba huyu ameiba kutoka kwa andiko la mtu mwingine. Ikizingatiwa katika mfumo huu wa *digital* watu ni rahisi kuiba. Kwa hiyo tumeshaona namna ya kudhibiti eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu ya sekondari ngazi mbalimbali tunafanya uhakiki. Kwa mfano, mara hii ya mwisho hata sisi wenyewe Mawaziri tumekuwa tukitembelea baadhi ya shule za kidato cha sita kuona kwamba taratibu na sheria zinazingatiwa katika sehemu za mitihani. Mfano, safari hii nimeenda shule ya Ifunda na shule ya *Iringa Girls*. Hivyo tunasimamia kikamilifu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali la mwisho, Mheshimiwa Anna Gidarya.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Pamoja na kuwa lugha yetu ya Taifa ni kiswahili lakini kumekuwa na mkanganyiko katika mfumo wetu wa ufundishaji wanafunzi. Shule nyingi za Serikali kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba wanafundisha kwa kiswahili lakini wakifika sekondari wanaambiwa wazungumze lugha ya kiingereza. Sambamba na hilo, tatizo hili liko kwenye vyuo vyetu vya Serikali ya Mitaa hususan Hombolo. Masomo yote yanafundishwa kwa kiingereza ilhali watu hawa wanaenda kusimamia watu ambao hawajasoma.

Je, Serikali haioni ni muhimu kubadilisha mitaala hii kuondoa mkanganyiko huu katika sera ya ufundishaji?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi tumalize.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza tunamshukuru kwa kuwa ni mdau wa kiswahili na kwa namna ya pekee



nimpongeze Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kuwa Balozi wa Kiswahili Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu ya msingi kiswahili imekuwa ndiyo lugha ya kufundishia na kiingereza inakuwa kama somo. Tunafanya hivyo kwa sababu tunaamini Watanzania wengi lugha ya kiswahili japokuwa ni lugha ya pili, lakini wana uelewa zaidi na hivyo kuwawezesha kuelewa vizuri elimu yao ya msingi katika lugha ambayo wamekuwa nayo. Hali kadhalika tunapokwenda kwenye sekondari ndipo sasa wanapotumia lugha ya kiingereza kama lugha ya kufundishia na kiswahili kama somo na hiyo sasa inaenda vilevile kwa upande wa zile shule zinazotumia lugha za kiingereza toka awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu hakatazwi kuweka msisitizo katika lugha ile ambayo anafahamu inaeleweka na wanafunzi kwa uzuri zaidi ili kumfanya yule mwanafunzi kile kilichofundishwa aweze kukitafsiri katika lugha yake iliyo rahisi na kukielewa vizuri zaidi. Ieleweke kwamba lugha pekee siyo maarifa. Lugha pamoja na yale maarifa unayofundishwa ndiyo yanayomfanya mwanafunzi kuwa imara na kuweza kutumika katika nyanja mbalimbali zinazohitajika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tumemaliza kipindi chetu cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo ya wageni. Wageni waliopo kwa siku ya leo, tunao wageni watatu wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe ambao ni Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu Mstaafu na Mheshimiwa Kasmir Mabina, Mratibu wa CHADEMA Kanda ya Pwani, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Tunawakaribisha sana muone shughuli za Bunge zinavyoendeshwa. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa CPA Tawi la Tanzania Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni anaomba tuwatangazie kuwa Waheshimiwa wote siku ya Jumapili tarehe 14 Mei saa nne asubuhi katika ukumbi wa Bunge, kutakuwa na warsha kuhusu majukumu ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola na Kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (*The Role of the Commonwealth Parliamentary Association – (CPA) In Fostering Partnership Towards Achieving Sustainable Development Goals*) Kwa hiyo, mnakaribishwa kwenye semina hii muhimu nadhani kwa utaratibu ule ambao mnaufahamu maana ni Jumapili.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anatumangazia kwamba kesho saa 10.00 jioni kwenye Uwanja wa Jamhuri hapa Mjini Dodoma kutakuwa na mechi ya kirafiki ya mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club* na timu ya *Iringa Veterans* wageni ambao ni wa Mheshimiwa Mwamoto. Wote mnakaribishwa kwenye mechi hiyo ya kirafiki.

Kuna tangazo lingine muhimu linawahusu Wabunge wote wanaotokana na Chama cha Mapinduzi kwamba leo baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana mnaombwa mfike kwenye ukumbi wa Msekwa bila kukosa. Hayo ndiyo matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, naambiwa kuna mgeni mwingine ambaye yuko kwenye Jukwaa la Spika, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji Profesa Kitila Mkumbo, karibu sana Profesa, tunakutakia kila la kheri katika utumishi wa umma kwa Wizara hiyo muhimu. (*Makofi*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda nitachukua miongozo mitatu tu.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Aah, na nyuma huku.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu tuwe na utulivu.

**MBUNGE FULANI:** Kuna dharura.

**MWENYEKITI:** Dharura ipeleke kule inapopaswa kuwa.

Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Rhoda, wa mwisho Maji Marefu. Tunaanza na Profesa Maji Marefu.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nasimama kwa Kanuni ya 68(7) naomba nisiitaje kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo sasa Tanzania kumekuwa na matatizo makubwa sana hasa ya mafuriko hasa kwenye Mkoa wangu wa Tanga. Kila tunapojitahidi kumekuwa na tatizo la kwamba Kamati ya Maafa mpaka ikae. Leo hii ninapokuambia kuna watu zaidi ya 1,000 hawana chakula, hawana mahali pa kuishi hawana msaada wa aina yoyote, lakini cha zaidi ni kwamba tulikuwa tunaiomba Serikali itawasaidiaje hawa ili ikingoja hizo Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya zikae wakati kuna watu sasa hivi wanaathirika na wanaweza kufa wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nasimama kwa Kanuni ya 47(1) na naomba niisome; "Baada ya muda wa maswali kuisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kwa Shughuli za Bunge kama zinavyooneshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi katika Mkoa wa

Tanga kuna mafuriko makubwa sana, jana pia yametokea maporomoko katika milima ya Usambara eneo la Lushoto. Tunavyozungumza hivi sasa, jana barabara ya Arusha - Mombo ilifungwa, pia barabara ya Pangani - Tanga ilifungwa. Barabara ya Mombo - Lushoto pia ilifungwa na barabara ya Kilindi kwenda Morogoro imefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaona kwamba Mkoa wa Tanga umegeuka kuwa kisiwa lakini kuna athari kubwa katika Halmashauri ya Korogwe Vijijini katika eneo la Mkumbala ambapo kaya zaidi ya 600, wakazi 1,000 kama alivyosema Mheshimiwa Stephen Ngonyani wako katika wakati mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii naomba sasa Serikali ilione hili jambo kwamba ni jambo kubwa la kimkakati kwa sababu hata Wakala wa Barabara Mkoa wa Tanga (*TANROADS*) amezidiwa. Barabara hizi zote ninazozungumza zinaunganisha Mkoa wa Tanga na Mikoa mingine. Naomba nitoe hoja kwa Bunge lako, japo kwa dakika chache tujadili jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hakuna cha kutoa hoja. Mnajua Kanuni zilivyokaa. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1) na mimi pia naomba nisiisome kwa ajili ya kuokoa muda. Kwa takribani siku mbili tumekuwa tukijadili bajeti ya Wizara ya Maji, ukisoma michango ya Wabunge ni dhahiri kwamba Wabunge wanapendekeza kwamba bajeti ya Wizara hii iongezeke. Siyo tu wamependekeza iongezeke, wametoa na mwongozo iongezeke kwa kiasi gani na zitoke wapi fedha za kuongeza bajeti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama Kitabu cha Maendeleo - Kitabu cha Nne, utaona kwamba sehemu

kubwa ya kupungua wa bajeti ya Wizara ya Maji ni kwenye eneo la *Rural Water Supply and Sanitation*, utaona kwamba kwa ujumla bajeti ya ndani fedha za ndani (*local*) za miradi kwenye bajeti ya maji zimepungua shilingi bilioni 282, katika hizo shilingi bilioni 282; na katika hizo shilingi bilioni 152 ni za kwenye maji vijijini peke yake, shilingi bilioni 88 ni kwa miradi ya maji ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wametoa mapendekezo ya ile nyongeza ya shilingi 50 ambayo itaweza kuziba hili *gap* la fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya maji na kwa kuwa tayari kuna *consensus* hiyo miongoni mwa Wabunge wote wa pande zote bila kujali vyama vya siasa. Taratibu za Bunge zinataka hata kama tunakubaliana tukipitisha bajeti hii jioni itakuwa haina maana yoyote, kwa sababu ni lazima hatua ya kuleta *addendum* kwa ajili ya fedha hizo iweze kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Mapato hatuna kwa hiyo kwenye Kitabu cha Mapato Waziri wa Fedha atakapokuja ataonesha hizo fedha lakini Kitabu cha Matumizi ndiyo tunakipitisha leo. Kwa uzoefu wako, huoni kwamba inabidi kwanza kabla ya kuendelea na mjadala wa Wizara hii, tuweze kupata *addendum* ya Kitabu cha Nne inayo-*allocate* hizo fedha zitakazokuwa zimepatikana kutokana na shilingi 50 ili jioni tutakapokuwa tunapitisha bajeti hii, tupitisha bajeti ambayo tayari zile shilingi 50 zimeongezwa na kwenye *revenue book* itaongezwa. Kwa hiyo, kwenye *Finance Bill* tutakuwa tayari tumeshaifanyia maamuzi katika kikao hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako katika eneo hilo kwa kuzingatia Kanuni ya 69(1) ili jioni tuweze kufanya maamuzi ambayo tayari ni *meaningful* na Bunge liweze kufanya kazi yake inavyostahili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa kutumia Kanuni ya 47 na masharti yake yote

kwenye Kanuni ya 48. Bunge linaisimamia Serikali na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63. Nchi yetu zaidi ya wiki moja, mbili zilizopita na hasa sasa hali ya Taifa, Taifa liko kwenye maafa. Ukiangalia Visiwa vya Pemba zaidi ya kaya 600 zimezama, Unguja kaya 200, *school* zote za Unguja na Pemba zimefungwa. Wananchi zaidi ya 4,000 hawana mahali pa kuishi, Mikoa ya Tanga hali ni tete, Dar es Salaam hali ni tete, Pwani hali ni tete na maeneo mengine mengi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo ni pamoja na Mikoa ya Morogoro na Kilimanjaro.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge omba Mwongozo.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninaomba, utu wa mwanadamu uzingatiwe na kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa Tanzania, tutenge muda angalau wa dakika 15 au 20 tujadili hali hii ambayo ni ya maafa na namna gani tunaweza tukatoa majibu sahihi kwa wapiga kura wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kwa mujibuwa Kanuni nilizozitaja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja ya kuahirisha Bunge nasimama kwa Kanuni ya 47(1)...

**MWENYEKITI:** Kuahirisha Bunge? Mheshimiwa Mbunge umesemaje, kuahirisha Bunge!

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge na nasimama kwa Kanuni ya 47(1).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umesemaje? Kuahirisha Bunge?

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge, nasimama kwa Kanuni ya 47(1). Kuna jambo la dharura ambalo linatokea hivi sasa katika Mkoa wa Katavi hususan katika Hospitali ya Wilaya ya Mpanda. Katika zoezi ambalo linaendelea la uhakiki wa vyeti *fake*, jana wagonjwa zaidi ya 20 wamekaa kwenye mabENCHI wakisubiri Daktari mpaka saa mbili usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba maelezo ya Serikali nini hatua ya dharura ili kuhakikisha sasa nafasi hizi zinazibwa kwa sababu wagonjwa wanakufa wakiwa katika mabENCHI. Sasa naomba kutoa hoja na Wabunge waniunge mkono katika hoja hii ili tujadili.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Ph.D hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo hiyo na Waheshimiwa Wabunge hao watano. Nianze na mwongozo wa Mheshimiwa Stephen Ngonyani maarufu kwa jina la Profesa Maji Marefu. Narudia msimamo wa Kanuni na msimamo ambao tumeusema mara nyingi hapa. Kanuni ya 68(7) ni kwa jambo ambalo limetokea mapema humu Bungeni na unataka niseme kama linaruhusiwa au la. Kwa hiyo, hakuna mwongozo nilioombwa ulioletwa sahihi na Mheshimiwa Profesa Maji Marefu kupitia Kanuni hiyo.

Mheshimiwa Rhoda Kunchela, mwongozo wangu ni kama huo uniliotoa kwa Mheshimiwa Profesa Maji Marefu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Lazima liwe tukio, jambo ambalo limetokea mapema hapa Bungeni na siyo huko nje.

Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Shangazi wote hao wameangukia kwenye Kanuni ya 47(1) ambayo Kanuni ya 47 kama wote mnavyojua lazima isomwe na Kanuni ya 48. Kanuni ya 47(4) inampa Spika mamlaka ya kuweza aridhike, apime kama ombi hilo anaona ni jambo ambalo kweli linahitaji kusitisha shughuli zilizo mbele yetu ili tujadili hoja hiyo ya dharura. Akisharidhika, ndiyo aliyetoa hoja

anasimama tena sasa aeleze kwa kifupi halafu iungwe mkono ndiyo mnaanza kuijadili kwa muda ambao Spika atakuwa amepanga.

Kwa hali ninavyoiona mimi, suala hili halihitaji sisi tulijadili hapa kwa sasa. Ni tukio ambalo ni kweli limegusa nchi yetu maeneo mengi nasi tunawapa pole sana wananchi wetu ambao wameguswa kwa njia moja au nyingine na matukio ya mvua hizi ambazo zimekuja na nguvu sana na kwa kasi *torrential rains*, mliyokuwa mnafuatilia *satellite* ya wakubwa haya walitabiri katika maeneo mengi itakuwa hali hii. Naamini kwa hilo upande wa Serikali kwa sababu Serikali tunayo humu Bungeni, yawezekana kama siyo sasa, baadaye wakalitolea maelezo ya kutosheleza wakiangalia nchi nzima, maana Serikali ina mikono mirefu, ina macho mapema kwa kuiangalia nchi yetu, sisi Wabunge tuko hapa tunapata taarifa kutoka kwa wananchi wetu Majimboni sawa, lakini Serikali ina uwakilishi katika kila eneo la nchi yetu. Kwa hiyo, naamini kwa hili watalisemea vizuri zaidi kuliko kutumia muda wa Bunge kujadili kitu ambacho kila mmoja atakuwa anaangalia kwa upande wake.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo Mwongozo wangu. Hatutafika katika kuruhusu mjadala ufanyike sasa hivi.

Mheshimiwa Zitto anasema tutumie Kanuni ya 69(1) tuahirishe shughuli hizi. Mwongozo wangu kwa hili, Waheshimiwa Wabunge ni kweli katika mjadala unaoendelea tangu juzi, Waheshimiwa Wabunge wengi kama siyo wote waliopata nafasi ya kuchangia kila mmoja kwa *style* yake wametoa ushauri na mapendekezo kwa Serikali, lakini kwa *approach* inayopendekezwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe sitakubali tufike huko. Kwa nini nasema hivyo?

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu za Bunge kupitia Kanuni ya 105 mnaona utaratibu uliowekwa ambao ni mzuri sana, kwamba baada ya mijadala yote kwa Mafungu yote kuisha, Kamati ya Bajeti na Serikali tuna siku



Saba za kushauriana tena kwa kina, siyo kwa hoja hii tu, kuna hoja nyingine ambazo tumeanza nazo ambazo zitafika huko kwenye Kamati ya Bajeti na Serikali ndiyo watakaa waone. Kupitisha Fungu hapa leo au jana, juzi tulivyofanya haina maana kwamba Fungu hilo haliwezi tena kufunguliwa. Kitakachofanyika, baada ya Kamati ya Bajeti na Serikali kukubaliana katika maeneo yapi ambayo wanadhani tunaweza tukaongeza fedha, Serikali itakuja na *addendum* siku ambayo *Appropriation Bill* inapoletwa ingawa huwa hatuijadili, *Appropriation Bill* huwa haijadiliwi inapitishwa katika hatua zake zote lakini itakuwa na *addendum* kuonesha sasa mafungu hayo ambayo yameongezewa fedha.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu kwa Mheshimiwa Zitto ni kwamba tusiende kupitia Kanuni ya 69(1) tuende kwa *route* ya Kanuni ya 105 ili tuipe Serikali na Kamati ya Bajeti kufanya kazi hiyo kwa kutendea haki siyo Wizara hii ya Sekta ya Maji lakini na Sekta zingine ambazo mmezisemea kwa nguvu. Huo ndiyo Mwongozo wangu kwa suala hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo tunaendelea. Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Hoja ya kuahirisha majadala.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yetu yanaendelea. Jana Mheshimiwa Naibu Spika alisoma orodha ya wachangiaji, nadhani tutaanza nao kwa uwiano wetu ule. Nitaanza na Mheshimiwa Aisharose Ndogholi

Matembe atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian John na Mheshimiwa Subira Mgalu ajiandae. Hawa ni dakika tano, tulikubaliana hivyo na hii nataka kuipeleka na Upinzani kuwa dakika tano tano ili wachangie wengi aaalah! Haya dakika ni tano mkono wangu wa kulia na mkono wa kudshoto pia. *(Kicheko)*

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa maisha ya wananchi wangu wa Mkoa wa Singida na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenijaalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Naipongeza sana Serikali ya CCM na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya ya kuwaletea Watanzania maendeleo ya haraka na yenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi Serikali ya Awamu ya Tano imeweza kufanya mambo mengi na makubwa. Mfano, ujenzi wa reli ya kisasa, uboreshaji wa miundombinu ya barabara na madaraja, utoaji wa huduma bora za afya na elimu na kujenga nidhamu katika rasilimali za Taifa letu. Hii yote inaonesha jinsi gani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alivyo makini na timu yake. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kwamba maji ni uhai katika maisha ya mwanadamu. Maeneo ambayo hayana maji hakuna maendeleo, shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinategemea uwepo wa maji, hivyo basi ningeshauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutunisha Mfuko wa Maji kwa kuongeza tozo ya maji ya lita ya *petrol* na *diesel*/kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100 ili kutunisha Mfuko huo kwani mfuko huo wa maji umekuwa ni mkombozi mkubwa kwa maendeleo ya miradi mingi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanufaika wengi wa Mfuko huu wa Maji ni wale wanaoishi mijini. Hata ukitazama katika kitabu cha bajeti ya maji ukurasa 192 hadi 193 unaweza ukaona kwamba miradi mingi iliyonufaika ni ile iliyoko mijini hivyo ningeliomba Serikali kuangalia uwezekano wa kupeleka angalau asilimia 70 ya makusanyo ya tozo hii iende maeneo ya Vijijini ambako ndiyo kwenye matatizo makubwa ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na kufanikisha malengo ya uchumi wa viwanda ni vema sasa Serikali ikaangalia uwezekano wa maeneo mengi kupata maji kwa urahisi. Vilevile kuunda chombo cha usimamizi wa miradi ya maji vijijini kama ilivyo REA ili kupambana na changamoto za maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Mkoa wa Singida ambao ni wachapakazi na wabunifu, kama maji yanapatikana wakati wote wanaweza kutumia fursa hii kwa kulima mazao ya chakula na biashara kwa mwaka mzima na kuongeza pato la Taifa. Lakini kwa Mkoa wa Singida mambo yamekuwa ndivyo sivo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na adha kubwa wanayopata wananchi wa Mkoa wa Singida kutokana na ukosefu wa maji safi na salama, na changamoto nyingi zilizopo katika Mkoa wa Singida bodo bajeti ya mwaka huu ya miradi ya maendeleo ya maji imepunguzwa kutoka shilingi bilioni 6.7 kwa mwaka huu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Emmanuel Papian.

**MHE. EMMANUEL J. PAPIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza napongeza kazi inayofanywa na Wizara na watalaam wake na pili nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya na jitihada nyingi zote za kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ambayo imetengwa hii ya shilingi bilioni 600 ambayo tunalalamika kwamba iende shilingi bilioni 900, mimi ninaona kwamba Wizara imepanga bajeti ambayo ndiyo halisi, kwa sababu hata hii shilingi bilioni 600 yenyewe tukisema leo tuiombe yawezekana hizo fedha zisifike. Fedha ambazo zimetoka ni chini, asilimia 19, ina maana kwamba hata hii tukiomba yenyewe yawezekana isiwe halisi. Sasa mimi niombe na kushauri kwamba Bunge lako hili likubali tutengeneze ile shilingi 50 iongezeke kwenye mafuta ambayo ndiyo pesa halisi ambayo yawezekana ikawa ni halisi ya kwenda kupeleka kwenye miradi yetu ya maji, angalau ikaongeza Mfuko wa Maji kupata pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa wizara wanafanya kazi kwa nguvu kubwa, lakini huku chini kwenye halmashauri zetu watendaji wa Idara za Maji hawafanyi kazi ipasavyo. Idara ya Umwagiliaji Wizarani kuna tatizo la watu kukaimu, watu wengine wamestaafu. Hili suala la umwagiliaji nchini naomba litizamwe kwa kiwango kikubwa, suala la kukaimu linasababisha watu kushindwa kufanya kazi na kufanya maamuzi kwenye maeneo yao. Wale waliostaafu, kama hakuna watu wengine ambao wamewarithi ambao mmekuwa *trained* na kujua namna ya umwagiliaji nchini basi wale wapewe *contract* kwa muda wafanye *training* ya hao wengine ili waweze kusukuma kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa linalofanya nchi yetu ipoteze fedha nyingi ni tathmini ya miradi ya maji kuwa gharama kubwa sana. Mradi mdogo wa shilingi milioni 20 mtu ana *tender* shilingi milioni 200, hizi fedha zinavyotoka inalazimisha mradi kuwa nusu nusu na haifiki mwisho na mwisho wa siku miradi mingi ya maji nchini inakuwa viporo na haifiki mahali inapotakiwa.

Kwa hiyo tunaomba tulitazame hili, lakini kwenye *tendering documents* Wizara iangalie, Serikali iangalie ni namna gani tunaweza kwenda kwenye uhalisia unaoweza kufanya miradi hii iweze kukamilika na fedha za Serikali zisiweze kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafadhili, miradi mingi ambayo inakuwa *supported* na wafadhili mimi nadhani hawa wafadhili na wenyewe kuna jinsi wanatupiga chenga. Leo wameleta fedha, kesho wameahidi, keshokutwa wame-*cancel*, miradi haiwezi kuendelea, hii ni danganya toto. Nchi ijitizame upya ni namna gani tunaweza kutokana na haya masuala ya wafadhili, asubuhi amekushika tai, jioni amekuachia tunakuja Bungeni tunaahidi vitu ambavyo haviwezekani. Tujitizame upya tupunguze hili suala la utegemezi wa wafadhili ambao wanatufikisha mahali ambapo sipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kiteto wamenimba niombe Wizara ya Maji, maeneo ya Ndidu, Makame, Loolera tupewe bwawa moja angalau kwenye hii tarafa ili basi wale wafugaji wapate maji. Kanda hii ya maeneo ya hizi kata tatu hawahitaji maji safi na salama, wanahitaji ilimradi ni maji, ukinywa usiharisha, usife, ng'ombe wasife, yawe meupe, yawe meusi, yawe *blue* wao wanahitaji kitu kinachoweza kuitwa maji na Serikali ikawaambia haya ndiyo maji, kwa sababu wamelia miaka mingi hakuna mabwawa, mifugo inakufa, wananchi hawawezi kupata maji ya kutumia. Maji haya yote sisi tunayatumia kwa maana ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza na naomba Wizara yako kwamba tupate bwawa moja la maji kwenye tarafa moja kwa mwaka huu, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunaomba, kuna mabwawa ambayo wananchi wanachimba wenyewe; ukichukua fedha Wizarani, ukaangalia namna gani ya ku-*rescue situation* kwa haraka, uka-*fund* wale watu wanaochimba yale mabwawa kwa mikono yao tunaweza

kuwa na mabwawa madogo madogo kwenye maeneo ambayo wakati Serikali haijapanga ile miradi mikubwa basi wananchi wana mabwawa madogo madogo ambayo wanaweza kuwasaidia maji kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nishukuru kwa Bwawa la Dongo ambalo limeingizwa kwenye mpango, lakini niombe Serikali...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. EMMANUEL J. PAPIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimwita Mheshimiwa Subira, lakini tumeelewana, atafuata baada ya Mheshimiwa Mohamed Aziz Abood.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya ya kutekeleza ahadi za maji katika Jimbo letu la Morogoro Mjini. Tunamshukuru alituahidi atatupa mradi wa maji na kweli sasa tumepata mradi wa maji, naishukuru sana Serikali, ila ninachoomba kwa Mheshimiwa Waziri tuharakishe huu mradi wa maji ambao tulimepewa na Wafaransa ili kuondoa kero hii ya maji, na hasa wakazi wa Morogoro wanazidi kuongezeka wakiwemo Wabunge wengine humu wakihamia Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna eneo la uwekezaji ambalo linahitaji maji mengi kwa ajili ya kuwekeza kwenye viwanda na wawekezaji wengi wakija kitu cha kwanza wanachouliza ni maji. Kwa hiyo, tunaomba Wizara iharakishe kazi hii ya mradi huu wa maji ili tuweze kupata maji kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro bado kuna tatizo la maji. Huu mradi ni mradi wa muda mrefu lakini sasa hivi bado tuna tatizo la maji. Bwawa la Mindu limejaa lakini miundombinu inayokwenda na kusambaza katika maneo mbalimbali ya Morogoro bado ni tatizo. Kwa hiyo, naomba Wizara ilianganalie hilo ili kuongezea bajeti upande wa Morogoro kwa ajili ya kuweza kutengeneza miundombinu mipya ambapo maeneo mengi kuna miundombinu chakavu; na hasa maeneo ya Kihonda, Tungi, Lukobe, Mkundi na Kiyegeya. Cha kushangaza zaidi wananchi wa Mindu ambao wanalilinda lile bwawa la maji kwao hakuna maji wala miundombinu ya maji, kwa hiyo, naomba Wizara walianganalie hilo ili tuweze kuondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya *World Bank* ambayo wananchi wamechangia. Sasa kuna tatizo ambalo Mheshimiwa Waziri naomba hili mlifanyie kazi, kuna kata mbili kata ya Bigwa na Kingolowila, kuna mitaa minne ambayo wananchi wamechangia mradi huo lakini mradi huo unataka kuchukuliwa na kupewa *MORUWASA*. Ila wananchi sasa wanadai wanasema miradi wameshachangia wao wanahitaji wao wenyewe waendeshe hiyo miradi ya maji kwa kutumia vikundi vyao vya ushirika. Tatizo linalokuja ni kusema kuwa sheria hairuhusu. Mimi nadhani wakati wananchi walipokuwa wakichangia ilitakiwa waambiwe kwamba mradi huu hamtoweza kuendesha wenyewe. Sasa hivi kuna mgogoro mkubwa sana katika maeneo haya. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, elimu ya kutosha inatakiwa kwa wananchi ili kuepukana na tatizo hili la kudai kuendesha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wamepewa *MORUWASA* na bei wanayowapangia sasa hivi ni kubwa, kwa hiyo, hawakubaliani nao na mradi umesimama na wananchi bado wanaendelea kukosa maji. Tunaomba hili tatizo lifanyiwe kazi ili tuweze kulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine kubwa bado linaendelea na hasa tunategemea kupata mradi mkubwa wa maji, Mjini Morogoro. Tatizo ni bili za maji

wananchi wanalipa maji ambayo kwa mwezi mzima au miwili hajapata lakini anapata bili ametumia maji, ni kutokana na mita zenyewe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Subira Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Midimu na Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji. Kwa kuwa dakika ni tano nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa kazi nzuri. Pia mchango wangu niuelekeze moja kwa moja kwenye Mradi wa Maji wa Wami – Chalinze Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na namshukuru sana, na maelekezo yake na namna ya maelezo ya Serikali kwenye hotuba hii, na namna ambavyo mkandarasi yule amepewa siku 100 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi wa awamu ya tatu; nilikuwa nadhani kwa kuwa changamoto za upatikanaji wa maji Jimbo la Chalinze zimekuwa kubwa, na kwa kuwa mkandarasi huyu anaonekana hata miradi mingine *performance* yake si nzuri, je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna haja ya kumbadilisha mkandarasi huyu? Kwa sababu siku alizompa zinakamilika tarehe 31/05 na leo tuko tarehe 11?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa swali la nyongeza nililoliuliza juzi Mheshimiwa Naibu Waziri alinjibu amefikia asilimia 45. Hata hivyo mradi huu unakabiliwa na changamoto nyingi, maji yanayotoka sasa hivi ni machafu,



wananchi wanapata taabu, maji hakuna na hata bili wanazopewa wengi wamekatiwa lakini wanaendelea kulipia *service charge*. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri, na kwa kuwa Jimbo letu la Chalinze na Wilaya ya Bagamoyo kuna wawekezaji wengi wamejitokeza hususan, naomba nimsemee hapa mwekezaji wetu anayejenga kiwanda cha usindikaji matunda pale Msoga, Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa rasilimali inayohitajika ni maji na kwa kuwa maji sasa hakuna na kiwanda karibu kinafunguliwa, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kukubaliana na makubaliano ambayo yameingiwa mradi wa *CHALIWASA* pamoja na mwekezaji wetu huyu, kwamba yupo tayari kununua baadhi ya vifaa kwa ajili ya kuboresha mradi ule ili maji yapatikane ambayo mimi nadhani yanaweza yakasaidia kiwanda, yakatusaidiwa na wananchi wa Chalinze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mradi wa Chalinze autazame kwa macho ya huruma, hali si shwari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwa kupitia bajeti hii kwenye hotuba yake nimeona kwenye ukurasa wa 90 mpaka 92 namna gani ambavyo Serikali imeonesha kabisa chanzo hiki cha shilingi 50 kwa lita moja ya *diesel* au *petrol* haitoshi. Kwa hiyo, nadhani kwa kukiri kwao kwenye hotuba hii sasa ni nafasi ya Bunge letu na Kamati yetu ya Bajeti kuweza kuongeza hicho kiwango ambacho Serikali yenyewe imekiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye ukurasa wa 120 Serikali imeonesha kwamba mahitaji ya ujenzi wa miradi mipya ya maji ni makubwa na wameomba wawekezaji wengine au wadau mbalimbali kujitokeza ku-*support* jitihada hizo na ndiyo maana hapa ninamwomba Mheshimiwa Waziri, nilishamweleza, hivi aone ombi la mwekezaji wetu kuomba kugharamia sehemu za ukarabati wa uchakavu wa miundombinu ya mradi wa maji Chalinze

ili waweze kukatana kwenye bili. Kwa nini suala hili linachelewa hivyo? Uwekezaji ule ni zaidi ya bilioni mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Wilaya ya Kisarawe nayo ina changamoto kubwa ya maji, Wilaya ya Rufiji nayo ina changamoto kubwa ya maji. Hivi karibuni kuna binti yetu amepoteza maisha kwa kuchota maji katika Mto Rufiji. Kwa nini sasa Mto Rufiji usitumike kuwa chanzo cha maji katika Wilaya ya Mkuranga, Kibiti na Rufiji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utaona miradi mingi, mfano mradi kupitia DAWASA, upanuzi wa bomba la maji Ruvu Chini na Ruvu Juu yote imepita katika Mkoa wa Pwani lakini kwa bahati mbaya sana hatuna Mamlaka ya Maji ya Mkoa, tunatumia mamlaka ya maji DAWASCO ambayo tunadhani inazidiwa na utoaji huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri atueleze, ni kwa nini Mkoa wa Pwani tunakosa kigezo cha kuanzisha Mamlaka ya Maji, wakati ukizingatia vyanzo vingi vya maji vinavyopeleka maji katika maeneo mengine viko katika Mkoa wa Pwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika kuongezea mchango wangu, kwa nini kata za Mzenga, Mafizi hazina maji wakati ni kilometa 28 kutoka bomba kuu la maji linalopeleka maji Dar es Salaam? Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba bajeti imepungua kwa kiwango hiki nadhani pia atakapokuja kufanya majumuisho atueleze pengine kuna sababu ya msingi. Pengine katika hiyo bilioni 600 tutaongeza maji kwa kiwango cha asilimia ngapi, na Watanzania wangapi wataongezeka katika kupata huduma ya maji kwa bajeti hii iliyopitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Bagamoyo Mjini kuna miundombinu ya DAWASA imejengwa pale lakini hawapi maji. Kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri... *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashoria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga, na Mheshimiwa Njalu Silanga ajiandae.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya. Kwa muda mfupi amefanya kazi na zimeonekana, Mwenyezi Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza ahadi ya kuleta maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Mkoa wa Simiyu na Wilaya zake tano za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu, na hela tayari zimeshakuja, wananchi wana imani na Rais wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu sikivu maji yakifika Mkoa wa Simiyu iweze kusambazwa kwenye shule za msingi na sekondari pamoja na vituo vya afya na zahanati. Nasema hivyo kwa sababu wanafunzi wanahangaika sana, muda mwingi wanachota maji usiku, asubuhi wakienda darasani wanashindwa kusoma wanasinzia tu, ni bora Serikali itoe kipaumbele katika mashule yetu yapate maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Simiyu ni wachapakazi wazuri na ni wakulima wazuri, nina imani maji yakifika watalima kilimo cha umwagiliaji, njaa itakuwa ni ndoto katika Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali yangu kwa ajili ya kutuletea shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ukarabati wa mabwawa Wilaya ya Itilima na mabwawa yale ni Mwamapalala, Nobora, Sunzula, Sawida, Chinamiri na Lugulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu sikivu sasa iweze kusambaza maji kwenye kata ili kutimiza azma

ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mwanamke ndoo kichwani. Iweze kusambaza kwenye kata zifuatazo, kata za Nkuyu, Migato, Mwaswale, Mwamtani, Nkoma, Kindilo na Sawida. Maeneo haya niliyoyataja wanawake wanahangaika sana, muda mwingi wanaupoteza kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ukizingatia wanaochota maji ni wanawake si wanaume. Mwanamke anachota maji usiku, saa zingine anakutwa na matatizo huko njiani. Naiomba Serikali iweze kuzingatia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Deo Sanga, na badala ya Mheshimiwa Njalu, Mheshimiwa Ndaki Mashimba ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza naunga mkono ushauri wa Kamati ya Kilimo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, pamoja na Mawaziri, Waziri wa Maji, Naibu Waziri pamoja na wataalam wa Wizara hii ya Maji pamoja na Mawaziri wote wa Wizara zote kwa kazi nzuri wanazozifanya za kutekeleza Ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kama mchumi. Imezungumziwa hapa kwamba fedha zilizotengwa kutoka mwaka jana, shilingi bilioni 900 ya 2016/2017 na sasa zimetengwa fedha pungufu utofauti na nani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naipongeza sana Wizara kupitia wataalam, wametenga kitu ambacho ndio uhalisia ambao fedha zitakwenda kwenye miradi. Kwa sababu fedha zilizotengwa mwaka jana hatukuzifikia na

ndiyo maana wameonesha hapa tumefikia asilimia 19. Kwa hiyo, nawapongeza sana wataalam wa Wizara hii kwa maana wametenga sasa fedha ambazo zinakwenda kutekeleza uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu ambao wamesema iongezwe tozo ya shilingi 50. Naungana nao kabisa kwamba angalau itaongeza fedha katika huu Mfuko wa Maji. Kamati ya Bajeti watakwenda kukaa kuona namna ambavyo hii tozo yashilingi 50; nadhani tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo mazuri Mheshimiwa Waziri atakaposimama, katika miradi ile iliyopata fedha kutoka Serikali ya India ambapo kuna miradi 17 katika Tanzania Bara na Zanzibar ikiwemo na Makambako; watueleze kwa sababu tayari hapa baadhi ya Wabunge tumekuwa na wasiwasi kwamba fedha hizi ambazo zimekuwa zikitoka nje tumekuwa hatuzipati. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama atueleze kwa kina uhakika wa kupata fedha hizi ili wananchi wangu wa Makambako wajue fedha hizi zitakwenda kutekeleza mradi ambao Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba shughuli ya maji Makambako itatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna Mradi wa Bwawani wa Bwawa la Makambako ambao ni tofauti na mradi huu mkubwa. Mradi huu ulishatangazwa na Mamlaka ya Maji Iringa (*IRUWASA*) wanaosimamia. Na ilivyotangazwa suala hili liko Wizarani. Nataka nipate majibu nini sasa kinaendelea ili wananchi wa Makambako wajue mradi huu sasa umefikia hatua gani kwa sababu umetangazwa na una muda mrefu tangu watangaze, zaidi ya miezi miwili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, niwaombe Wizara, fedha kwa mfano zilizotengwa mwaka jana mpaka sasa mtusaidie wenzetu ma-*engineer* walioko huko, wataalam wa maji, mpaka sasa kuna baadhi ya miradi haijatangazwa. Sijajua kuna kigugumizi gani? Mtusaidie Wizara wanaohusiana na mambo ya Mkoa kule na kadhalika

ambapo fedha hizi zilizotengwa katika eneo langu zingeweza kusaidia kupata maji katika vijiji vifuatavyo; vijiji vya Mbugani, Mawande, Mtulingala, Mahongole, Usetule na Ibatu wangepata maji. Lakini vilevile Mheshimiwa Waziri nisaidie kuna mradi mkubwa ule wa Tove ambao unahudumia vijiji kadhaa, vimeishia pale Ilunda. Ilunda pale kuja kwenye kijiji cha Ikelu ni kilometa mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi unasimamiwa na nani? Nani ambaye anazuwia wananchi pale Ikelu wasipate maji? Naomba utakaposimama hapa Waziri uniambie kwa sababu maji pale yako mengi na kadhalika, hawapati maji pale...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, naona jirani yangu wa Jimbo la Itilima yupo, Mheshimiwa Njalu Silanga atafutiwa na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya. Niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, ni wazee lakini ni vijana kwa sababu wametembelea karibu miradi yote ya nchi yetu ya Tanzania. Niwapongeze watumishi wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Niwapongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Simiyu tumeweza kufanikiwa Mradi wa Ziwa Victoria utakaogharimu Euro milioni 300. Mradi huo utavinufaisha vijiji 253, lakini katika Jimbo langu la Itilima vijiji 64 vitanufaika na mradi huo.

Niiombe Serikali, hususan suala la wakandarasi ambao wanatekeleza miradi katika maeneo yetu iweze kuweka kipaumbele pale *certificate* Halmashauri zinazopeleka kwenye Wizara, waweze kulipa haraka ili shughuli hizi ziweze kufanyika kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua fedha ni kidogo, lakini fedha hii iliyotengwa inaweza ikafanya kazi, hususan pale ambapo itakapotoka. Pia niiombe Serikali iweze kupokea ushauri na mapendekezo tuliyoyatoa, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji kwa kutambua kwamba, fedha hizo zitakazotokana na maji na ndizo hizo sasa zinazoweza kufikisha asilimia 19.8 ya miradi inayoendelea hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niiombe Wizara, pale kwenye suala la upangaji wa bei katika miji ambayo wanakuwa wamekamilisha miradi, katika sheria yetu inachukua siku 45, tumefanya ziara tumekutana na malalamiko mengi kwa wananchi kwamba inachukua muda mrefu na kusababisha kufanya vurugu katika baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, niiombe Serikali pale ambapo wanakuwa wamekamilisha waweze kufanya utaratibu wa haraka zaidi hususan kwenye eneo la *EWURA*, kutoa bei elekezi ili wananchi katika maeneo hayo waweze kupata maji yenye bei salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendana na udhibiti wa mapato katika nchi yetu niiombe Serikali iweze kufanya utaratibu wa kufanya kama mfumo wa vocha hasa kwenye miji mikubwa ambayo inaendelea kukua ili tuondokane na suala la maji kuwakatia wananchi. Pale ambapo mwananchi atakapokuwa na bili zake na kadi yake atakuwa anajiongoza kulingana na mapato yake na utumiaji wa maji katika maeneo yake. Tukifanya hivyo tutakuwa tumepunguza lawama na tutakuwa tumeipunguzia Wizara majukumu ya kupambana na suala la ukataji wamaji bila sababu. Maji yake yale atakayokuwa ameyalipia ndiyo yatakayofanyakazi katika nyumba yake na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuipongeza Wizara, katika Wilaya yangu ya Itilima nilikuwa na mabwawa 17, lakini mabwawa 6 tayari nimeshapata fedha na shughuli zinaendelea kupitia Mkandarasi DDCA. Niiombe tu Serikali iendeleo kujenga uwezo katika Kampuni ya Serikali DDCA ambayo inafanya kazi nzuri na inawaridhisha Watanzania hususan watu wa Itilima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo niendeleo kuiomba Serikali katika mji wetu wa Bariadi, kwa maana ya kwako Mheshimiwa Mtemi Chenge, pale Somanda kuna tenki kubwa limejengwa lenye uwezo wa kubeba lita 65,000 pamoja na Sima, mji ule unakua kwa kasi. Niiombe Serikali pia iweze kutilia mkazo eneo lile liweze kupata maji safi na salama, ili wananchi wa Mkoa wa Simiyu waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo tu kuipongeza Wizara, niwapongeze Mawaziri, kazi ni ngumu. Watanzania wote tunahitaji kung'aa, lakini tunawategemea ninyi. Pamoja na kwamba ni wazee, lakini ni vijana ambao mmeaminika katika Taifa hili muweze kufanya kazi ambayo italeti tija katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kutunza muda pia, tunakushukuru. Mheshimiwa Kapufi na Mheshimiwa Mchimwa ajiandae. Pia watani zangu hawa, Mheshimiwa Katani Ahmed Katani ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo na mimi niungane na wazungumzaji wote wanaozungumzia habari ya Wizara kuongezewa fedha. Sambamba na hilo, wenzetu wa sheria wana usemi wao wanaosema; *"Justice must not*



*only be done, but must be seen to be done*" ikiwa na tafsiri gani? Leo hii tunapozungumzia habari ya Wizara na fedha, inawezekana mwaka wa jana bajeti ile ilikuwa kubwa, safari hii tunapotamani tena kuwa na bajeti kubwa, tatizo ninaloliona mimi si ukubwa wa bajeti, ni utekelezaji kwa maana ya fedha zifike kwa walengwa, hilo ndilo tatizo ninaloliona. Kwa hiyo, kwa tafsiri hiyo, kama tuliweza kutekeleza kwa asilimia 19 vipi kama fedha ikienda hata kwa nusu ya bajeti ikiwafikia walengwa? Kila mmoja hapa atapunguza kupiga kelele, mimi ndiyo naliangalia kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye mji wangu wa Mpanda nafahamu miundombinu ya maji katika mji ule imechakaa, sehemu kubwa ni mabomba ya chuma, nilikuwa naomba Wizara iliangelie suala hilo. Leo hii tuna maeneo ya Makanyagio, Majengo, Majengo A na B, zote hizo kwa kweli hazifikwi na maji kutokana na uchakavu wa miundombinu. Nafahamu tunalo Bwawa la Milala, tuna changamoto ya uwepo wa viboko. Bwawa lile lilikuwa na uwezo mkubwa wa ku-*supply* maji, niendeleo kuomba wahusika waliangelie hilo, ili kukidhi suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu tunao Mradi wa Ikorongo, ule mradi peke yake haukidhi mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Mpanda. Tuna maeneo ya Mwamkuru, maeneo haya naendelea kuyaombea visima. Kuna wakazi wengi, lakini ukiangalia maeneo yale mpaka leo hii suala la visima ni tatizo. Eneo hilo hilo la Mwamkuru tuna skimu ya umwagiliaji ya Mwamkuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nasikitika kusema tunakwenda mwaka wa saba skimu ile haijafanya kazi. Ni tatizo, kwa hiyo nilikuwa naomba Waziri atakapokuja hapa aniambie tunafanya nini katika eneo hili, na ukiingatia watu wale kwa kupitia skimu za kwao wenyewe wamekuwa wakizalisha chakula cha kutosha. Leo hii mwarobaini ilikuwa ni skimu hii ambayo ingeweza kusaidia eneo lile likafunguka na chakula kikapatikana cha kutosha. Naomba niambiwe kwa nini tunakwenda mwaka was aba sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema yote hayo, nilikuwa naomba pia nielezee uelekeo pekee wa kusaidia mji wetu wa Mpanda kwa kweli ni kuyatoa maji kutoka Ziwa Tanganyika. Najua hii tunapozungumzia habari ya Ikorongo ni chanzo cha muda mfupi, tutapoteza muda mwingi kuzungumzia chanzo ambacho hatuna uhakika wakati chanzo cha uhakika kipo. Niombe na kwa wakati tofauti nimeshaongea na Mheshimiwa Naibu Waziri, allangalie hili lianze kuingia kwenye mpango wa kuyatoa maji Ziwa Tanganyika na kuyaleta katika maeneo hayo, hata mikoa mingine ya jirani. Kwa kweli pale kilometa ni chache. Kilometa za kutoka Karema kuja Mpanda Mjini hazidi mia au ni mia na kidogo, ni umbali mdogo huo. Nilikuwa naliomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusisitiza, eneo la umwagiliaji ni ufumbuzi wa kutosha katika nchi hii. Mimi niombe, kwa maana ya umwagiliaji, leo hii tusilalamike; niliwahi kusema hapo mwanzo kwamba nchi hii tumebahatika kuwa na vyanzo vingi. Sizungumzii habari ya Bahari ya Hindi, nchi nyingine zinahangaika ku-*treat* maji ya bahari, sisi hatujafika huko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda ndio huo. Tunaendela na Mheshimiwa Mchimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Katani.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kuunga mkono hoja zote za Kamati ya Kilimo, Mifugo pamoja na Maji kwa sababu mimi ni Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa ujumla kwa jinsi wanavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu makubwa ya Bunge ni kuishauri Serikali. Kamati yetu mwaka jana tuliishauri Serikali, tukaomba tuongeze tozo kutoka shilingi 50 kuwa shilingi100; lakini kwa bahati mbaya Serikali haikukubaliana na ushauri wa Kamati na mwaka huu Kamati yetu tena imeishauri Serikali, tuongeze tozo kutoka shilingi 50 mpaka shilingi 100. Haya yanajieleza wazi, tunaona kuna *gape* hapa, kama hii tozo ingekuwa imetozwa toka mwaka jana hili *gape* linalozungumzwa sasa hivi lisingekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali iwe inasikiliza ushauri wa waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa naomba anieleze kwa nini Serikali ina kigugumizi cha kusaini mkabata wa Tanzania na Australia ambao ulikuwa unaweza kutoa maji katika majimbo matatu ya Wilaya ya Mufindi pamoja na Wilaya ya Kilolo, kwa nini Serikali inapata kigugumizi? Hela ziko wazi, tulichotakiwa ni kusaini tu ule mkataba; kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa naomba atupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Mufindi Kaskazini lina kata 11, lakini cha kusikitisha hakuna hata kata moja yanye maji. Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni zetu moja ya vipaumbele muhimu tulisema tupate maji, lakini ukienda kwenye kata za Ikwea, Sadani, Igombavanu, lhalimba kote hakuna maji. Ifike wakati hawa Waheshimiwa wenzetu Mawaziri waje watusaidie kujibu hoja huko kwenye maeneo yetu, lini maji yatapatikana katika maeneo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mufindi miongoni mwa Wilaya kubwa hapa nchini, ina majimbo matatu, lakini cha kusikitisha tumepata bilioni 1.5 kwenye Jimbo la Mufindi Kusini, Mufindi Kaskazini pamoja na Mafinga Mjini. Kwa nini tunapata hela? Uwiano wa kugawa hii hela unapatikana vipi? Kuna baadhi ya maeneo zimekwenda shilingi bilioni 200, *why?* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike sehemu kuwe kuna uwiano ambao unaridhisha. Unakuta kuna maeneo mengine yanaonekana yako bora zaidi kuliko maeneo mengine. Waziri aje atwambie wanatumia vigezo gani kupeleka shilingi bilioni 200 kwenye maeneo mengine na kwenye eneo lingine hakuna hata senti tano? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya taasisi kama *RDO* zinafanya kazi kubwa sana za maendeleo katika maeneo yetu. Hii taasisi ya *RDO* inasaidia kuleta *support* ya maji katika kata ya Ndabulo, lakini kwa masikitiko makubwa sana Serikali hatuwaungi mkono. Inafika sehemu hata vifaa ambavyo vinasaidia kuleta maji katika maeneo yale vinachajiwa (*be charged*) *VAT*. Watu wanatoa maji bure kwa wananchi, leo tunaendelea kuwa-charge *VAT*. Badala ya kuwasaidia hawa watu tunawa-demoralise.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya *World Bank* kama miradi ya Ukami, Mapanda pamoja na Igomaa, mpaka leo mwaka wa saba miradi hii hajiatekelezwa na hela zilishalipwa. Atakapokuja Waziri hapa atueleze kwa nini miradi hii hajikamilika na Serikali inatakiwa ichukue hatua gani kusudi hii miradi ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mzee Pinda aliahidi kutoa shilingi milioni 295 kwa ajili ya kuendeleza bwawa la kilimo pale Nundwa, lakini mpaka leo hela hizi hazijatolewa. Kwa hiyo, mimi namuomba sana Mheshimiwa Waziri, baada ya bajeti hii aje atembelee kwenye maeneo yetu aone hali halisi katika maeneo yetu ili kusudi aweze kutusaidia watu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini na Wilaya ya Mufindi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgimwa, tunaendelea na Mheshimiwa Katani huyu ni dakika kumi atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Ruge na Mheshimiwa Lathifah Chande kwa dakika tano, tano.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja ya baadhi ya wachangiaji waliotaka tuongeze tozo kwenye mafuta kwenye jambo hili la maji. Hata hivyo nisikitike sana wakati nasoma hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, nimeona alichokifanya mwaka huu ni ku-*copy* na ku-*paste* tu kwenye Mradi wa Maji wa Makonde. Kile kilichoandikwa mwaka jana ndicho alichokiandika leo, na pesa zenyewe zinazozungumzwa ni pesa za kutoka kwenye *Basket Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tume-*fail* na jambo hili la Mradi wa Makonde na kumbuka mradi huu Mheshimiwa Waziri unahudumia Wilaya takribani nne, majimbo matano ya Newala, Tandahimba, Nanyamba, Newala Vijijini, ni mradi huu tunaongumza. Mwaka jana mmeweka bajeti hii ya *Euro* milioni 87 ambazo mlisema mnakopa kutoka India, lakini mwaka huu mlíchokiandika mwaka jana ndicho mlíchokiandika mwaka huu. Watu wetu watatuamini vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana mwaka jana tumewaeleza Serikali imetenga dola bilioni 87 ambazo hazijatekeleza chochote kile. Mwaka huu tunarudi Majimboni mwezi wa saba tunakwenda kuwapa *scenario* ile ile ya mwaka wa jana, wanataka kutuamini nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Rais alivyokuja Jimboni kwangu Tandahimba miongoni mwa ahadi alizokuwa ameahidi ni pamoja na kuona kwamba Watanzania wanaondokana kabisa na tatizo la maji. Mheshimiwa Naibu Waziri umefika Tandahimba, vizuri sana, umeona unapofika mwezi wa sita, wa saba, ndoo moja ya maji mpaka shilingi 2,000 hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amefika Tandahimba, Tandahimba hakuna tatizo la vyanzo vya maji, Mto Ruvuma ni kilometa 15 tu kutoka Wilayani lakini kuna kata ambazo ni kilometa 8 tu kutoka Mto Ruvuma maji yamejaa. Ukienda kata za Mihambwe, Mchichira, Mahuta, Kitama pamoja na Tandahimba Mjini kote kuna vyanzo vya

maji, lakini watu wake hawana maji. Ukiangalia hotuba yako hii vizuri, hii uliyoiandika, mijini mmetengenezea pesa za kwenda kule tena pesa za ndani. Mijini ambako matatizo ya maji si makubwa kama vijinini. Lakini kwenye mradi ule wa Makonde mmetenga shilingi bilioni moja. Tena fedha za nje hizo hizo kwa ajili ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule una zaidi ya miaka 30, miundombinu yake imechakaa, na Mheshimiwa Naibu Waziri unajua. Pesa zenyewe tunazotengea ni hizo hizo za nje. Sasa kuna u-*serious* kweli kwa watu wale wa Kusini, watu wale wa mradi wa Makonde kweli kupata maji? Sasa mje mtusaidie hapa, mnapopeleka maji mijini ambako *at least* asilimia 72 wana maji vijijini kule, mimi jimbo langu lina kata 31 katika majimbo makubwa kabisa, na umbali kutoka kata moja na nyingine ni umbali wa kilomita 15 kilometa 16, watu wana shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tena ikiwezekana tunapomaliza bajeti Mheshimiwa Waziri uje mwenyewe uone kutoka Mkwiti kwenda Tandahimba watu hawana maji watatembea umbali gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kata za Luagalo, Chaume pamoja na Nambahu kuna shida ya maji; kila unakotembea Tandahimba kuna shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana mnapotengeneza bajeti hizi nadhani watu wa nishati walifikiria mpango mbadala wa nishati vijijini (*REA*), na ninyi watu wa maji sasa tuwe na jambo la mbadala la maji, vijijini kwa sababu ndiyo sehemu ambako kuna waathirika wakubwa wa tatizo la maji. Badala ya kukaa hapa tunazungumza vitu vingine suala la maji liwe *priority* kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ni waombe tu walizungumza wazungumzaji hapa wakizungumza kwenye mafuta. Mimi niombe watu wanakunya bia kweli kweli; bia zinanyweka kweli kweli, tusitegemee chanzo kimoja tu cha

mafuta kwenye kule tuweke shilingi shilingi mia, mia au shilingi mia mbili kule ili itusaidie mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niendee kusikitika sana; bajeti ya mwaka jana ambayo imetekelezwa kwa kiwango kidogo sana na bajeti hii ya mwaka huu ina utofauti mkubwa sana na mimi napata shida na sijui Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaposhauri hili jambo kwamba tuongeze bajeti; kama ya mwaka jana tulishindwa kuitimiza mwaka huu tukasema tuongeze, mimi nidhani bajeti hii iliyokuwepo sasa tuone vyanzo vyake vya pesa vinakamilika na tusitegemee vyanzo vya kutoka nje.

Haya tuliyoyaomba kwenye mafuta, kama alivyozungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wakati alipotoa ufafanuzi mwanzo kuhusu suala la maji kwamba mtakapokaa kwenye kile kikao cha bajeti mtakapokuja hapa na majumuhisho basi tuone kwenye mafuta tumeongeza shilingi mia kwenye bia tumeongeza shilingi mia mbili. Tuongeze ongeze ili tatizo la maji Tanzania liwe limekwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri jana nilikutumia ki-*note* hapa kidogo, ki-*memo* nikiwa naomba ili tuwasaidie Wizara tulisaidie Taifa, sisi tumeomba Mamlaka ya Maji Tandahimba kwa vyanzo vya maji tulivyokuwa na mapato yetu haya ya korosho na ikitokea na Serikali ikakubali kutupa asilimia tano ya bei ya soko maana yake ni kwamba tunaweza tukaisaidia Serikali Tandahimba kukawa hakuna tatizo la maji. Sasa niombe tu barua zetu kwa sababu tumeshapeleka TAMISEMI kama ulivyoniambia kwamba nipeleke TAMISEMI, tulishapeleka na walitupa majibu kwamba wameshaleta dokezo kwenu; kwa hiyo tatizo liko kwenye Wizara yako; ukaangalie makabirasha yako vizuri. Kama Tandahimba tutapata Mamlaka ya Maji tukapokuja mwaka kesho kutwa hapa tutakuwa tunazungumza lugha nyingine nzuri kidogo kwenye jambo la maji. Vilevile niendeleo kukuomba Mheshimiwa Waziri Tandahimba pale nishukuru sana ulitupa pesa ambazo zingeweza kusaidia kuweka mashine ya *pump* pale Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bahati mbaya nyingine kubwa mmetupa *engineer* wa maji wa Wilaya tuliyokuwa naye miaka zaidi ya tisa hakuna maji Tandahimba na mambo mengine ya ajabu sana tumewahi kumpa pesa mpaka za Halmashauri pale kuweza kujenga *pump* pale maji hayatoki. Watu wa utumishi walimpa *transfer* ya kumwondoa Tandahimba aende sehemu nyingine kwa sababu ana muda mrefu, lakini mmefanya *lobbying* mmerudisha tena pale, yaani maana yake mnamleta *engineer* ambaye mnajua hawezi kusimamia mambo ya maji, mnamuacha pale tuendelee kupata shida watu wa Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nakuambia Mheshimiwa Waziri kuwa *engineery* yule mliyemleta tukimaliza Bunge mkiendelea kumuacha pale na sisi hatuna maji tutamwondoa sisi kwa maandamano makubwa kabisa. Nazungumza kwenye Bunge hili, tutamwondoa kabisa kabisa. Haitawezekana anapewa pesa; kuna mradi wa maji amekuja Naibu Waziri wa TAMISEMI; Mheshimiwa Selemani Jafo, unazinduliwa mradi wa maji ambao inatoka hewa badala ya maji, na manasema mradi umekamilika. Mradi unakamilikaje ikiwa maji hakuna na mnauzindua na mnasema tumekabidhi mradi tayari na ikiwa mamiolioni ya fedha Watanzania mmelipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Mheshimiwa Selemani Jafo pale Mahuta, amezindua mradi ule wa maji wa Mkupete, umezinduliwa mradi hewa, watu wa Mkupete hawana maji, hata Mheshimiwa Waziri ukija mradi ule mmetumia mamilioni ya pesa maji hayatoki. Bado mnataka *engineer* yule tukae naye, anazindua miradi ambayo haina maji na viongozi mnakuja na mnasema mradi umezinduliwa, maji hakuna tunakaa na *engineer* kama yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunahitaji *engineer* ambaye atatoa matokeo chanya ya maji. Hata ukatuletea profesa na ma-*degree* manne matano saba mkasema huyu ndiye professor wa maji na maji hatuyapati. Sisi wana Tandahimba tunasema huyu ni profesa uchwara tu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji mtuletee mtu anayetupa maji na si kutuletea vyeti tu na vyeti vyenyewe ni vya hewa na tunaona balaa lake hili. Kwa hiyo, tunahitaji mtu mwenye *capacity* ya kule maji. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kule kwetu uje, ile sehemu imekuwa ni sehemu ya mwisho kwenye kila jambo. Barabara mwaka jana mmeona walivyotufanyia, wametenga kilometa 50 mpaka leo tunapozungumza tunapozungumza ni *story*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa isiwe watu wa Kusini ni watu wa *story* tu, tumeshateseka kwa muda mrefu kusini tulishasahauliwa muda mrefu, kwa hiyo kwenye *priority* ya mambo haya, mnaposema maji tengeni maji pelekeni Kusini ili na sisi tujione ni Watanzania na tuna haki sawa na Watanzania wengine badala ya kutupa miradi tunarudi majimboni tunaisifia Serikali, maana unavyoleta kabrasha hili ninapokwenda mimi ninawasomea wananchi pale. Nasema safari hii bwana Serikali imetenga dola bilioni 87 saba kwa ajili ya maji, watu wanashangilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bahati mbaya Makamu wa Rais alikuja Tandahimba mwaka wa jana akawahakikishia watu wa Tandahimba kwamba tumepata pesa mtapata maji, maji hakuna. Haya mnayoyafanya ndiyo kaburi la Chama cha Mapinduzi maka 2020 haya. Haya mnayoyafanya haya msije mkaleta mabomu, watu hawana maji hawawezi kuchagua CCM wakati haitekelezi mahitaji yake, hawawezi, msije mkatafuta labda akina Nape wanasema hivi sijui ... (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kwa heri, ahsante. Imetosha Mheshimiwa muda wako ndio huo. Mheshimiwa Catherine Ruge. Mheshimiwa Mhe. Lathifah Chande, Mheshimiwa Joyce Sokombi ajiandae, dakika tano.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwa mara ya

kwanza kabisa katika Bunge lako hili Tukufu. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa Watanzania, kwa familia, kwa Wabunge, ndugu jamaa marafiki na bila kusahau Mbunge wa Arusha Mjini Mheshimiwa Godbless Lema kwa msiba uliolikumba Taifa hili siku chake zilizopita, Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kuchangia, kwamba Serikali iweze kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kuzingatia umuhimu wa maji katika maisha yetu ya kila siku. Serikali inaweza ika-*pull resource* kutoka kwenye sekta nyingine na tuweze kuipa kipaumbe Wizara hii ya Maji ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nisikitike kusema kwamba pamoja na kuwa na vyanzo vingi vya maji katika nchi yetu, kwa maana ya maziwa, mito, mabwawa na mabonde mbalimbali changamoto ya maji imekuwa ni ya muda mrefu. Tangu mimi nimezaliwa mpaka sasa hivi bado namwona mama yangu na wanawake wengine wa Kitanzania wakiwa wanabeba ndoo kichwani ikiwa ni zaidi ya miaka 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya maji inawaathiri pia wanafunzi wa kike kwa sababu mashuleni hakuna maji, hasa sehemu za vijijini. Hii inafanya watoto wa kike wakiwa katika hedhi washindwe kuhudhuria masomo kati ya siku tatu mpaka tano, jambo ambalo hupunguza ufaulu wa masomo kwa sababu ukichukua siku tano katika mwaka ina maana wanakosa masomo takriban siku 60 kwa mwaka. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie jinsi gani inaweza kuboresha miundombinu ya maji katika shule zetu ili tuweze kuwasaidia watoto wa kike waweze kufaulu vizuri kwa kuweza kuhudhuria masomo yao kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu miundombinu ya maji katika jimbo la Serengeti ninalotoka mimi. Ukiangalia bajeti hii ya mwaka 2017/2018 ni shilingi

milioni 858 tu zilizotengwa katika jimbo la Serengeti. Kuna changamoto nyingi sana ambazo zinalikabili shirika la maji safi na taka la *MUGUWASA* ambalo lina wakazi 47,000 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni nyingi ikiwa mojawapo *pump* ni moja ambayo haikidhi mahitaji, lakini pia kuna tenki moja tu ambalo halitoshenzi kwa wananchi wa Mugumu Mjini, mji ambao ambao unaundwa na kata saba zilizoko pale. Kwa hiyo, niombe Serikali iweze kuongeza bajeti katika eneo hili ili kuweza kuboresha miundombinu ya maji katika mji wa Mugumu kwa sababu miundombinu ni ya zamani sana na imechoka, lakini pia gharama za uendeshaji ni kubwa sana za Mamlaka ya Maji ya Mugumu Mjini kwa sababu makusanyo ya mwezi ni shilingi milioni saba lakini wanalipa ankara za umeme shilingi milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kabisa mamlaka ya maji Mugumu Mjini inajiendesha kwa hasara. Kwa hiyo, tuangalie nishati mbadala ambayo inaweza kuendesha ile *pump* ya Manchira ili tuweze kupunguza gharama za uendeshaji, lakini pia tupunguze gharama kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo inaikumba *MUGUWASA* ni kwamba kuna upungu wa mita kwa wateja. Kati ya wateja 1,536 ni wateja 509 tu ambao wameunganishiwa mita za maji. Kwa maana hiyo hii inaikosesaha mapato Muguwasa. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie jinsi ya kuisaidia *MUGUWASA* kuweza kusambaza mita ili wateja wote waweze kupata mita na hivyo waweze kuchangia mapato ya *MUGUWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako...

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja Kambi Rasmi ya Upinzani.

**MWENYEKITI:** ...Mheshimiwa Lathifah Chande atafuatia na Mheshimiwa Sokombi na Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabla ya yote napenda kutoa pole zangu kwa familia zote zilizokumbwa na msiba huu mkubwa, kwa kweli ni janga kubwa katika Taifa letu. Vilevile ningependa kutoa pole kwa Mbunge wa Mkoa wa Arusha Mheshimmwa Godbless Lema. Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia katika Wizara hii hususan juu ya Sera ya Serikali ya 2002 iliyoelekeza kwamba wananchi waweze kupata huduma ya maji ndani ya umbali usiozidi mita 400, lakini ni dhahiri kwamba imeonesha hadi sasa hii sera imeshindikana kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba maji ni uhai. Mwanadamu akose kila kitu lakini si kukosa maji. Sasa pale ambapo Serikali inaweka mipango ya maendeleo, hata kama ikaweza kufanyia kazi mipango yote isipokuwa hili suala la maji basi nisawa sawa na bure. Kwa sababu mwananchi analazimia kutumia muda mwingi katika kutafuta maji kuliko katika kufanya shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inavyosema kwamba uchumi unakua kwa asilimia saba ni bure kama mwananchi analazimika kutembea umbali wa hadi kilometa tano hata kumi kwa ajili ya kutafuta maji. Hii sera imeshindikana si kwa vijijini tu, mfano mkubwa ni mkoa wetu wa Lindi ambako maji ni janga kubwa mno kiasi cha kusababisha maji kuwa yenye thamani kama dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi, Hospitali ya Sokoine hakuna maji, kweli

hospitali inakosa maji au kwa kuwa Mawaziri mnapata maji hadi majumbani mwenu? Akina mama wanaenda kujifungua hospitali huku hakuna huduma ya maji wagonjwa wanaenda hospitali wanaolazwa pale wanakosa huduma ya maji, jambo ambalo linasababisha kuwa *prone* katika kupata magonjwa ya mlipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wauguzi wanakosa huduma ya maji, madaktari wanakosa huduma ya maji kweli Serikali inaliona hili tatizo na kukaa kimya bila kukuchua hatua yoyote? Kusema ukweli hili ni suala la kusikitisha mno kwa sababu hadi vyoo navyo vinakosa maji pale hospitalini, naomba mliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hapo tu unapoingia vijijini vile vile hali ni mbaya zaidi katika mkoa wetu wa Lindi. Hatuna maji katika Wilaya za Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Mchinga, Mtama pamoja na Kilwa. Ni sawa sawa na kwamba sisi hatustahili kuwa na haya maji, kitu ambacho ni muhimu kuliko vitu vyote ambavyo binadamu anahitaji. Ukienda Liwale si vijijini tu, ukienda Ruangwa siyo vijijini tu bali hata mjini tunakosa maji, naomba mliangalie hili. Wananchi wanalazimika kutembea umbali wa kilometa tatu hadi kilometa kumi kwa ajili tu ya kutafuta maji, na mwisho wa siku hawapati maji safi na salama kwa sababu wanaishia kufuata na kutumia maji ya madimbwi na maji ya mabwawa ambayo pia wanyama wanatumia maji hayo hayo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Sijui ungekuwepo leo, hali ya maji ni hiyo lakini unavyoielezea! Mheshimiwa Joyce Sokombi, naambiwa hayupo.

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Yupu? Waheshimiwa msiwe mnanitania mimi, huwa sipendi matani. Na ni vema mka- *apologize* wale

mlionitumia *message* hizo. Mheshimiwa Sokombi dakika tano.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika zangu tano achangeie Mheshimiwa Kunti.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi na mimi ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Maji. Kwa kuwa dakika chache lakini Wizara hii nyeti naomba niende moja kwa moja kwenye kitabu cha Waziri na bahati nzuri mimi nina vitabu viwili vyote, cha mwaka jana na kitabu cha mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa Ntomoko ambao niliusemea pia katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Mradi huu wa Ntomoko unabadilishwa tu maneno kwenye vitabu vya Mheshimiwa Waziri. Kitabu cha mwaka wa jana alituletea mradi wa Ntomoko kwamba unahusisha Halmashauri mbili za Wilaya ya Chemba na Wilaya ya Kondo. Kitabu cha mwaka huu hali ya huduma ya maji kutoka chanzo cha Ntomoko imeshindwa kukidhi mahitaji na kupunguza vijiji, yaani tunabadilishiwa maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mradi huu Mheshimiwa Waziri unalifahamu vizuri. Mradi wa Ntomoko ni *disaster*, haiwezekaniki. Leo mnakuja kutuandikia hapa ilhali mnajua kabisa nini kinachoendelea kuhusiana na suala zima la Ntomoko. Mheshimiwa Waziri, suala hili kama mnashindwa kuwawajibisha watu ambao wameweza kutenda dhambi kwa Watanzania wenzao kwa kupoteza fedha nyingi shilingi bilioni 2.4 wamezilamba, maji hakuna, wananchi wanapata shida ya maji, mna kazi ya kutubadilishia maneno kwenye vitabu, hatuwatendei haki wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela zile si hela ambazo watu wale wanaomba, fedha ile wananchi wa Wilaya ya Chemba na wao ni miongoni mwa Watanzania wanaolipa

kodi, wanatakiwa wapate hii huduma muhimu ya maji. Wilaya ile ina shida ya maji haijapatikana kuona. Kituo cha Afya cha Hamai hakina maji, nilisema, mwaka jana niliwaambia Wizara, mnaendelea kutubadilishia maneno kwenye hivi vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja, naomba aniambie suala la Ntomoko hatma yake ni nini? Wananchi wa Chemba tumesema huu mradi hatuutaki kaeni nao ninyi, tutafutieni mradi mwingine ambao tutapata maji. Hamuwezi kuwa mnaendelea kutubadilishia vijiji vyote, kata zote 26 hakuna maji. Mlitupa hivyo vijiji kumi navyo vimekuwa shida hakuna maji, mnataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya maeneo ambayo mnaendelea kufadhiliwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni miongoni mwa Mkoa wa Dodoma ndimo mnamopata kura humu, lakini bado hata hamuwakumbuki watu hawa, kwa nini mnafanya namna hiyo? Waswahili akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli. Sasa kama rafiki huyu mnamuona hana maana atakapokuja kupata rafiki mwingine msije mkamlaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la maji *DUWASA*. Sijaona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kikiniambia kwamba kutokana na ujio wa Makao Makuu kuhamia Manispaa ya Dodoma ambayo ndiyo itakayobeba watu wengi, sijaona mpango mkakati wa upatikanaji wa maji katika Mji wa Dodoma. Tuna kata 41 katika Manispaa ya Dodoma, ni kata 18 tu ndizo zina maji; na katika hizo kata 18 haizidi mitaa 50 ambayo inapata maji katika hizo kata 18. Sasa tuna huu ujio, Mheshimiwa Waziri hujatuambia nini mkakati wa Serikali kuhakikisha maji yatapatikana pamoja na ongezeko kubwa la watu linalokuja kuingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DUWASA* hii ina majanga ya madeni kwenye taasisi za Serikali, na naomba nizataje na utakapokuja hapa Mheshimiwa Waziri naomba uniambie

madeni haya yatalipwa lini na taasisi za Serikali. Inakuwa ni aibu na ni masikitiko makubwa sana mwananchi wa kawaida anakatiwa maji, hapati maji mpaka alipe bili ya maji, taasisi za Serikali hamtaki kulipa maji mnadaiwa mabilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DUWASA* inadai shilingi bilioni 1.9; kati ya hizo Jeshi la Polisi linadaiwa shilingi milioni 600, Magereza shilingi milioni 200; JWTZ inadaiwa shilingi milioni 100, JKT shilingi milioni 500, Makamu wa Rais... *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Kwa heri, ahsante, imetosha, ahsante. Mheshimiwa Ruth Mollel, hayupo, Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanasema kwamba fedha hii iongezwe ili kuweza kutoa huduma bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza sana, sisi Wabunge tumekuja hapa nia na madhumuni ni kuishauri Serikali na kuhakikisha kwamba tunaisimamia pia. Huwezi kuamini kabisa kwamba bajeti ya mwaka wa jana mpaka mwezi huu wa Aprili kulikuwa na utekelezaji wa asilimia 19.8. Hata hivyo sisi hatuoni kama hili ni janga na hatuoni kama hili ni tatizo kubwa sana, kwamba tunaweka bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika nchi na Watanzania wanapata maji halafu utekelezaji unakua asilimia 19.8, haya ni maajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hata kama leo tunasema tunataka kuongeza hizi fedha zifikie labda za



mwaka jana, lakini kama tutakuwa tunatekeleza asilimia 19 mpaka 20 haitaweza kutusaidia hata kidogo. Tatizo kubwa ni kwamba Serikali haitaki kupeleka fedha. Ninampongeza sana ndugu yangu Kitila Mkumbo ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara hii, lakini pia na watendaji wote, lakini nawaonea huruma sana kwamba wameingia katika wakati mgumu sana kwa sababu wanakwenda kufanya kazi maeneo ambayo hawapelekwi fedha, kinachoendelea ni lawama na kuonekana kwamba sio watendaji wazuri wa kazi wakati wana uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali ihakikishe kwamba inawatimizia Watanzania mahitaji yao. Kwa sababu haiwezekani kabisa tukawa tunakaa Waheshimiwa Wabunge humu tunapanga bajeti halafu utekelezaji unakuwa asilimia 19, hii ni aibu kubwa na hii inaonyesha ni jinsi gani ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inazidi kuwahadaa na kuwadanganya Watanzania kwa jinsi ambavyo inataka kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kuangalia pia katika Mji wangu wa Tunduma. Mji wa Tunduma ni Mji ambao upo mpakani mwa Zambia na Tanzania, lakini mji huu unahudumia nchi karibuni kumi. Unahudumia nchi zote za Kusini mwa Tanzania kwa mfano nchi ya Zambia, *South Africa*, Namibia, Angola, Congo na Botswana zote zinapita pale na mpaka wa Tunduma ni nguzo kubwa sana ya Bandari ya Dar es Salaam, asilimia 71 ya mizigo inayoshuka kwenye Bandari ya Dar es Salaam inapita kwenye mpaka wa Tunduma, lakini kuamini mpaka wa Tunduma wananchi hawana maji, wageni wanaokuja pale hawapati maji na wageni wale sasa wanakwenda kulala Zambia upande wa Nakonde, hii ni aibu kubwa sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuhakikishia kwamba mpaka wa Tunduma unaingiza kwa mwaka zaidi ya shilingi bilioni 80 lakini leo hakuna maji safi na salama kwenye mpaka wetu wa Tunduma. Kwa hiyo, ninaomba sana wakati Mheshimiwa Waziri anakuja hapa kuzungumza ajaribu kutueleza kwenye mpaka wa Tunduma tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata bajeti ya mwaka wa jana tulikuwa na bajeti ya shilingi milioni 753 lakini hakuna hata shilingi iliyokwenda kwenye Mji wa Tunduma kwa ajili ya utekelezaji wa maji. Waziri anatakiwa atueleze kwanini fedha hizi hazijakwenda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwaka jana pia kwenye bajeti kulikuwa na mradi ambao ulitaka kujengwa kwenye Mji wa Tunduma, mradi ulitaka kujengwa na kampuni ya *ACCPAC International* kutoka Ubelgiji; ulikuwa na thamani ya *Euro* milioni 100. Mradi ule mpaka leo ni hadithi na hakuna kinachoendelea, tunataka kujua na wananchi wa Mji wa Tunduma wanataka kujua ni lini mradi mkubwa huu ambao unatakiwa kutekelezwa utakwenda kutekelezwa haraka haraka iwezekanavyo kwenye Mji wa Tunduma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu tunaona tena fedha zimefunguzwa. Mwaka wa jana tulikuwa tumetengewa shilingi milioni 753, mwaka huu wamefunguza mpaka kufika shilingi milioni 600; tunataka kujua pia ni kwa nini fedha zimefunguzwa ikiwa mwaka wa jana hatukupata hata shilingi moja iliyokwenda kwenye miradi ya maji kwenye Mji wa Tunduma, tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti lakini nilichoshangaa tena kwenye Mkoa wa Songwe ambako kuna Wilaya ya Ileje, Momba, Mbozi na Wilaya ya Songwe tumetengewa fedha shilingi bilioni nne katika Mkoa mzima wakati kuna Mikoa mingine wametengewa shilingi bilioni 20, ama kumi na tisa, wametengewa fedha nyingi, tatizo nini? Kwa nini Songwe tumetengewa fedha kidogo kiasi hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anakuja kusema aje tu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Atakuja kukueleza Mheshimiwa Waziri, ahsante sana tunaendelea.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijagawa hizi dakika tano.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana. Mimi nafuata mlíchokubaliana.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Umeikata siyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mnakubaliana wenyewe halafu mnakuja kunihusisha mimi. Haya tunaendelea, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mbunge wa Jimbo la Uzini.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nachukua fursa hii kwanza kupata nafasi hii. Niishukuru Wizara kwa kuwasilisha bajeti hii ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa haraka haraka nilitaka kuzungumza mambo mawili, moja, suala zima la bajeti. Ni kweli bajeti imeshuka lakini bajeti iliyokuwepo ndio uhalisia. Si vema kuwa na bajeti kubwa isiyoweza kufikia malengo, ni vema kuwa na bajeti ambayo kweli tutaweza kuisimamia na kuweza kupata kile ambacho tulichokuwa tumekikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niungane na wenzangu wote kuitaka Serikali kwamba suala la shilingi 100 katika Mfuko wa Maji hili si la kuweka kigugumizi, kwa sababu imekuwa ni kila siku, suala hili limezungumzwa sana mwaka wa jana. Kama fedha hizi zingelipatikana tungelikuwa na zaidi ya shilingi bilioni mia tatu na sitini kwa mwaka na miradi mingi ingeweza kutekelezeka mbali na kutegemea fedha kutoka Serikalini moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuungane, kwa hili suala la shilingi 100 kama Serikali haitakubali kuongeza basi tuchukue hatua zinazofaa; kwa sababu Serikali haliigharimu chochote, Serikali ni kukubali tu shilingi 100 zikatwe kwenye

mafuta, haina gharama yoyote. Niiombe sana Serikali hapa ilizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tunakabiliwa na changamoto kubwa ya uzalishaji wa mazao mbalimbali kupitia kilimo cha *irrigation*. Kwenye eneo la *irrigation* fedha hazikwenda kabisa. Tuna miradi mingi na maeneo mengi ya Tanzania tunahitaji tuweze kuwa na kilimo cha umwagiliaji maji. Mimi langu ni kutoa rai kwa Serikali na Wizara hii na hasa Makatibu Wakuu na Kamisheni ya Umwagiliaji Maji tuzingatie rai nitakayoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu mimi nilisema tokea kipindi kile cha nyuma kwamba Mfuko wa Umwagiliaji Maji ufufuliwe. Upo siku nyingi lakini hauna fedha hata shilingi, hautengewi fedha. Nilitoa wazo kwamba fedha hizi sisi tunaweza kuzipata kupitia mashirika ya simu. Tukatoa tu kiwango cha watu milioni 20 ambao wanamiliki simu hapa Tanzania wakikatwa shilingi 100 tu kila muamala wa shilingi 1,000 kwa siku 30 tu unazalisha zaidi shilingi bilioni 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi tayari unaweza kutengeneza zaidi ya hekta 2400; hekta ambazo zitaweza kukuzalishia zaidi ya tani 330,060 kwa mwaka kama wakulima wataweza kulima mara mbili, kiwango ambacho kwa kweli ni *full security* ya nchi hii. Lakini ni chanzo cha uzalishaji wa viwanda mbalimbali katika nchi yetu. Tatizo letu liko wapi? Wenzetu wengine wametoa mawazo hapa wamesema watu wanakunywa bia kwa wingi, kwa nini tusikate shilingi 100 au shilingi 200 tukaweza kufufua huu mfuko na tukaweza kupunguza matatizo ya ukame na ukosefu wa maji katika maeneo yetu mbalimbali kwenye uzalishaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali tuzingatie haya, mengine tutakuwa tunapiga tu blabla kwa kusema kwamba tupate fedha moja kwa moja kutoka Serikali kuingizwa kwenye umwagiliaji maji si rahisi. Tuangalie Mifuko ya *NSSF*, *PPF* na mashirika mengine tukate kiwango kidogo kidogo. Mimi nimetoa mfano mdogo kwa siku 30 tu watu wangapi wanatumia shilingi 1,000 kwa miama ya simu?

Tukifanya miezi sita nchi yote hii tumeifanya kuwa umwagialiji maji na tutakuwa na uhakika wa uzalishaji wa chakula nchini mwetu na ile dhana nzima ya Tanzania ya viwanda itatimia kupitia huko. Nafikiri tufunue mawazo tuangalie kwa upana zaidi kuliko hali ilivyo sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilichokuwa nimekiomba ni kwamba Serikali iangalie maeneo yale kame zaidi. Wazo la kuwasaidia hasa wafugaji katika maeneo mbalimbali kuepusha ile wanaita *migration, movement* ya wanyama kutoka eneo moja kwenda lingine kwa ukosefu wa maji. Suala la ujengaji wa mabwawa katika maeneo mbalimbali ndilo mkombozi wa suala hili, na litaunguza sana migogoro ya wafugaji na... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rehani. Lakini nakukumbusha nenda ukaangalie kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye simu ndipo utaelewa tunachokiongelea kwa nini tunaangalia maeneo mengine. Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Hassan Elias Hassan Masala, Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa *initiative* na kusukuma Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria ambao sisi wakazi wa Mkoa wa Tabora tumekuwa tukiusubiri kwa muda mrefu. Nimshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu ambao tulishiriki pamoja pale Tabora katika sherehe ya kutia saini mkataba, na kwa taarifa zilizopo ni kwamba mwezi ujao wakandarasi wataanza kazi na kwa sisi tunaochunguza chunguza tayari zile Kampuni za Kihindi zimeshaonekana maeneo ya Solwa kule wakianza kufanya fanya shughuli za awali. Kwa hiyo, nishukuru kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nzega nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa

kuanza kutekeleza ahadi ya Rais ya shilingi milioni 200 ambayo ni fedha za awali kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji wakati tunasubiri mradi huu wa miezi 36. Sasa hivi Nzega angalau tumeanza kupata maji kwa mgao kwa wiki mara mbili. Mwanzo tulikuwa hatupati, angalau kwa mwezi walikuwa wanapata mara moja. Lakini sasa hvi ime-*improve two hundred*. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati anakwenda *Christmas* ile milioni 200 iliyobaki inafiki lini Nzega? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja, pamoja na shukrani zote hizi za dhati, niseme jambo la kusikitisha. Leo Nzega tuna siku tano hatuna maji na sababu ni moja tu, Mamlaka ya Maji ya Nzega ambayo imeanzishwa mwaka mmoja uliopita imekatiwa umeme na Shirika la *TANESCO* kwa sababu ya deni la shilingi milioni 206 ambalo chanzo chake ni Serikali Kuu kutokupeleka fedha za *OC* kwa zaidi ya miaka mitano, wananchi wanaadhibiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Bunge hili ningepomba, tunamnyooshea kidole Waziri wa Maji, jukumu na matatizo ya maji haya *cause route* ya haya yote tunayoyajadili ni *Ministry of Finance*. *This is a biggest problem*, kila sehemu tatizo fedha hazijaenda za maendeleo. Nataka niwape mfano mdogo, mimi natoka Kamati ya Huduma za Jamii, tuna matatizo ya *x-ray* kutokuwa *serviced* kwa sababu ya deni la Philips. *Who is the problem? Ministry of Finance* hawajamlipa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mamlaka za Maji za nchi nzima zinadaiwa shilingi bilioni nane na Shirika la Umeme, lakini mamlaka hizi kwa ujumla wake zinadai taasisi za Serikali shilingi bilioni 39. Watanzania wanalipa *bills* zao tunawakatia maji kwa sababu taasisi za Serikali Kuu hazijalipa umeme. Anayeadhibiwa ni *common man on the street*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo Katiba ya Chama changu hapa. Moja ya dhumuni, wajibu wa mwanachama, Wajibu Namba Tatu; "Kujitolea nafasi yake, kuondosha

umaskini, ujinga, maradhi na dhuluma na kwa jumla kushirikiana na wananchi wote katika kujenga nchi yetu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa sehemu ya dhuluma ya wananchi wa Nzega kukosa maji kwa uzembe unaotokana na maamuzi ya Serikalini, *I will never be part of this*. Sitaunga mkono Bajeti ya Serikali kwa sababu moja tu, Waziri wa Fedha aje hapa atuambie Waheshimiwa Wabunge anamalizaje deni la TANESCO ili Mamlaka za Maji zisikatiwe umeme kwa uzembe unaotokana na Serikali Kuu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa tumejadili sana kuongeza fedha na mimi nashukuru Waziri wa Fedha popote alipo apigiwe simu au Naibu wake atuhakikishie hapa kwenye *Finance Bill* wanaongeza tozo la shilingi 50... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea, Mheshimiwa Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu ni machache, moja, Jimbo langu la Kigoma Kaskazini tuna vijiji 46, katika vijiji 46 vijiji ambavyo maji yanatoka ni vijiji 14. Ningemuomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie na sisi watu wa Kigoma Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma na mikoa mingine, niombe sana Mheshimiwa Waziri umefika wakati tuyatumie maji ya *Lake Tanganyika* kwa ajili ya kupeleka maji Kigoma na *all the way* mpaka Tabora. Kwa sababu kutumia mito, mito inakauka. Ukienda leo uangalie Malagarasi ng’ombe walioingia mle na hali ya Malagarasi tukitumia kama itasaidia kwa wengine ni nguvu sana.

Mimi niombe Waziri, imefika wakati tufanye maamuzi ya kuchukua maji ya *Lake Tanganyika*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Maji. Nimewasiliza sana wenzangu hapa ndani, bajeti haitoshi. Kwangu bajeti hii inatosha, nitasema kwa sababu gani. Watu wote humu ndani naomba tuchukue Kitabu cha Nne, ukichukua Kitabu cha Nne nenda kila mkoa kwenye *sub vote* 3280 kuna *Rural Water Supply*, kila mkoa kuna fedha, lakini hizo haziko kwenye Wizara ya Maji. Naweza nikataja baadhi ya mikoa, Ruvuma wana shilingi bilioni nane, Kilimanjaro wana shilingi bilioni nne, Kagera wana shilingi bilioni nne, Tanga wana shilingi bilioni mbili, Kigoma wana shilingi bilioni tatu. Ukizijumlisha zote hizi na ukaja na za bajeti, bajeti ya maji inatosha. Sasa ambalo nataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha atupe *commitment*, fedha hizi zitoke zote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka wa jana ilikuwa bilioni 900, zimekwenda asilimia 19; na Waheshimiwa Wabunge tusipende ma-*figure* makubwa sisi tujaribu kuhangaika fedha tunazopitisha ziende. Haya ndiyo maswali ya sisi kujjuliza, kwa sababu kama tunakaa hapa miezi mitatu tunapitisha bajeti halafu zinakwenda asilimia 19 halafu mwaka ujao sisi tunasema hapana bajeti haitoshi iongezeke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mbona hatuongelei asilimia 80 ambazo hazijaenda? Kwa hiyo mimi nasema kama ni bilioni mia sita ikitokea zikaenda zote mwaka huu maana yake ni kwamba tutakuwa tumefanya asilimia 75 ya yale ambayo tungefanya mwaka jana, asilimia 75 ni pakubwa mno. Kwa hiyo,...

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.



**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye anaongea sasa hivi, *essence* ya kutaka kuongeza ni kwa sababu hata hiyo asilimia 19 ambayo imepatikana chanzo chake ni pesa ya tozo. Kwa hiyo, suala la kuongeza ni la msingi kulliko jambo lingine lolote. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, ananishangaza kidogo. Mimi sijaongelea habari ya tozo hapa, naongelea habari ya bajeti, anataka kuniambia shilingi bilioni 900 za mwaka jana zote zilikuwa za tozo, unataka watu wote hapa tuamini kwamba shilingi bilioni 900 zilikuwa za tozo? Sijaongelea jambo hilo, ninachoongea mimi, naongelea bajeti ya Serikali...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** ...bajeti tuliyopitisha ilikuwa shilingi bilioni 900...

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba, hebu subiri. Mpe Taarifa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na kila mtu humu ndani anajua kwamba namheshimu sana Mheshimiwa Serukamba na ni kaka yangu, lakini Mheshimiwa Serukamba anataka kulipotisha Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti za mikoa hata mwaka wa jana zilikuwepo na zimepita kwenye Kamati ya Maji, Kamati hiyo ndiyo imekuja kuleta malalamiko hapa kwamba bajeti haitoshi. Mwenyekiti wewe ni Mbunge mzoefu, umekaa hapa muda mrefu sana, ni nadra kwa Waheshimiwa Wabunge kupinga Taarifa ya Kamati kwa sababu Taarifa ya Kamati ni ya Wabunge wenyewe na hakuna mtu hapa...

**MWENYEKITI:** Mpe Taarifa tu, usichangie.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** ...nataka nimpe Taarifa Mheshimiwa Serukamba kwamba bajeti za mikoa alizozitaja zilikuwepo pia mwaka jana na zina tatizo hilo hilo la kwenda. Tunapozungumzia nyongeza, tunazungumzia kuhakikisha ya kwamba nyongeza na fedha kuweza kufika jinsi ambavyo inatakiwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea Taarifa?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, / *hope* dakika zangu zimelindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge nilichoongea mimi hapa hakuna ninayempinga hata mmoja. Ninachosema, nataka kuwaonesha Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye fedha zinazokwenda mikoani kwetu nyingine ziko kwa ma-RAS, hakuna anayesema mwaka jana, mwaka juzi zilikuwepo. Kwa hiyo, tunapoongelea bajeti ya maji ya mwaka jana ilikuwa ni shilingi bilioni 900 *plus* hizo za mikoani na ninavyosema mwaka huu ni shilingi bilioni 600 *plus* zilizo kwa RAS na fedha za RAS hazipiti Kamati ya Kilimo, kuna Kamati ya TAMISEMI; Kamati ya TAMISEMI Ndiyo inaangalia fedha zote za TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI kule kuna fedha za elimu, kuna fedha za maji, kuna fedha za kilimo, kuna fedha za kila kitu, kuna fedha za afya. Unapotaka kuongelea maji *in Tanzania* huwezi kusema zile unaziondoa, na zenyewe ni sehemu ya kutatua tatizo la maji kwenye mikoa yetu. *Argument* yangu ni fedha ziende, kwamba Waheshimiwa Wabunge tusikae hapa eti Mheshimiwa Waziri akija ameweka *1.4 trillion* tusimame tumpongeze halafu mwaka unaofuata zimeenda shilingi bilioni 200, tunapata nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema hapa, fedha iliyopangwa iende, ikienda nina hakika hali ya maji kwenye

nchi yetu itabadilika. Lakini tukianza kunyoosheana vidole, yule amepangiwa nyingi mimi chache haina maana. Sisi twende kwenye *plan* yetu, zimetoka shilingi bilioni 600 tuiombe Serikali kwa mara ya kwanza waweke *commitment* kwamba zote shilingi bilioni 600 zitakwenda; na baada ya shilingi bilioni 600 ninazongelea kuna nyingine kwenye mikoja yetu. kwa hiyo unaweza ukakuta tunaongelea bajeti ya maji *in totality* zaidi ya shilingi bilioni 800 si fedha ndogo. Kama kuna mtu ana hoja ya kuongeza tozo...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** ... ni jambo lingine, hakuna anayelipinga...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** ...kwa hiyo...

**MWENYEKITI:** Taarifa nazikataa.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kusema kwamba jambo la msingi tuhangaikie fedha zetu ziende, na hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la *DAWASCO* na *DAWASA*. Umefika wakati kwa *spirit* ile ile ya kubana matumizi, nikuombe vyombo hivi viunganishwe ili viweze kubana matumizi viweze kufanya kazi nzuri katika Mji wa Dar es Salaam...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimechukua nafasi ya Mheshimiwa Mgumba, nilikuwa nimemuomba zile dakika zake tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njeza, mnapaswa Meza ijue, lakini nakuheshimu, endelea.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniheshimu, na mimi nakuheshimu sana na huwa sikosi nafasi ukikaa hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapa pole wale wenzetu wote waliofiwa kwa ajali ya gari kule Arusha, na mimi kwenye jimbo langu tulikuwa kati ya watu ambao tuliathirika kwa kufiwa na mtoto wetu kwenye kijiji cha Irambo. Kwa hiyo, poleni sana Watanzania wote na tunategemea haya mambo hayatajirudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza hawa Waheshimiwa Mawaziri na Wizara nzima, ni watu ambao kwa kweli Wabunge watakubaliana na mimi, ukiongea nao hatakukatalia kitu, wana moyo wa kusaidia sana, hata ukienda Wizarani watakupokea vizuri sana. Hata hivyo, labda kitu kimoja tu, ukiwa na moyo inabidi vilevile uwe na maini. Nafikiri hapa leo tunazungumzia ni namna gani hawa tuwasaidie kwa moyo wao ule vilevile wamepewe na maini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maji ni muhimu sana kwa Tanzania, lakini mimi nakubaliana na wenzangu wote kwamba hii bajeti iongezeke. Tozo ya kuongeza ya shilingi 50 ni muhimu na tusipinge hapa, kuna wengine wanafikiri ukiongeza hiyo labda itaongeza *inflation*, hapana. Mafuta tunanunua kwa dola, 2015 dola ilikuwa 2150, leo ni 2200, hata tukiongeza hiyo shilingi 50 haina *impact* yoyote

kwenye *inflation*; na ukiongeza hiyo shilingi 50; na kwa ripoti ya EWURA tuliingiza mafuta kwa ajili ya matumizi ya Tanzania kama shilingi bilioni 3.4, ina maana tunaweza kuongeza kwenye bajeti zaidi ya shilingi 170,000,000,000, ni hela nyingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoomba mimi hapa, kwa sababu kuongeza mapato ni suala lingine, je, haya mapato unakwenda kuongezea kwenye kikapu gani? Unaweza kwenda kuongeza kwenye kikapu ambacho kimetoboka, na hilo ndilo tatizo tulionalo. Kwa sababu Sekta ya Maji kwa *experience* niliyonayo kwenye jimbo langu haina *control* kabisa, hela zote zinazopelekwa hazifanyi kazi ile inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2010 Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilipewa zaidi ya shilingi bilioni 6.2 lakini leo hii ninapozungumza katika miaka yote hiyo hakuna mradi hata mmoja ambao unafanya kazi kwa hizo pesa zilizokwenda. Sasa tunaweza kuzungumzia hapa kuongeza pesa, unaongeza maji kwenye kikapu ambacho kimetoboka, unafanya kazi ya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninachoomba hapa yawepo mambo mawili, iongezwe pesa kwenye bajeti kusaidia maji lakini vilevile kuwe na udhibiti wa pesa za maji. Udhibiti huo utasaidiwa kwa kuunda kile chombo cha Wakala wa Maji Vijijini na hiyo utekelezaji wake uje mara moja. Nalisema hilo kwa uchungu mkubwa kwa sababu Wabunge hapa ni mashahidi, niliuliza swali kuhusu matatizo, changamoto ya maji Mbalizi nikajibiwa kuwa hakuna matatizo ya maji Mbalizi na maji yapo ya ziada na wananchi mpaka leo wanashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo miradi ambayo sisi tulipewa, yote, ukiangalia orodha ya Wizara inaoneshwa hiyo miradi imekamilika. Sasa unauliza, huyu ni nani anayemdanganya Mheshimiwa Waziri? Ukionesha miradi imekamilika wananchi nao kule wanajua kuwa miradi imekamilika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mapunda na Mheshimiwa Makilagi aijanadae.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu, na kwa kuwa muda ni mfupi, naomba moja kwa moja niende kuunga mkono mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sababu za kuunga mkono hoja ni kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na watendaji wake chini ya Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge, watendaji wote wa Mamlaka za Maji nchini wanafanya kazi ya kupigiwa mfano. Ni ukweli usiopingika kwamba Waziri na timu yake wako vizuri na wanafanya kazi nzuri, fedha zote wanazozipata wanakwenda kutekeleza miradi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, zipo changamoto mbalimbali ambazo Serikali inatakiwa izifanyie kazi na ninaomba niungane na Wabunge waliozungumza kwamba upo sasa umuhimu wa kuhakikisha fedha zote zinazotengwa na Serikali zinapelekwa kama zilivyopitishwa. Kwa sababu huwezi kumlaumu Waziri, huwezi kulaumu watendaji kama hujawapelekea fedha za kutosha. Tunatenga fedha hapa, lakini fedha haziendi kama zinavyokusudiwa na taarifa inaonesha imepelekwa kwa asilimia 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru sana Serikali kwa kuimarisha miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na Pwani, lakini vilevile na Mkoa wa Mara.

Ushauri wangu, naomba niishauri Serikali, ule mradi wa maji Pwani – Dar es Salaam pia uhudumie wananchi wa Mkuranga na Kisarawe kwa sababu pia miundombinu inatoka kule. Vilevile niwapongeze kabisa kwa dhati Mamlaka ya *DAWASA* kwa kazi nzuri sana ya kusimamia miundombinu ya maji maana kama wasingejenga inawezekana pesa zingepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee niwapongeze *DAWASCO* kwa kazi nzuri ya uendeshaji, na ushauri umetolewa kwamba ipo haja ya kuangalia mamlaka hizi na kuziunganisha na mimi naungana nao. Pamoja na hayo naomba nitoe angalizo kwa Serikali, tusikurupuke. Kwa sababu mimi ninayezungumza nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya *DAWASA* miaka tisa na nyuma huko tulikuwa na *NUWA* na baadaye tukaja na *City Water* na baadaye tumekuja na *DAWASCO*, tuliona Mamlaka ya *DAWASA* ibaki ijenge miundombinu, itafute fedha isimamie miradi na *DAWASCO* wabaki kuwa waendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ushauri wangu, naomba kabla ya kufikia kuziunganisha hizi mamlaka hebu angalieni historia ilikuwaje mpaka zikawa sasa mamlaka mbili kwa lengo la kubana matumizi. Hoja ni nzuri, lakini tusikurupuke, tuifanyie kazi polepole ili tulete tija tusije tukarudi kule nyuma ambapo tulikuwa tumetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru sana Serikali kwa kuimarisha miundombinu katika Mji wa Musoma, naomba niishukuru sana maana sasa Musoma tunakwenda kupata maji ya kutosha. Ushauri wangu pale chanzo cha maji kinapotoka Mji wa Musoma kinatoka pia Musoma Vijijini. Ninaomba kata ya Etaru, kata ya Nyegina, kata ya Nyakatende na wenyewe wapate maji kutokana na chanzo kile. Tukiacha bila kupata maji wale wananchi wa lile eneo wanaweza wakaharibu ile miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee Mradi wa Bitiama – Kyabakari – Mgango, mradi wa kihistoria, mradi wa kwa Baba wa Taifa, sasa ni miaka 30 mimi nausia mradi huu. Ni juzi hapa niliusikia wakati Mwandosya akiwa

Waziri, amekuja Mheshimiwa Dokta Mwakyembe amezungumza, leo anauzungumza Mheshimiwa *Engineer* Lwenge.

Mheshimiwa wenyekiti, nimepitia kwenye kitabu hiki upembuzi yakinifu umemalizika taarifa imepelekwa *BADEA*, na mwaka uliopita ilikuwa ni hivyo hivyo. Nataka leo Serikali ituambie, hivi kama leo *BADEA* hawatoi fedha Serikali ina mkakati gani na hasa kwa kuzingatia kule maji yanakwenda mpaka kwa Baba wa Taifa, Baba wa nchi hii ambaye ametufanya wote tuko kama hivi tulivyo? Wananchi wa kule wana adha kubwa sana, wamezungukwa na mito, wamezungukwa na maji, lakini hakuna kinachoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu wote waliosema tozo ya maji iongezeke, na mimi naungana nao kwa sababu tumeona kile kiwango cha shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta imeleta tija sana kwa nchi yetu. Naomba iongezeke shilingi 100 ili wanawake wa Tanzania wapunguziwe adha wanayoipata, wanawake wanatembea umbali mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti nimegundua hata wanawake wanaojifungua kabla ya kufikisha umri tatizo ni maji, hata wanawake wanaozaa watoto bila kufikisha umri tatizo ni maji, mimba zinazotoka mpaka watoto wanafariki ni maji kwa sababu wanatembea muda mrefu kwenda kutafuta maji wakati wataalam wanawashauri wapumzike. Vifo vya watoto wanaofariki chini ya miaka mitano asilimia 40 ni watoto wanaozaliwa kabla ya umri na tatizo kubwa ni kwa sababu wanawake wanafanya kazi za shurba. Ataenda kutafuta maji, arudi akalime, arudi akamuhudumie baba, arudi akapike. Jamani, sheria inasema ni umbali wa mita 400 tu, ninaiomba Serikali isiwe na kigugumizi katika kuongeza tozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena tumefanya *research* kabisa sisi wenzenu tumekwenda, wananchi hawana shida kuongezewa shilingi 100, tena haitaleti madhara yoyote



katika kuongezeka mfumuko wa bei na kuongezea wananchi mzigo wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu aliye na gari ni kidogo ana maisha mazuri na wananchi wakiona matokeo wako tayari kuchangia shilingi 100. Ninaomba tusiogope, hebu twende na mpango huu, ije *Finance Bill* hapa Bungeni tuiptishe kwa kauli moja twende kuwakomboa wanawake na wananchi... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana, Mungu akubariki sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Ryoba na Mheshimiwa Nachuma ajiandae.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichagie kidogo angalau kwa muda huu mchache. Kwanza nampongeza Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kazi anayoifanya inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nizungumzie huduma ya maji katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki. Katika ukurasa wa saba Mheshimiwa Waziri mmesema kwamba hadi kufikia Machi, 2017 mmeweza kuwafikishia wananchi wale wanaoishi vijijini asilimia 72. Inawezekana ni sawa lakini si sawa katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki. Hali halisi ya Manyoni Mashariki ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyo vijiji 58, kati ya hivyo ni 19 tu vimepata maji. Vilevile nina vitongoji 248, kati ya hivyo 37 tu ndivyo vimepata maji, ambavyo ni sawasawa na asilimia 14.9. Ukijumlisha kwa maana ya *Rural Manyoni* ni

asilimia 18.3 tu ya wananchi ndiyo wameweza kupata maji, hii 72 na 18 pengo ni kubwa mno na inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi hii inaridhishwa na kilichopo ndani ya kitabu hiki cha bajeti. Ukiangalia jedwali namba 5(c) ukurasa wa 156 mpaka 157 *item* namba 10, orodha ya ile mkoa ambayo inatakiwa kujengewa miundombinu ya kusambaza maji ile mkoa kame ile, Manyoni Mashariki haipo, nimejaribu kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama vile haitoshi, jedwali namba 8 ukurasa wa 174 mpaka 184, zile *scheme* za umwagiliaji, Manyoni Mashariki, pamoja na kwamba tuna Bwawa la Mbwasu, bwawa la kimakakati lile ambalo linatakiwa lichimbwe na upembuzi yakinifu ulishafanyika, inasikitisha halipo kwenye orodha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi, jedwali namba 9(a) ukurasa wa 185 fedha za mfuko wa maji zilizopelekwa katika Halmashauri hadi Machi mwaka huu Manyoni Mashariki haipo inasikitisha. Kama vile haitoshi, jedwali namba 13 ukurasa wa 196, orodha ya visima vilivyochimbwa 272 katika nchi hii Manyoni Mashariki haipo; jambo hili linasikitisha sana ni lazima tulalamike. Kuna msemaji amesema huwezi kulalamika, lakini ni lazima mimi niseme kwa nini Manyoni Mashariki tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani Wizara kwa kuzingatia haya fedha ambayo imetolewa mwaka huu katika bajeti hii tumepewa shilingi milioni 611 tu. Tulidhani angalau tungepewa angalau shilingi bilioni nne Manyoni Mashariki lakini hii haitoshi pia nilidhani kwamba Wizara wangepanga mji wa Manyoni katika awamu ile ya kwanza, katika zile fedha za Mfuko wa India; zipo awamu tatu, Manyoni imepewa awamu ya tatu, kwa nini tusingepengiwa angalau awamu ya kwanza kwa sababu tuna kiu ya maji kwanini mnatuweka kwenye awamu ya tatu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuokoa muda nitoe ombi kwamba Kamati ya Bajeti mtakapokaa na Serikali hebu

itazameni Manyoni Mashariki kwa jicho la peke yake, kwanini mnatubagua? Lazima nilalamike, hivi mimi ninakuja kuwapigia tu wenzangu makofi hapa, halafu narudi mikono mitupu kweli kabisa? Hapana, hebu itazameni Manyoni Mashariki tumekosa nini sisi? Sisi ni Watanzania wenzenu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Lakini pia naomba nikubaliane...

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtuka hebu subiri taarifa ingawa inakula sana muda wangu hizi

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Ukienda page 173 ya kitabu hiki kuna dola milioni 503 za kutoka India. Dola milioni 503 ni karibia trilioni 1.1 za Tanzania. Fedha hizi nazo zinaingia kwenye maji kwahiyo nilitaka kutoa taarifa, tunapoongelea bajeti ya maji ya mwaka huu maana yake ni dola milioni 503 kujumlisha shilingi bilioni 600, *unless* niambiwe kwanini fedha hizi ziko hapa lakini hazipo kwenye vitabu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa ndiyo maana sitaki taarifa hizi kwa sababu sehemu nyingi mnalolipatia Bunge taarifa ni za kupotosha, tunaendelea Mheshimiwa Mtuka. (Makofi)

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba ulinde muda wangu, naikataa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa, sijui kwanini kuna Waheshimiwa wengine hawasililizi, hizi ni za mwaka wa jana, lakini pia nimeomba hizi pesa za India, nimesema nilidhani kwamba hizi fedha za India, Manyoni ingepewa awamu ya kwanza zipo awamu tatu hapo

Mheshimiwa aliyenipa taarifa hebu apitie vizuri pale ziko awamu tatu wamegawanya Manyoni iko awamu ya tatu, tuna kiu, nimesema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe na mimi nikubaliane na ile tozo ya shilingi 50 kwenye mafuta iongezwe ifike shilingi 100 mtusaidie na hii fedha ianzie Manyoni Mashariki jamani. Pia nakubaliana ya kwamba iundwe Wakala sasa wa Maji Vijijini kama ambavyo ilivyo *REA*, tusiiweke Seriakli kuu, Serikali Kuu tunaona pesa inapotea na usimamizi siyo mzuri naomba wakubaliane na hilo iundwe wakala kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante mimi nina dakika kumi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Naam.

**MWENYEKITI:** Dakika tano sitaki matani.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Naomba nianze na hii ya ukurasa wa 173. Mheshimiwa Waziri kwanza nichukue nafasi hii nikupongeze wewe na Naibu wako, kwa kweli ni moja ya Mawaziri ambao mnajitahidi ila shida tu ni kwamba hamna hela, kwahiyu hapa hata tukiwaadhibu hakuna lolote. Sasa mimi niwashawishi Wabunge kwamba wakubali, wasikubali Wizara ya Fedha ile shilingi 50 iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji, hatuwezi kufanya hadithi hapa ya kuwafurahisha wananchi huko nje, lakini sisi Wajumbe wa Kamati ya Maji hukio ndani ndiyo tunafahamu uhalisia wa shida ya maji nchi hii sasa hiyo iongezeke, Mheshimiwa Waziri wewe furahi hiyo lazima iongezeke.

Sasa nilitaka wakati mnakuja kujibu Mheshimiwa Waziri hebu nisaidie, kwenye ukurasa wa 173 Mji wa Mugumu kwenye usambazaji wa maji kuna hizi fedha *billions almost 19* kutoka Serikali ya India. Nataka kujua na wananchi wa Serengeti wa Mugumu wanataka kujua ni lini zinakuja ili kazi ya usambazaji wa maji ianze, maana ile ya uchujio inaendelea vizuri na nikushukuru sana kwa kusukuma naona Yule mkandarasi anakwenda *speed* kweli kweli Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme moja tu, kwamba kuna hii Programu ya Maji Vijijini vimechimbwa visima vingi lakini wananchi wetu wa vijijini hawawezi kuendesha kwa kutumia majenereta na hata maeneo mengine ambayo yana umeme bado wnanachi wetu wanakuwa ni shida kuendesha miradi hii. Kwa hiyo mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri kama jinsi tulivyoenda Shinyanga tukaona ule mradi wa Maganzo wanatumia *solar*, wanatumia na zile *prepaid meter*, naomba Wizara ichukue jukumu la kuhakikisha ya kwamba, miradi ya maji vijijini wanatumia umeme wa jua katika uzalishaji wa maji, hilo ni la msingi sana bila hivyo hii miradi itakuwa hapa tu na haifanyi kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kwenye umwagiliaji, unapokuja ku-*wind up* niambie mabwawa ya umwagiliaji ya maji ambayo tayari yamekwishatumia fedha za Serikali ya Bugerera kule Nata, Nyamitita kule kata ya Ling'wani, Mesaga kule kata ya Kenyamonta nataka kujua *progress* yake ikoje? Kwa hiyo, unapokuja ku-*wind up note that*, ninahitaji kusikia na wananchi wa Serengeti wanahitaji kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambi lingine nilitaka niseme, ukiangalia Sera ya Maji ya Namibia, wao kwenye sera yao wanaita *Water For Survival*. Wanatenga asilimia 60 ya bajeti yao kwa ajili ya maji kwa nini? Maji ndiyo chakula, bila maji hatuwezi kupata mazao ya chakula, leo Tanzania kila kona wananchi wanalia njaa. Lakini kama tungelikuwa na kilimo cha umwagiliaji kila kona naamini kungekuwepo

na chakula cha kutosha; lakini leo tunalia. Ukiangalia kwenye takwimu maeneo ambayo ardhi inatumika kwa ajili umwagiliaji ni sehemu ndogo sana.

Kwa hiyo, mimi ningependekeza kwamba kwenye bajeti zinazokuja, kama kweli tunahitaji kufanya mapinduzi ya viwanda katika Taifa hili ni lazima tuwekeze kwenye miradi ya maji ya umwagiliaji. Kama hatuwezi kuwekeza kwenye miradi ya maji ya umwagiliaji hayo mapinduzi ya viwanda sijui viwanda vya namna gani, labda viwanda vya kuchomelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nachuma dakika tano

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwamba, Mtume Muhammad Karne ya sita alishawahi kusema kwamba *"Manla-yashkurunnasa la-yashkurullah"* yaani yule ambaye hawezi kumshukuru binadamu mwenzake basi hata Mwenyezi Mungu kwa neema alizompa hawezi kumshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe na kiti chako, lakini kwa namna ya kipekee kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuja Mtwara kuzindua mradi mkubwa wa utanuzi wa Bandari ya Mtwara Mjini, ninamshukuru sana na nimuombe tu Mwenyezi Mungu aendelee kutusainia mikataba mingine magati yale matatu yaliyobaki yaendelee kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichangia moja kwa moja kwenye Wizara hii ya maji, mwaka jana niliuliza swali hapa namba 197 ambalo niliulizia suala zima la ujenzo wa maji kutoka Mto Ruvuma kuja Manispaa ya Mtwara. Majibu ya Mheshimiwa Waziri, alieleza Bunge lako hili Tukufu kwamba kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya

China kwa ajili ya kupata mkopo nafuu wa utekelezaji wa mradi huo. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017 na kazi zitakazofanyika ni pamoja ujenzi wa chanzo, mtambo wa kutibu maji, bomba kuu la kupeleka maji Mtwara Mikindani pamoja na kujenga matenki lakini pia na usambazaji wa maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiangalia katika kitabu hiki, Mheshimiwa Waziri amepanga vizuri sana, ameweka na ameeleza kwamba mradi huu bado mpaka leo haujapata pesa wakati mwaka jana walitueleza kwamba mradi huu wa kutoa maji Mto Ruvuma na kusambaza maji Mtwara Mjini ungeweza kuanza katika bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba atueleze Mheshimiwa waziri kwamba tunavyoelezwa hapa ndani ya Bunge hili na kwenye *Hansard* inaeleza kwamba pesa zimetengwa, lakini huu mradi mpaka leo naambiwa majibu yale yale ya mwaka jana mabyo alitueleza, aje na majibu ambayo kimsingi yatawaridhisha wananchi wa Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nieleze tu kwamba baadhi ya maeneo ya Mtwara Mjini na hasa kata ya Ufukoni na kata ya Mitengo maji hatuna kabisa na mimi kama Mbunge niliweza kutenga pesa zangu baada ya kuona kwamba huu mradi ni mradi wa muda mrefu na utachukua muda mrefu kuweza kuanza, lakini pia kumalizika, nikapeleka pesa zangu milioni 10 kwa ajili ya kichimba kisima pale. Hata hivyo niliweza kuomba Idara ya Maji, kuna gari pale wanalo la Wizara ambalo linafanya utafiti na kuchimba maji lakini pesa alizonieleza ni pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwambiwa kwamba tutashirikiana na Mbunge tuweze kuchimba kisima maeneo ya Comoro ambako utafiti tayari nilishatoa pesa yangu ya mfukoni tukafanya utafiti, lakini mpaka leo wananinyima gari la kwenda kuchimba kisima pale ili wananchi waweze kupata maji ni jambo la ajabu sana. Nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, atusaidie gari kwa sababu huu mradi bado haueleweki kwa sababu kila siku tunapewa

dana dana kwamba watu wa Benki ya China hawajatoa pesa; kila nikiuliza naambiwa watu wa Benki ya China hawajatoa pesa na wananchi kule wanapiga simu sana na wanadai sana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mle ambamo tathmini imeweza kufanyika kutoka Kitaya, Jimbo la Nanyamba mpaka Mtwara Vijijini, vijiji vile 26 wote wanahitaji fidia lakini mpaka leo, miaka zaidi ya mitatu hivi sasa wale wananchi wamechukuliwa maeneo yao na fidia hawajalipwa, wanasumbua kweli kweli Wabunge wote wa Mtwara Mjini na Mtwara Vijijini wanatusmbua sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie hilo, atupatie gari tuweze kuchimba kata hizi ambazo Mtwara mjini hatuna maji, nitasaidia na mimi Mbunge ili tuweze kuondoa tatizo hli la maji. Pia nizungumzie.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, muda wenyewe ndiyo hivyo tena, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ya kusimamia na kuliongoza Taifa hili kwa *speed* inayotakiwa. Nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa Profesa Kitila Mkumbo, ninahakika akiungana na wenzake pale wanaweza kufanya kazi kubwa sana ya kusukuma nchi hii mbele pamoja na vijana wadogo wakina Luhemeja ambao sasa hivi



wamepata nafasi ya kushughulikia matatizo ya maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambayo wanaifanya Wizara ni kazi nzuri sana, lakini kuna baadhi ya mambo wanakutana hapa na upinzani mkubwa hasa wa takwimu zao, mimi nadhani wanatakiwa vilevile kufanya vile vile kazi ya *RITA* ya kusajili vizazi na vifo. Wanatakiwa wasajili visima vilivyokufa na vilivyo hai. Pengine kwenye orodha, wana orodha ya visima lakini vimeshapigwa radi siku nyingi vingine vimepigwa tetemeko wao kwenye vitabu wameandika kwamba visima vinatoa maji. Watajikuta wanapata matatizo makubwa bila sababu za msingi, sajilini takwimu za visima ambavyo havifanyi kazi na vinavyofanya kazi, mtapata kwa uhakika kwamba maji yapo kwa kiasi gani si kuleta tu kwamba kuna visima kadhaa na maeneo kadhaa yanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata visima vya zamani ambavyo vimekufa Halmashauri hazina uwezo wa kuvifufua. Kuna baadhi ya maeneo walikuwa na maji sasa hivi hawana maji. Kwa mfano ukija kutazama kwenye Jimbo la Mtera kuna Kata kadhaa zinahangaika kupata maji. Kata ya Handali, ukienda kutembelea Idifu, ukienda kutembelea Mlowa Bwawani wote hawana maji lakini ukija hapa unakuta takwimu vijijini ni 72. Kwa hiyo, nina uhakika wakisajili visima vilivyo hai na vilivyokufa wanaweza wakaja na mahesabu ya uhakika. Lakini nchi hii tuigawe kwenye vipande, kuna baadhi ya maeneo yanasubiri muda mrefu sana kupata huduma hii, tujue tu kwamba tutapata lini, nayo tukijua hiyo inaweza kutusaidia. Tumeona kuna ongezeko kubwa sana la huduma za maji mijini tumekubali na sisi tunayaona lakini kuna baadhi ya maeneo hata wananchi waelewe tu kwamba mwaka gani basi hii huduma muhimu ya maji itawafikia vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji ni Wizara mtambuka sana, na nashangaa tunapoijadili Wizara hii halafu Wizara ya Fedha haina Waziri wala Naibu Waziri humu ndani ya Bunge, hii si sawa. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais

aliwaweka wawili mmoja akiwa hayupo mwingine yupo, hii ni dharau kubwa sana kwa Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, tungependa, tunapojadili Wizara muhimu kama hizi Mawaziri wa fedha wawepo, Bunge maana yake karibu ni Wizara tatu tu; ni kiti cha Spika, Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha maana humu tunazungumzia hela sasa tukiwa tunazungumzia pesa wahusika wa fedha hawamo kidogo inatupa matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu hapa vinazungumzwa, jana kulikuwa na Mbunge mmoja alikuwa anaicheka Serikali na kuibeba kwanini Rais ameanza na ndege asianze na maji. Jamani, nataka leo nitoe somo kidogo hapa. Ndege ni sawa sawa na mkulima mwenye kilo moja ya mahindi ndani hana chakula na mvua zimeanza kunyesha, anatakiwa achague akaange ile kilo moja afe au apande apate mahindi mengi ili aweze kuishi? Mheshimiwa Rais alipoleta ndege amelea biashara ili izalishe tupate hela za kutengeneza maji mengi zaidi, kwa hiyo, badala ya kumbeza tumuunge mkono, Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, nchi haiendeshwi kwa hapana.

Nataka niwambie, kwamba duniani kuna aina tatu za upinzani; uko uoinzani shinikizo wanashinikiza hoja, upo upinzani kioo na uko upinzani *serious*, huu wa Tanzania ni upinzani kioo. Kama hujachana wanakwambia hujachana kesi inaisha unaendelea na shughuli zako. Kwa hiyo, Serikali msuwe na wasiwasi tuendelee kujipanga kufanya kazi za maendeleo ya nchi hii, tusishughulike na upinzani kioo ambao kaa hawajachana wanakwambia umechana kasoro Zitto tu ndiyo anajitahidi na kwa sababu yuko peke yake. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi umeona walivyomuabisha Makamu Mwenyekiti wa Chama, amekuja Profesa Safari kugombea hapa amepewa kura 30 na hawa, hawamtaki Makamu Mwenyekiti wa Chama chao awe kiongozi, hawa ndiyo wanaweza kupewa Serikali, haiwezekani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umekwisha.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** ...watu ambao hawaheshimiani, haiwezekani. Kwa hiyo, nakushukuru sana, mimi naunga mkono hoja, lakini nawaambia Serikali msihofu upinzani tufanye kazi. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya Waheshimiwa Wabunge huyo ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa mchana tunaye Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali dakika zake kumi, tunaye Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza dakika zake tano na tunao sasa wachangiaji wengine watano pia dakika tano, tano; Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Musa Ntimizi na kama muda utaruhusu tutaendelea na Mheshimiwa Kwandikwa, Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

Matangazo, Waheshimiwa Wabunge wanaotokana na Chama cha Mapinduzi kikao hicho sasa si *immediately* baada ya hapa ni saa 8:00 mchana lakini kitakuwa badala ya Msekwa kitakuwa Jengo Jeupe.

Halafu Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anatangazo hapa tena mlisikilize vizuri; washiriki wa *Miss UDOM* na waandaaji wa mashindano hayo ambapo kesho ndiyo mashindano yenyewe yatafanyika katika Hoteli ya *Royal Village* - Dodoma, mnataarifiwa kwa hilo tangazo la msingi sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wametajwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wakati akisitisha shughuli za Bunge. Mheshimiwa Hamidu Bobali, hayupo; Mheshimiwa Conchester Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia japo muda kwa mfupi, lakini nitoe machache kuhusu hoja yetu iliyo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukua nafasi hii kuungana na Wabunge wote na waliochangia kwamba Wizara hii ipewe fedha za nyongeza katika bajeti yake. Hatuwezi kuongea mengi. Waheshimiwa Wabunge wameongea mengi kuhusu matatizo ya maji katika nchi yetu. Maji yamekuwa ni janga katika nchi na nitashangaa Wabunge ambao wanasema bajeti inatosha. Bajeti haitoshi, iliyotolewa haikutosha, basi tuombe Serikali iweze kukubaliana na maoni ya Wabunge kwamba tozo ya sh.50 iongezwe ili tupate sh.100/= kutokana na lita za *petrol* na *diesel*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo naona linatukabili sisi ni namna ya kusimamia fedha ambazo zitatolewa katika bajeti. Tunapoongelea miradi ya maji, siyo kwamba miradi ya maji haijawahi kuwepo. Inawezekana katika nchi yetu, tusingekuwa na kilio kikubwa cha matatizo ya maji kama fedha ambazo zilitolewa huko nyuma kutengeneza miradi ya maji katika kupitia mradi wa *World Bank* pamoja na ile miradi ya vijiji kumi, zingesimamiwa inavyotakiwa. Zingesimamiwa, ina maana tungekuwa tumepunguza kwa kiwango kikubwa matatizo ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, pamoja na kwamba tunatoa kilio fedha ziongezwe, fedha hizi Waheshimiwa Mawaziri zisimamiwe ili tusije tukarudi kule nyuma kama ilivyokuwa katika miradi ya awali. Nashangaa pale watu wanapokuja hapa na kuimba nyimbo za kujisifu, lakini walioharibu na kushindwa kusimamia miradi hii ni Serikali iliyoko madarakani. Tunasifu Awamu ya Tano, lakini kulikuwa na ya Pili, ya Tatu na ya Nne. Ina maana wao walikuwa hawafanyi kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka ni kwamba miradi isimamiwe. Fedha tunazomba kama Bunge tunawapa Serikali mafungu, basi mafungu hayo yasimamiwe kikamilifu ili miradi iweze kuleta matokeo mazuri na iweze kuonekana. Kwa mfano, kama sisi ambao Kamati zetu zinazunguka kutazama miradi hii, iwe ya umwagiliaji, iwe ya mabwawa ya matumizi, haifanyi kazi vizuri. Fedha zinatumika vibaya!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, aende pale Tabora, kuna ule mradi wa Nala, ni mabilioni ya pesa. Kuna miradi mingine ambayo Halmashauri inashindwa kulipa Wakandarasi na inapaswa ilipe fidia au ile hasara ya kuchelewesha kulipa. Kwa hiyo, unakuta Halmashauri hizi nazo zinajikuta zimeingia katika malipo makubwa kwa sababu ile miradi ya awali haikulipwa inavyotakiwa. Kwa hiyo, mambo yanakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachoomba tulie kuongeza pesa, Serikali itusikie iongeze pesa hiyo, lakini isimamiwe inavyotakiwa ili miradi hii iweze kuleta matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nataka kusema ni kwamba katika mikoa mingine kwa mfano Mikoa ya Kagera, Mungu alikuwa ametujalia vijito vidogo vidogo ambavyo wanawake walikuwa wanavitumia kuchota maji, lakini vijito vyote hivyo vimekauka kwa sababu ya shughuli za kibinadamu katika hivyo vyanzo vidogo

vidogo. Hii hali inapotokea, wanasiasa wananyamaza hasa katika ngazi ya Halmashauri. Hata ile Wizara inayohusika na Mazingira haichukui hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake, ile mito midogo midogo iliyokuwa inatiririsha maji mazuri ambayo watu walikuwa wanatumia kabla ya kupewa haya maji ya bomba, kulikuwa na hiyo mito, lakini sasa hivi yote imekauka. Imekauka kwa sasabu hakuna juhudi maalum za kuelimisha Watanzania, watu wamejisahau na mara nyingi wanasiasa wanaogopa kuchukua hatua kwa sababu ya kufikiria kwamba labda hawatachaguliwa tena. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Maulid Mtulia, ambaye anachangia kwa dakika tano, wamegawana na Mheshimiwa Hamidu Bobali.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Dakika tano zimekwisha!

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami nipate fursa ya kuchangia katika Wizara hii nyeti sana ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzangu walivyolalamika na kuonesha kwamba bado tuna tatizo kubwa la maji, nami Dar es Salaam tatizo lipo; na ukingalia takwimu za Mheshimiwa Waziri, zinaonesha kwamba katika maji tumetoka asilimia 72 tumekwenda asilimia 75, lakini kwa masikitiko makubwa, sisi watu wa Dar es Salaam hatuna mbadala wa maji. Unapotupa maji asilimia 75 maana yake hii asilimia 25 nyingine tunaitoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna mito kusema kwamba tutakwenda kuteka maji kwenye mito, hatuna maziwa, hatuna visima. Kwa hiyo, maana yake kutoa maji

asilimia 75 Dar es Salaam ni kuwaambia wananchi wa Dar es Salaam asilimia 25 watumie maji machafu; na hata hivyo visima ukichimba havichimbiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Dar es Salaam kuna maeneo mengi hakuna maji. Mengi sana, Majimbo yote, Dar es Salaam yote; ukienda kwa kaka yangu Mheshimiwa Mnyika utakuta kuna maeneo mengi hakuna maji, ukienda kule Kigamboni hakuna maji, ukienda huku Kawe hakuna maji. Sasa sisi tuna tatizo hilo kubwa sana la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo lingine ambalo hatuwezi kulalamika sana ambalo ni tatizo la fedha na Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa wamechangia kwamba tuongeze tozo ya sh.50/=. Mimi bahati nzuri nipo kwenye Kamati ya Nishati na Madini na kama kuna jambo ambalo lina tozo kubwa, basi mafuta yana tozo kubwa sana. Sipingi kuongezwa sh.50/= lakini nataka nitoe njia mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hii Mamlaka yetu ya *EWURA* ambayo inasimamia tozo hizi za kwenye mafuta; na kuna vinasaba ambavyo tunavigharamia, lakini katika tozo la vinasaba kwa Tanzania tunafika mpaka shilingi sita na senti kidogo, lakini ukienda wenzetu wa Kenya na Uganda wana shilingi moja na shilingi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua teknolojia yawezekana ni ya juu sana kwa sababu sisi tunatumia *chemicals*, wenzetu wanatumia *marking* kwa maana wakati mwingine ni kubadilisha tu rangi ya mafuta, inajulikana kwamba haya yamechakachuliwa, haya hayajachakachuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali sasa wanapokwenda kukaa, watazame; wakati umefika sasa, ni bora kutumia teknolojia ambayo tunadhani itakuwa na gharama nafuu hata kama ubora wake utakuwa siyo sawa na ubora wa sasa ili isiwe tu kila tunapopata tatizo tunaongeza tozo la mafuta ambayo athari yake kimsingi ni

lazima itarudi kwa mwananchi. Huyu mwananchi tunataka kumkomboa ili apate maji, lakini huyo huyo tunamwongezea mzigo. Kwa sababu huduma zote mwananchi anazopata kijijini lazima atatumia mafuta. Hakiendi chochote lazima mafuta itatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, badala ya kutumia shilingi sita, tutumie zile shilingi mbili au shilingi moja ili sasa upungufu iwe ndiyo pesa ambayo tunaweza tukaitumia tukaingiza kwenye maji ili mwananchi asipate mzigo wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tuna tatizo la ukosefu wa maji na takwimu hapa ninazo. Ukiangalia vitabu vya Mheshimiwa Waziri, ameeleza hapa. Mwaka 2016 maji ilikuwa kila mwananchi anaweza kupata mita ya ujazo 1,952, lakini katika kitabu chake cha 2017 ameonesha kwamba inapungua mpaka 1,800. Ukiangalia 2025 inakadiriwa maji yatapungua mpaka *millimeter* 1,500.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Juliana Shonza, atafuatiwa na Mheshimiwa Desderius Mipata na Mheshimiwa Musa Ntimizi ajiandae. Mheshimiwa Mipata!

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nakushukuru wewe na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima. Naunga mkono watu wote wanaosema pesa za maji ziongezwe kwa sababu ya umuhimu wenyewe. Mimi kwangu nina matatizo katika miradi kadhaa inayoendelea. Jimboni kwangu kuna miradi ya maji ya vijiji 10. Mradi wa Kawa umetumia zaidi ya shilingi bilioni mbili na nusu, lakini maji hayajaanza kwenda kwa wananchi. Hii ni hasara kubwa. Kwa hiyo, wananchi hawaoni tija wala thamani ya pesa ambayo imetengwa kwao. Naomba Wizara isukume jambo hili liwezekane. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika kuna Mradi wa King'ombe. Katika mradi huu tumetumia zaidi ya shilingi milioni 720, lakini mradi huu bado una shida katika maeneo mbalimbali, hasa katika maeneo ambayo bomba lake liko juu. Naomba Serikali ihakikishe kwamba maeneo ambayo bomba linaonekana linakatwakatwa ovyo ovyo, waweke sehemu ile chuma ili huduma ya maji iwafikie kwa uhakika. Wananchi wote wanaohujumu, mimi nalaani vitendo hivyo na hatuwezi kuviunga mkono hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mradi wa siku nyingi sana wa maji kutoka Kate kwenda Isale, unapita Vijiji vya Ntemba, Kata, Ntuchi, Ifundwa na Msilihofu. Huu mradi ni muhimu sana, umekuwa ukiahidiwa na Maraisi wote wawili, akiwepo Jakaya Kikwete na huyu ambaye tupo naye kwenye madaraka sasa. Pesa zilitengwa zaidi ya sh.2,800,000,000/=. Naomba, sasa hivi Wilaya ya Nkasi mlitutengea pesa sasa hazionekani. Naomba mradi huu nao uanze kufanya kazi mara moja ili wananchi wa vijiji hivyo waweze kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile upo mradi wa Kijiji cha Kisura. Mradi huu nao umekuwa ukisuasua, una zaidi ya shilingi milioni 400. Naomba Wizara itoe msukumo wa kutosha katika jambo hili ili maji yaweze kupatikana. Vijiji vyote kwa ujumla kwa Kata ya Nkandasi, Kata ya Kipande na vile vile Kata ya Nsintali bado maji ni taabu kubwa sana. Naomba pia utafiti ufanywe katika maeneo haya ili maji yaweze kupatikana katika vijiji vinavyohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika mradi wa umwagiliaji. Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina Majimbo mawili; Jimbo la Nkasi Kusini na Nkasi Kaskazini. Miradi inayotajwa hapa kwenye umwagiliaji, yote miwili imekaa kwenye Jimbo moja. Jambo hili nimekuwa nikilizungumza kila wakati. Sisi kwenye Jimbo la Nkasi Kusini tulishabainisha uwepo wa Miradi ya Bonde la Mto la Kate na Bonde la Mtisi lililopo Kijiji cha Namansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa mapendekezo, tunaomba tu pesa za kuanza kujenga miundombinu, lakini sijawahi kupata hata wakati mmoja. Naomba ufike wakati haki itendeke. Maana yake, ninapimwaje mimi? Tupo Jimbo moja lakini miradi ipo sehemu mbili, inapata pesa lakini iliyopendekezwa upande wa pili haipati pesa. Naomba na hilo mliangalie kwa umakini sana ili kutujengea pia siasa nzuri. Bila kufanya hivyo, maana yake tutakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yote yaliyokwifanywa na Halmashauri, kinachotakiwa sasa ni kuomba pesa ili miundombinu ianze kujengwa hasa katika bonde hili la Kate ambalo kwa kweli ni kubwa la kutosha na linaweza kuzalisha chakula ambacho kitakuwa ni msaada mkubwa sana, mkijua kwamba mazingira yetu sisi Mkoa wa Rukwa ni wazalishaji wazuri sana wa chakula.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa anayefuata kuchangia ni Mheshimiwa Salma Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, hatimaye nikushukuru wewe kwa kuniona na kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza sana Mawaziri wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. Sambamba na hilo, naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri ambayo

anaifanya. Kikubwa zaidi, niipongeze Serikali kwa kipaumbele ambacho imeweka kwenye Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naomba niwape pole Watanzania wote kwa matatizo ambayo yametokea nchini kwetu na siyo matatizo mengine bali ni matatizo haya ya mvua ambayo ipo kila kona na yameweza kuathiri maisha ya wananchi wa Tanzania. Vile vile nirudie kutoa pole kwa watoto wetu ambao wamepoteza maisha wakati wakiwa kwenye harakati zao za masomo wakielekea huko kwa ajili ya kufanya mitihani ya kujipima wao wenyewe. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, maji ni utu, maji huleta heshima na ustawi kwenye familia; lakini siyo familia pekee, bali na jamii kwa ujumla. Kwa mantiki hiyo, tunaamini kwamba Tanzania ina changamoto kwenye eneo hili la maji. Kila mtu kwa njia moja au nyingine anaguswa na changamoto hii ya maji, iwe ni wa mjini iwe ni wa kijijini anaguswa na changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi changamoto hii inamgusa mwanamke, kwa sababu mwanamke ndiye mtafutaji wa maji katika familia. Kama nyumbani hakuna maji, mwanamke hawezi kukaa kitako; lazima atoke sehemu moja hadi nyingine kuhakikisha kwamba amepata maji ili maisha yaendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, tunaiomba Wizara ya Maji iongeze hiki kiwango, lakini kama siyo kuongeza, tuangalie vyanzo vingine ambavyo vitatusaidia kuongeza hii bajeti yetu ya maji. Kama Waheshimiwa Wabunge wengine waliotangulia walivyosema, tuchukue ile tozo ya sh.50/= tuongeze kwenye maji hatimaye tuwe na sh.100/=. Tukiweka sh.100/= itatusaidia kuongeza bajeti yetu. Kwa mantiki hiyo basi, ile bajeti ya mwaka 2016 ndiyo irejee na kuwa bajeti ya mwaka huu kwa taratibu zake zinazohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naelekea kwenye Jimbo letu la Lindi Mjini. Tatizo la maji kwenye Jimbo la Lindi Mjini ni kubwa, tena sana. Lindi Mjini hakuna maji, Lindi Mjini hali ni tete. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuja Lindi na akasema ifikapo tarehe 3 Julai, lazima tuhakikishe kwamba maji yamepatikana. Serikali mtuambie, je, maji yatapatikana au hayatapatikana? Tunasubiri kauli ya Serikali ili mwanamke huyu tumtue mzigo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Muda wako umemalizika, tunashukuru.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Ha! Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba mengine niyaandike kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Elias Kwandikwa atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo ajiandae.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hii hoja muhimu ya maji. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema mawili tu kwa haraka haraka. Kwanza kikubwa ni kuishukuru Wizara kwa sababu Jimbo la Ushetu ni Jimbo ambalo liko katika Wilaya hii ya Kahama, lakini utaona kipindi kilipita tumekuwa na shida kubwa sana ya maji na kwenye bajeti hii ambayo tunaitekeleza niseme wananchi wa Ushetu wanashukuru kwamba tumekuwepo na miradi kwenye kata nane na katika kata tatu tayari wananchi wameanza kupata maji. Kwa hiyo, naishukuru sana na kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kata hizi za Idahina, Ukune, Chambo, Bulungwa, Nyamilangano, Kinamapula Kata ya Ushetu yenyewe na Kata ya Ulowa, tulitenga fedha mwaka 2016/2017, kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kukamilisha hii miradi ambayo inaendelea ili wananchi waendeleo kunufaika na kuachana na adha ya ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka nizungumzie, wananchi wa Ushetu wanahitaji maji ya Ziwa Victoria. Kama nilivyosema kipindi kilichopita, Jimbo la Ushetu linachukua eneo la asilimia 57 ya Wilaya ya Kahama, lakini maji ya mradi wa Ziwa Victoria yamefika Kahama Mjini, lakini maji haya hayajasambazwa Ushetu. Wananchi wa Ushetu wanaomba maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu wataalam wa Wizara wako hapa, nikumbushe, kulikuwa kuna maombi ya maji mwaka 2014, tuliahidiwa kwamba Mkandarasi Mshauri angeenda kwa ajili ya kusanifu ili maji yaende Ushetu. Sasa mradi uliishia njiani. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie ili tuweze kupata maji katika Kata za Ukune, Kisuke, Nyamilangano, Uyogo, Ushetu na Ulowa; na kuna vijiji vipatavyo 32. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia kwenye mradi wa maji ambao utakuwa ukipitia kwa majirani zetu katika Halmashauri ya Mbogwe, sehemu ya Masumbwe, tunaweza pia tukapeleka maji kwenye Kata za Idahina, Igwamanoni, Nyankende ambako kuna vijiji 40 vinaweza kunufaika. Kwa sababu lengo la Wizara au la Serikali ni kuhakikisha kwamba mwaka 2020 tunaweza kuwa na maji vijijini kwa asilimia 85. Kama hatupati maji ya Ziwa Victoria itakuwa ni ndoto. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali izingatie hili na nimefanya mazungumzo na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji namshukuru sana na naamini yale tuliyokubaliana kwa ajili ya kutusaidia Ushetu ataweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu nizungumze juu ya ubora wa *report* za miradi. Waheshimiwa Wabunge

wengi hapa wamekuwa wakizungumza wanaona kwamba miradi inajirudia, lakini utagundua kwamba ile *reporting system* yetu tuiangalie vizuri, Wizara ya Fedha isaidie kwamba twende kwenye *IPSAS accrual* ili tuweze kupata *report* ambazo zitakuwa zinaleta maana. Kwa maana ya mchanganyiko wa *cash basis* na *accruals* inatuchanganya sana. Kwa mfano utaona kwa upande wa Halmashauri ya Ushetu tumepokea fedha shilingi bilioni 506 lakini haiwezi kueleweka mapema kwamba hizi fedha zilikuwa zimetengwa mwaka upi wa fedha. Kwa hiyo tukienda vizuri kwenye hizi *report* itaweza ku-*report* miradi yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri tu Wizara ya Fedha isaidie sana ili hizi *report* za miradi ziende kwenye ile *reporting system* ambayo nafikiri itakuwa ni nzuri zaidi ili kututoa katika mchanganyiko ambao tunaweza kukanganyikiwa zaidi. Kwa hiyo, nafikiria niseme hili, kwa sababu nimeona maeneo mengi sana yamekuwa yakituchanganya; tukienda kwenye *accrual* ziko faida nyingi. Hii itaweza pia kutusaidia kuoanisha bajeti na matumizi kwa kipindi husika. Kwa hali ilivyo sasa hivi mchanganyiko unakuwa ni mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda nishauri kwamba, tume-*adopt accrual basis of accounting*, kwa hiyo, nafikiri Serikali isukume sana ili zoezi likamilike, itatusaidia sana kuweza kupata *report* zenye ubora zaidi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bashungwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajiandae.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii muhimu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Magufuli na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendelea kuchapa kazi ya kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kujenga uchumi wa viwanda unaendana sambamba na kuboresha huduma za jamii ikiwemo kuhakikisha tunapata maji safi na salama kwa kila Mtanzania. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri na hizi jitihada.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri, wanafanya kazi nzuri, ni wasikivu na kwa kweli nawapongeza kwa kuleta mpango mzuri wa bajeti kwa ajili ya mwaka 2017/2018. Niwape moyo kwa sababu katika bajeti iliyopita hata wenzetu wa Upinzani walikuwa wanasema tuwe tuna *realistic budget*. Sasa Wizara imeleta bajeti ambayo inatekelezeka na badala yake wenzetu wanasema kwamba iongezwe na wakati hao hao mwaka 2016 walikuwa wanasema tunaleta bajeti ambazo ziko *ambitious*, tuzi-*reduce* ziwe *realistic*. Sasa bajeti imekuja *realistic* lakini bado unaona wanapinga. Kwa hiyo, mpinzani ni mpinzani. Kwa hiyo, niwape moyo, Serikali chapeni kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeze Kamati ya Maji ya Bunge kwa kuleta hoja ya kuongeza tozo kwenye Mfuko wa Maji. Nawapongeza sana kwa sababu ni muda muafaka kuleta hiyo hoja ili tuweze kuiunga mkono. Nashukuru Waheshimiwa Wabunge wengi wameunga mkono hoja, kwa sababu ukiangalia fedha kutoka kwa wahisani zinazidi kupungua, kwa hiyo, lazima kama nchi tuhakikishe tunaweka utaratibu wa kutoa huduma muhimu kama huduma ya maji kwa Watanzania kwa kutegemea fedha za ndani. Kwa hiyo, naishukuru sana Kamati ya Maji ya Bunge kwa kuleta hii hoja, naomba tuiunge mkono na naamini Serikali ni sikivu, itaichukua na kuifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hoja hii inatekelezeka kwa sababu tayari tuna uzoefu kwa upande REA. REA tulivyoitengea mfuko, unaona sasa hivi yale matumaini ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya umeme, yanatekelezeka. Kwa hiyo, tukifanya hivyo kwenye upande wa maji, naamini kabisa tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa niende Jimboni. Naishukuru sana Serikali; namshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa Mradi wa maji wa Rwakajunju kwa kutenga Dola milioni 30 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu ambao tumeusubiri sana Karagwe. Naishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha Dola milioni 30, lakini naomba sana sasa twende kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2016/2017 fedha hii pia ilikuwa imewekwa lakini mchakato ulichukua muda. Kwa hiyo, naiomba Serikali tuweke jitihada ili wana Karagwe tuwatue akina mama ndoo vichwani na watoto wetu ili tuweze kutumia muda huu kufanya kazi za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu wa Rwakajunju napenda kuiomba sana Wizara izingatie vile vijiji ambavyo vinatoa haya maji vinavyopakana na Ziwa Rwakajunju. Kuna kijiji cha Kafunjo,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Mheshimiwa Hassan Masala, ajiandae.



**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nami kwa kuniona. Kabla ya yote nimponze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi wanazozifanya. Hongereni sana, endeleeni kuchapa kazi. Tunajua mna kazi kubwa lakini kazi mnayoifanya nayo ni kubwa, Watendaji wenu wa Wizara tunawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuweza kumteua Katibu Mkuu Profesa Kitila ambaye anatokea *ACT*. Nataka kuwaambia Wapinzani, ukionekana unafaa kwenye CCM kazi utafanya. Usikate tamAa, Bwana Kitila fanya kazi na nina imani wale watakupa ushirikiano mzuri ili utekeleze Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, kwanza kuna ndugu yangu mmoja, Mheshimiwa Kangi Lugola, simwoni hapa, jana alisema watakaopitisha hii bajeti ataenda kupiga miluzi nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Mheshimiwa Kangi Lugola ana shibe. Pale Jimboni kwake Mwibara maji yako hatua tano. Anaweza kuamua kuvua samaki wa saa nne, wa saa nane, wa saa tisa; ni kama kata mbili hazina maji. Yeye maji yamemzunguka. Ila namshauri, akitaka kupiga miluzi, apige kule Mwibara, akivuka geti sisi kwenye Chama tutamdhiti. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ku-*declare interest*, mimi kabla ya kuwa Mbunge nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya *DAWASA*. Waheshimiwa Wabunge, mliochangia naomba nikwambieni wazi, tunaweza tukachangia lakini hujaingia ndani ya nyumba kujua kuna nini? *DAWASA* imeundwa kwa mujibu wa Sheria; *DAWASCO* anakasimiwa Mamlaka na *DAWASA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inaonesha, huko nyuma tulikuwa na kitu kinaitwa *NUWA*. Tukaiondoa *NUWA* kupunguza mzigo, ikaja *City Water* na *DAWASA*. *City Water*

akafeli, alivyoondoka *DAWASCO* akapewa nafasi hiyo ili aichukue kwa mkataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo yanasemwa hapa, kwamba nani mzuri? Haiwezekani mwenye nyumba akawa sio mzuri, mpangaji akawa mzuri. Sisi wote tunaishi Dar es Salaam, kazi kubwa aliyonayo *DAWASCO* ni kukusanya kutengeneza matengenezo madogo, akishapata zile bili kutoka kwa watu, anapata pesa; lakini anayetengeneza miundombinu ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, anaitwa *DAWASA*. Kwa hiyo, haiwezekani mtu akatengeneza miundombinu, wewe ukakusanya pesa, ukaonekana uko vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara na Serikali yangu, hebu tuwe makini. Msemaji wa saa hivi amesema, anaipongeza *REA* na *TANESCO*. Kwa nini imetoka *TANESCO* tukaenda *REA*? Kwa nini? Unaipunguzia mzigo *TANESCO*; *REA* imepatikana, inafanya kazi zake vizuri. Leo mna mpango wa kuiunganisha, naomba Wizara muwe makini sana, tusije tukarudi tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo *TANROAD* ipo kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi. Kwa nini hatusemi Wizara ya Ujenzi iende ijenge? Leo tunataka kuanzisha Mfuko wa Maji Vijijini, kwa nini tunauanzisha mfuko? Suala hili ni kumwondolea mtu mzigo mkubwa ili angalau wafanye wengi, ufanisi uweze kupatikana. Leo kwa Dar es Salaam ufanisi upo. Maji yanatosha, *DAWASCO* wapo, *DAWASA* wapo, hili neno linatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, wazo lenu labda ni zuri sana, lakini mrudi kwenye historia, kwa nini tulitoka huko na tukafika hapa? Kama hatukwenda vizuri, tunataka kuanzisha mgogoro mpya katika Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam leo limepanuka, lilikuwa na Wilaya tatu, leo lina Wilaya tano; watu wameongezeka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleee tena niseme, kwa sababu ukienda kwa *DAWASA* leo, ndani ya Ilani yangu ya

Chama cha Mpinduzi tumesema katika ukurasa wa 106 kwamba tutajenga bwawa la Kidunda. Ni *DAWASA* hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna tatizo la *TANESCO* kukata umeme kwenye Mamlaka za Maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MBUNGE FULANI:** Dakika moja.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini wananchi hawadaiwi, anakuwa anadaiwa Mamlaka za Maji; sasa mkikata maji kule *TANESCO* mnawaumiza wananchi kwenye miji!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani ujumbe utakuwa umewafikia wahusika.

Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Masala na Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama ajandae.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Sikuisema vizuri?

**MBUNGE FULANI:** Hongera!

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dakika ni chache sana, nami nichukue fursa hii kuwatakia pole Watanzania wote ambao wamekubwa na majanga mbalimbali hususan ya watoto wetu kule Arusha; lakini pia Watanzania wote kule Rufiji ambao wamekumbwa na matatizo mbalimbali ya ujambazi ambayo niseme tu kwa hali ya kawaida, tatizo hilo la ujambazi limeacha wajane wengi na watoto wengi yatima. Naliomba Bunge lako wakati mwingine tunapochangia

kwenye mambo ya sherehe, basi mnikumbuke kule Rufiji, mnifikirie kwani nina wajane wengi na watoto yatima wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo pia kutoa pole kwa wale wote waliokumbwa na mafuriko makubwa kule Rufiji hususan Kata yangu hii ya Mohoro, kwa kina Chii kule mpaka kwa mzee Mikindo, Kata ya Mwasemi, Kipugila, Ikwiriri, Umwe, Mgomba, Ngarambe pamoja na Chemchem.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe watu wa Rufiji msemu mmoja katika *Quran* unaosema kwamba *kullama yuswiibana, illamaa qataba Allah lana*, ikimaanisha kwamba *nothing will happen to us, except what Allah has decreed for us*. Hakuna linaloweza kutokea mpaka pale ambapo Mwenyezi Mungu amelipanga litokee baina yetu. Mwenyezi Mungu ametuandikia kila jambo litakalotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendeleo kuwatia moyo wananchi wangu wa Rufiji wasibabaike na jambo linaloendelea na hili ni tatizo la amani, waendeleo kuijenga nchi yao, kwani Tanzania hii ni ya kwetu sote nasi tutaendeleo kuwapigania huku katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini pia wale ambao wamesoma vitabu mbalimbali watakumbuka kitabu cha "*Comperative Government and Politics*," watatambua ni namna gani Mheshimiwa Rais ataweza kulisaidia Taifa hili hapo mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nampongeza sana na tuseme tu kwamba nchi hii inamhitaji sana. Mabadiliko makubwa katika nchi kama Bangladesh ambao wameweza kubadilika kwa kipindi cha miaka 10, tunaamini kabisa kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli anaweza kuivusha Tanzania kutoka hapa ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi ya kuzungumza, lakini niseme kwa uchache tu kwamba suala hili la maji limezungumzwa katika Ilani yetu ya Uchaguzi. Ukiangalia Ilani yetu ya Uchaguzi; Serikali imeundwa na Chama cha Mapinduzi na utekelezaji ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Pia tunaongozwa na Kanuni za Uongozi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa mujibu wa Ilani, katika ukurasa wa nne wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, inasisitiza Serikali kufanya yale yote yanayoletwa ndani ya Serikali kwani ni yale ambayo yanaongozwa na Ilani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 66 wa Ilani yetu ya Uchaguzi inasisitiza katika kusogeza huduma za kijamii karibu na kwa wananchi. Suala la maji safi na salama limezungumzwa katika ukurasa wa 83 wa Ilani, nami nataka nijikite katika ukurasa wa 85 wa Ilani yetu ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo imedhamiria kutua ndoo kichwani kwa mwanamke. Niseme tu kwamba kwa mujibu wa ukurasa 85, Ilani imedhamiria kuongeza asilimia 53 ya maji vijijini mpaka kufikia asilimia 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, kule kwangu Rufiji niliwahi kufanya ziara katika kijiji kimoja pale Kikobo. Wananchi wa Kikobo wamehama kijiji kile kwa sababu ya tatizo la maji na walichonieleza ni kwamba kule Dar es Salaam ukiwa na pesa kidogo unaonekana unatoka kipara kichwani, lakini akinamama wa eneo la Kikobo wanatoka vipara kwa sababu ya kubeba ndoo kwa muda mrefu. Wanasafiri na maji kwa zaidi ya kilometa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo hili ni kubwa sana kwa nchi yetu, nami niseme tu kwamba sisi tulishaanza utekelezaji wa Ilani. Mimi binafsi nilishaanza uchimbaji wa visima mbalimbali katika eneo langu, yale maeneo korofi kabisa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechimba visima katika Kata ya Mgomba Kusini, Mgomba Kati, Ikwiriri Kati, Nambanje, Mpalange, Mtanange tunakwenda kuchimba

pamoja na Mpima; lakini pia Mpalange kwa Njiwa kote tunakwenda kupeleka visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo korofi ambayo tunaamini kabisa Serikali ikiweza kutusaidia, tutaweza kutatua kero ya maji. Hapa nazungumzia katika Kata ya Chumbi, hususan katika Kijiji cha Nyakipande, pamoja na Miangalaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa, napenda niwapongeze watani wangu hawa wawili kwa kazi nzuri wanayoifanya.

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Dah!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja pamoja na marekebisho yatakayofanywa na Wizara. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hassan Masala atafuatiwa na Mheshimiwa Leonidas Tutbert Gama na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kuniona. Bila kupoteza muda naomba pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu zetu ambao wamepoteza wapendwa wetu kule Mkoani Arusha. Pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naungana na kaka yangu kiongozi wangu Mzee Bulembo kumpongeza

Mheshimiwa Rais kwa kumchagua Profesa Kitila, Mwalimu wangu. Naomba nimtakie kazi njema ya kututumikia Watanzania, naamini hutotuangusha katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika mambo machache yanayohusu eneo la Jimbo langu la Nachingwea. Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa nyakati tofauti wamefika katika Jimbo la Nachingwea, wameona hali ya upatikanaji wa maji katika vijiji vya Jimbo la Nachingwea. Hapa kuna mradi mkubwa wa Mbwinji ambao unahudumia Wilaya ya Masasi, Wilaya ya Nachingwea pamoja na Wilaya ya Rwangwa.

Mheshimia Naibu Spika, iko ahadi, vile vile iko fedha ambayo mwaka 2016 tulitengewa kwa ajili ya kusambaza maji katika vijiji ambavyo viko umbali wa kilomita tano. Naomba kupitia nafasi hii, niwakumbushe juu ya hali ya upatikanaji wa maji katika vijiji vinavyozunguka Jimbo la Nachingwea. Tafadhali sana naomba wayafanyie kazi maombi ambayo tayari yako katika ofisi yao kwa ajili ya kutoa fedha ambayo tayari ilishapitishwa katika bajeti iliyopita ili tuweze kuwapa wananchi maji ya uhakika na maji salama ambapo wamekuwa wanapata shida kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Naipanga, Mkotokwiana, maeneo ya Chemchem, ni maeneo ambayo wanaathirika kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, utekelezaji wowote utakaofanyika, basi tutakuwa kweli tumekwenda kuwatua mama zetu ndoo kichwani kwa ajili ya kuwapunguzia adha wanayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala la ulipaji wa bili za umeme. Ndani ya Wilaya yangu ya Nachingwea, zaidi ya wiki mbili tumekaa bila kupata maji kwa sababu ya umeme, ambapo kimsingi siyo kosa la wananchi. Wananchi wanalipa bili zao, lakini

wamelazimika kukaa bila maji kwa sababu tu Wizara imeshindwa kulipia bili ambazo kimsingi wananchi hawahusiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima kwamba jambo hili kwa kweli tusingependa lijurudie kwa sababu tunawapa adhabu wananchi ambao wao wanatimiza wajibu wao wakulipia bili zao za maji. Kwa Wilaya ya Nachingwea peke yake kupitia *MANAWASA*, zaidi ya shilingi milioni 100 zinatakiwa zilipwe. Kwa hiyo, naomba tafadhali hiyo fedha ilipwe ili wananchi wa Jimbo la Nachingwea waweze kupata maji ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri wa Maji, kupitia Naibu Waziri ambaye alishakuja Jimboni Nachingwea, alikuja katika Kijiji cha Chiola, nafikiri anakumbuka ule mradi; na kuna ahadi ambayo aliitoa na wale wananchi wananiulizia: Ni lini utekelezaji wa yale ambayo tayari aliyaahidi pale ya kuleta wataalam kuja kuchunguza ule mradi? Ni lini tutakwenda kuukamilisha? Sina majibu, namwomba mzee wangu kwa sababu tumefanya kazi nzuri katika Jimbo hili, tafadhali sana anisaidie ili wale wananchi waweze kupata maji ya uhakika na maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo nataka nilizungumzie ni suala la Miradi ya Umwagiliaji. Katika Jimbo la Nachingwea, tunayo miradi miwili; tunao Mradi wa Matekwe, huu ulishapewa fedha kipindi cha nyuma zaidi ya shilingi milioni 500, lakini mpaka sasa hivi mradi huu sijauona hata kwenye kitabu unatajwa kwa namna yoyote; sijui kama umefutwa! Zile fedha zilizotolewa kama zimepotea, basi tunaomba tuelezwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masala muda wako umekwisha.



**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Hamidu Bobali ajiandae.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza, kwanza kabisa nianze kwa kushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki hii ndiyo nimeingia Bungeni baada ya kuwa kwenye matibabu nchini India kwa muda wa zaidi ya mwezi mmoja. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia matibabu mema, afya njema na sasa kurudi salama. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashukuru sana Uongozi wa Spika, Naibu Spika, Katibu wa Bunge, pamoja na timu nzima ya Watumishi wa Bunge kwa huduma nzuri walizotupatia za kwenda matibabu India na kurudi salama. Mwisho, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali maombi ambayo vile vile yalipitia Wizara ya Afya, yalipitia pia kwa wataalam kutoka Hospitali ya Taifa, Muhimbili ya kunipa kibali kwenda kupata matibabu na sasa nathibitisha kwamba nimerudi salama na niko tayari kuitumikia nchi yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifanye kazi moja ya kuwaomba Waheshimiwa Wabunge; pamoja na maombi yenu ya kuniombea, nataka nishauri Waheshimiwa Wabunge wote tujenge tabia ya ku-*check* afya zetu, kwa sababu ni kweli ukinitazama nilivyo, huwezi kuamini kama afya yangu ilitetereka, lakini ni kwa sababu ya kujenga tabia ya kuangalia afya yako, wataalam wanaweza kukwambia bwana wewe unajiona mzima, lakini sio mzima. Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii niwaombe Wabunge wote tujenge tabia hiyo ili kuhakikisha afya zetu zipo katika mazingira mazuri zaidi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba nichukue nafasi hii niunge mkono juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yangu ya Awamu ya Tano chini ya Rais wetu mpendwa, Dkt. John Pombe Magufuli na Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Maji. Kazi inayofanywa na Serikali ni nzuri sana, inatia moyo na inaonesha dhahiri kwamba tunakokwenda inaelekea tunakwenda vizuri. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri; kazi yao wanayoifanya ni nzuri sana, tunawapongeza, tunaomba waendeleo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kidogo upande wa maji hasa kwa upande wa Wilayani kwangu. Wilayani Songea nina Kata 21. Katika Kata 21 kuna *SOUWASA* wanahudumia Kata 11 na Kata 10 zinahudumiwa na Halmashauri, ukiangalia mazingira ya Songea huwezi kutazamia kwa nini tuwe na tatizo la maji? Kwa sababu tuna mito ya kutosha, tuna mabonde ya kutosha, hali nzuri ya hewa na mvua ya kutosha. Kwa hiyo, maana yake naiomba sana Wizara ya Maji, hebu tujipange vizuri tuone namna gani tunaweza kuboresha huduma za maji katika Mji wa Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Halmashauri inatoa asilimia 46 tu ya kiwango cha maji kinachotakiwa kwa wananchi wa Songea, lakini wenzangu wa *SOUWASA* walijenga bwawa kubwa kwa ajili ya kukusanya maji, kwa ajili ya kuhudumia Mji wa Songea. Lile bwawa bahati nzuri limekamilika, lakini mpaka sasa kuna watu wanadai fidia zaidi ya miaka sita hawajapata fidia zao, naomba Wizara iniambie kuna mpango gani wa kuwalipa fidia hawa wananchi ambao wametoa maeneo yao na kuwezesha kuweka bwawa la maji na hivi sasa bwawa lile limeshaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli siyo busara kwa watu ambao wametoa eneo ambalo linachangia huduma za maji Mjini Songea, lakini hawapati haki yao waliyostahili. Naomba Wizara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, atafuatia Mheshimiwa Hamidu Bobali.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba niendelee kama walipoanzia wenzangu kupongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu katika kuhakikisha kwamba matatizo ya maji Chalinze yanafikia mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kupata nafasi ya kukutana na Mheshimiwa Rais, tukazungumza naye na kumweleza juu ya tatizo kubwa wanalopata wananchi wangu wa Jimbo la Chalinze. Alimwagiza Waziri Mkuu na Waziri Mkuu alikuja, alipofika katika kile chanzo chetu cha Wami, aliyoyaona, mwenyewe anayajua. Mheshimiwa Waziri alikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu ninaposimama leo hii, nataka nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba katika kipindi kile ambacho tulimpa yule Mkandarasi pale, sasa zimebaki wiki mbili na nusu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anasimama, napendelea wananchi wa Chalinze wamsikie, anasemaje juu ya yule Mkandarasi na Wizara inajipangaje sasa kutoa maelekezo mapya baada ya kuonekana kwamba kazi ile inasua sua?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri jambo. Kwenye suala la maji katika Jimbo la Chalinze anajua kwamba, kuna viwanda ambavyo vinaendelea kujengwa sasa, lakini viwanda vile vinaweza kupata matatizo ya kuanza

kutokana na kukosekana kwa maji. Mimi kama Mbunge nilifanya *initiative* za kuzungumza na wawekezaji wenzetu wa *Trifod* na Bwana Shubash Patel wakakubali kutoa vifaa kwa ajili ya kusaidiana na *CHALIWASA* chini ya *Engineer* wetu Christa Msomba ili kuhakikisha kwamba pale kwenye chanzo chetu wakati ninyi Serikali mnajipanga, wao wawekezaji wako tayari kuja kusaidia kuweka miundombinu vizuri. Inaonekana kwa upande wa ma-*engineer* au Wizarani kumekuwa na utata kidogo katika kutoa ruhusa ya wao kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, uko msemu kule kwetu Pwani wanasema, “anapokuja mgeni, basi mwenyeji ndio anapata nafuu au anapona.” Hawa wawekezaji wanataka kumsaidia kazi ya kuweza kujenga chanzo pale, wakati yeye yuko Bungeni hapa anaomba pesa kwa ajili ya kuweza kujenga miundombinu. Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa jicho la karibu sana. Wananchi wa Chalinze hawahitaji siasa, wanataka maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, liko jambo la mabwawa. Wananchi wa Chalinze wameahidiwa mabwawa hasa wale wanaotoka katika Kata ya Kibindu. Kuna bwawa tuliahidiwa na Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe kwamba atatujengea bwawa kubwa na wananchi wa Kibindu wataondoka katika taabu kubwa ya maji wanayoikabili. Kule Mjembe walitoa eneo pamoja na wananchi wa Gole, lakini mpaka leo ninapozungumza Mheshimiwa Waziri, hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kitabu cha hotuba ya bajeti hapa, nayo ameelekeza kwamba atajenga mabwawa mengi, lakini cha kusikitisha zaidi bwawa lile la Mjembe Gole limepotea hewani, silioni humu ndani na sijui tunaelekea wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri Mheshimiwa Maghembe yuko humu ndani, kwa hiyo, akimwuliza anaweza kumthibitisha hilo na akampa maelekezo ni jinsi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, nitoe ushauri pia katika eneo la mabwawa. Tunaona maji mengi sana yanayopotea, tunaona maji mengi sana ambayo yanaingia baharini ambayo sisi kama Taifa tumeshindwa kuyatumia kwa ajili ya manufaa ya walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Waziri, nimeona humu ndani ametenga fedha kwa ajili ya Bwawa la Kidunda, lakini tunatambua aliwahi kusema mzee wetu mstaafu Alhaj Ali Hassani Mwinyi, Rais wetu aliyemaliza muda wake, kwamba kupanga ni kuchagua. Natambua kwamba katika bajeti hii hajapanga lolote kuhusiana na ujenzi wa mabwawa zaidi ya lile la Kidunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri, yale maji yanayopita pale Ruvu kwenye Kituo chetu kinachozalisha maji kwa ajili ya wanywaji wa Dar es Salaam, yanakwenda yanamwagika baharini; nimeshuhudia juzi nikiwa kwenye ndege wakati nakuja Dodoma, maji mengi yametapakaa katika bonde lile, hata wananchi wa Bagamoyo wanashindwa kwenda mashambani. Jawabu lake ni kutengeneza bwawa lingine ambalo linaweza likazalisha maji mengi na likapeleka maji hata katika maeneo ya Miji kama ya Pangani hata kule Tanga Mjini ambapo wajomba zangu nao wanalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niongee juu ya jambo kubwa la kukatika kwa umeme. Wengi wameyasilimulia hayo, lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, ndani ya Halmashauri ya Chalinze, *CHALIWASA* wananchi wanalipia maji, isipokuwa kuna tatizo kwa upande wa Serikali kupe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nianze kwa kusema kwamba katika hotuba ya Kambi ya Upinzani niliweka utafiti kadhaa uliofanywa na TWaweza na sisi tunawaamini TWaweza kwamba ni Taasisi iliyosajiliwa na inachokifanya nadhani Serikali wanajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kwamba tumeendelea kurudia kosa ambalo mwaka 2016 tulilifanya la kuendelea kutenga fedha nyingi za nje tukitegemea kwamba tuzipeleke kwenye miradi ya maji vijijini, fedha ambazo hazitoki. Ukisoma randama, inaonyesha kwamba katika hizi shilingi bilioni 623 za maendeleo zilizotengwa mwaka huu, shilingi bilioni 214 zinategemewa kuwa ni fedha za wahisani. Kwa bahati mbaya, kati ya hizo 214 shilingi bilioni 130 zinakwenda kwenye miradi ya maji vijijini. Wasiwasi wangu ni kwamba, tutaendelea kufanya kosa lile lile, Waheshimiwa Wabunge watakuja hapa mwakani kulalamika kwa sababu fedha hizi hazitatoka na miradi ya maji vijijini itakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazungumzaji waliopita wamesema, kwamba kulikuwa na haja leo Mheshimiwa Waziri wa Fedha awepo, namwona Naibu Waziri wa Fedha yupo. Atakapokuja kuchangia aseme, kwa nini fedha za mwaka 2016 za Wahisani hazikutoka? Unakuta mradi ambao Wahisani waliahidi shilingi bilioni 41 wametoa shilingi bilioni moja; ni kana kwamba wanatutania, huu ni mzaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili lazima tuliweke wazi, kwamba hizi fedha shilingi bilioni 214 za Wahisani ambazo mnazitegemea, ni fedha ambazo mimi naziona kama kiini macho, sizitegemei kupatikana. Lazima Serikali ije na maelezo, kwa nini fedha za Wahisani hazitoki? Isiwe tunaishia tu kwamba tunapanga tunazitumaini shilingi bilioni 200 zitakuja, halafu hazitoki na Serikali haiji na maelezo kwamba kwa nini hatukupata fedha kutoka kwa Wahisani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwamba sh.50/= iongezeke ili fedha za Mfuko wa Maji uweze kuongezeka. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji, tumetembelea miradi mingi. Hizi fedha asilimia 19.8 zinazosemwa, kati ya hizo, zaidi ya 8% mpaka 9% ni fedha za Mfuko wa Maji. Kwa hiyo, kama siyo Mfuko wa Maji kuwa na fedha, leo tungekuwa tunazungumza chini ya asilimia 10 ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii. Kwa hiyo, tunahitaji fedha iongezeke ili angalau mwakani bajeti iwe imetekelezwa kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie miradi ya skimu za umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri aje atueleze, kuna skimu nyingi nchi hii, karibu kila Halmashari. Zilianzishwa mwaka 2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017, fedha zimeliwa. Mfano mzuri ni Skimu ya Umwagiliaji Narunyuu pale Kiwalala kwenye Halmashauri yetu, shilingi milioni 600 imeliwa, halafu Mkandarasi anasema kwamba *Designer* alikosea. Kwa hiyo, hizi shilingi milioni 600 zimeliwa, nani ana-*compensate*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio hiki hakipo Lindi Vijijini tu, kipo karibu nchi nzima. Aje na maelezo, kuna miradi mingi na kwenye hotuba ya kambi tumeorodhoshwa. Aje atujibu kwa nini miradi ya umwagiliaji imetafuna fedha za Watanzania halafu imeishia katikati na hakuna maelezo? Atueleze, hao waliohusika na wizi huu wamewajibikaje? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie suala la Bonde la Rufiji. Nasikitika sana, leo nchi hii tunalia na njaa. Bonde la Rufiji lina maji *the whole season*. Ukipita pale unakutana na maji, yapo. Bonde liko zuri, kwa hiyo, katika kilimo cha mwagiliaji kwa nini hatulitumii? Leo tunalalamika kwamba tuna njaa, wenzetu, jirani zetu hapo *South Sudani* wana vita, wenzetu Wakenya wanahitaji chakula, Ethiopia wanataka chakula; tunashindwa kutumia chanzo ambacho tungeweza kukitumia kama pato letu la Taifa? Lingeongeza pato; lakini pia leo tusingekuwa na malalamiko kwamba chakula hakuna nchi hii. Tungekuwa na chakula ambacho tungeweza kusaidia hata Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba maelezo ya kina. Kwa nini bonde la Rufiji halitumiki? Sisi tunaopita pale kila siku kwenda Lindi na kurudi, tunajisikia aibu. Mwaka 2016 nilisema hapa, wale *RUBADA*; kitu kinachoitwa *RUBADA*, kama kuna watu wanaofilisi nchi hii, wale wanaongoza, kwa sababu hakuna wanachokifanya. Wako pale, sasa hivi wamekuwa kama madalali wa kuuzwa ardhi, madalali wa kuingiza mifugo; ng'ombe kuingia pale, hakuna zaidi ya hilo. Kwa hiyo, naomba maelezo ya kina juu ya suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mbogwe Mkoani Geita naomba kuelezea kuvunjwa moyo kwa hatua ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuliweka kando ombi letu la maji ya Ziwa Victoria kufikishwa Wilayani Mbogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumia muda wangu mwingi nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mbogwe kuiomba Wizara na kuelezea kwa undani kuhusu tatizo la muda mrefu la ukosefu wa maji hasa nyakati za kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kihistoria Wilaya ya Mbogwe ilikuwa ni sehemu ya Mkoa wa Shinyanga na Wilaya ya Kahama na kwamba Wilaya zote za uliokuwa Mkoa wa Shinyanga zimepatiwa maji ya Ziwa Victoria, mfano, Kahama, Shinyanga, Kishapu, Maswa, Bariadi na Meatu, ziko vizuri na sasa maji hayo yanapelekwa Mkoani Tabora. Sisi tunatengwa hasa baada ya Wilaya yetu ya Mbogwe kuhamishiwa Mkoani Geita.



Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mahitaji ya maji na suluhisho lake la kudumu hasa katika nyakati hizi mbaya za mabadiliko ya tabianchi. Licha ya kwamba kwa sasa maeneo yetu bado yana misitu na miti kiasi, lakini suala la uharibifu wa mazingira litasababisha ukame utakaosababisha uhaba wa maji na suluhisho la kudumu ni kupata maji kutoka Ziwa Victoria ambayo yako jirani kabisa katika Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwamini Mheshimiwa Waziri Lwenge na Naibu wake Mheshimiwa Kamwelwe kutokana na ahadi ambazo wamekuwa wakiwapatia wananchi wa Wilaya ya Mbogwe kuwa ipo siku maji ya Ziwa Victoria yatafika Wilayani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, nimevunjika moyo baada ya kuipitia na kuisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuona ndoto ya maji ya Ziwa Victoria imeyeyuka na kupotelea mbali. Hata hivyo, bado nikiwa Mbunge, nitaiishi ndoto hiyo na kumwomba Mungu siku moja maji ya Ziwa Victoria yafikishwe Mbogwe tokea Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbogwe tunaomba maji ya Ziwa Vivtoria. Mungu ibariki Serikali ya Tanzania na Mungu ibariki Mbogwe na ombi letu la maji ya Ziwa Victoria lifike kwa Mwenyezi Mungu na limfikie Mheshimiwa Rais na Mawaziri wetu wa Maji, waiishi ndoto yetu ya kupata maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze mchango wangu kwa kuniwezesha kuchangia Wizara hii muhimu kwa ustawi wa wananchi wetu. Katika nchi yetu, tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama bado ni sugu sana. Hata hivyo, bado Serikali haijaonesha nia thabiti ya kupambana na janga hili. Ndiyo maana hadi leo katika bajeti ya Serikali haioneshi umuhimu wa Sekta ya Maji ingawa sera inamtaka mwananchi kupata maji kwa umbali wa mita 400, lakini hadi sasa kwenye

Halmashauri zetu tatizo la maji bado ni kubwa sana. Bajeti ya Wizara ya Maji haiwezi kujibu tatizo la maji nchini, kwani fedha zilizotengwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Umwagiliaji ni muhimu sana kwa Taifa letu kwa hivi sasa, kwani kilimo cha kutegemea mvua kimepitwa na wakati hasa ukizingatia hali ya mabadiliko ya tabianchi. Serikali bado haijaonesha umuhimu katika sekta hii, kwani miradi mingi ya skimu ya umwagiliaji haijapewa kipaumbele, ndiyo maana hata pale mradi unapotekelezwa chini ya kiwango, Serikali haioneshi nia ya kufuatilia hatma ya miradi mingi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, katika Wilaya ya Liwale kuna miradi mitatu ya umwagiliaji ambayo kati ya hiyo mradi wa Ngongowele umekufa kabisa japokuwa umeshatumia zaidi ya shilingi bilioni moja. Mradi huu sio watu wa Kanda wala Wizara walioonesha nia ya kujua hatma ya mradi huu na miwili iliyobaki bado nayo inasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Maji mgao wake bado ni wa kiupendeleo. Sijui ni vigezo gani vinatumika kugawa miradi inayofadhiliwa na mfuko huu. Mfano, katika Halmashauri yangu ya Liwale, sasa ni miaka miwili mfululizo fedha hizi hatujawahi kupewa katika mradi hata mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Liwale ni Wilaya ya zamani sana, lakini hali ya upatikanaji wa maji vijijini ni duni sana na wala sijaona juhudi za Serikali katika kukabiliana na shida hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kutafuta chanzo mbadala wa maji katika Mji wa Liwale uliokuwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, fedha kiasi cha shilingi milioni 200 zilitolewa mwaka 2014, lakini hadi leo mradi huu umekwama bila maelezo yoyote toka kwa wahusika. Fedha za mradi huu zinaendelea kutumika bila kufikia lengo la kutolewa kwake. Hali ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Liwale ni mbaya sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri aje Liwale

ajionee mwenyewe jinsi watu wa Liwale wanavyoteseka juu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye mgao wa fedha za Mfuko wa Maji nchini, miradi ya maji vijijini nayo inakumbwa na mgao usiozingatia haki katika kuwafikia wananchi wetu. Katika Jimbo la Liwale hadi leo miradi hii imekamilika katika vijiji vitano tu kati ya vijiji 79. Hii ni ile miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Je, ni vigezo gani vinatumika katika kugawa miradi hii? Katika kitabu cha bajeti, Liwale haijatajwa popote kuhusu miradi ya maji vijijini wala mjini.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumetokea kero kubwa ya maji kwa wananchi wengi wa mijini kufuatia madeni ya umeme. Manispaa ya Kigoma-Ujiji imehusika moja kwa moja na suala hili kufuatia deni la shilingi bilioni 1.2. Hivi sasa kuna Mradi mkubwa wa Maji Kigoma. Naishauri Serikali kwamba mradi huu tutumie umeme wa jua kuendeshea mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mradi ufanyiwe marekebisho hayo, kwani kutumia umeme wa *TANESCO* siyo endelevu, kwani gharama ni kubwa. Kuna wafadhili wengi sana wanaowekeza kwenye nishati jadidifu, tuzungumze nao ili miradi inayoendelea sasa itumie nishati mbadala. Suala hili niliongea mwaka 2016/2017. Naomba Serikali litazameni hili, undeni kikosi kazi cha kulitazama hili la umeme wa jua kuendesha miradi ya maji mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji inayoendelea au kupangwa, inahitaji *inputs* ambazo nyingi zinaagizwa kutoka nje. Serikali inataka kuendeleza viwanda, ni vema kufungamanisha miradi hii na dira ya maendeleo ya viwanda. Tutazame orodha ya miradi na vituo vinavyotakiwa vikiwemo mabomba, madawa na kadhalika. Kisha tuone namna ya kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha vifaa vinavyotakiwa kwenye miradi hii, hata ikibidi kuwapa *guarantee* sekta binafsi, tufanye hivi tuache kufanya miradi bila kutazama picha kubwa. Miradi

mikubwa ya maji yaweza kuchochea maendeleo makubwa ya viwanda, kuongeza ajira na kutokomeza umaskini. Tusifanye kazi kwa kutazama eneo moja, bali tuwe *multidisciplinary*.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tutafute tozo fulani kisha fedha hiyo izungushiwe (*Ring Fencing*) kama *REA*, vinginevyo tunajidanganya. Hali ya maji huko vijijini ni mbaya kuliko mnavyodhani. Ni aibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Nyakalura uliigharimu Serikali shilingi bilioni moja lakini mpaka leo hakuna maji. Harufu ya rushwa kwenye mradi huo iko wazi, chukueni hatua, wananchi wanalalamika. Mji wa Kabindi unakua kwa kasi na sasa idadi ni takriban 25,000, hakuna maji kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara hii kufanya kazi kubwa, naomba nichangie kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilolo haina tatizo la maji, bali ina tatizo kubwa la usambazaji wa maji. Wilaya ina Tarafa tatu; Kilolo: tatizo lipo Kata za Udekwa, Ukwega, Ng'uluwe na Idete. Mazombe: tatizo kubwa liko Ilula na lrole tatizo ni kubwa. Mahenge: hawa wanategemea sana kilimo cha umwagiliaji hivyo naomba Mheshimiwa Waziri atume timu toka Wizarani kwenda kuangalia tatizo kubwa ambalo lipo kwenye eneo hili. Mfano, Kata ya Mahenge kuna mabwawa ya umwagiliaji lakini changamoto ni idadi ya watu kwamba imeongezeka lakini *intake* zipo vile vile. Hivyo, ni bora timu yako ipite huko hasa katika vijiji vya Ilindi na Magana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Nyanzwa, hapa pia changamoto ni ongezeko la watu. Sasa bwawa leo linahitaji kupanuliwa na ahadi za viongozi, kama aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda alitoa ahadi ya kuboresha bwawa

hilo. Eneo hili pia hawana kabisa maji salama na safi ya kunywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ruaha Mbuyuni, pamoja na tatizo la udogo wa mabwawa lakini pia kuna matanki ya maji yamejengwa, lakini fedha za kuyasambaza maji hayo hakuna. Ombi langu kubwa ni kuomba Wizara hii itume timu kwenda katika eneo hili na kubaini malalamiko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu alitoa ahadi ya kumaliza tatizo la maji Ilula, wakati wa kampeni. Sasa Mheshimiwa Rais anatarajia kwenda kuwashukuru wananchi hao, sasa wananchi lazima watampokea Mheshimiwa Rais kwa mabango, kwani bado tatizo lipo.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Sanjo ina vijiji 24 na wananchi 120,000. Ina hali mbaya sana, haina hata bwawa wala mito, lakini imezungukwa na Ziwa Victoria. Maji yanatakiwa yatoke Lutale ambapo ndiyo chanzo, yaende Vijiji vya Kageye, Kayenze, Itandula, Langi, Makamba, Shilingwa, Kongolo, Chabula, Bugando, Nyashiwe, Ihayabuyaga, Welamasonga, Matale, Sese, Ihushi, Isangijo, Busekwa, Bujora, Kisesa, Kanyama, Wita, Welamasonga na Igekemaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Ndagalu ina vijiji 26 wakazi 86,000. Tarafa hii haina hata mto wala bwawa sasa wanafuata maji kilometa hadi 58. Tunaomba watu hawa muwaonee huruma, chanzo cha maji kitoke Nsola kwenda Misungwi, Kitongo, Lumeji, Nyang'hanga, Iseni, Mwamibanga, Buhumbi, Nyashoshi, Ng'haya, Mwabulenga, Nkungulu, Kayenze 'B', Chandulu, Bugatu, Salama, Kabila, Ng'wamagoli, Jinjimili, Nhobola, Kabale, Nyasato, Mahaha, Shishani, Isolo, Igombe, Ndagalu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa hii ya Ndagalu hata visima virefu havipo. Naomba tusaidiwe hata kwa dharura

visima virefu kila kijiji pamoja na bwawa la Kabila likarabatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Katibu Mkuu, *Engineer* Kalobelo alifika akaona shida iliyopo akatuma wataalam kutoka *MWAUWASA* walifanya ziara wakaandika andiko la miradi hii miwili na Mkurugenzi alileta kwenye bajeti, Baraza likapitisha na tukapeleka hata Wizara ya Maji kwa Mkurugenzi wa Maji Bwana Mafuru, pamoja na kwa Naibu Katibu Mkuu *Engineer* Kalobelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kutoona miradi hii kwenye bajeti. Jamani wanionee huruma hata waniwekee fedha za kuanzia ili kila mwaka waendeleo kuniwekea, hususan naamini tutaongeza sh.50/= kwa kila lita ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukinisaidia hii, utakuwa umeokoa maisha ya Watanzania wengi sana wa Jimbo la Magu.

Mhshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukurani.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Naungana na Kamati yangu ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu kuongeza tozo kwenye mafuta ili kuboresha Mfuko wa Maji. Ni vyema Serikali ikakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuongeza tozo kwenye Wizara hii ili kuongeza pesa ambazo zitapelekwa kwenye Majimbo mbalimbali kutatua kero kubwa ya maji ambayo inawaumiza akinamama wengi waliopo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu kuna mradi mkubwa wa Kihata ambao tumeuomba mara nyingi hapo Wizara ya Maji. Kwa masikitiko makubwa, mpaka leo hatujajibiwa. Ni vyema Serikali ikawa inatoa *support* kwenye taasisi zinazojitolea kuwekeza katika Sekta ya Maji. Katika Jimbo la Mufindi Kaskazini kuna *NGO* inaitwa *RDO*, imewekeza kwa kiasi kikubwa katika Sekta hii ya Maji, lakini Serikali

imekuwa haitoi *support* ya aina yoyote. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri tukutane na NGO hii ili Serikali iweze kuwekeza pia. Ni vyema sasa Serikali ikasimamia na kujua kwa nini misaada ya *World Bank* haijakamilika mpaka leo; na pesa zinapotea bure? Ni vyema Mheshimiwa Waziri anapohitimisha atuambie ni hatua zipi zitachukuliwa na Serikali kwenye hii miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la mto Liandimbela mpaka leo imekuwa hadithi. Mwaka 2014 Mheshimiwa Pinda Waziri Mkuu Mstaafu aliahidi shilingi milioni 295 kwa ajili ya kuendeleza bwawa la umwagiliaji wa Nundwe. Mpaka leo maji ni tatizo, lakini hakuna uwiano wa kupeleka fedha za maendeleo katika Majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Mjini Kakonko ulitengewa fedha shilingi milioni 300 katika bajeti ya 2016/2017 na mradi ulishatangazwa na wazabuni kupatikana. Mradi haujaanza kwa sababu ya mikataba kutosainiwa. Nashauri kwamba mkataba usainiwe ili Mkandarasi aanze kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mkubwa wa Mto Mgembezi – Kakonko ni mpya, unahitaji nguvu ya kifedha. *Intake* ilishajengwa, bado kuweka mabomba na *tank (reserve)*. Mradi ukikamilika, utanufaisha Kata za Kusuga, Kakonko, Kanyonza, Kiziguzigu na Kasanda. Ushauri wangu ni kwamba Serikali iweke kipaumbele kwa maji haya ya mteremko (*gravity water*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya *World Bank* iliyopo Wilayani Kakonko yote imekwama kukamilika wakati fedha zilishatolewa. Miradi hiyo iko Vijiji vya Muhanga, Katanga, Kidudaye na Nyagwijima. Ushauri wangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri afike Kakonko kukagua miradi hiyo ili atoe ushauri wa nini kifanyike ili wananchi wanufaike na miradi hiyo.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika hotuba hii na kuiwasilisha kwa utaalim mkubwa. Nawaomba waendeleo na ari hii ili wafikie lengo tulilojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya maji katika nchi yetu ni makubwa sana na yanaongezeka kila siku. Maji haya mbadala ni muhimu katika dunia kwani unapokosa maji na uhai haupo. Naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayochukua katika kuondoa matatizo ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa vijijini wanaendelea kujichimbia visima katika maeneo yao. Nashauri Serikali iendeleo kuwaunga mkono kwa njia zote, yaani kwa utaalim na kifedha kwa sababu uwezo wao vijijini siyo mkubwa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inatakiwa kuweka mipango mizuri ili kuweza kujitegemea, tuepuke kuwa wategemezi wa misaada kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2016 ilionesha kuwa Serikali ya India imetusaidia *fund* ya dola milioni 208,033 kwa miji sita katika nchi nzima pamoja na visiwa vya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi viongozi wa Majimbo tumekuwa tukiwaeleza wapiga kura wetu juu ya fedha hiyo na kuwaomba waendeleo kustahimili mambo yatatengemaa. Mpaka sasa baada ya mwaka mmoja kupita hakuna matokeo yoyote mazuri juu ya fedha hii. Hivyo,



namwomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo mazuri ni nini kimesababisha mpaka leo kutopatikana kwa fedha hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya hali ya hewa yanaongezeka ulimwenguni. Misimu ya mvua imekuwa haitegemeki kwa kasi za ukulima. Hivyo, ni vyema Serikali ikachukua juhudi zaidi katika kuendeleza Sekta ya Umwagiliaji ili iweze kufikia kiwango kizuri cha mahitaji. Asilimia 24 iliyopo hivi sasa ni ndogo sana kwa sekta hii. Nchi yetu ina vyanzo vingi vya maji ambavyo vikiboreshwa vitaweza kusaidia sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Jimbo la Mbozi vinakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji. Baadhi ya Vijiji hivyo ni Iyenga, Ilea, Itumpi, Magamba, Mtunduru, Utambalila, Maninga, Mahenje na vijiji vinginevyo. Hivyo katika miradi ya maji vijijini ni vizuri Serikali ikavikumbuka na vijiji hivi vya Jimbo la Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Mlowo wenye idadi ya watu wasiopungua 60,000 unakabiliwa na tatizo sugu na la muda mrefu sana la maji. Bajeti ya mwaka uliopita 2016/2017, Mji Mdogo wa Mlowo ulitenga fedha kwa ajili ya maji. Kwa bahati mbaya na masikitiko makubwa sana, hadi sasa hakuna shughuli yoyote inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atatue tatizo la maji Mji Mdogo wa Mlowo kwani wananchi wanateseka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vyanzo vingi vya maji Wilaya ya Mbozi mfano, Mto Lukululu, Mto Mkama na mito mingine. Ni vyema Serikali ijikite kuwapatia maji wananchi wa Mbozi kutoka katika vyanzo hivi. Pia maji ya ardhini hayapo mbali, maeneo mengi yanapatikana mita 75 kuelekea ardhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana ushirikiano wa Wizara na Watendaji wake wanaonipatia wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa miongozo wanayotupatia Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe. Naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe imeleta Wizarani maombi ya kupatiwa vibali vya kujenga miradi ya maji kwenye Wilaya yetu. Kwa mijini, tunaiomba Wizara iharakishe miradi ya Mji wa Ushirombo kwani Wilaya hii pamoja ukongwe wake haina mtandao wa maji mjini hasa kwenye Kata za Igulwa, Kateute, Bulaugwa na Ushirombo. Wananchi kama ilivyo kwenye maeneo mengine ya Wilaya, wanapata shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Uyovu tuna chanzo cha maji kikubwa ambacho kama kitapatiwa fedha, kinaweza kusambaza maji kwenye mji mdogo wa Runzewe ambako maeneo ya Kabuhima, Azimio, Kanembwa na baadhi ya maeneo ya Kabagale. Naiomba Wizara itusaidie kupata fedha kwa ajili ya kupanua mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umwagiliaji iliyopo Bukombe imesimama muda mrefu. Mradi wa Nampangwe na Bugelenga imesimama. Pamoja na kutumia fedha nyingi za Serikali lakini fedha ya kukamilisha haijatolewa jambo ambalo hadi leo wananchi wanaona halina manufaa. Naomba miradi hii ipatiwe fedha ili ikamilike na wananchi wa maeneo haya waweze kulima kwa tija katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yakipewa kipaumbele yataondoa kabisa tatizo la njaa kwenye Mkoa wa Geita na Mikoa ya jirani.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru wewe na kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kunipa fursa ya kusimama na kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu ya maji ambayo ndiyo uhai wa mwanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja; na sababu zangu za kuunga mkono hoja hii ni kama zifuatazo:-

Kwanza, taarifa ya Waziri juu ya utekelezaji wa kazi zilizofanyika mwaka 2016/2017 na mpango wa utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imeandaliwa vizuri na hasa kilichonivutia ni taarifa ya hatua iliyofikiwa ya kila mradi wa maji ukiachilia mbali ile miradi michache iliyosahaulika.

Pili, naunga mkono kwa kuwa Serikali ya CCM chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais - Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa, wanaonesha kwa vitendo dhamira ya CCM na dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwatua wanawake ndoo kichwani. Pamoja na pongezi, naomba nijielekeze kutoa ushauri kwa Serikali katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kupeleka fedha za maendeleo, bado Serikali haijapeleka fedha za kutosha katika miradi ya maendeleo. Hadi Machi, 2017 Serikali ilikuwa imepeleka shilingi bilioni 181.2 sawa na asilimia 19.8 tu. Ni ukweli usiopingika kuwa upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo uko chini sana, hivyo utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya maji unakwama kwa sababu hakuna fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali, kama kweli ina dhamira ya kuwatua ndoo wanawake kichwani, basi ni lazima Serikali ihakikishe kuwa inapeleka fedha zote zilizotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya miradi ya maji iliyopangwa kwa mwaka wa fedha husika. Hapa

nashauri, fedha ambazo hazijapelekwa zipelekwe sasa kabla ya mwaka huu wa fedha 2016/2017 kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono pendekezo la Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji la kuongeza sh.100/= ya kila lita ya petroli na dizeli. Ntoa ushauri huu kwa sababu tozo ya sh.50/= ya dizeli na petroli inayotolewa sasa imeleta matokeo mazuri sana ya miradi ya maji. Hivyo, tukiongeza tozo ikawa sh.100/=, kasi ya ujenzi wa miradi ya maji itaongezeka na dhamira ya Mheshimiwa Rais na CCM ya kuwatua ndoo wanawake kichwani itatekelezwa na wanawake wataachana na adha wanayopata ya kutembea masafa marefu kwenda kutafuta maji badala ya kufanya kazi zitakazowakomboa kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia fedha zitakazopatikana kutokana na tozo zipelekwe mapema katika miradi ya maji iliyopo vijijini ili kuwatua akinamama ambao hasa ndio wanaoathirika zaidi na shida ya kukosa maji. Katika kitabu cha maoni ya Kamati ukurasa wa 15 inaonesha kuwa asilimia 46 tu ya wakazi wa vijijini ndiyo wanapata maji safi na salama. Kwa hiyo, fedha za tozo kwenye mafuta zielekezwe kusaidia upatikanaji wa maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru Serikali na *BADEA* na *SFD* kwa mpango uliopo wa kutekeleza Mradi wa Mugango na Kiabakari (Butiama) kwa Dola za Kimarekani 30.69 ingawa mradi huu mpaka sasa haujaanza kutekelezwa. Pamoja na kuishukuru Serikali na Wadau kwa hatua zinazoendelea za kumpata Mkandarasi na kupeleka taarifa hizo *BADEA* kwa ajili ya kupata kibali cha ujenzi unaotarajiwa kuanza mwaka 2017/2018. Hapa naomba niseme kwamba, mradi huo umechukua muda mrefu kuanza, kiasi kwamba wananchi wanakaribia kukata tamaa juu ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kwa Serikali; kwa kuwa mpango wa mradi huu ni wa muda mrefu na mpaka sasa wananchi wanaelekea kukata tamaa na mradi huu, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie hawa

wadau wetu wa maendeleo watatoa lini hicho kibali na mradi uweze kuanza ili wananchi zaidi ya 80,000 waweze kupata maji safi na salama? Je, kama wadau wetu hawako tayari kutoa fedha hizi, Serikali ina mpango gani juu ya kutoa fedha ili mradi uanze bila kutegemea fedha za wafadhili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji – Mji wa Musoma, naishukuru Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kwa kuboresha huduma ya maji safi na salama katika Manispaa ya Musoma kwa gharama ya shilingi bilioni 45 ambapo mradi unalenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 10.14 za sasa hadi kufikia lita milioni 34 kwa siku ambazo zitakidhi mahitaji ya wananchi wa Musoma hadi mwaka 2025 na utekelezaji wa mradi umefikia kiwango cha asilimia 90. Tunashukuru sana. Pamoja na shukrani hizi, naomba kushauri yafuatayo juu ya mradi huu:-

(i) Ijengwe miundombinu ya maji ili wananchi waliopo kwenye chanzo cha maji cha Kata ya Etaro, Nyigina wapate maji kutokana na chanzo hiki; na

(ii) Pia kwa kuwa matenki ya maji yanaweza kuhifadhi maji mengi, nashauri ijengwe miundombinu itakayopeleka maji haya Kata ya Nyakanga, Bukabwa na Butiama kwa kuwa wataalam wa mradi huo wanasema inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kujenga miundombinu ya maji katika mradi wa Dar es Salaam na Pwani. Naipongeza *DAWASA* na *DAWASCO* kwa kusimamia mradi huu kwa kiwango cha hali ya juu. Pamoja na pongezi hizi, naishauri Serikali ihakikishe mradi huu unawanufaisha wananchi wa Mkoa wa Pwani, Kisarawe, Mkuranga, Bagamoyo na Kibaha kwa sababu vyanzo vya maji vya miradi hii viko Mkuranga na Kibaha na matenki ya maji yamejengwa Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Bwawa la Kidunda ni wa muda mrefu takriban miaka 20 mradi

haujaanza. Napenda kujua Serikali ina mkakati gani ili kuhakikisha mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu uvunaji wa maji ya mvua na kilimo cha umwagiliaji. Napenda kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Maji ije na mpango wa kuvuna maji kwa kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji hasa katika Mikoa ya Kanda ya Kati kama vile Singida, Dodoma na Shinyanga. Uvunaji wa maji ya mvua utasaidia kukuza kilimo cha umwagiliaji hapa nchini hasa katika mikoa ambayo imekuwa haipati mvua za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, katika Mkoa wa Dodoma kumekuwa na ongezeko kubwa la watumishi kuhamia Dodoma ambapo zaidi ya watumishi 2000 wamehamia Dodoma huku chanzo cha maji kikiwa ni kile kile cha Mzakwe. Sambamba na hilo ujenzi wa mabwawa kama vile bwawa la Farkwa umekuwa ukisuasua. Katika mwaka 2017/2018, Serikali iendelee kufanya utafiti ili kupata vyanzo vipya vya maji ili kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji bado kuna changamoto ya kupeleka fedha katika miradi ya umwagiliaji. Katika kitabu cha maoni ya Kamati inaonesha kuwa Serikali ilipeleka asilimia tatu tu kwa mwaka 2002, lakini kwa mwaka 2003 na 2004 Serikali haikupeleka hata shilingi moja pamoja na kuwa bajeti ya umwagiliaji ilitengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Maji ni uhai, kila chenye uhai kinahitaji maji. Hivyo napongeza juhudi kubwa inayochukuliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Wizara hii kwa jitihada ya kuwafikishia huduma hii wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mahitaji ya maji ni makubwa katika nchi yetu na tunashuhudia wakati huu wa mvua za masika maji mengi yanavyopotea, tunaiomba Wizara ya Maji iandae *program* mahususi ya kuvuna maji ya mvua ambayo kwa sasa yanapotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mwingine ni kuwaelimisha wananchi au taasisi, mfano shule, vituo vya afya na kadhalika, wavune maji kupitia mapaa ya nyumba na kuyahifadhi. Kwa wafugaji wenye mifugo mingi waelimishwe kujiandalia mazingira yatayowezesha kuhifadhi maji hasa wakati wa mvua ambapo maji mengi hupotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama kwa asilimia kubwa ndio wanaosumbuka na watoto wao kutafuta maji. Nashauri kuvitumia vikundi vya akinamama katika *program* mbalimbali za kuvuna maji na kuyahifadhi kwa matumizi endelevu. Tutumie na vikundi vya vijana kubuni njia nafuu za kuvuna maji kwa matumizi ya kilimo na mifugo katika kipindi hiki cha mvua, kwani maeneo mengi mvua zimefika kwa wingi na maji yanapotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa kuongezea tozo kwenye mafuta ili kuongeza Mfuko wa Maji.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Maji na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai; bila maji hakuna maisha ya binadamu wala viumbe hai vingine. Tatizo la uhaba wa maji nchini na duniani linazidi kuongezeka. Hii kama wataalam wanavyosema, inaashiria, vita kubwa duniani itakayotokea itakuwa ni vita ya kuvigombea (*scramble for*) maji. Hivyo ni muhimu kwa nchi yetu, Serikali yetu kupanga vizuri juu ya mipango mizuri ya usambazaji maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe bado tuna vijiji vingi havina maji safi na salama. Mfano vijiji vya Matiganyora, Nyombo, Lole, Igongolo, Tage, Mende, Kichiwi, Ilengititu, Ibiki, Kidegembye, Havanga, Iyembele, Isoliwaya, Kanikelele, Iwafi, Lima, Welele, I Kang'asi na Igombola havina maji. Tunaomba vijiji hivi navyo viwekwe kwenye mpango wa kupewa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji imekuwa ikitekelezwa kwa kuchelewa sana na wakati mwingine imekuwa haikamiliki vizuri. Hii ni kutokana na kucheleweshwa na taratibu za manunuzi na zabuni. Mara nyingi wanaochelewesha zabuni hizi na taratibu za manunuzi ni watendaji wetu waliopo kwenye Halmashauri zetu. Hivyo nadhani umefika wakati Serikali iwapime Watendaji wetu waliopo kwenye Halmashauri kwa idadi ya miradi ya maji iliyokamilika ndani ya muda ndani ya Halmashauri zao. Mfano, Mhandisi wa Maji wa Halmashauri atabaki kwenye nafasi yake kwa kupimwa kwa *speed* yake ya kusimamia miradi ya maji, ubora wa kazi ilivyofanyika, utoaji wa elimu bora kwa watumiaji wa maji kupitia Kamati za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado fedha inayotengwa kwenye Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji haitoshelezi mahitaji ya maji safi na salama nchini. Hivyo, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba iongezwe sh.50/= kutoka kwenye kila lita ya mafuta. Tatizo la maji mijini na vijijini linawaingizia gharama kubwa wananchi, kutokana na gharama ya kununua maji kwa wale wanaouza maji; gharama ya muda ambao akinamama wanatumia kwenda kutafuta maji; gharama kubwa wananchi wanazotumia kutibu magonjwa yanayotokana na ukosefu wa maji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa maji nchini ni muhimu tuongeze sh.50/= kwenye bei ya mafuta ili fedha hizi ziende kwenye mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu tumejaliwa kuwa na vipindi vya mvua ya kutosha kila mwaka. Maji yanayotokana na mvua hayatumiki vizuri, yamekuwa



yakipotea tu. Ni muhimu Serikali ipitishe sheria ndogo ya uvunaji wa maji toka kwenye majengo yetu, pia maeneo ambayo yana mvua nyingi. Ni vizuri tukaanzisha utaratibu wa kujenga mabwawa ya maji ili yatumike wakati wa kiangazi kwa shughuli mbalimbali, pia uvunaji wa maji maeneo ya mvua nyingi itasaidia kupunguza mafuriko maeneo ambayo maji haya huelekea, yaani maeneo ya uwanda wa chini (*low land*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Vunjo maeneo mengi hayana maji safi na salama toshelezi. Mfano ni Kata za Mwika Kusini, Makuyuni, Kahe Mashariki, Kahe, Kirua Kusini, Kilema Kusini, Momba Kusini na Kirua Magharibi. Sehemu nyingine tajwa hapo juu, miundombinu ya maji ni ya zamani sana, ni chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Momba Kusini walishirikiana na Mbunge, wameanza utaratibu wa kitaalam wa kuwa na andiko ambalo linakadiria mahitaji ya takriban shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumekubaliana kila kaya kuchangia sh.10,000/= lakini chanzo cha fedha hizi hazitoshelezi. Je, Serikali itasaidia kiasi gani katika mradi huu kama kichocheo? Kutoka chanzo cha maji ya uhakika kimepatikana Kisumbe, Mamba (*South Water Supply System from Kisumbe Spring*). Nashauri elimu shirikishi kwa wananchi namna bora ya kuyatawala, kuvuna/kuyasimamia na kuyatumia maji.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge walioipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoendelea kutekelezwa kupitia miradi mbalimbali ya maji. Kama Mjumbe wa Kamati ya LAAC nilifanikiwa kutembelea miradi kadhaa ya maji na umwagiliaji katika Mikoa, Wilaya za Lindi Manispaa, Nachingwea, Singida Manispaa pamoja na Tabora

Manispaa. Kwa ujumla wake kati ya miradi yote tuliyotembelea haikutekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara kuunda *team* maalum kufanya tathmini ya miradi yote ya maji na umwagiliaji iliyotekelezwa kuanzia mwaka 2012/2013. Hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni wakati wa Mbio za Mwenge Wilayani Mbinga kulikuwa pia na uzinduzi wa mradi wa maji katika Kata ya Mkako Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Mradi huu ulikataliwa na wananchi kwa sababu umetokelezwa chini ya kiwango kwani mabomba yameunganishwa kwa moto badala ya *connectors*. Naomba Wizara ipeleke wataalam wake ili kubaini ubadhirifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaleta malalamiko haya rasmi kwa maandishi ofisini kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ikamilishe visima vinne katika *program* ya visima 10 katika kila Jimbo. Visima hivyo vinne vipo katika Kata ya Litumbandyosi. Ushauri wa ujumla ni kwamba yapo maeneo ambayo kama wananchi watashirikishwa kikamilifu kwenye miradi ya maji, itapunguza sana gharama za miradi husika. Mfano, Wilayani kwetu Mbinga kuna vyanzo vingi vya maji vya *gravity*. Wananchi wapo tayari kujitolea kufanya kazi kama uchimbaji mitaro na kazi nyingine za kutumia nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ituletee wataalam Wilayani Mbinga ili kutengeneza miradi shirikishi ya maji katika miji, Kata ya Maguu, Ruanda, Matiri, Nyoni, Litembo, Mikalanga, Ilela, Kambarage, Mkumbi, pamoja na Kindimba Juu. Hii inaweza kuwa *model* kwa maeneo mengine katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai. Tunataka kumtua mama ndoo kichwani. Naomba tozo ya mafuta ile ya sh.50/= bado ni ndogo na inahitajika kuongezwa ili tuweze kuingiza katika mfuko na maji tumsaidie kumtua mama ndoo kichwani. Ombi langu ni kwamba asilimia 70 iende vijijini na 30 iende mijini ili kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu waja wake wote. Nakushukuru wewe kwa nafasi hii muhimu sana kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai. Kila kitu duniani kama hakuna maji basi hakuna viumbe hai. Kwa hiyo, maji ni muhimu kwa maisha na maendeleo ya binadamu kwa jumla. Takriban karibu Waheshimiwa Wabunge wote wamelalamikia maji katika majimbo yao. Wananchi wanapata tabu sana, wanakunywa maji machafu ambayo siyo salama. Akinamama wanaenda umbali mrefu sana, kwa hiyo, wanakumbana na matatizo makubwa na mengi sana. Mfano, ndoa zao ziko hatarini kuvunjika, wanabakwa pia wanadumaa katika kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ione kilio cha Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wao, Serikali iongeze bajeti ya maji kwa kupunguza matatizo haya katika Majimbo yetu. Naomba nizungumzie uhifadhi wa maji ya mvua. Pamoja na matatizo makubwa tuliyonayo ya maji, lakini bado Serikali yetu haiko makini juu ya ukusanyaji wa maji ya mvua ambayo hupotea kwa wingi sana. Mvua takriban hunyesha kwa vipindi lakini mvua zinakuwa kubwa ambazo husababisha mafuriko. Wananchi hupoteza makazi yao, mashamba yao na hata kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ingetafuta wataalam wafanye utafiti kujenga miundombinu na mabwawa ya ukusanyaji maji katika sehemu mbalimbali

katika Mikoa ya Tanzania. Maji tutakayokusanya yatakuwa akiba ambayo yatasaidia jamii katika shughuli mbalimbali za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mafuriko. Mafuriko yamesababisha adha na uharibifu mkubwa sana hasa kwa wakulima. Wakulima wamepata hasara kubwa sana, mazao yao ya vyakula yamesombwa na maji, mashamba yao yamekuwa kama bahari na kwa msimu huu hawavuni chochote. Kwa hiyo, hawana makazi, hawana chakula. Naomba Serikali ifanye mitaro ya kupitisha maji kwa usalama pasipo kuleta usumbufu kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie uharibifu wa bomba za maji. Bomba nyingi za maji hupasuka ama kutoboka, lakini huchukua muda mrefu sana pasipo matengenezo. Hivyo, hupelekea maji mengi sana kupotea na haya yanasababishwa na wataalam wa maji kubaki maofisini tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuwa makini katika jambo hili. Wafanyakazi wa Maji wafanye kazi kwa ufanisi kuondoa tatizo la upotevu wa maji ovyo.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na muweza wa mambo yote.

Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kusimamia majukumu yako kwa juhudi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuchangia katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni kwamba mara kadhaa nimekuwa nikishauri juu ya mfumo mzima wa kudhibiti maji ya mvua. Nchi yetu haina uhakika wa kupata mvua za kutosha kwa kipindi cha mwaka. Aidha, baadhi ya maeneo katika nchi yetu hayapati mvua kabisa, yaani ni kame, lakini pia mvua zinazonyesha nchini kwetu bado hatujazitendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa kwamba Tanzania ni mabingwa wa kumwagilia bahari kwa maana kwamba mvua zinazonyesha hapa nchini na kutuletea maji mengi, tunashindwa kuyadhibiti angalau kwa kiwango kidogo na badala yake yote yanakwenda zake baharini na kupotea. Kwa kipindi kifupi maji hupotea mara moja na ukame ukarudia palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba Serikali ifanye juhudi ya makusudi ya kuliangalia suala la udhibiti wa maji ya mvua kwa kutafuta uwezo kwa njia tofauti ili kuweza kujenga mabwawa ya kisasa ili kuongeza na haya yaliyopo tuweze kuhifadhi maji ya mvua ili yaweze kutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya uhifadhi wa maji ya mvua ni pana sana na ina gharama sana, lakini pindi Serikali ikilikubali na kulifanikisha, litatua changamoto nyingi za kijamii na kiuchumi. Serikali ikiwa italitilia maanani suala la uchimbaji wa mabwawa na uhifadhi wa maji ya mvua, kuna faida nyingi za kijamii na kiuchumi ambazo zinaweza kutatua na kuondoa lawama, lakini pia na kuimarisha ustawi wa hali za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwepo wa mabwawa nchini, watu watapata matumizi mbalimbali ya maji majumbani kama kupikia, kufulia na matumizi mengine. Aidha, yataimarisha uchumi kwa watu kufanya shughuli za ufugaji wa samaki na kuongezea vipato vya wananchi; lakini pia kuwapatia ajira vijana. Hivyo uwepo wa mabwawa ya kutosha nchini ni ukombozi wa maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna changamoto kubwa ya malisho na unyweshaji maji kwa mifugo. Uwepo wa mabwawa utatupunguzia kero kubwa juu ya mifugo yetu kwa upande wa unyweshaji. Pia uwepo wa mabwawa unawasaidia wakulima katika suala zima la umwagiliaji, shughuli ambayo inawapatia faida kubwa wakulima wetu nchi nzima kwa kilimo cha mbogamboga na nyanya. Hii pia

ni ukombozi mkubwa kwa wananchi juu ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwarobaini wa kuondoa ukame na shida ya maji nchini, suala la udhibiti wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa ni la msingi sana. Hata hapa Dodoma mvua iliyonyesha mwaka huu; kama maji yale yangedhibitiwa, Dodoma ingekuwa ni Mkoa wa neema mwaka mzima. Ila la kusikitisha, mvua imepita na maji yamepita, nchi inarudia hali ya ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuondokana na mazoea, tugharimike, tuhifadhi maji ili yatufaidishe kwa maendeleo.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yake yote kwa ujumla kwa kazi nzuri na hotuba nzuri yenye mtazamo wa kukidhi na kufikia matarajio ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuchangia katika suala zima la maji hasa vijijini. Hakuna asiyefahamu kuwa Lushoto ni Wilaya ya milima na mabonde na yenye vyanzo vingi vya maji; lakini tunu ile tuliopewa na Mwenyezi Mungu hatuitumii ipasavyo, tena ndio sehemu kubwa ya wananchi wanaokosa maji. Kuna tatizo kubwa sana la maji katika Kata za Makanya, Mbwei, Kilole, Ngwelo, Malibwi, Kwekanga, Kwai, Migambo, Ubiri, Gare, Ngulwi, Kwemashai.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote haya yana uhaba mkubwa wa maji na ukizingatia maeneo yote haya yana vyanzo vikubwa vya maji, lakini Serikali haijapeleka hata nguvu za kusaidia wananchi hao, kwani kilio chao ni cha muda mrefu sana. Pamoja na kuleta suala hili katika Ofisi za Wizara ya Maji lakini mpaka sasa hatujatengewa pesa yoyote ya maji vijijini na katika Jimbo langu sijawahi kupewa hata mradi mmoja mkubwa, zaidi ya kurukwa kila mwaka. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu itufikirie watu wa Jimbo

la Lushoto na sisi tuweze kupata maji kama wenzetu wa maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, naishukuru Serikali yangu Tukufu kwa kunitengea shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya maji katika Mji wa Lushoto, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naungana na wenzangu kwa hoja ya kuongeza tozo ya mafuta ya sh.50/= ili iwe sh.100/= kwa kila lita ya mafuta, kwani hii itapelekea upatikanaji wa maji kwa haraka kwa wananchi wetu. Pamoja na hayo, Serikali iweke msisitizo katika Halmashauri zetu na ufuatiliaji madhubuti kuhakikisha wanatenga pesa hizi za vyanzo vya ndani ili pesa hizo nazo ziweze kusaidia maji vijijini kuliko ilivyo sasa, kwani Halmashauri nyingi zinadharau mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali yangu Tukufu kujenga mabwawa kwa ajili ya kusaidia wakulima pamoja na wafugaji. Kama nilivyosema, mvua nyingi sana zinanyesha katika Wilaya ya Lushoto, lakini maji yale yanaharibika na kuleta maafa pamoja na kuharibu miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali yangu Tukufu baada ya kuyaachilia maji haya ya mvua kwenda kuharibu miundombinu, tujenge mabwawa ili maji haya yaweze kusaidia wananchi. Sambamba na hayo, katika Vijiji vya Wilaya ya Lushoto kuna maeneo ambayo mpaka sasa wananunua ndoo ya maji sh.500/= hadi sh.1,000/=. Vijiji hivyo ni vya Kwemakame, Kweulasi, Mbwei, Kilole, Mshangai, Malibwi, Handei, Miegeo, Kizara, Masange, Kongei na Gare.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu, katika bajeti ya mwaka huu nitengewe pesa kwa ajili ya vijiji hivi. Kama unavyojua, tuliwaahidi wananchi tena kwa kujigamba kwa kujiamini kwamba mkinichagua mimi pamoja na Rais wa Chama cha Mapinduzi tatizo la maji tutalimaliza, lakini mpaka sasa naulizwa na wananchi kuhusu maji, nakosa majibu ya kuwapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niihakikishie Serikali yangu Tukufu, wananchi wanayo imani kubwa sana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ninachokiomba kwa heshima na unyenyekevu mkubwa katika Wizara hii initengee pesa ili nikamalizane na wananchi wangu hawa, pamoja na kuendelea kujenga imani kwa wananchi na viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali yangu kuhusu hawa Wahandisi walio wengi, hawafanyi kazi kwa weledi, kwani hawa ndio wanachangia kurudisha nyuma miradi hii kwa kutosimamia vizuri. Kwa hiyo, wataalam hawa ambao hawana uwezo wasimamiwe na Mainjina wa Mkoa ili kusukuma miradi hii ya maji kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 nami ndiyo nitakuwa miongoni mwa Wabunge watakaopitisha bajeti hii kwa kusema ndiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iongeze tozo ya sh.50/= kwenye mafuta ili isaidie masuala ya maji, asilimia 70 iende vijijini na asilimia 30 mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bili za maji ni kubwa sana hasa katika Mkoa wa Njombe na hasa katika Halmashauri ya Njombe Mjini. Naomba Serikali ifuatilie suala hili la bili lifungwe, maana wananchi wanalalamika sana kwa sababu ya bili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Njombe ni tajiri wa mito, lakini wananchi wanahangaika sana maji hayatoki; hata Njombe Mjini maji hayatoki, lakini watu wanaendelea kulipa bili kubwa. Maeneo ambayo maji hayatoki ni Mtaa wa Mpechi, Joshoni, Idunditanga, Sido, Ramadhani, Kibena na maeneo mengine. Naiomba Serikali iwasaidie wananchi hawa kwa kuwaboresha miundombinu ya maji ili maji yaweze kutoka.



Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingi vya Mkoa wa Njombe havina maji. Katika Wilaya ya Wanging'ombe kulikuwa na maji huko nyuma, lakini kwa sasa mabomba haya hayatao maji, yamesharibika; akinamama wanapata shida, wanakwenda umbali mrefu kutafuta maji. Naomba miradi hiyo ya maji ifike vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na miradi ya umwagiliaji; maeneo mengi ya nchi yetu haijamalizika na miradi mingi haikuwa kwenye kiwango chenye kuonesha kuwa hata ikimaliza haitanufaisha Watanzania na hasa ile miradi iliyosimamiwa na Kanda. Kanda hizi kwa asilimia kubwa, miradi waliyoisimamia haikumalizika, ilikuwa ni tatizo. Hivi ni kweli walikuwa ni wataalam waliosimamia miradi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai kwa viumbe vyote. Ni vema Serikali tukipanga vipaumbele vyetu, ni lazima maji tuipe bajeti kubwa na siyo kuipunguzia bajeti. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuongeza hiyo sh.50/= ili bajeti iongezeke. Hivi zile pesa za msaada wa India zimefikia wapi na hata kule Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jitihada ya Serikali kwa wafadhili kwa utekelezaji wa kusambaza maji mijini na sasa tuongeze nguvu katika kusambaza maji vijijini, kwani kuna wananchi kwa asilimia kubwa zaidi ya asilimia 70 wanahitaji maji, ingawa hadi sasa tumefanikiwa kwa asilimia 19.8 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo ambazo hazikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa kweli tumedhamiria kwa dhati kuwatua ndoo kichwani akinamama, Serikali isingepunguza bajeti ya maji kutoka sh.939,631,302,771/= hadi sh.648,064,207,705/=, kwa mwaka 2017/2018 bali kuongezea au tukabakia na bajeti ya 2016/2017 na kuendeleza mikakati

ya kutatua upatikanaji wa fedha za kuwezesha tatizo la maji kutoweka kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kala, Kipili, Kirando, Katete na Wampembe, Kabuve, Samazi ni maeneo ya mwambao wa Ziwa Tanganyika, lakini hawana maji safi na salama. Kata ya Muze, Mtowisa, Mfinga, Zimba, Milepa, llemba, Kalumbaleza maeneo ya bonde la Rukwa wakiwa na Ziwa Rukwa hawana maji safi na salama. Vile vile Kata ya Mambwe, Nkoswe, Mambwe Keunga, Ulumii, Mnokola, Mwazyee, Katazi, Mkowe, Kisiimba, Mpombwe maeneo mengi haya hakuna maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bajeti ya 2017/2018, kwa mchanganuo wa fedha za maendeleo kwa Mkoa wa Rukwa wa sh.4,307,846,000/= hazitatosheleza mahitaji, kwani kutoka kwake zote ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nashauri kwa ujumla kwamba tozo ya sh.50/= ni vema ikaongezeka hadi kufikia shilingi 100/= ili makusanyo yake yaelekezwe kwenye mahitaji ya maji, kama tulivyoamua kwenye umeme na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema tukawa pia na Wakala wa Maji Vijijini ambaye atasimamia na kufuatilia utekelezaji wa usambazaji wa maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mvua, kuwepo na utaratibu wa kuvuna maji na kuandaa mabwawa ya kuhifadhia maji. Maji yanayoporomoka kutoka milimani hadi bonde la Rukwa na kuingia Ziwa Rukwa na kujaza udongo na kupunguza kina cha Ziwa hilo, ni vema utaratibu ukawepo wa kuyakinga (kuyavuna) maji hayo yakasaidia wananchi kupata maji safi na salama na pia wananchi watakuwa na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Fedha ihakikishe Wizara ya Maji na Umwagiliaji inapatiwa fedha kwa asilimia 75 kama siyo wote, kwa utekelezaji wa utatuzi wa maji kwa wananchi wetu.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi kuhusu miradi mingi ya umwagiliaji iliyoanzishwa katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini, kwani haijakamilika na hivyo kupelekea fedha nyingi za walipa kodi kuwa zimetumika lakini hakuna matunda yaliyopatikana. Mifano ni mingi sana, lakini kwa sasa naomba kupata maelezo juu ya skimu mbili zilizopo katika Halmashauri yetu ya *Lindi DC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Kinyope iliyopo katika Jimbo langu ambayo ilikusudiwa kumwagilia hekari 400, lakini hadi sasa mradi unaonesha kuwa umekamilika ilhali bado, mradi ule haujatatua changamoto zilizopo pale, badala yake imeongeza maji kuwa yanamwagika hovyoy katika mashamba ya wakulima, jambo ambalo linapelekea kilimo kuwa kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu ya pili, ni ile ya Narunya iliyopo katika Kata ya Kiwalalu, Jimbo la Mtama ambapo shilingi milioni 600 zimetumika, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea na badala yake maelezo yanayotolewa ni kwamba *designer* alikosea. Sasa Je, nini hatima ya mradi ule?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni vile visima viwili ambavyo vilichimbwa Jimboni kwangu Mchinga na Wakala wa Serikali wa Uchimbaji na Visima (*DDCA*). Naomba tafadhali miundombinu ya visima vile vikamilishwe. Pia naomba kupatiwa visima vingine viwili katika Vijiji vya Maloo na Makumba. Vijiji hivi vina shida kubwa sana ya maji. Wananchi wa vijiji hivyo wanatembea zaidi ya kilometa tano kufuata maji. Tafadhali sana naomba Mheshimiwa Waziri anipatie maji katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni kuhusu kutotumika kwa bonde la Mto Rufiji ambalo ni *very potential* kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini bonde lile halitumiki kabisa. Hawa watu wa *RUBADA* hawafanyi juhudi yoyote kuhakikisha kuwa kilimo cha umwagiliaji kinashika kasi katika bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali sana, naomba Mheshimiwa Waziri achukue juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa bonde hili linatumika ipasavyo ili tuondokane na taarifa za njaa katika Taifa ambalo lina ardhi ya kutosha na maji mengi yanayoweza kutumika katika kilimo cha umwagiliaji.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa sana katika nchi yetu, tunapaswa kuisaidia jamii yetu kwa kupanga namna nzuri ya kutatua tatizo hili. Kuundwa kwa Wakala wa Maji Vijijini kutatuongezea sh.50/= + Sh.50/= tutapata Sh.100/= ili kuweza kutatua tatizo hili, kama *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi inayoendelea kutekelezwa, tuna tatizo kubwa la fedha kwa Wakandarasi ambao wanapoleta *certificates* zao hawalipwi kwa muda unaotakiwa. Mfano, Mradi wa maji wa Haydom umeshindwa kulipwa na vyeti vyao vipo Ofisini kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna wakati mwingine hulipwa nusu ya walichokidai, hebu Mheshimiwa Waziri atusaidie mradi huu uishe kwa kuwapatia fedha Miradi ya Haydom, Arry, Ampa, Bashau. Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Bwawa la Dongobesh, naomba ahadi yake aliyoitoa Haydom na Dongobesh itekelezwe kwa kuleta fedha kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutembelea Wilaya ya Jimbo langu. Ombi langu ni kuwatimizia wananchi huduma hii ya maji. Maji mengi wakati huu wa mvua nyingi hupotea. Naomba tusaidiwe na wataalam ili tupange kuyazuia maji kwa kujenga mabwawa ya kumwagilia maana kilimo peke yake chenye uhakika ni kilimo cha kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapanga bajeti lakini fedha hazitoki kulingana na tulivyopanga. Hivyo, ni vema kupeleka fedha kwa wakati ili kuona matokeo ya haraka. Narudia ili ukumbuke, "fedha za miradi ya Dongobesh –

Bwawa; Haydom – Mradi wa Maji; na Arry – Tumati, Mradi wa Maji.”

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni yangu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 72 unataja miradi ya visima katika Kata za Gongolamboto, Chanika, Pugu Mpera, Kitunda na Ukonga. Kata hizi pia zilitajwa mwaka wa fedha 2016/2017 na hadi sasa visima hivyo havijakamilika. Naomba kujua ukweli wa miradi hii kama kweli ipo. Nashukuru Waziri na Naibu wake kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 73 ametaja miradi tarajiwa katika Kata za Msongola, Chanika, Gongolamboto, Pugu na Kitunda. Kata hizi nazo zimekuwa zikitajwa kila mwaka bila mafanikio. Kwa uhakika kuna shida kubwa ya maji katika Jimbo la Ukonga na hasa kwenye maeneo ya huduma za umma kama shule, zahanati, Polisi, Ofisi za Mitaa na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa maji ni mbaya katika maeneo ya Msongola-Mpera, Msongola-Mvuti, Msongola-Mbondou, Msongola-Uwanja wa Nyani, Buyuni-Zavala, Buyuni, Buyuni-Kigezi, Zingiziwa-Nzasa, Chanika, Pugu Station, Kivule-Bombambili, Pugu, Ukonga, Gongolamboto na Msongola-Yangeyange. Naomba kujua kwa uhakika utekelezaji wa miradi ya maji Ukonga na Kata zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kuwa maji ni uhai katika maisha ya mwanadamu, maji ni maendeleo, maeneo ambayo hakuna maji hakuna maendeleo na asilimia kubwa ya shughuli za kijamii na

kiuchumi zinategemea uwepo wa maji. Naishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza tozo ya maji kwa lita moja ya petroli na dizeli kutoka Sh.50/= hadi Sh.100/= ili kutunisha Mfuko wa Maji ambao umekuwa mkombozi mkubwa wa maendeleo ya miradi ya maji maeneo mengi nchini lakini wanufaika wengi wamekuwa ni wale wanaoishi mijini. Nashauri Serikali itazame zaidi maeneo ya vijijini angalau kupeleka 70% ya makusanyo ya tozo ya Mfuko wa Maji maeneo ya vijijini ambapo ndio kwenye shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama maji yanapatikana wakati wote wanawake wa Mkoa wa Singida ambao ni wachapakazi na wabunifu wanaweza kutumia fursa hii kwa kulima mazao ya chakula na biashara kwa mwaka mzima. Hata hivyo, kwa Mkoa wa Singida mambo yamekuwa sivyo ndivyo pamoja na adha kubwa wanayoipata wananchi wa Singida kutokana na ukosefu wa maji safi na salama na changamoto nyingi za maji katika Mkoa wa Singida bado bajeti ya miradi kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 imepunguzwa ambapo tumetengewa shilingi bilioni 4.7 tofauti na mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo tulipewa shilingi bilioni 6.7 jambo hili si sawa. Naiomba Serikali yangu kuangalia upya bajeti hii na kuiongeza kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, Singida ipo katikati ya nchi na ni mkoa unaokuwa kwa kasi, unategemea vyanzo vya maji ya visima virefu na vifupi ambavyo maji yake ni ya chumvi na hata hivyo hayakidhi viwango vya mahitaji. Pili, hali ya hewa ya Mkoa wa Singida ni kame hivyo ingetakiwa kupewa kipaumbele katika miradi mikubwa ya maji. Maeneo mengi ya Mkoa wa Singida yanakabiliwa na ukosefu wa maji safi na salama na tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu licha ya Serikali kuambiwa tatizo hili mara kwa mara bila kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi Mkoa wa Singida hususan wanawake wameteseka sana na adha kubwa ya ukosefu wa maji. Ni vyema Serikali ikasikia kilio cha wakazi

wa Mkoa wa Singida na kuchukua hatua madhubuti na za haraka kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na mito mikubwa, maziwa na bahari, ni lini tutatumia kikamilifu rasilimali hizi? Ni kwa nini tusitumie vizuri uwepo wa Ziwa Manyara ambalo lipo umbali wa kilomita 177 kuvuta maji kuja Singida ama kutoka Ziwa Viktoria kupitia Tabora, Nzega, Igunga hadi Singida? Tutaendelea kuwatesa wanawake wa Mkoa wa Singida mpaka lini na kuhatarisha ndoa zao kwa kutoka usiku kufuata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama bado kuna changamoto nyingi zinazoikabili Idara ya Maji ya Mkoa wa Singida (*SUWASA*). Changamoto hizo ni ukosefu wa vitendea kazi, uhaba wa watumishi na ucheleweshaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji. Ni jambo la kushangaza mkoa ambao unatakiwa kupewa kipaumbele kutokana na jiografia yake lakini unaongoza kwa uhaba wa watumishi. Kuna wahandisi 12 tu lakini wanaohitajika ni wahandisi 28, mafundi sanifu wanaotakiwa ni 52 ila waliopo ni 20 na kwa kuwa kazi nyingi za miradi ya maji ni *field work* sasa kwa mazingira haya tutafanikisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa mzima hauna *GPS machine*, kuna magari matatu ambayo yapo juu ya mawe na pikipiki moja tu. Je, kwa staili hii kazi zinaweza kufanyika kweli kwa ufanisi? Mkoa wa Singida unahitaji *crane truck* 15, *computer* nane, *GPS machine* sita, pikipiki 10 ili kuwezesha maofisa wa maji kufika wilayani na vijijini kutatua kero ya maji na hata Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji- Singida (*SUWASA*) hana gari. Naomba Serikali ipeleke vitendea kazi ili kuwawezesha wananchi wa Mkoa wa Singida kupata huduma bora za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya miradi ambayo tuliamini ingekuwa mkombozi wa wananchi wa Singida lakini mingi imekwama kukamilika kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo ukosefu na

ucheleweshwaji wa fedha kutoka Serikalini. Kuna miradi ambayo tayari imeshafanyiwa usanifu ya Manyoni na Kiomboi lakini haijapata fedha mpaka sasa. Miradi mingine ni ya Mkwa, Iyumbu, Ulyampiti na Sepuka ambapo inasubiri fedha toka Serikalini. Niishauri Serikali ipeleke fedha kwa wakati ili kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Singida Vijijini na Wilaya ya Manyoni ni wilaya zinazokabiliwa na upungufu na ukosefu mkubwa wa maji safi na salama na wakazi wake wanategemea zaidi maji ya visima virefu na vifupi. Mfano, Wilaya ya Singida visima vyake vingi ni vibovu na miundombinu yake ni chakavu ambayo haijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa fedha na kutopelekwa fedha hizo. Ukarabati wa miradi ya visima vifupi na virefu ambavyo vilikuwa vinafadhiliwa na fedha za *WDPS* kutoka Serikali Kuu, fedha hizi kwa muda mrefu hazijaletwa. Sasa ni vyema Serikali ikaangalia uwezekano wa kupeleka fedha hizo ili wananchi wa Mkoa wa Singida wa Wilaya ya Singida Vijijini waweze kupata huduma bora za maji ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea changamoto hizi hapo juu, naunga mkono hoja na nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa namna ambavyo wanashughulika kutatua kero ya maji pamoja na changamoto zinazoikabili Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii. Pamoja na hayo pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka kipaumbele cha maji kwa kuzingatia pia kuwa ipo katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Injiniya Lwenge, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Injiniya Kamwelwe pamoja na timu nzima ya Wizara hiyo kwa uzinduzi wa miradi mikubwa ya maji ya Ziwa Viktoria na kadhalika.



Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, maji ni uhai, bila maji hakuna maisha. Huduma ya maji mijini imekuwa ni tatizo. Kwa mfano, kule Jijini Mbeya maji hukatika mara kwa mara na kuletewa bili kubwa ya maji na nina uhakika hili ni tatizo katika miji mingi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 71, unazungumzia kuhusu uboreshaji huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu. Kwanza *sewage system* yake ni mbovu sana katika jiji lote hususan mvua ikinyesha na hivyo kusababisha uharibifu wa mazingira na magonjwa ya mlipuko. Katika eneo la Mbezi *Beach* Juu kuelekea Hospitali ya Masana–Goba *Road*, maji yamekuwa hakuna kwa miaka mingi na hakuna dalili ya ufumbuzi wa tatizo hili, zaidi tu ya wananchi kupigwa danadana kuwa kuna bomba la mradi wa Wachina. Wananchi wamekuwa wakinunua maji kwa gharama kubwa kwa miaka mingi sana bila suluhisho wala ufumbuzi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbeya Jiji kulikuwa na mradi mkubwa sana uliozinduliwa kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani (*KFW*) lakini hadi leo maji yanakatika hovyona bila taarifa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji kujua Serikali ina mkakati gani katika suala zima la Mfuko wa Maji. Mfuko huu utasaidia sana kutatua kero nyingi zisizo za lazima kimkakati mijini na vijijini. Mfuko huu unatakiwa uwe mkubwa kibajeti ili kuboresha huduma ya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu miradi ya maji mikubwa miwili; mradi wa Rukoma na mradi wa Kandaga. Miradi hii ilianza bajeti ya 2012/2013 hadi bajeti

hii ya 2017/2018 haina mwelekeo wowote wa kukamilishwa. Tatizo la miradi hii ni mgawanyo wa Halmashauri ya Wilaya mbili yaani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijijini na kuzaliwa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na miradi hii ikabaki Halmashauri mama ya Wilaya ya Kigoma Vijijini na miradi mingine mikubwa kama Uvinza, Nguruka, Ilagala na Kalya ilihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na inaendelea vizuri.

Mhshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara isiache kutupia macho miradi ya Kandaga na Rukoma ili Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijijini watumalie na kutukabidhi kwenye Halmashauri ya Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii minne inayotekelezwa na Halmashauri ya Uvinza kwa maana ya Mradi wa Nguruka, kiasi kilichobaki ni Sh.1,865,024,153; Mradi wa Ilagala kiasi kilichobaki ni Sh.491,628,240; Mradi wa Uvinza thamani ya pesa zilizobaki ili mradi ukamilike ni Sh.1,040,943,442 na Mradi wa Kalya kiasi kilichobaki ni Sh.185,170,935. Jumla tunahitaji Sh.3,582,766,770 ili tukamilishe miradi hii minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kitabu cha bajeti cha Mheshimiwa Waziri, bajeti ya miundombinu ya maji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni Sh.1,723,135,000. Utaona ni kwa namna gani miradi hii iliyoanza tangu bajeti ya 2012/2013 haitakamilika na kusababisha wananchi wa maeneo husika kukosa maji safi na salama na ikizingatiwa kati ya vijiji 61 ni vijiji vitano tu ndivyo vinavyopata maji safi na salama tena ya visima vifupi. Tuombe Wizara ione namna ya kutuongezea fedha pale ambapo wakandarasi watakapokuwa wamelipwa hizi 1.7 bilioni na wakawa wameleta *certificate* zao kwa ajili ya malipo ili basi miradi hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pia masikitiko yangu kwa Wizara ya Fedha na Mipango kupunguza bajeti ya maendeleo ya miradi ya maji kutoka shilingi bilioni 900 kwenye bajeti ya 2016/2017 hadi shilingi bilioni 600 kwa bajeti

ya mwaka huu wa bajeti 2017/2018 unaoanza tarehe 1/07/2017. Inasikitisha sana tena sana na kwa mpango huu wa upunguzaji wa bajeti ya maendeleo ya miradi ya maji inaonesha jinsi gani Serikali haina dhamira ya dhati ya kumaliza miradi ya maji inayoendelea kwenye majimbo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza tunavyo visima virefu na vifupi kama cha Mganza, kisima cha Shule ya Msingi Mliyabibi, kisima cha Sanuka na maeneo mengine havijafanyiwa marekebisha kwa miaka mingi sana na kusababisha visima hivi kutotoa maji na badala yake wananchi wa maeneo haya wanabaki kuona visima ambavyo hawana faida navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua bajeti ya mwaka 2017/2018 ni finyu ila tuombe Wizara iliangelie Jimbo la Kigoma Kusini kwa jicho la huruma kwani hali ya upatikanaji wa maji safi na salama ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kuzungumzia suala la umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri anatambua fika Jimbo langu ndiko Mto Malagarasi ulipo na mto huu unapita takribani vijiji 22 na mradi wa maji safi na salama wa Mto Malagarasi unahusisha Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchambuzi yakinifu unaoendelea kwenye mradi huu mkubwa lakini pia tunalo Bonde la Mto Malagarasi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji hasa kilimo cha mpunga. Tumwombe Mheshimiwa Waziri pale panapokuwa na fursa ya kusaidia wakazi wa Tarafa hii ya Nguruka ili waweze kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na ukizingatia Tarafa hii inalima sana mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kipekee kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi kwa Serikali kwa kuendelea kutekeleza Mradi wa Same – Mwanga – Korogwe. Mradi huu ni vema ukakamilishwa mapema kwa mujibu wa mpango kazi ili wananchi waweze kunufaika. Aidha, ni vema Serikali ikaona umuhimu wa kuhakikisha dola milioni 97.6 zinapatikana ili Vijiji vya Hedaru, Mabilioni, Gavao, Makanya, Mgwasi, Bangalala, Mwembe, Njoro, Ishinde, Ruvu, Bendera na vinginevyo vipate uhakika wa maji kwa wananchi 264,793 wa Wilaya ya Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa uboreshaji unaoendelea katika Jiji la Dar es Salaam katika sekta ya maji. Wizara ione haja ya kuharakisha utafutaji wa fedha ili kuanza ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Kidunda na Kisima cha Kimbiji na Mpera. Aidha, natoa rai Serikali ikamilishe ujenzi wa Tanki jipya la Changanyikeni na Kituo cha Kusukuma Maji Makongo katika mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Serikali kuona umuhimu wa kuweka mfumo mpya wa kusambaza maji katika maeneo yasiyokuwa na mtandao wa mabomba. Ni vema basi mkandarasi apatikane na fedha za ujenzi wa mifumo hii mipya zitafutwe mapema ili wananchi wa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo waweze kusambaziwa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya, ili kuweza kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji, ni muhimu visima vingi zaidi vikachimbwa ili wananchi ambao hawapati maji waweze kupata. Aidha, maeneo kama ya Kigamboni na mengineyo yaangaliwe ili nayo yaweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni muhimu pia Kijiji cha Suji – Malindi -Kitunda (Same, Kilimanjaro) waweze

kusambaziwa mfumo wa mabomba ili waweze kupata maji ya kutosha na waweze pia kujihusisha na kilimo cha umwagiliaji maana mfumo uliopo sasa ni wa zamani sana na uliwekwa wakati eneo hili lilikuwa na wananchi wachache. Aidha, maji kupitia Msitu wa Shengena yapo, ni suala tu la kutandaza mabomba yenye uwezo mkubwa ili nao wapate maji ya kutosha. Eneo hili ni la mlimani, hawajanufaika na Mradi wa Same – Mwangi – Korogwe, hivyo, ni vema na maeneo ya milimani nayo yaangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo, nitoe ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara/Serikali ije Bungeni na mpango mkakati (*strategic plan*) wa kuhifadhi vyanzo vya maji nchini. Nchi hii ina mito, maziwa na hata mabwawa madogo ya asili. Ni vizuri Serikali ikafikiria namna bora ya kuhifadhi vyanzo vya maji. Mfano, Mkoa wa Kigoma una vyanzo zaidi ya 1,000. Serikali ije na mpango shirikishi ambao utazishirikisha Mamlaka na Halmashauri zetu ili kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo vinaharibiwa kwa kasi ya ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji utakaofadhiliwa na Serikali ya India kwa USD 500, kati ya miji itakayonufaika na fedha hizo ni pamoja na Mji wa Kasulu. Nashauri sana *process* hii iharakishwe ili wananchi wetu wanufaika na huduma ya maji. Aidha, katika Mji wa Kasulu, maji yaliyopo/yanayotoka ni machafu na yamejaa tope. Tafadhali Wizara ije na mpango wa dharura kwa ajili ya maji katika Mji wa Kasulu. Maji ni machafu, Wizara chukueni hatua za dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji ya muda mrefu katika Wilaya ya Kasulu iliyoanza miaka ya 1980, mfano Mradi wa Maji wa Ruhita (*Ruhita Water Scheme 1984*) ni mradi wa siku nyingi. Nashauri Wizara itume wataalam wa maji

waende Wilaya ya Kasulu wasaidiane na Halmashauri ya Mji wa Kasulu (*Kasulu TC*) ili Miradi ya Maji ya Ruhata, Kanazi, Mrufiti na Msambara itazamwe upya hatimaye mkakati wa *rehabilitation* uanze/uandaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba ya bajeti ya Wizara hii na naunga mkono. Sote tunajua upatikanaji wa fedha na kazi nzuri iliyofanyika kwa kipindi hiki kinachoisha cha mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii wamejitahidi kutimiza wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara hii iongezwe ili kutoa nafasi shughuli nyingi za upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama ziweze kufanyika. Hivyo, nashauri kuwepo na tozo ya Sh.50 kwa bidhaa ya mafuta ili kuchangia kutunisha Mfuko wa Maji. Wizara na Kamati husika wawasilishe ombi kupitia Kamati ya Bajeti ili hoja ya kutoza kiasi hicho iingizwe kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha kama tozo/kodi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwepo mkakati wa kutunza vyanzo vya maji ambalo ndiyo suala la msingi zaidi ili maji kwa matumizi ya wananchi yapatikane. Wizara kupitia bajeti hii iwe na mikakati itakayopelekea suala la uhifadhi wa vyanzo vya maji kutekelezwa nchi nzima na kila Halmashauri iweze kutenga fedha za kutekeleza mkakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lambo la maji Lutubiga – Busega. Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Wilaya ya Busega na kujionea bwawa la maji ambalo liligharimu fedha nyingi ambalo lilichimbwa na Serikali kupitia Wizara hii lakini halina wala halijawahi kutoa maji kwa matumizi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa hili limekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Kijiji cha Lutubiga, Kata ya Lutubiga, Wilaya ya Busega ambao wana uhitaji mkubwa

sana wa maji na kwamba hawajapata maji licha ya bwawa hilo kuchimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia bajeti hii, naiomba Wizara kwanza itume wataalam ili kutathmini hali hiyo na urekebishaji wa bwawa hili uweze kufanyika mara moja. Hii itasaidia kuwapatia wananchi ambao wamekuwa wakiteseka kwa kukosa maji ilhali tayari Serikali imekwishalipa fedha nyingi ambazo makosa tu kidogo ya kitaalam yamepelekea kukosekana kwa maji, hivyo basi, Wizara ichukue hatua stahiki mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali iliyo chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Busokelo ni jimbo changa na miundombinu ya maji ni tatizo kubwa sana, hasa Mji wa Lwangwa, Kandate, Ntaba na maeneo mengine. Miradi wa Masoko na Mwakaleli I na II ni miradi ya miaka mingi sana lakini hadi sasa haijakamilika. Kwa sababu hiyo, naomba Serikali iweze kutimiza ahadi ya viongozi wetu wa Serikali. Naomba majibu ya Serikali, ni lini Miradi ya Masoko, Mwakaleli I na II itakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya pamoja na matatizo ya upungufu wa fedha. Bajeti ya mwaka 2016/2017, fungu la maendeleo walitengewa Sh.915,193,937,771 lakini walipata Sh.181,209,813.609, sawa na asilimia 19.8. Mwaka huu 2017/2018 wametengewa Sh.623,606,748,000, pana tofauti ya Sh.291,587,189. Upungufu huu ni mkubwa na ningeshauri kiwango kikubwa kiongezwe kabla ya Juni katika kipindi hiki.

Sioni mantiki ya kuongeza fedha kwa tarakimu badala ya kupeleka fedha ambazo zimepitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji Muheza bado ni kubwa sana. Ndoo moja ya maji ni Sh.800 hadi Sh.1,000/= mjini, bado huko vijijini. Ukombozi wa maji Muheza Mjini ni maji kutoka Mto Zigi kilometa 22.7. Mradi huu ni kati ya miradi 17 ya mkopo wa India (ukurasa wa 173) lakini kila siku tunaambiwa *financial agreement* bado. Tunaomba ishughulikiwe ili fedha hizo, dola milioni 14.754 zitolewe ili kazi ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji kutoka Pongwe mpaka Mjini Muheza tenda zilikwishafunguliwa lakini bado wakandarasi hawajateuliwa. Tunaomba mradi huu unaoshughulikiwa na Tanga UWASA tupate majibu haraka ni nini kinachoendelea. Nawashukuru Mawaziri wote kwa ubunifu wa mradi huu na Tanga UWASA.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa maji Muheza pia miundombinu ni mibovu. Hivyo, miradi yote miwili ikikamilika bila kurekebisha miundombinu hiyo miradi hiyo itakuwa haijakamilika kikamilifu. Hivyo, nashukuru kwa kuwekewa shilingi bilioni tano kwa ajili ya mifumo ya maji mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji vijijini, nashukuru kwa kutengewa shilingi milioni 931.373 ingawaje zimepungua kutoka zile za mwaka 2016/2017. Ningeshukuru kama zingerudishwa ambazo ni Sh.222,105,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo vinazunguka vyanzo vya maji vya Mto Zigi inabidi visaidiwe kupata maji safi na salama kwa kuwekewa mabomba na dawa kwenye maji yote yanayotiririka kutoka milimani, hususan Tarafa za Amani, Mbomole, Zirai, Kwezitu, Mbarai, Kisiwani, Moshewa, Kwemidimu na kadhalika. Wakisaidiwa naamini wataendelea kuvitunza vyanzo hivyo na kuwafanya wasichafue vyanzo hivyo.



Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri yafuatayo:-

- (i) Suala la maji litolewe kabisa TAMISEMI na lishughulikiwe moja kwa moja na Wizara kama umeme;
- (ii) Tozo inayotozwa ya Sh.50 kwa ajili ya Mfuko wa Maji iongezwe na kuwa Sh.100, hii itasaidia kupunguza tatizo la maji hapa nchini; na
- (iii) Ni muhimu tuanzishe Wakala wa Maji Vijijini kama REA, huenda ikasaidia kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie changamoto zilizopo katika Mkoa wetu wa Iringa kama ifuatavyo:-

- (i) Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa kwa baadhi ya miradi kama Tanangozi, Kidabaga, Malangali na Mbalamaziwa;
- (ii) Ukosefu wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipya vijijini kama Mkonge – Igoda, Ukelemi na Uyela – Nyololo, Njiapanda na Makungu;
- (iii) Uwezo mdogo wa wakandarasi na wataalam washauri kifedha na kitaalam katika kujenga na kusimamia mradi wa maji;
- (iv) Ukosefu wa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya uchangiaji wa huduma ya maji na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini; na
- (v) Upungufu wa wataalam wenye sifa katika Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya LAAC ilipotembelea katika Mkoa wetu wa Iringa ilibaini yafuatayo:-

(i) Miradi mingi ilikosewa wakati wa usanifu, hivyo, visima vingi kwa sasa havina maji na kama yapo basi sio ya kutosha;

(ii) Miradi mingine chanzo cha maji kimehama na hivyo kukosa maji katika chanzo;

(iii) Baadhi ya wakandarasi hawana uwezo wa kifedha na kusababisha miradi kutokamilika kwa wakati; na

(iv) Ucheleweshwaji wa wakandarasi kupatiwa malipo wanapowasilisha *certificates* mpaka kupeleka mahakamani kwa baadhi ya miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua tatizo linalosababisha Serikali kutotumia mito mingi tuliyonayo katika mkoa wetu kama Mto Ruaha, Mto Lukosi, Mto Mtitu katika kutatua tatizo kubwa la maji badala ya miradi ya visima inayotumia pesa nyingi na hakuna maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umwagiliaji. Katika Mkoa wetu wa Iringa na hasa Jimbo la Iringa, ipo miradi miwili ya umwagiliaji ya *Ruaha Irrigation Scheme*, huu upo Kata ya Ruaha na *Mkoga Irrigation Scheme*, huu upo katika Kata ya Isakalilo. Miradi hii ni ya siku nyingi sana, Serikali haijaweza kuitengea pesa ili iweze kukamilika na kutoa ajira kwa wananchi. Nataka kujua vigezo vinavyotumika kupeleka hizi pesa za miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji wa maji. Ni lini Serikali itatoa elimu katika suala hili ili Halmashauri zetu ziweke utaratibu wa kuhakikisha maji yanavunwa wakati wa mvua nyingi ili kuwa na akiba ya maji wakati wa kiangazi? Hayo maji yangeweza kusaidia katika shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bustani za mboga (vinyungu). Mkoa wetu wa Iringa ni mkoa ambao wananchi wake wanafanya shughuli za kibiashara hasa za mbogamboga kutumia maeneo hayo nyevunyevu kujipatia kipato lakini Serikali imepiga marufuku. Sasa nini mpango

wa kuwasaidia hawa wananchi waliokuwa wanategemea kilimo hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo naiunga mkono, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mbozi kuna Mamlaka ya Maji ya Mji wa Vwawa na Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Mlowo. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, aliahidi kuunganisha mamlaka hizi mbili na kuunda mamlaka kubwa itakayoshughulikia kutafuta, kusambaza na kusimamia maji katika miji hiyo ambayo ni sehemu ya Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe. Ni lini Wizara itaanza kutekeleza ahadi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa maji safi na salama katika Mji wa Vwawa. Hivi sasa hakuna maji kabisa Mji wa Vwawa na yaliyopo ni machafu sana kwa sababu hayachujwi kabisa, yanasambazwa kama yalivyo. Bajeti iliyotengwa ni ndogo sana. Naomba Serikali ifanye kila linalowezezana kutuongozea bajeti ya kurekebisha miundombinu ya maji pale Vwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi ulioandaliwa miaka mingi iliyopita uliotegemewa kusambaza maji katika Vijiji vya Iyula, Iduwili, Ipyana, Idunda, Igale, Luanda, Senjere na Lumbila. Serikali ina mpango gani wa kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Lukehe – Mlangali ambao ungesambazwa vijiji 14 katika Wilaya, baadhi ya fedha ziliwahi kutolewa na zikatumika vibaya. Naomba kupata maelezo ya kina juu ya hatma ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Vijiji vya Ihanda na Ipunga pamoja na kata zake, Serikali ilitoa zaidi

ya Sh.320,000,000/=, mradi uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Fedha hizo hazijulikani zilipo na mpaka leo hakuna maji katika Kata za Ihanda na Ipunga. Naomba tamko la Serikali juu ya mradi huu na hatua zilizochukuliwa dhidi ya fedha hizi. Naomba kupata majibu ili wananchi wa Jimbo la Vwawa na Mkoa wa Songwe waweze kuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa bajeti yenye matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafia ni kisiwa na kutokana na jioografia yake hiyo hakuna mito yenye kutiririka mwaka mzima. Ukweli kuwa chanzo kikuu cha maji kisiwani Mafia ni uchimbaji wa visima virefu na vifupi. Kwa masikitiko makubwa miradi ya maji iliyoletwa Kisiwani Mafia ni michache sana hivyo kisiwa cha Mafia kina shida kubwa ya maji. Kupitia Bunge lako Tukufu kwa namna ya kipekee, tunaiomba Serikali ituongeze miradi ya maji kutokana na mazingira magumu ya upatikanaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kuvusha maji kutoka Kisiwa Kikuu cha Mafia eneo la Kiegeani kwenda Kisiwa kidogo cha Jibondo takriban kilometa tisa umekuwa kwenye hatua mbalimbali za michakato kwa takribani miaka mitano sasa. Kupitia Bunge lako hili Tukufu tunaomba Serikali iharakishe mchakato huu kwani Kisiwa cha Jibondo kwa asili na ardhi yake ni mawe matupu na hakuna namna yoyote hivyo kulazimisha kuchimbwa kisima kilometa tisa nje ya Kisiwa Kikuu cha Mafia na kupitisha mabomba chini ya maji mpaka Kisiwa cha Jibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kwa kuwa mradi huo haupo wananchi wanalazimika kukodi mashua za uvuvi kuja Kisiwa Kikuu na madumu ya maji na kuchota maji na kuvuka nayo. Nyakati za pepo kali za kusi na kaskazi zoezi

hili linakuwa gumu na wananchi wanatumia maji ya chumvi ambayo ni hatari kwa usalama wao. Hivyo, tunaomba Serikali kuharakisha mradi huu ili kuondoa adha hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza Wizara na Serikali kwa kuwasilisha hotuba na utekelezaji wa miradi 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgao wa bajeti za Halmashauri. Ukifuatilia mgao wa bajeti kwenda katika Halmashauri kwa vyanzo vya ndani unahitaji marekebisho kwa uhitaji na matatizo ya kila Halmashauri hayakuzingatiwa ipasavyo. Mfano Nsimbo, 34% ya watu ndiyo wanaopata maji. Hivyo basi, tunashauri Wizara igawe Sh.1,000,000,000 kwa kila Halmashauri ambapo itakuwa Sh.185,000,000,000 kwa idadi ya Halmashauri 185.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mgao huo, kila Halmashauri itaweza kutatua kwa kiasi matatizo ya maji. Baada ya mgao huo, ndipo Wizara iongeze kwa kila Halmashauri kulingana na miradi mikubwa na kero za maji kwa eneo husika. Vilevile ni muhimu kwa Wizara kuangalia idadi ya watu ambao hawapati huduma ya maji na kuwapatia mgao ambao utatatua kwa kiasi tatizo la maji kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maji ya 2002 iliyoeleza kwamba wananchi wapate maji ndani ya mita 400 bado ufanisi wake haujaonekana. Hivyo, sera hii ifanyiwe utafiti na kuwe na kigezo cha kugawa fedha kwa Halmashauri ambazo hazijafikia malengo ya Sera ya Maji, kigezo cha mita 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maji Vijijini. Ni muhimu sana Serikali kuboresha Mfuko wa Maji Vijijini kwa kuwa ndiyo maeneo ambayo wananchi wanateseka sana

kwani ndiyo ambao hawapati maji. Hivyo basi Sh.50 kwa kila lita katika mafuta iongezwe na fedha ipatikane kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umwagiliaji. Serikali ifanye ufuatiliaji wa miradi ya umwagiliaji. Mfano Mradi wa Kijiji cha Katambike, Kata ya Ugala, Halmashauri ya Nsimbo - Katavi mpaka sasa bado haujaanza kufanya kazi na haujakamilika. Hivyo, tunaomba Serikali ifanye haraka kumaliza mradi huo ili wananchi wafaidike.

Mheshimiwa Naibu Spika, vizibo vya umwagiliaji. Serikali ikamilishe kizibo cha Mwamkuli katika Manispaa ya Mpanda. Pia Serikali iendeleze vizibo vile ambavyo vimejengwa na watu binafsi ili wananchi wa Kata ya Itenka ambao wanalima zao la mpunga waweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Chemba, Wilaya ya Chemba, vipo visima kadhaa katika Kijiji cha Mondo, Daki, Chandama, Mapango, Machiga na Pangai ambavyo vimechimbwa huu ni mwaka wa pili Serikali haijatoa fedha kukamilisha miundombinu ili watu wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili mradi wa maji wa Ntomoko bado unasuasua na kuna dalili kwamba mradi huu hautakidhi haja ya vijiji 13 kama ilivyopangwa awali. Naiomba Serikali isimamishe kutoa shilingi milioni 800 zilizobaki kulipwa mkandarasi na zipelekwe Chemba ili zitumike kuchimba visima katika Vijiji vya Hamai, Chivuku, Kirikima, Songolo na Madaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naishauri Serikali sasa ijenge mabwawa mawili katika Vijiji vya Itolwa na Chivuku ambapo maji ya mvua yanapotea sana na hiyo itaondoa

kabisa tatizo la maji katika eneo hili la *Lower Irangi*. Eneo hili limekuwa na shida kubwa ya maji lakini kama hatua hiyo itachukuliwa ni dhahiri tatizo hili litakuwa limekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Jumuiya ya Watumia Maji (*COWSO*) liangaliwe upya kwani sera hii imekuwa na tatizo kubwa na wananchi au Kamati za Maji hazina utaalum na matokeo yake miradi mingi inakufa. Nashauri Halmashauri za Wilaya zichukue jukumu la kusimamia mradi huu badala ya *COWSO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya mradi wa maji ya bwawa la Farkwa imeanza. Naiomba Serikali ikamilishe malipo ya wananchi wa Mombase na Bubutole haraka ili kuepusha watu wanaoweza kufariki kabla ya kulipwa na matokeo yake watu wanashindwa wakawazike wapi kwa sababu tathmini ya makaburi inakuwa imeshafanywa. Naomba Serikali kabla ya kuleta maji Dodoma ianze na Makao Makuu ya Wilaya ya Chemba ambapo tatizo la maji ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, fedha itengwe kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi hasa majumbani (*house hold water treatment*). Hii itasaidia kupunguza maradhi yanayotokana na maji kuchafuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchakavu wa miundombinu. Wilaya ya Muheza ni moja kati ya Wilaya ambazo zina miundombinu chakavu sana. Je, Wizara imeandaa utaratibu gani ili kuboresha miundombinu hii kwa kuwa kuna miradi mingi inaanziwa lakini kwa uchakavu huu haiwezi fanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *treatment plant*. Mji wa Korogwe unahitaji chujio na *treatment plant* yenye gharama ya shilingi bilioni sits. Wafadhili toka Australia wameonesha utayari wa kutoa mkopo wa riba nafuu kwa Mji wa Korogwe.

Je, Serikali iko tayari kusaidia Mji wa Korogwe kupata mkopo huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji wa maji. Wizara imeandaa utaratibu gani wa kusimamia Halmashauri ambazo hazijatengeneza Sheria Ndogo katika Halmashauri zao ili kila anayejenga nyumba yenye bati (shule na hospitali) aweke mifumo ya uvunaji maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, nashukuru Serikali kwa kuendelea kutuboreshea huduma za maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji toka Ziwa Viktoria. Utakumbuka maji ya Ziwa Viktoria yamefika katika Mji wa Kahama na yanapelekwa Nzega na Tabora lakini hayakusambazwa Jimbo la Ushetu ambalo liko Wilayani Kahama. Jimbo la Ushetu linashikilia 57% ya eneo la Kahama, wananchi wa Ushetu wanahisi kutengwa kwani maji haya yanawazunguka. Pia maji yanayotoka Mto Malagarasi watayatazama tu majirani zao wa Halmashauri ya Ushetu. Kwa kuwa tulifanya kikao na Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wa Wizara tarehe 3/5/2017 na kugundua kuwa tulikuwa tumeahidiwa kuunganishwa mwaka 2014, naiomba Wizara ianze tena mchakato wa kutuletea maji katika Halmashauri ya Ushetu toka mradi wa Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, umwagiliaji. Naiomba Wizara iongeze juhudi za utafiti ili tuweze kutafiti maeneo ambayo tunaweza kutengeneza mabwawa ili yasaidie kwenye kilimo cha umwagiliaji. Ushetu tunayo maeneo yenye rutuba na ambayo yanafaa kuweka skimu za umwagiliaji. Maeneo hayo ni kwenye Kata za Uyogo, Idahina na Sabasabini. Wizara itusaidie utalam huo na kuelekeza nguvu ili tuweze kuchangia malighafi za viwanda vyetu.



Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mipya. Utaratibu wa kutekeleza miradi mipya iliyotengewa fedha haujaeleweka kwani Halmashauri zinasubiri fedha ili kuweka kandarasi. Tunaomba zoezi lisimamiwe vema na sisi Wabunge tushirikishwe ili miradi ianze kwa wakati na *certificate* zitoke ili miradi ikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai wa binadamu, kila mtu anahitaji maji safi na salama ili awe na afya bora. Kila kiumbe kilicho ulimwenguni kinahitaji maji, maji ni uhai, maji ni kilimo, maji ni viwanda kila kitu kinahitaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko Kamati ya LAAC na nimetembelea miradi katika mkoa ya nchi yetu na kujionea hali halisi ya miradi ya maji na umwagiliaji. Miradi mingi imejengwa chini ya viwango, utakuta mradi ni mkubwa na unagharimu fedha nyingi lakini wananchi hawapati maji. Aidha, *pipe* ni nyembamba haiwezi kusambaza maji kwa vijiji vyote, kwa mfano vijiji sita watapata vijiji viwili, hili ni tatizo. Ikumbukwe hii ni Wizara kubwa na yenye mahitaji makubwa. Naomba bajeti ya maji iongezewe fedha ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umwagiliaji Inalia. Mradi huu uko katika Manispaa ya Tabora, ni mkubwa na umegharimu fedha nyingi, jumla ya Sh.246,536,679, hizi fedha ni nyingi. La kusikitisha, mradi huu umekamilika zaidi ya miaka saba sasa lakini haujafanya kazi kwa sababu wamiliki wa mashamba haya mpaka leo hawajalipwa fidia ya mashamba yao na kupelekea mgogoro mkubwa baina ya Halmashauri na wenye mashamba. Mradi una ukubwa wa ekari 110 na wale wananchi waliopewa wameukataa kutokana na mgogoro huo. Je, Serikali ni lini watawalipa wananchi hao

fidia ili mashamba hayo yaweze kuendelezwa? Namwomba Waziri aende akatatue mgogoro kwa sababu waathirika wakubwa ni wanawake kuhusu matatizo ya maji, wanapoteza muda mrefu kutafuta maji na wengine ndoa zao kuvunjika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyoo mashuleni kukosa maji ni tatizo kubwa lakini ni tatizo kubwa zaidi kwa mtoto wa kike pale anapokuwa kwenye siku zake za hedhi inambidi akae nyumbani na kusababisha kukosa masomo. Je, Serikali ina makakati gani kuhakikisha tatizo la maji linaondoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kuboresha miundombinu na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa maji, changamoto kubwa ya utekelezaji wa bajeti ya maji ni ufinyu wa mapato uliopelekea Wizara kupokea asilimia 19.8 tu ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kufikia Machi 2017 kwa mwaka 2016/2017. Changamoto nyingine ambayo ni sugu ni fedha za miradi ya maji kutumika vibaya kutokana na kutokuwepo na usimamizi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, miradi karibu yote ya kuanzia mwaka 2013/2014 ya shilingi bilioni 6.2 ambayo pesa imelipwa zaidi ya nusu miradi hiyo mpaka sasa haifanyi kazi. Kati ya miradi hiyo, ripoti ya CAG inaonesha kuwa malipo yalifanyika bila ukaguzi na kwa kazi ambazo hazikufanyika. Mradi wa Swaya/Lupeta zimelipwa shilingi milioni 120 kati ya shilingi milioni 520 na kazi iliyofanyika haizidi shilingi milioni 50. Pia mradi wa Mbawi na Jojo wa shilingi milioni 804, zimelipwa karibu asilimia 100 lakini mradi haufanyi kazi. Pia mradi wa Horongo/Itimu/

Mwampalala zimelipwa shilingi bilioni 1.2 (100%) na uko chini ya kiwango na malipo yalifanyika bila kuzingatia utaratibu wa malipo ya Serikali ikiwemo kutofanyika kwa ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa usimamizi wa miradi ya maji, fedha za miradi ya maji zinatumika vibaya na wananchi wanaendelea kukosa huduma ya maji salama. Pamoja na miradi hiyo kutofanya kazi, ripoti za Wizara ya Maji zinapotoshwa kuonyesha kuwa miradi iliyotajwa hapo juu na mengine ambayo wala haijaanza imekamilika wakati wananchi walengwa katika vijiji hivyo hawana maji. Ripoti hizo za kupotosha zimepelekea kwa makusudi hata majibu ya swali la maji katika Mji Mdogo wa Mbalizi kujibiwa kwa kupotosha kuonyesha hakuna uhaba wa maji na pia kuonyesha vyanzo vya maji ambavyo havipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi kupitia Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wamenigiza kumwomba Waziri wa Maji atembelee hiyo miradi aliyodanganywa na pia Bunge lielezwe hao wahusika wa upotevu wa fedha za miradi iliyotajwa ni hatua gani zimechukuliwa kwani hadi leo hii miradi iliyotajwa hapo juu haifanyi kazi. Kutokana na changamoto za usimamizi usioridhisha, naunga mkono mapendekezo ya kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini (*Rural Water Agency*). Kuanzishwa kwa Wakala huyu kutaongeza tija ya bajeti ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ya kuongeza tozo ya mafuta kwa kila lita ya dizeli na petroli kutoka Sh.50/= ya sasa kufikia Sh.100/=. Ripoti ya *EWURA* ya mwaka 2015 inaonyesha lita 3,380,097,164 zilingizwa nchini na kwa tozo ya Sh.100/= kwa lita, mfuko ungekusanya shilingi bilioni 338. Hili ongezeko la tozo ni muhimu kutekelezwa haraka iwezekanavyo ili kunusuru hali ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina vyanzo vingi vya maji ya mserereko. Pamoja na kuwepo vyanzo vingi, zaidi ya asilimia 60 ya wananchi

hawana maji salama. Kuna Vijiji vichache kama vya Ngole, lwala, Idugumbi na Chombe, wananchi wamejihamasisha na kuanzisha miradi ya kujitolea. Vijiji vya Mjete ni eneo la ukame na hakuna maji kabisa. Pia kuna vijiji zaidi ya 100 pamoja na kuwepo vyanzo vizuri vya maji ya mserereko lakini hawana maji salama. Wizara iangalie namna ya kupeleka miradi ya maji katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja hii muhimu katika Taifa letu. Naungana na wananchi wa Mkoa wa Arusha na Taifa zima kwa maafa ya vifo vya wanafunzi na Walimu wa shule ya *Lucky Vincent*. Mungu awafanyie wepesi wafiwa wote na Mungu awalaze marehemu wote mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Injini Gerson Lwenge, Naibu Waziri Mheshimiwa Injini Isaack Kamwelwe, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya pamoja na ufinyu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kuchangia kwa kuonesha masikitiko kuwa Wizara muhimu kama hii ambayo inagusa moja kwa moja maisha na ustawi wa jamii nzima ya Watanzania imepewa bajeti ndogo. Nina imani kabisa kuwa Watanzania wakipatiwa maji safi na salama watakuwa na ustawi mkubwa wa kiafya, kiuchumi na kimazingira. Maji yataboresha afya za wananchi na kupunguza maradhi na vifo. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii tunahitaji kuona bajeti kubwa zaidi ikitengwa kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwahi kupendekeza kuwa Serikali izingatie changamoto za maji vijijini zaidi na wazingatie kwa njia mbili. Kwanza, yale maeneo yenye maji ya kutosha lakini wanahitaji miundombinu tu lakini pili ni yale maeneo yenye ukosefu kabisa ya maji kutokanana ukame

au mvua isiyotosha. Mikakati ifanywe kutokana na changamoto zilizopo kuliko kutoa suluhisho aina moja kila sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ileje na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ni maeneo yenye maji mengi sana mwaka mzima kwa sababu ya mito, vijito na chemichemi nyingi kwa hivyo tusingetegemea kuwa wilaya na mikoa hii iendelee kuwa na tatizo la maji la miaka mingi namna hiyo. Je, ni lini sasa Wilaya ya Ileje na mikoa tajwa itapatiwa miundombinu tosha ya kueneza maji katika kata zote lakini zaidi kwa maeneo ya Tarafa ya Bulambya (Humba, Isongole, Chitete, Izubo, Mbebe, Mlale, Dubigu na Malangali).

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya wanategemea maji ya Mto Songwe ambayo ni machafu sana. Hata kule kwenye mabomba maji ni machafu sana. Tunaiomba Wizara itukamilishie hii miradi ili tuondokane na adha hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ileje ina skimu nyingi za umwagiliaji na zote hazifanyi kazi kikamilifu kwa sababu ya upungufu mdogo mdogo ambao kwa kweli haustahili kukwamisha mradi wa kipindi kirefu namna hiyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atuwezeshe kumalizia skimu zote za umwagiliaji Ileje ili kilimo cha uwagiliaji kifanyike kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ileje na Kyela ni sehemu ya mradi wa Bonde la Mto Songwe unaoendeshwa kati ya Serikali ya Tanzania na Malawi zinazopitiwa na Mto Songwe. Mradi huu upo Mkoa mpya wa Songwe na Ileje na Kyela Mbeya na kwa upande wa Malawi ni wilaya mbili zipo pembezoni mwa Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la mradi huu wa Mto Songwe ni kutunza maji yanayosababisha mafuriko kipindi cha mvua na kuathiri wakazi wa nchi hizi mbili wanaoishi karibu na Ziwa Nyasa. Utekelezaji wa mradi huu ulilenga kujenga mabwawa matatu kandokando mwa Mto

Songwe mpakani mwa nchi hizo, karibu na Ziwa Nyasa. Mabwawa haya yangetumika kuzalisha umeme na pia kufanya kazi za umwagiliaji karibu hekari 3,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameanisha kuwa mradi huu uko kwenye awamu ya tatu. Je, hizo awamu mbili zilizopita zilihusu masuala gani? Vilevile Mto Songwe umekuwa ukihamahama kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi huku ukiharibu rasilimali za wakazi wa bonde na kingo zake kutokana na mafuriko. Je, Serikali ina mkakati gani wa kudumu wa kudhibiti uharibifu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa Kata ya Bupigu lleje walizuliwa kutumia Bonde la Mto Songwe kwenye kata yao kwenye eneo ambalo lilikuwa lichimbwe bwawa kubwa mojawapo tangu wakati mradi ulipoanza hadi sasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kushughulikia bwawa hilo sasa au kuwaruhusu wananchi waendeleo na shughuli zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Songwe una urefu wa kilomita 200 ndani ya Ziwa Nyasa, eneo la Bonde ni *square kilometer* 4,243, *square kilometer* 2,318 ziko Tanzania na *square kilometer* 1,025 ziko Malawi. Bonde lina wakazi 341,104 kati yao 210,005 ni wa Tanzania na 131,099 ni wa Malawi. Bonde la mto lina eneo la hekta 6,200 zinazofaa kwa shughuli za uzalishaji na hii ni sababu nyingine kubwa ya kuwa na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inaweza kutupatia mkakati wa maendeleo ya bonde hili na ratiba nzima ya utekelezaji na fedha ya kuendeleza mradi huu? Je, Serikali itakaa lini na Halmashauri ya lleje na Kyela kwa maana ya kutoa taarifa ya kina ya mipango ya utekelezaji wa mradi huu na nini utakuwa ushiriki wa Halmashauri hizi moja kwa moja lakini hata *indirectly* kwenye mradi huu? Je, kuna mpango gani wa kukutanisha Halmashauri za upande wa Tanzania na wa upande wa Malawi? Kutokana na mpango mkakati wa mradi huu nini kinategemewa kuwa matokeo

makubwa ya mradi huu kwa nchi kwa ujumla lakini kwa lleje na Kyela kiuhalisia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, naunga mkono hoja ya kuangalia uwezekano wa kuiongezea bajeti Wizara hii na kuziweka fedha hizi kwenye Mfuko Maalum wa Maji Vijijini ili zisitumike vinginevyo. Tunapendekeza asilimia 70 ya fedha ya mfuko huu iende vijijini na asilimia 30 lende mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kwa kuwa wasikivu kwa sisi Wabunge. Pongezi pia zimwendee Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa mipango yenye kuleta matumaini ya kumtua mama pamoja na watoto wetu ndoo vichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kutenga \$ 30m kwa ajili ya mradi wa Lwakajunju (Kayanga), Ukurasa wa 85 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Naomba Wizara ifanye hima mradi huu uende kwenye utekelezaji, kwani kiasi hicho hicho kilitengwa *Financial Year 2016/2017*, lakini hakukuwa na *disbursement, same amountime-carry forward Financial Year 2017/2018*. Sasa naomba *this time* twende kwenye utekelezaji kwani mradi huu ndio uhai wa kura za Mheshimiwa Rais, Mbunge na CCM kwani ndiyo ilitusababishia ushindi 2015. Mradi huu naomba usifanye kosa la kushindwa kuacha huduma ya maji kwa vijiji vyenye chanzo (*Lake Lwakajunju*) yaani Kafunjo, Nyakashenyi, Kijumbura, Bweranyange, Kijumbura, kutasaidia ulinzi shirikishi kwa *additional benefits*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliomba Halmashauri ya Karagwe kuleta taarifa ya maeneo yenye uhaba mkubwa wa vyanzo vya maji. Rejea barua yenye Kumb Na. DE 208/287/OIN/96 ya tarehe 15/04/2016 na majibu ya hiyo barua Kumb Na. KGR/HWK/T.6/9. Vol. 1/02 ya tarehe 22/04/2016. Vijiji

hivi ni Nyakahita, Kigarama, Kashanda, Chonyonyo, Chabuhora na Kishoju. Naomba sana Wizara itusaidie kwenye utekelezaji wa bajeti iliyowasilishwa na Wizara. Aidha, naomba niongeze Kijiji cha Rwenkorongo nacho kina shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nawapongeza tena kwa kazi nzuri na Mwenyezi Mungu awajalie afya njema. Ahsante.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu iliyoletwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Spika, tatizo la maji limekuwa ni changamoto kubwa kwa Taifa letu hususan, Mkoa wangu wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida hii ya maji inamgusa mwanamke moja kwa moja. Wanawake wamekuwa wakipoteza muda mwingi kutafuta maji badala ya kujitafutia maendeleo yao ya kiuchumi. Tatizo hili la maji si tatizo mjini tu, bali vijijini nao wamesahaulika kwa muda mrefu. Ili nchi yetu iweze kufikia malengo ya Tanzania ya uchumi wa kati lazima tihakikishe hii nguvu kazi (wanawake) ambao ndio wazalishaji wakubwa tunawaondolea adha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba tuongeze tozo ya sh.50 kwa lita, ili tuwe na chanzo chenye uhakika. Kama hii haitawezekana, basi tupunguze kwenye *other sources* kama *Road Funds* na *REA*. Nina imani kubwa na Serikali na Wizara kuwa watapokea ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mlimba lenye vijiji 61 na kata 16 maji tunayapata wakati wa mvua (masika) na yakija yanaharibu makazi, barabara, mashamba na kadhalika. Kuhusu maji safi na salama, wananchi wa Jimbo la Mlimba kwao ni tabu sana.



Mfano, katika Mji Mdogo wa Mlimba, Kata ya Mlimba kuna kisima kimoja ambapo maji yanapatikana kwa mzunguko wa wiki mara moja tu. Kata nyingine 15 na kwenye shule za sekondari, za msingi na kwenye zahanati hakuna maji kabisa. Hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri/Naibu Waziri aje Mlimba ili ajionee mwenyewe hali ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwenye Taarifa/ Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu mradi wa mfereji wa umwagiliaji Kijiji cha Njage kuwa mradi huo unaleta tija. Ukweli ni kwamba mradi huo hauna faida wala tija kwa wananchi kwani, ingawa ni umwagiliaji mfereji huo hauna maji wakati wa kiangazi, bali wakulima hulima wakati wa masika tu, hivyo hulima kwa mwaka mara moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Mawaziri waje Jimbo la Mlimba washuhudie miradi iliyopo huko ambayo haina mwendelezo. Napendekeza pesa ikusanywe kwa kuweka tozo kwenye sigara, maji ya chupa, soda, bia, ili ziingie kwenye Mfuko wa Maji na fedha hizo mjini zipelekwe asilimia 30 na vijijini asilimia 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba kupongeza kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nkasi Kusini tuna miradi ya maji inayoendelea. Miradi hiyo imekuwa ya muda mrefu na imeacha matumaini yakipotea kwa wananchi. Naomba Serikali iione miradi hii kwa namna ya pekee na ilete tija kwa wananchi wake. Naitaja kama ifuatavyo:-

Mradi wa Maji wa Bwawa la Kawa ni wa muda mrefu, umetumia fedha zaidi ya bilioni mbili, wananchi bado hawajaanza kupata maji katika Vijiji vya Frengelezya, Nkuudi na Kalundi. Pia natoa mapendekezo kuwa, mradi huu utakapokamilishwa upeleke maji Sekondari ya Kipande na Kijiji cha Myula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa kutoka Kate Milimani kwenda Vijiji vya Nkata, Ntemba, Kitosi, Ntuchil, Ifundwa, Msilihofu na Isale ni mradi muhimu, uanze mara moja. Najua kwa sasa mtaalam mshauri yuko *site*, tuna fedha kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji King'ombe. Mradi una upungufu kwenye njia zake, mradi una mabomba yako nje nje, dosari zirekebishwe na naomba ukamilike na nashauri wananchi waulinde mradi wao. Nitamshambulia sana mtu anayehujumu njia ya maji, gharama ya mradi ni kubwa, zaidi ya milioni 720.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Kijiji cha Mpasa naomba uanze kutekelezwa. Wananchi wanasubiri kwa muda mrefu na imani inawatoka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Chala Mji Mdogo. Nimeona Wizara imetenga bilioni mbili kwa ajili ya upembuzi wa kina kushughulikia miji kadhaa ukiwepo wa Chala.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fedha hii iongezwe, sidhani kama inatosha. Angalia Ukurasa wa 164(31) wa Hotuba. Mji wa Chala una shida ya maji kwa kiwango cha juu sana na mamlaka yake imeanza haina mapato yoyote kwa kuwa hakuna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Kisura (Kijiji). Kazi inaendelea vizuri kwa sasa, japokuwa ilichelewa sana. Kasi hii iendelee hadi mwisho wa mradi, wananchi wanapata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la Kutafiti Maji kwenye Vijiji vya Kasu, Katani, Milundikwa na Kantawa. Vijiji hivi havina maji ya uhakika, naomba Serikali ifanye kazi ya kutafiti ili kusaidia vijiji vyote na Sekondari za Kasu na Kambi ya Jeshi, pia Milundikwa. Naomba vilevile Kata za Wampembe, Ninde na Kizumbi wafanyiwe utafiti maji ya mseleleko yanaweza kupatikana.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, bila maji maisha hayawezi kwenda mbele. Naishauri Serikali iongeze tozo ambapo asilimia 70 ielekezwe vijijini na asilimia 30 iwe mijini, kwa kuwa kuna vijijini ndiyo kuna shida sana ya maji. Wanawake wa vijijini wamekuwa wakipata adha kubwa kwa ukosefu wa maji safi na salama. Wanashindwa hata kufanya shughuli za kiuchumi na maisha kuwa duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka nyingi za maji zinadaiwa bili za umeme kwa kushindwa kulipa na wao pia wanazidai taasisi nyingi za Serikali, hivyo kufanya wananchi wanaolipa bili za maji kukosa maji. Naishauri Serikali iweze kulipa madeni ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa yenye Majimbo mawili ya Kalenga na Isimani imekuwa na shida kubwa sana ya maji safi na salama wakati kuna vyanzo mbalimbali vya maji kama vile Mto Mtitu, Ruaha pamoja na chanzo kinachoitwa Ibofwe. Maombi mbalimbali ya fedha yametolewa, lakini utekelezaji wake haupo na inakatisha tamaa sana kwa wananchi ambao ni wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iweze kutoa fedha ili maji yapatikane katika majimbo haya. Kuna maji ardhini ambapo pia, Serikali inaweza kuwekeza kwa kuchimba visima na maji yapatikane. Kwa hiyo, fedha ziwe zinatolewa kwenda kwenye Wizara hii ili waweze kufanya kazi ya kufumbua tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali pia, ihimize uvunaji wa maji kwa kushauri kila anayejenga nyumba yenye bati kibali kitolewe tu kama ataweka na mfumo wa uvunaji maji, uchimbaji wa mabwawa na malambo hasa wakati wa masika ili kuvuna maji yatakayowasaidia wananchi; ni jambo la kutiliwa mkazo kwa Wizara hii. Naitaka Serikali/

Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha aniambie utekelezaji wa haya niliyoeleza ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye eneo la uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji. Ni jambo lisilopingika kuwa vyanzo vyetu vingi vya maji vimeingiliwa na shughuli za binadamu kama kilimo, utalii, ufugaji na kadhalika na hivyo kutishia uhai wa vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chemchemi za Qangeded katika Bonde la Ziwa Eyasi, Wilayani Karatu ni chanzo muhimu sana kwa kilimo cha umwagiliaji ambako zaidi ya kaya 35,000 katika vijiji saba vya Kata za Baray na Mangola wananufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni chanzo hicho kimeshindwa kabisa kuwahudumia wananchi hao baada ya maji mengi kuchukuliwa na watu wachache karibu na chanzo, wanaochukua maji yote katika mashamba yao na hivyo kusababisha zaidi ya wakulima 30,000 walioko chini ya chanzo (*down stream*) kutokufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa alitembelea Bonde la Eyasi na baada ya wananchi kumlilia juu ya hifadhi ya chanzo cha Qangeded, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza na kutoa Kauli ya Serikali kuwa chanzo hicho kihifadhiwe kwa umbali wa hadi mita 500 na kwamba mashine zote zilizoko mtoni ziondolewe mara moja. Kauli hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilishangiliwa sana na wananchi wa Bonde la Eyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haijatekelezwa hadi leo. Bado mashine za kunyonya maji zipo mtoni na pamoja na kuwa alama za mipaka ya chanzo zimewekwa majuzi, bado mipaka (*beacons*) haijawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku ni kumdhallilisha Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kuidhallilisha Serikali. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja hii awaambie wakulima wa Bonde la Eyasi wanaotumia chanzo cha Qangeded ni lini watatekeleza Kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? Wizara kwa kushirikiana na wadau wavitambue na kuviwekea mipaka na kuvitangaza vyanzo hivyo vya Qangeded kuwa maeneo tengefu ili kuvilinda na kuvihifadhi vyanzo vya Qangeded.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kupeleka fedha za maendeleo katika miradi mbalimbali na taasisi zake kwa asilimia 34, ni hatua nzuri ukizingatia zaidi ya miaka miwili kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia fedha za maendeleo hazikuwa zikipelekwa, lakini sasa zimeanza kupelekwa, ni hatua ya kupongezwa badala ya kubeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo. Serikali imetoa Mwongozo wa kusitisha miradi yote ya maji kutosimamiwa na Wakandarasi Washauri kwa kupunguza matumizi na badala yake kazi hiyo ya usimamizi wa utekelezaji wa miradi ifanywe na wataalam wa mkoa na halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia hiyo nzuri ya kubana matumizi, lakini Serikali imesahau kupeleka fedha katika halmashauri husika za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya maji na mingine na kusababisha miradi mingi kutekelezwa chini ya kiwango na kuchukua muda mrefu kukamilika kwa kukosa usimamizi wa karibu wa kitaalam kwa watumishi wenye weledi wa kazi hii. Naomba kushauri Serikali yangu kupeleka fedha za

usimamizi na ufuatiliaji kuwezesha halmashauri na mikoa kusimamia miradi hii ili kupata thamani halisi ya fedha ya miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Chalinze III. Mradi wa Chalinze III ni wa muda mrefu sana na mpaka sasa haujakamilika. Katika mradi huu na sisi watu wa Morogoro Kusini Mashariki ni wanufaika wa mradi wa Chalinze III katika Vijiji vya Kidugalo, Chiwata, Maseye, Kinonko, Ngerengere, Sinyaulime na Lubungo, pamoja na Kambi zetu za Jeshi za Kinonko, Kizuka na Sangasanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya usambazaji maji na matanki ya kuhifadha maji imejengwa zaidi ya miaka tisa iliyopita kiasi kwamba mingine imeanza kuchakaa, lakini maji hayajawahi kutoka hata siku moja. Nataka kupata kauli ya Serikali kuwa ni lini watu wa jimbo langu katika vijiji hivi watapata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mkandarasi yupo *site* kufuatilia na kukagua miundombinu ya maji na kutaka kujenga kidaka maji (*intake*) ya kupokea maji kutoka Ruvu Chalinze kwenye chanzo cha maji. Nataka kujua, ili mkandarasi aweze kujenga kidaka maji hicho, ni eneo gani litajengwa tanki ili aweze kujenga? Kwani mpaka sasa mkandarasi anashindwa kujua wapi ajenge kidaka maji kwa sababu hajui mwelekeo wa bomba kuu litatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kulipwa wakandarasi wa maji. Katika Halmashauri yangu ya Morogoro tulikuwa na bajeti ya shilingi bilioni 5.19 mwaka 20/06/2017, lakini mpaka sasa tumepata shilingi bilioni 1.09 tu sawa na asilimia 19.84 ya bajeti ya mwaka na sasa tumebakiza miezi miwili muda wa mwaka wa fedha kibajeti kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshapeleka madai ya *Certificate* zaidi ya mara tatu, lakini mpaka sasa hatujapata majibu yenye thamani ya shilingi milioni mia nane ya kumlipa mkandarasi wa Mradi wa Fulwe, Mikese na wengine, ili

waweze kumaliza miradi hii kwa wakati. Ombi langu kwa Serikali ni kutuletea fedha hizi, ili kuwalipa wakandarasi kabla ya mwaka wa bajeti kwisha kwani, bajeti ya mwaka huu imekuwa ndogo kuliko ya mwaka jana, yaani ni shilingi bilioni 1.7 toka shilingi bilioni 5.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Bwawa la Kidunda mwaka wa jana ndani ya Bunge lako Tukufu, Serikali kupitia Wizara hii ya Maji iliomba bajeti ya shilingi milioni kumi na saba kwa sababu ya kulipa fidia kwa watu wangu waliopisha mradi wa Bwawa hili la Kidunda; Matuli, Kwaba, Mkulazi, Diguzi, Chanyumbu na watu wa Kitongoji cha Manyunyu na pia kutengeneza barabara ya kutoka Ngerengere mpaka Kidunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hakuna fidia iliyolipwa ya shilingi bilioni nne wala barabara iliyotengenezwa katika eneo hilo, ingawa barabara hii ilitengenezwa sehemu korofi na mwekezaji wa *Shamba Number 217, Mkulazi Holding Company Limited*. Kwa sasa barabara hiyo imejaa maji na kuharibika kabisa kutokana na kwamba haikutengenezwa yote na kwa kiwango kilichotarajiwa na *DAWASA*. Kwa kuwa, bajeti tulitenga ya shilingi bilioni 17 na Hazina wametoa shilingi bilioni 10 kati ya fedha hizo, lakini sasa Wizara wanasema wametenga shilingi bilioni 1.5 tu ya mwaka 2016/2017 na shilingi bilioni mbili katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ambayo haitoshi kwa fidia wala ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kupata Kauli ya Serikali; kwanza, ni lini wananchi watalipwa pamoja na fidia kwa kuwa muda mrefu umepita? Pili, ni lini Serikali itajenga barabara hii ya kwenda Kidunda, ukizingatia bajeti tulishapitisha na fedha kutolewa na Hazina? Tatu, kwa kuwa, watu waliopisha mradi ni wakulima waliopoteza nyumba zao na mashamba yao yaliyokuwa katika sehemu walizopisha mradi, lakini walikopeleka wamepewa viwanja tu kama vile wao ni watumishi wa Serikali au wafanyabiashara wakati ajira zao ni kilimo; na kwa kuwa bila mashamba maisha ya wananchi hawa yatakuwa

magumu sana na kwamba haiwezekani kuishi, je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kumega Msitu wa Mkulazi ulio karibu na makazi mapya ili wananchi hawa wapate sehemu za kulima na kuendesha maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bili ya maji. Kuna malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba bili za maji ni tofauti na ilivyokuwa awali, pia hata kusoma wanakuwa wanakadiria tu na kupelekea kuleta hali ya sintofahamu kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mita za maji kuchezewa. Suala hili limekuwa ni tatizo na mambo haya yanafanywa na watumishi wenyewe wa Idara ya Maji au watu wanaokuwa wafanyakazi wa Ofisi za Idara ya Maji kwenye Halmashauri zetu na miko ya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa vyanzo vya maji. Elimu inatakiwa kutolewa kwa wananchi wetu ili wajue athari za kuharibu vyanzo vya maji kwani hatuwezi kukomesha tatizo hilo bila kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya maji ni mibaya. Suala hili linahitaji Wizara tatu kukaa kwa pamoja ili kuimarisha tatizo la maji katika Halmashauri zetu. Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya uvunaji maji ya mvua. Kumekuwa na matatizo sugu ya ukosefu wa maji katika Mkoa wa Rukwa wakati mvua zimenyesha na kusababisha mafuriko na kuuwa watu na maafa. Kwa nini Serikali isiwe na utaratibu wa kuhifadhi maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kukaa pamoja na kupanga utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi



wanaozunguka vyanzo vya maji kulima mazao ambayo hayataathiri vyanzi vya maji na pia kutowaathiri wananchi kupata njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Idara ya Maji wasio waaminifu wamepelekea malalamiko makubwa kwa wananchi kwa kuwapa vifaa vibovu au kuchezea mita na kusababisha billi zisizo na uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji itengeneze mita kama ilivyo LUKU za umeme ili kuondoa malalamiko kwani kila mtu au mteja anajua amelipa kiasi gani na ametumia kiasi gani kumaliza kabisa malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu. Ili kulinda vyanzo vya maji, wananchi wakielimishwa vizuri juu ya kulinda vyanzo vya maji matatizo mengi yataisha au kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa iliyotengwa ni ndogo iongezwe kulingana na umuhimu wa maji katika maeneo mengi nchini. Pesa iliyotengwa haiwezi kumaliza tatizo la maji nchini. Nashauri Serikali iongeze pesa.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nashukuru ofisi na kiti chako kwa kuendelea kutenda haki juu ya mijadala ya Bunge. Katika Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Mtwara Mjini umekwama kwa nini? Ni muda mrefu hivi sasa Mtwara Manispaa haina maji ya kutosha na Serikali ilianzisha mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma hadi Mtwara Mjini ili kuondoa tatizo la maji. Bajeti ya 2016/2017 Mheshimiwa Waziri alisema tayari fedha zimetengwa, usanifu umekamilika na taratibu za kutafuta mkandarasi zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza ni kwamba mpaka leo ukiuliza unapata majibu ya Mheshimiwa Waziri kuwa hakuna pesa na pesa zilitarajiwa kutoka *Exim Bank* ya China. Kwa nini tunadanganya umma wakati pesa hakuna? Kwa nini tumechukua maeneo ya wananchi kwa miaka mitatu hivi sasa bila kuwalipa fidia juu ya mradi huu? Kwa nini mpaka leo Serikali haina majibu ya kina juu ya suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa wanapiga simu na wanasema wamechoka, Serikali haioni kama wananchi huwa wamechukuliwa maeneo yao na kuwazuia kufanya shughuli za kimaendeleo kama vile kilimo na hatimaye kuwadumaza wananchi wa Mtwara? Mradi huu unapelekea wananchi wa Mtwara waone kuwa wanaonewa kwa kutowalipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji Nchini; Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake cha bajeti ametaja miradi mingi itakayotekelezwa kupitia bajeti hii lakini cha ajabu mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma/Mtwara haupo kwenye orodha hii, huku ni kututenga wana Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji Mbagala. Mkoa wa Dar es Salaam upande wote wa Mbagala ambako kuna watu wengi kuliko maeneo yote hakuna mtandao wa *DUWASA/DAWASCO*, hali hii haikubaliki. Watu wa Mbagala wanahitaji maji safi na salama. Jambo la ajabu kuna *bore holes* Kimbiji ambako ni karibu na Mbagala lakini mtandao hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano na China (*Exim*) yanaendelea mpaka lini? Mheshimiwa Waziri anasema ili mradi wa Mtwara uanze majadiliano yanaendelea, kila mwaka anatoa kauli hii. Naomba kuuliza majadiliano haya yatakwisha lini? Kuendelea huku hakuna mwisho ili tuwapatie maji safi na salama kutoka Mto Ruvuma? Sisi Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara Mjini na Nanyamba tumeongelea sana suala hili na Serikali haitoi majibu ya kina badala yake inasema tu fedha hakuna. Haya ni majibu rahisi wakati wananchi wamezuiwa maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pesa Ndogo Zilizotengwa kwa ajili ya Mtwara Manispaa. Kutokana na mradi wa kuleta maji kutoka Mto Ruvuma kukwama mwaka 2015/2016 na 2016/2017, nilitarajia mwaka huu wa fedha Wizara ingetenga fedha kwa ajili ya mradi huu. Hata hivyo nasoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 147 pesa zilizotengwa hazihusishi fidia na gharama za mradi huu mkubwa, bado Wizara haioneshi kama Wanamtwara wana umuhimu wa kupata maji safi na salama.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maji ni uhai na kichocheo kikuu cha uchumi wa Taifa. Watu wanapokosa maji safi na salama ni tatizo katika Taifa. Wanafunzi wanapokosa maji kwa wakati wanaathirika kwa uchafu katika mazingira yao na husababisha kufeli kwa sababu katika mabweni wanafuata maji mbali sana. Kata ya Misunkumilo wanafunzi wa Mpanda *Girls* wanapokosa maji wanasafiri karibuni kilometa tano kufuata maji katika shule ya Milala Sekondari au Bwawani, usalama mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji kuchelewa kwisha. Hili ni tatizo kabisa. Miradi Katavi inachukua muda mrefu kwisha, je, ni utaratibu gani unatumika ili kuokoa hela hizi za wananchi na huku miradi inaharibika? Kwa mfano, Mradi wa Maji Kata ya Mwamapuli Wilaya ya Mlele – Katavi na Mradi wa Maji na Umwagiliaji Kata ya Ugala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha namna gani Serikali haikujipanga katika miradi hii, mmetumia pesa nyingi lakini mpaka sasa miradi haifanyi kazi. Je, ni lini mtakamilisha miradi hii kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Ikonongo katika Manispaa ya Mpanda; ni lini mradi huu utakamilika? Wizara waache maneno mengi waseme ni lini watakamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu *UDOM*. Mfumo wa maji taka na mabweni uko karibu lakini pia mradi huu umekwama, mabweni hayapati maji wakati Serikali

imewekeza pesa nyingi sana. Je, nini mkakati wa dharura kukinusuru Chuo Kikuu *UDOM*?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufisadi katika Miradi ya Maji; kwa kuendelea kuona miradi ikisimama na bado wananchi hawapati maji na wananchi kukosa majibu ya maswali yao kuhusu ukosefu wa maji inaonesha ni namna gani hawa wakandarasi wameamua kuwatesa wananchi. Serikali itoe majibu ili wananchi wajue mbaya wao ni nani kati ya Serikali au mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyanzo vya Maji Kuharibiwa Vizibo. Naishukuru Serikali kwa kuchukua hatua ya kuvunja vizibo ambavyo havijafuata utaratibu wa kupata leseni na kufuata utalam katika ujenzi katika Mkoa wa Katavi. Sasa nini kifanyike? Kuvunja vizibo hivi kusiwe na ubaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ni Ndogo, iongezwe. Uhitaji wa maji ni muhimu kuliko kitu chochote. Ukosefu wa maji safi na salama umeleta usumbufu, magonjwa na vifo kwa watoto wachanga kuharisha kwa kunywa maji machafu, homa ya matumbo, kuugua *typhoid* na kufariki kwa rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, nini hatua ya dharura Wizara ikishirikiana na mamlaka husika za maji katika mikoa ili kunusuru maisha ya Watanzania huku mkishirikiana na Wizara ya Afya ili tuondoe kero hii kwa wananchi?

**MHE. BALOZI. DKT. DIODORUS B. KAMALA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nibainishe kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Nkenge kuna miradi ya maji ambayo tayari imepokea fedha zote za miradi husika ya maji lakini maji hayajapatikana. Miradi hiyo ni Mradi wa Maji wa Ruzinga, zimetumika zaidi ya shilingi milioni 400 na mradi wa maji wa Igurugati ambao umetumia zaidi ya shilingi milioni 300. Aidha, kuna miradi mingine

ambayo nayo haitoi maji kama ilivyotarajiwa. Miradi hiyo ni miradi ya maji Kilimililite, Kakunyu, Kenyana na Kibeho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifuatilie kwa karibu miradi tajwa na hasa mradi wa Maji wa Ruzinga na Mradi wa Maji wa Igurugati ulio katika Kata ya Bugandika. Pia mradi wa Maji wa Kakunyu nao umeshindwa kutoa maji. Miradi yote tayari ilipokea fedha ya Benki ya Dunia lakini maji hayajapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru nikipata maelezo ya kina kuhusiana na miradi niliyobainisha.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufafanuzi wa vigezo vinavyotumika kugawa fedha za Miradi ya Maendeleo ya Maji Vijijini. Kwa mfano katika ukusara wa 140 jedwali 5(a) Monduli imetengewa shilingi 646,914,000. Jambo ambalo ni kinyume kabisa na matarajio ya mapendekezo ya bajeti ambayo ilikuwa bilioni nne. Ni namna gani tutatekeleza miradi ya wananchi kwa kiasi hiki kidogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itusaidie kuimarisha chanzo cha maji Ngaramtoni (kisima) ili kukidhi uhitaji wa maji ambapo kwa sasa miradi mingine imeanzishwa kwa kutumia kisima cha awali. Serikali haijapanga fedha miradi ya vijiji viwili; sehemu ya vijiji kumi ambavyo vilikuwa vimebaki awamu ya pili.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kujitahidi kwa dhati kabisa katika kuhakikisha kuwa suala la maji linatimia kwa nguvu zote, ukizingatia kwamba maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zilizopo napenda kuishukuru Wizara kwa kututengea fedha kwenye mradi wa *HTM* ambao kwa muda mrefu ulitakiwa uwe umeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Jimboni kwetu na kuahidi kwamba tukiwa tunasubiri mradi mkubwa kutoka kwenye ufadhili wa India, basi Serikali itatoa shilingi bilioni mbili ili kukarabati mradi wa *HTM* uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru *Engineers* wamekuja na wameshafanya kazi zote za michoro ya ukarabati wa *HTM* na wameshakabidhi Wizarani. Basi naomba utekelezaji ufanyike kama ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri alivyowaahidi wakazi wa Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho yake atufafanulie ni lini mradi huu mdogo unaanza, wakati tukiwa tunasubiri ule mkubwa? Ahsante.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zangu kwa Serikali kwa hatua kadhaa zinazochukuliwa kuboresha sekta ya maji na umwagiliaji nchini, nina mapendekezo yafuatayo:-

(i) Serikali iongeze bajeti kutoka bilioni mia sita hadi *at least* bilioni mia tisa iliyokuwepo.

(ii) Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha Wakala wa Maji kama ilivyo *REA*.

(iii) Tozo ya Sh.50/= kwa lita ya dizeli na petroli iongezwe kufikia Sh.100/= kwa lita.

(iv) Suala la majengo nchini kuwekewa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua lisiwe la hiari bali liwe la kisheria ili kupata maji ya kutumia lakini pia kuzuia mafuriko nchini.

(v) Suala la sekta binafsi kujengewa mazingira ya kushiriki kikamilifu kwenye sekta ya maji hasa umwagiliaji, kupitia ubia wa Serikali na sekta binafsi (*PPP*).

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yote kwa ujumla. Naomba kujua yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwisho wa mwaka wa fedha Mradi wa Maji Mwangi – Same utakuwa umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya maji Mji wa Same, Makanya na Hedaru ni mbaya sana, je, Serikali itachimba lini visima virefu kabla ya mradi mkubwa wa maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niombe Serikali iwasimamishe kazi wakandarasi wanaojenga Mradi wa Maji wa Nguluma Mlola kwa sababu wakandarasi hawa walitoa ahadi mbele ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa Mradi wa Maji wa Ngulu ungekamilika tarehe 30 Aprili, 2017 lakini mpaka sasa hakuna hata dalili za kumaliza mradi ule pamoja na mradi wa Mlola. Miradi yote miwili imefikia asilimia 70 ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Serikali yangu iwasimamishe au wapewe *deadline* ya kumaliza miradi yote hii miwili maana imekuwa kero kubwa kwa wananchi.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa mapendekezo yangu kuhusu Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji. Ni ukweli usiopingika kuwa suala la maji bado ni changamoto hususan kwa Watanzania waishio vijijini. Hivyo ni lazima kama Serikali kuja na mipango kabambe inayotekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha kwamba Bajeti ya Maji ambayo imekuwa ikitengwa haitoshelezi kulingana na mahitaji halisi ya Watanzania lakini tatizo kubwa ni kuwa fedha hiyo huwa haitolewi yote kama inayoidhinishwa na kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali kupitia Wizara ihakikishe kuwa fedha inatolewa kama iliyoidhinishwa na hii kwa sababu maji ni uhai na kwamba bila maji hakuna maisha. Ni vyema Serikali ikabuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo ni vyanzo vya ndani na ambavyo ni vya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo naungana na maombi na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi juu kuongeza tozo ya sh.50/= na kuwa sh.100/= kwenye kila lita moja ya mafuta ya *diesel* na *petrol* ili kuwezesha miradi mbalimbali ya maji kuweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuonesha kuwa Serikali iko *committed* katika kumaliza tatizo la maji hususan vijijini ambako ndiko hasa changamoto ya maji iko kubwa, nashauri katika hayo makusanyo yatakayopatikana baada ya kuongeza tozo ya sh.50/= ni vyema asilimia 70 ya fedha hiyo ikaenda vijijini na asilimia 30 ikaenda mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri kuwa ile sera ya uvunaji maji ni vyema Serikali sasa ikalitilia mkazo na kuhakikisha kwamba kila Halmashauri inatoa maelekezo ya kuhakikisha wananchi wetu wanapojenga nyumba wakumbuke kuweka *system* ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niombe itakapooongezwa tozo ya sh.50/= Wizara iangalie pia Mkoa wa Songwe ambao ni mpya na unakabiliwa na upungufu wa maji hususan kwa vijijini. Wanawake wanapata shida sana, mfano Wilaya ya Mbozi, Kata ya Vwawa na Mlowo, shida ya maji ni kubwa mno. Mheshimiwa Waziri wa Maji alituhidi kutuletea mradi mkubwa wa maji lakini mpaka sasa hatujui mpango huo umefikia wapi. Pia, naomba watukumbuke kutuletea mradi wa maji katika Mji Mdogo wa Tunduma, lakini pia Wilaya ya Ileje na Wilaya ya Songwe.

**MHE. ESTHER A. MAHAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na siha njema sisi sote katika Bunge lako Tukufu. Pili, nipende kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt.



John Pombe Magufuli pamoja na Serikali na watendaji wote hasa wa Wizara hii muhimu ya Maji na Umwagiliaji kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kujitahidi kumtua mwanamke ndoo kichwani kama ilivyo ahadi ya chama chetu cha CCM kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri shahiri hakuna asiyejua umuhimu wa maji katika muktadha mzima wa afya bora, uhai na maendeleo endelevu ya kila familia. Hii ni kutokana na kwamba hata mwili wa binadamu tu una asilimia 75 ya maji, hivyo maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali inafanya kila iwezalo ili kumaliza kero ya maji katika maeneo mengi nchini. Binafsi ningeshauri tozo ya mafuta ifikie sh.100/= kwa kila lita moja ya *diesel/petrol*; iongezwe kwenye Mfuko wa Maji ili wanawake waweze kuondokana na kero ya kutafuta maji kwa masaa mengi, hali inayosababisha ndoa zao kuvunjwa, kukosa muda wa kufanya shughuli nyingine za ujasiriamali ili waweze kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisikitike tu kuwa pamoja na bajeti ya maji iliyotengwa katika bajeti ya 2016/2017 kufikia zaidi ya bilioni mia tisa, bado fedha zilizopelekwa hadi Aprili mwaka huu kuwa asilimia 20 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote wanaomba kuongezwa fedha hizo zilizopungua hadi bilioni mia sita katika bajeti hii ya mwaka 2017/2018. Naomba nitofautiane nao kimtazamo kwani hata hizo bilioni mia tisa zilizotengwa hazikupelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali yangu Tukufu kwamba, kwa kuwa kuna Halmashauri takriban 185 nchini, basi haidhuru kila Halmashauri ingetengewa shilingi bilioni moja ili kupunguza makali ya kero ya maji katika kila Halmashauri, halafu bajeti tengwa ya zaidi ya bilioni mia nne zielekezwe kwenye miradi maalum (mikubwa). Hii itaondoa malalamiko mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie hali ya maji katika Mkoa wangu wa Manyara. Naomba kwa moyo wa dhati kabisa niishukuru Serikali yangu kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji kwa kuupatia fedha Mradi wa Maji wa Mto Ruvu katika Wilaya ya Simanjiro ambapo wakandarasi wapo *site* na kazi inaendelea vizuri sana. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba ahakikishe fedha zinaendelea kupelekwa na pia kuhakikisha mkandarasi anafanya mradi huu kwa umakini mkubwa na (*value for money*) thamani halisi ya fedha inayolingana na mradi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wananchi wa Simanjiro kwa aina ya jiografia ya wilaya, pamoja na mkoa wetu kuwa ni mkoa wa wafugaji bado tuna mahitaji makubwa ya maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na wanyama pia. Wakati Waheshimiwa Wabunge wakiomba Wizara hii kuongezewa fedha, ndipo na mvua kubwa inaendelea kunyesha kiasi cha kusababisha madhara makubwa kwa wananchi pamoja na miundombinu hapa nchini. Binafsi najjuliza ni kwa nini Wizara isijiongeze na kuchimba mabwawa wakati wa kiangazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mabwawa hayo yangeweza kutega maji hayo yanayopotea bure kipindi hiki cha masika. Haiwezekani tunalia ukame majira yote ya mwaka wakati tungeweza kuepuka baadhi ya kero isiyo ya lazima kwa kukusanya maji ya mvua kwenye mabwawa na majosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri pia Halmashauri zetu zitengeneze Sheria Ndogo (*bylaws*) zitakazowezesha kila nyumba, kaya yenye paa la bati kuwa na mfumo wa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kupunguza makali ya kutafuta maji mbali kipindi cha kiangazi. Naomba niendeleo kushauri kuwa katika sh.100/= hii, asilimia 70 iende vijijini na asilimia 30 iende mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyejua adha kubwa wanayoipata akinamama wa vijijini ambao

wanatumia asilimia 80 ya muda katika kutafuta maji ya ndoo moja au mbili kwa kutwa nzima. Ni imani yangu fedha hizi zikielekezwa kwa kiasi kikubwa vijijini tutakuwa tumewaokoa akinamama hawa na majanga mengi wanayoyapata wanapokuwa kwenye harakati za kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchache niseme tu Wilaya ya Kiteto katika Mkoa wetu wa Manyara asilimia zaidi ya 65 ni eneo kame sana ambapo hata wakichimba visima virefu bado wanakosa maji. Naiomba Wizara ya Maji na Umwagiliaji iangalie ni mbinu gani mbadala itakayotumika katika kuwasaidia akinamama hawa wa Kiteto waondokane na adha ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niishauri Serikali yangu sikivu kuanzisha Mfuko wa Maji Vijijini ili kusaidia katika suala zima la *monitoring*. Mfuko huu pia utasaidia kwa kiwango kikubwa kutambua maeneo yenye kero iliyopitiliza na kuweza kuyatatua kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, adha ya maji safi na salama ni chanzo kikubwa sana cha maradhi yatokanayo na ukosefu wa maji safi na salama (*waterborne diseases*) kama kipindupindu, kuhara, kutapika na kadhalika. Serikali yetu inapoteza zaidi ya fedha za kimarekani dola milioni 72 kila mwaka ili kutibu magonjwa hayo. Je, si vyema tukakinga kuliko kuponya kwa kuthubutu kupeleka fedha nyingi kwenye bajeti hii ili kuepukana na matumizi makubwa ya kugharamikia matibabu ya wagonjwa hao na hata vifo vinavyosababishwa na magonjwa hayo (*Waterborne diseases*)?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze maelezo yangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake aliyowasilisha Bungeni. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara. Sera ya Taifa inasema kuwa umbali wa kupata maji safi na salama

usizidi mita 400 kutoka kwenye makazi. Hali halisi kwa sasa bado ni changamoto kwani wananchi wanasafiri umbali mrefu sana kilomita moja na zaidi kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Ilani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 inasema hadi kufikia mwaka 2020 zaidi ya asilimia 70 ya wananchi vijijini watakuwa wanapata maji safi na salama. Leo ni mwaka 2017 ni miaka mitatu tu kufikia 2020 lakini utekelezaji hauonekani kabisa. Nimeangalia bajeti, fedha zilizotengwa katika mkoa wangu zimeelekeza tu katika kuboresha miji. Majimbo yaliyopo vijijini, sijaona mpango wowote. Je, tutawezaje sasa kufikia malengo ya asilimia 70 wakati kila bajeti hakuna mpango wowote?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa majumuisho ningependa kufahamu mpango wa kupeleka maji katika Jimbo la Busanda. Kwanza tumezungukwa na Ziwa Victoria, naomba nipate mpango wa Serikali wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naishauri Serikali iunde Wakala wa Maji Vijijini. Hii itasaidia utekelezaji wa miradi ya maji vijijini kama ilivyo *REA*. Miradi mingi ya maji vijijini tunaona inasuasua sana hasa ni kutokana na kutokuwa na usimamizi mzuri. Ni imani yangu kwa usimamizi kupitia Wakala wa Maji Vijijini utawezesha ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni juu ya ongezeko la fedha kufikia shilingi mia kutokana na manunuzi ya *petrol/diesel*. Fedha hii ipelekwe kwenye Mfuko wa Maji. Vile vile tunaomba asilimia 70 ya fedha hii ilenge kuboresha miradi ya maji vijijini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba katika bajeti iliyopita fedha hizi za Mfuko zilipelekwa kuboresha maji mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanaishi vijijini. Tukiboresha maji vijijini tutapunguza changamoto mbalimbali za magonjwa

yatokanayo na maji machafu (*water borne diseases*). Vile vile tutainua uchumi unaopotea kwa kufuata maji umbali mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu zuio la kulima vinyungu. Kilimo cha mabondeni (vinyungu) ni mkombozi wa wananchi wa Mafinga, Mufindi, Iringa na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Hata hivyo, Serikali mmezuia kilimo cha vinyungu bila kufanya tathmini ya kina. Watendaji wa Serikali wameshindwa kutafsiri maagizo na kupanikisha (*make panic*) wananchi kwa kutishia kufyeka mazao yao, kuweka alama za 'X' na kuwapa *notice* ya siku tisini. Ndugu zangu lazima kuwe na tafsiri pana kuhusu mabondeni na vyanzo vya maji. Kuna maeneo ambayo kwa vigezo vyovyote wananchi hata wakilima haiathiri suala la mtiririko wa maji au vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha mita sitini kisiwe *uniform*, kuna maeneo ingeweza kuwa mita kumi au ishirini. Nashauri *very strongly* tafsiri ya Sheria isipotoshwe. Kilimo cha mabondeni yapo maeneo hayahusiani na hayana *connection* na Mto Ruaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ziara ya Makamu wa Rais Mkoani Iringa kuhusiana na kuhuisha na kufufua vyanzo vya maji imetafsiriwa tofauti, sasa imekuwa ni vitisho, wananchi hawana amani. Nashauri na naomba suala hili lizingatie pia kuwa bado hatuna miundombinu ya kumwagilia, hivyo si kila eneo tuweke zuio la mita sitini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mafinga Mjini. Mji wa Mafinga pamoja na kuwa ni Halmashauri ya Mji bado kuna vijiji kumi na moja, naomba mipango ya Wizara izingatie kuwa pamoja na kuwa ni mji tuna maeneo ni vijiji, hivyo tuisahauliane katika mipango ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, pamoja na kuwa suala la utumishi ni la TAMISEMI na Utumishi, ikama ya

watumishi wa mamlaka ya maji ni wachache, Mhandisi wa Maji wa Halmashauri hana msaidizi, yuko peke yake. Naomba tuongezewe watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KAPT. (MST). GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji mradi wa maji Makonde hauridhishi. Tunapata maji ya bomba chini ya asilimia 30 ambayo ni kidogo sana ukilinganisha kitaifa. Moja, *booster station* ya kati ya Mkunya na Makote ilijengwa tangu 2006 lakini haijakamilika na haijakabidhiwa, kwa nini hawaifanyii kazi? Serikali ieleze mradi huu utakamilika na kukabidhiwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, mabomba na mitambo ya Mradi wa Maji Makonde yamechakaa. Chanzo cha Mkunya kinatakiwa kuwa na *pump* tatu lakini iko moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha Mitema kinahitaji *pump* sita ila ziko mbili tu. Mradi uliagizwa kutangaza tenda ya kubadilisha mabomba kwa shilingi bilioni mbili, mkandarasi alipatikana lakini fedha hazikutumwa. Serikali inunue kwanza *pump* na iharakishe upatikanaji wa mkopo kutoka India, ulioahidiwa, ili mradi uweze kukarabatiwa na kuongeza upatikanaji wa maji. Msimu wa mvua kwetu umekwisha wasio na visima hawawezi tena kukinga maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu ya umwagiliaji ya Chikwedu – Chipamanda. Tumelezwa mkataba bado kwa sababu taratibu za manunuzi zimechelewa Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya. Hili halikubaliki, halmashauri isimamiwe skimu iweze kukamilishwa tuweze kuendelea kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Wilaya ya Newala ilikuwa na mradi mdogo wa maji – Luchemo. Mradi huu ulikumbwa na mafuriko mwaka 1990 hivyo ukafa. Wizara

haijachukua hatua za kuufufua. Nashauri mradi huu ujengwe upya maana wananchi waliokuwa wanategemea mradi huo sasa hawapati maji safi ya bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa jana 2016 tulipata taarifa kuwa kuna fedha zilizopelekwa kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka Serikali ya Muungano (Fedha hizo zinatoka Serikali ya India) kwa lengo la kufanya utatuzi wa kero za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kero hiyo inazidi kuwa kubwa na kutishia vibarua vyetu kama Wabunge. Je, fedha hizo kweli zilipelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano ilipata mrejesho wowote juu ya suala hili? Serikali ya Muungano ina nini cha kusema kuhusiana na kadhia hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kuwa Serikali ya India ina makusudio ya kuikopesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dola za Kimarekani 500 milioni na hatimaye Zanzibar kufaidika na fedha hizo, Zanzibar mgao wake ni kiasi gani kati ya hizo? Je, nini kinachokwamisha mkopo tajwa usitolewe mpaka sasa na hasa ukitilia maanani kuwa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inatuelekeza utatuzi wa kero hiyo?

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hii. Nichangie hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Wizara. Nioneshe masikitiko makubwa sana kuona kuwa bajeti ya Wizara hii muhimu na inayomgusa kila Mtanzania badala ya kuongezeka, imepungua. Ni ukweli usiofichika kila Mheshimiwa Mbunge hapa ana shida ya maji katika jimbo lake. Kwa mfano mdogo tu bajeti ya Halmashauri yangu ya Kilindi ya mwaka wa fedha 2016/2017 ilikuwa shilingi bilioni

3.7 lakini mwaka huu imeshuka hadi shilingi bilioni 1.6. Hivi Wilaya hii yenye ukame mkubwa na yenye vijiji 102, kata 21 na vitongoji 650 bajeti hii itatosha kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inao Mfuko wa Maji, nasikitika kiasi kilichokusanywa ni kidogo sana. Ushauri wangu; badala ya kutoza sh.50/= katika lita ya mafuta ya dizeli na *petrol* tozo hii ipande iwe sh.100/= . Hii itasaidia kupunguza kero ya maji. Vile vile naamini tusipopunguza kero hii wananchi watakata tamaa na Serikali yao. Ikumbukwe wanaopata shida sana ni mama zetu na hasa waishio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa Miradi. Katika maeneo ambayo Serikali imetoa fedha nyingi hakuna utaratibu ulio rasmi kati ya Wilaya hii na TAMISEMI na hii imepelekea miradi mingi kutekekelezwa chini ya kiwango. Nishauri sasa miradi yote ya maji ifanyiwe "*Perfomance Auditing*" kupitia ofisi ya CAG.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili litaimarisha uwajibikaji na miradi mingi iwe na tija. Mfano mzuri ni mradi wa maji kutoka Wami kwenda Vijiji vya Chalinze, mkaguzi alibainisha namna ambavyo wakandarasi wanavyoisababishia Serikali hasara. Ni imani yangu Serikali itaona umuhimu wa kufanya ukaguzi wa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Visima vya Maji Makao Makuu ya Wilaya. Niipongeze Wizara kwa kunichambia visima vinne katika halmashauri yangu kwa msaada mkubwa kupitia Katibu Mkuu wa Wizara ambaye kwa sasa ni mstaafu. Visima hivyo vimeainishwa katika jedwali Na. 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Vijiji vya Sanje, Vilindwa, Nkama na Mafisa vimechimbwa lakini bado miundombinu ya kukamilisha miradi hii iweze kufanya kazi bado. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, maeneo haya yote yana shida kubwa sana ya maji. Miradi hii ikikamilika itasaidia mamlaka ya maji ya Songe iweze kufanya kazi kwa kujitegemea na ni takribani miezi sita sasa imepita toka wakala wa visima alipochimba.



Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki wa Sekta binafsi katika Sekta ya Maji na Umwagiliaji. Nipongeze juu ya wazo hili, ni wazo sahihi na pengine limechelewa. Naamini kabisa kwa changamoto hii ya tatizo la maji bila kushirikisha sekta binafsi kwa mpango wa PPP hatutaweza kufika mbali. Niishauri Serikali ifanye hima kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi jambo hili lianze haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni kubwa na yenye wananchi wengi. Kwa kushirikisha sekta binafsi ni wazi kutakuwa na gharama katika kuleta huduma hii ya maji, lakini vyema wananchi wetu wachangie katika kupata huduma ya maji kuliko kusubiri huduma ya bure kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchimbaji wa Mabwawa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona ametaja bwawa moja tu la Kwamaligwa, wakati katika Jimbo langu tunalo bwawa lingine la Jungu ambalo lipo katika hatua za umaliziaji, lakini sijaona mahali popote tulipotengewa fedha. Nitaomba sana majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa nini bwawa hili halijatengewa fedha, lakini pia Wilaya yote? Njia bora ya kuwapatia wananchi hawa huduma ya maji ni kuchimba mabwawa mengi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo bwawa moja tu la Kwamaligwa. Niombe Mheshimiwa Waziri tupatiwe mabwawa ya kutosha katika Jimbo langu lenye jamii ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi kuomba Mradi wa Maji. Wilaya ya Kilindi hatuna mto hata mmoja wala ziwa, nashangaa Wizara imeweza kutenga fedha katika maeneo yenye changamoto kama zetu wamepewa au kutengewa fedha nyingi za miradi ya maji lakini maskini Wilaya yangu haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri amtume Mheshimiwa Naibu Waziri au watumishi waliopo chini yake waje Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupata mradi mkubwa kama vile *HTM* ambao umefika Handeni kwa kutoa maji Mto Ruvu. Kwa nini Wizara imeshindwa kufikisha mradi huu Kilindi?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri alike na kutazama Wilaya ya Kilindi kwamba nao ni miongoni mwa maeneo yenye ukame na wanahitaji sana kupatiwa mradi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Maji ni Uhai. Maji ni kila kitu katika maisha ya kila siku ya binadamu; ndiyo maana ukaja msimamo kuwa maji ni uhai. Tukizungumzia uhai tunazungumzia maisha ya kuweza kuishi na kuleta afya njema ambayo yatatengeneza uwezo wa mwanadamu na viumbe vingine viweze kuishi na kuleta tija na mwisho kutimiza kiu yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Serikali ione sasa umuhimu wa kuvuna maji. Yaani iandae mkakati wa makusudi wa kuvuna maji hususani wakati wa mvua na hata maji yanayoporomoka katika milima yetu. Ni jambo la ajabu wakati wa mvua kuwa na mafuriko na baadaye mifugo na binadamu ikaanza kufa kutokana na ukame. Kuwe na utaratibu wa kujenga mabwawa ya kuhifadhia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwe na mfumo wa kuvuna maji kwa kuhakikisha nyumba zote zinazojengwa ziwe na mfumo wa kuvuna maji wakati wa mvua, hii itasaidia sana kero hili kuondoka. Pia suala la kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini limejadiliwa, sana na leo hii niulize Wizara na Serikali, uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini utanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni suala nyeti na hasa kwa sababu Rais wetu anatamani kuwatua kina mama na watoto kuwatua ndoo ya maji kichwani, hivyo kuna haja ya kutimiza azma ya Rais Mheshimiwa Dkt. John

Pombe Magufuli. Hivyo Serikali ione sasa umuhimu wa kuokoa taifa hili kwa kuwanusuru kina mama na watoto vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia tisa ya vifo vya watoto vinatokana na kutumia maji yasiyo safi na salama. Kuna maradhi ya milipuko kama vile *Typhod*, Kipindupindu na kuharisha na kutapika. Ni wakati sasa wa kupunguza vifo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mfuko tulioongeza tujue matumizi yake yakoje. Pia tunaomba kuwe na tozo, kila lita moja ya mafuta itozwe 100 kwa kila lita ziende kwenye maji au Mfuko wa Maji. Hali kadhalika asilimia 70 ipelekwe kweneye miradi ya maji vijijini na asilimia 30 miradi ya mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sasa wakati wa kumtua mama ndoo kichwani umefika; nazungumza hivyo kwa msisitizo; ni wakati sasa kina mama na watoto kufanya kazi nyingine za kimaendeleo badala ya kufuata maji sehemu za mbali na kutumia saa moja kutafuta maji au wastani dakika 33 kufuata maji. Ni shida na ni kero sana kwa wananchi; wananchi wanakosa kushiriki mambo mengi ya kimaendeleo. Hata hivyo zile mita 400 za kupata maji si toshelezi, hivyo Serikali ikishirikiana na Wizara walione hili kuwa ni bughudha na kero kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ione umuhimu wa hili na kuongeza bajeti ya maji ili tupate muda wa kufanya kazi za maendeleo. Pia lazima tuwe na msisitizo katika Kilimo cha Umwagiliaji kwani Kilimo ni Uti wa Mgongo hivyo tutumie mito yetu vizuri kwa kuweka mfumo mzuri wa kuweza kumwagilia ili kilimo hcetu badala ya kungojea mvua tu tutumie vyanzo hivi ili kuweza kukuumarisha kilimo chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali izingatie suala hili kwa upana na huruma ili iweze kumuokoa Mtanzania katika shida hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa utendaji wake na mipango yake ya kushughulikia tatizo la maji nchini kwetu, pamoja na utendaji wa Mawaziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa maandishi utajielekeza kwenye Mradi wa Maji wa Chalinze - Wami uliopo katika Halmashauri ya Chalinze, Wilaya ya Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali juu ya kusuasua kwa mkandarasi wa mradi huu wa Wami - Chalinze na kupelekea hali ngumu ya upatikanaji wa maji Jimbo la Chalinze, wananchi wa Chalinze wangependa kupata ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kwa kweli mradi wa maji Wami – Chalinze Awamu ya Tatu unasuasua, mpaka sasa kuna maeneo ndani ya Jimbo la Chalinze ambayo hayana maji ya bomba kwa zaidi ya miezi sita sasa.

(ii) Tunamshukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kutembelea mradi huu wa Wami - Chalinze mwisho wa mwezi Machi, tatizo lishughulikiwe mara moja na maji yawe yanatoka ndani ya siku 100 na mkandarasi alipewa siku 100 ya kuonesha kasi yake ya utekelezaji. Je, mpaka sasa ni kiwango gani cha tozo kwa kuchelewesha mradi?

(iii) Je, Wizara baada ya siku 100 alizotoa Waziri Mkuu kuisha na kasi ya mkandarasi kuwa ndogo, Wizara itakuwa tayari kufikiria upya juu ya mkandarasi wa mradi huu wa maji wa Wami - Chalinze Awamu ya Tatu, kwani kama sitakosea kuna kumbukumbu zinaonyesha mkandarasi huyu ana rekodi zisizoridhisha kwenye miradi mingine ya aina hii katika maeneo mengine.

(iv) Uendeshaji wa mradi huu wa maji wa Chalinze, Menejimenti ya *CHALIWASA* inaonyesha kushindwa kabisa. Uendeshaji wa mradi uko tofauti sana na wakati ukiwa chini ya mkandarasi toka China. Wananchi wengi wa Chalinze wanalalamika sana na *bill* zinazotolewa. Utokaji wa maji yenyewe usafi wa maji ni shida, waliokatiwa huduma ya maji bado wanachajwa *service charge*.

(v) Mamlaka ya Maji Chalinze (*CHALIWASA*) wamejitoa kuagiza vifaa vya kuunganisha maji hususan mabomba badala yake wameliacha jukumu hili nyeti kwa wateja wa maji wasio na uelewa kitalaam wa ubora wa vifaa vilivyo sokoni hususan mabomba. Je, taratibu na sheria zinaruhusu?

(vi) Kwa kuwa Mji/Halmashauri ya Chalinze sasa ni mji wa viwanda na kuna ujenzi wa viwanda, mfano ujenzi wa Kiwanda cha *Tiles* Chalinze, ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Matunda, Mboga cha Sayona kinachotarajiwa kukamilika hivi karibuni. Hata hivyo kutokana na tatizo la maji Chalinze linaweza kuathiri kabisa ufanisi wa uzalishaji wa viwanda hivi.

Kutokana na shida hii ya maji Chalinze uongozi wa kampuni hii ulikutana na uongozi wa *CHALIWASA* kujua tatizo ni nini, hasa moja ya tatizo walisema uchakavu wa *pump* na machujio ya maji na baadhi ya vifaa. Serikali kwa sasa haina fungu kwa ajili ya kazi hiyo. Kupitia mazungumzo hayo mwekezaji ambaye ni Kampuni ya *Sayona Fruits* ilionesha utayari wa kuagiza hivyo vifaa nje ya nchi ili uweze kufungwa na hatimaye gharama hiyo ijumuishwe na kukatwa kwa awamu kutoka kwenye *bill* ya maji ya kiwanda itakayopelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, menejimenti ya *CHALIWASA* inashauri iandikwe barua kwa Mawaziri wa Maji na Viwanda ili watoe ridhaa ya mwekezaji aendelee na utaratibu wa kuangiza hivyo vifaa. Mpaka sasa Wizara ya Maji haijatoa mwelekeo au maelekezo yoyote, jambo hili linaweza kufifisha ari za wawekezaji wetu. Kiwanda hiki kinatarajia kuzalisha/kusindika tani 60 kwa siku na

kimejengwa kwa gharama ya zaidi ya bilioni 150, na rasilimaji kubwa ni upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara kutoa msimamo wake kwenye barua ya maombi iliyoandikwa na mwekezaji Kampuni ya *Sayona Fruits* kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa maswali ya sera ya Serikali ya viwanda na wananchi wa Chalinze ambao watafaidika kwa uboreshaji wa miundombinu ya mradi huu wa maji Chalinze wa awamu zilizopita za kwanza na pili ambayo ni chakavu.

(vii) Suala la tatizo la maji katika Majimbo ya Kisarawe na Bagamoyo ni kubwa na moja ya sababu ni kumezwa na mipango ya Jiji la Dar es Salaam. Haiwezekani Kisarawe au Bagamoyo huduma za maji ziendeshwe na *DAWASCO/DAWASA* ambayo wenyewe wamezidiwa kiutendaji kutokana na mahitaji ya Dar es Salaam na maelezo yake kutokana na wingi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali/Wizara kuunda Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Pwani kama ilivyo kwa mikoa mingine na kuziimarisha kuzifufua Mamlaka za Maji za Wilaya ili ziwe na mamlaka kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi wa visima vya Kimbiji na Mpera ambapo ukikamilika unatarajiwa kuzalisha lita milioni 260 kwa siku ambapo maeneo yafuatavyo yatafikiwa; Gongo la Mboto, Chanika, Pugu, Ukonga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maeneo haya yapo karibu na Kisarawe, naishauri Serikali kuona uwezekano wa kuweza kupata huduma ya maji kutokana na tatizo kubwa la maji maeneo ya Kisarawe.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maji ya Benki ya Dunia katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru miradi iliyokamilika ni minne, miradi mitatu inasuasua kwa kuchelewa fedha na mitatu mingine haijaanza kabisa kutokana na matatizo mbalimbali. Hivyo, tunaomba miradi ile mitatu inayoendelea ya Mbesa, Mtina na Matemanga ipelekewe fedha ili ikamilike kwa sababu ni muda mrefu wakandarasi wanasuasua kukamilisha miradi hiyo. Vilevile miradi mitatu ya Mchoteka, Matemanga na Namasakata ianze kwa vile wananchi walishachangia sehemu ya fedha kama masharti ya miradi ile iliyohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Tunduru vyanzo vya maji ni vingi sana lakini miundombinu ni michache sana. Maji yanapatikana ndani ya mita 100 za urefu ardhini, hivyo tunahitaji gari la kuchimbia visima vifupi na virefu ili kupunguza gharama za upatikanaji wa maji. Nadhani kama Halmashauri yetu ingekuwa na gari la kuchimbia visima tungeweza kusaidia kupata maji kwa wepesi zaidi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji inayotumia *generator* wananchi wameshindwa kuendesha hivyo Serikali iangalie upya katika miradi ya jamii kuweka *solar* badala ya kutumia *generator* ambazo wananchi wameshindwa kununua *diesel* kuendesha mashine za maji. Hivyo, ninaomba miradi iliyobaki ni vema mashine na *pump* zinunuliwe zote zinazotumia *solar* badala ya *generator* ya *diesel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya umwagiliaji Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imebahatika kuwa na maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na maeneo kadhaa tayari yana miradi ya umwagiliaji, lakini tatizo wataalamu wetu wanatuangusha sana, miradi ile inatumika wakati wa kifuku tu, kiangazi miradi hii haifanyi kazi kutokana na upungufu mkubwa wa maji katika mito na mabwawa yanayotumika, ubovu wa miundombinu ya mifereji kutokana na mapungufu makubwa ya kitaalamu. Miradi hii inatumia fedha nyingi sana lakini haifanyi kazi

iliyokusudiwa. Ninaomba wataalam wetu kutumia utalaam wao kwa uangalifu sana ili kufanya miradi hiyo iwe endelevu, miradi ya umwagiliaji hailingani na kiasi cha pesa kinachotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tunduru bado tuna maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni vema basi tukafikiria kutumia maji ya kuchimba visima virefu na vifupi na kutumia mabomba ya kawaida badala ya kutumia mabanio ya kujenga mifereji inayotegemea maji ya mito au mabwawa ambayo kwa sasa yanakosa maji kipindi cha kiangazi, hivyo kutokuwa na uzalishaji kwa sababu maji yanapungua sana hayawezi kupanda kwenye mifereji na mitaro iliyojengwa na mifereji mingi inabomolewa wakati wa kipupwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maji ndiyo kila kitu katika maisha ya binadamu, basi ni vema tozo ya maji kwenye mafuta ingeweza kuongezwa kutoka 100 ili kuongeza fedha za miradi ya maji vijijini na ni vema ukaanzishwa Mfuko wa Maji Vijijini ili kuharakisha maendeleo ya miradi ya maji vijijini.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali imeendelea kupunguza tatizo la maji nchini. Singida Mjini katika bajeti ya mwaka 2016/2017 tulipewa shilingi bilioni mbili mpaka sasa hivi fedha hizo hazijaja. Naiomba Serikali ituletee fedha hizo tuweze kukamilisha miradi ya maji iliyopo. Bajeti hiyo ya mwaka 2016/2017 Serikali pia iliahidi kutupatia fedha za fidia shilingi bilioni tatu kwa wananchi wa eneo la Irao - Kisaki waliopisha mradi wa maji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya vijiji kumi vya maji vinavyofadhiliwa na Benki ya Dunia, miradi hii imejengwa Singida Mjini bahati mbaya wananchi hawana maji mpaka sasa hivi. Naomba Serikali ije ifanye tathimini ya miradi hiyo na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa waliohusika kukwamisha miradi hiyo.



**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa kutatua changamoto ya maji. Nimpongeze Waziri na watumishi wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweze kutazama upya upande wa tozo ya mafuta kuweka shilingi 100 ili Watanzania waweze kupata maji kwa kutumia mfuko katika fedha za maji zilizopelekwa hadi Machi kati ya shilingi 181,209,813,609. Utaona asilimia ni 52.7 ambazo ndizo zilizotokana na tozo hiyo, upo umuhimu mkubwa kuhakikisha kuwa pesa hiyo ndiyo inafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyikiti, ninaishukuru Serikali kwa kutupatia pesa kwa ajili ujenzi wa bwawa la Itabi, Wilaya yangu ya Itilima pamoja na kupata pesa za Halmashauri kuingia katika utekelezaji wa visima kumi na kupata shilingi milioni 49 kuweka *pump* kwenye mabomba pamoja na kupata fedha za mradi wa mabwawa sita ya Mwamapalala, Nhobora, Rugulu Sunzura, Chinamili na Sawinda yote hii ni juhudi ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa mipango yote hiyo iliyoanzishwa kwenye bajeti na kiwango cha pesa kilichopangwa na Serikali ifanye utaratibu mzuri wa upatikanaji wa fedha hiyo katika Wilaya ya Itilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na timu yao kwa kazi nzuri inayofanyika katika kuboresha huduma za maji hasa katika Halmashauri nyingine kasoro Halmashauri ya Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchungu nina masikitiko makubwa juu ya mwenendo wa miradi ya maji

katika Wilaya yangu. Nakumbushia barua yangu kwako Mheshimiwa Waziri juu ya tatizo la maji, katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 133, Ziwa Nyasa linaongoza kwa kuwa na ujazo mkubwa wa maji. Mwaka 2015/2016 milimita 1,359.78 na mwaka 2014/2015 milimita 1208.92. Ukurasa 135 Ruhuhu ni wa pili kwa wingi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara inatoa maji toka Mwanza kupeleka Shinyanga/Tabora zaidi ya kilometa 150, lakini wananchi wa Nyasa wana umbali chini ya kilometa 1- 3 kutoka Ziwa Nyasa na hawapati maji salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Kingirikiti kulikuwa na mradi mkubwa wa maji ulioteklezwa toka tukiwa Wilaya ya Mbinga, zaidi ya shilingi milioni 600 lakini mpaka leo hakuna maji. Nilitoa fedha zangu shilingi milioni 1.5 kusaidia upimaji wa maeneo ya kuboresha upatikanaji wa maji katika Kata ya Tingi, mpaka leo hakuna chochote kinachoendelea. Kituo cha Afya cha Lupalaba kina hali mbaya, niliomba hata ifanyike kazi ya kunusuru kata hiyo mpaka leo hakuna kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata ya Mbaha hasa kijiji cha Ndumbi hamna maji, hali ni mbaya. Mji wa Mbamba Bay Makao Makuu ya Wilaya hakuna maji, lakini maji ya Ziwa Nyasa yapo umbali wa mita 30 tu kutoka makazi na shughuli za watu, lakini bado watu hao wanakosa maji salama. Mheshimiwa Waziri, nadhani kuna tatizo Mhandisi waMaji wa Wilaya yangu nadhani anahitaji kusaidiwa, uwezo ni mdogo, yupo kwenye *comfort* sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kabrasha sijaona mradi *specific* kuhusu Wilaya ya Nyasa. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Naibu Katibu Mkuu, wote hawa ni wanangu kule Rukwa, Katibu Mkuu pia ni mwanangu kule Wizara ya Elimu, mbona hamnihurumii? Leo nimejipanga, kesho kusipoeleweka nitashika shilingi kiaina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitengewe fedha kisha nipewe wataalam wa kunisaidia, suala la maji

halijapata majibu kabisa kwenye Jimbo langu, Mbinga tupewe fedha mpaka waseme fedha za mradi wa Kingirikiti wamepeleka wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashika kifungu.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza uongozi wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pongezi ziende kwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Injinia Gerson Lwenge, Naibu Waziri Mheshimiwa Injinia Isack Kamwelwe, Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo na Naibu Katibu Mkuu Injinia Emmanuel Kalobelolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yangu ya uchangiaji ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Wizara kupewa fedha za kutosha. Takwimu za mwaka jana zinaonyesha Wizara ilitengewe fedha za maendeleo shilingi bilioni 915.2, hadi Machi zimetolewa shilingi bilioni 181.2 sawa na asilimia 19.8. Hakuna miujiza kuwezesha Wizara hii kupata asilimia 80.2 zilizobaki. Tunasisitiza Hazina kutoa fedha kwa wakati kwa Wizara hii. Mwaka huu fedha za maendeleo zimetengwa shilingi bilioni 623.6, fedha ambazo ni pungufu ikilinganishwa na mwaka jana. Kufidia pengo hili nakubaliana na wazo la kuongeze tozo kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100 kwa lita ya *diesel* na *petrol*.

Pili, miradi ya maji 17 ya *AMREF*. Kwa niaba ya wananchi wa Nanyamba napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kutoa fedha za kukarabati miradi ya maji iliyokuwa imejengwa kwa ufadhili wa *AMREF*, ukarabati unaendelea na Halmashauri Mji ilipokea shilingi milioni 400 ya awali. Ni matarajio yetu kuwa kiasi kilichobaki kitatoka mapema ili mkandarasi aweze kulipwa kwa wakati.

Tatu, ni kuhusu mradi wa maji wa Makonde. Mradi huu unahitaji ukarabati mkubwa, tunashakuru Serikali kwa kutenga fedha shilingi milioni 87.41 mkopo kutoka India. Ukurasa wa 62 wa kitabu cha bajeti imeelezwa utekelezaji unianza mwaka huu lakini ukurasa 173 imeandikwa mradi

wa Makonde upo *Phase III*. Hii maana yake nini? Wakati ukihitimisha Waziri atoe ufafanuzi kwa nini kuna maelezo ya kuwekwa *Phase III* mradi wa Makonde utapewa fedha baada ya kukamilika utekelezaji wa *Phase I and II*? Ufafanuzi unahitajika kuhusu utata huu unaotolewa na baadhi ya watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nakumbusha Wizara kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Makonde na kupeleka kata vijiji 23 vya Halmashauri ya Mji Nanyamba. Andiko la awali limeshawaliwa na usanifu wa mradi unaendelea.

Nne, mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma hadi Manispaa ya Mtwara Mikindani; mradi huu unatoa maji kijiji cha Mayembe chini kilichopo Halmashauri Mji ya Nanyamba na matarajio ni vijiji vyote vya jirani wapate maji, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika hapa na kuahidi vijiji vya Mayemba Juu, Chawi na Kiromba, vijiji vilivyotajwa 26 ni vichache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nashauri Wizara iangalie uwezekano wa usanifu mradi mwingine wa kutoa maji Mto Ruvuma na kupeleka vijiji vya Halmashauri ya Mji Nanyamba. Kata za Kiromba, Kiyanga, Mtiririko, Mbembako na Kitaya wanaweza kupata maji kutoka Mto Ruvuma.

**MHE. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya, tunashukuru kwa jitihada zenu zote japo bajeti hii ni finyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Wabunge wenzangu kuomba nyongeza ya bajeti hiyo. Maji ni uhai, maji ni afya na maji ni viwanda. Kila taasisi inahitaji maji mashule,vyuo, hospitali na kadhalika, tunaomba Wizara hii muhimu ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri Wizara kuungana na Wabunge kupiga vita, wafugaji

wanaonyweshwa mifugo yao kwenye vyanzo vya maji. Kwa mfano, Wilaya ya Kilombero ni bonde zuri kwa kilimo, lakini mifugo imesababisha mito kukauka, wakulima kunyanyasika na wageni wafugaji kwa sababu ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mfuko wa Maji Vijijini uanzishwe kama ilivyo kwenye umeme itasaidia sana.

Mwisho ninawapongeza sana kwa miradi mingi ya maji inayofanya vizuri sana, tunawaomba bajeti longezwe ili mfano vizuri zaidi.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote. Nitazungumzia maeneo mawili tu, kwanza utunzaji wa vyanzo vya maji na uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasisitiza Serikali izidi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji, narejea kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji ukurasa wa 16, Ibara ya 34 naomba kunukuu; "Wizara imeendelea kuvitambua, kuviwekea mipaka na kuvitangaza vyanzo vya maji kuwa maeneo tengefu ili kuvilinda na kuvihifadhi kwa ajili ya kuzuia uharibifu na uchafuzi wa vyanzo hivyo." Ombi langu ni kwamba hata vile vyanzo vya maji vya mamlaka mbalimbali vipatiwe hati miliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya uvunaji wa maji ya mvua bado iko chini kabisa, kwa masikitio makubwa sikuona kabisa msisitizo wa jambo hili kwenye hotuba. Ninaomba kujua Serikali ina mpango gani wa kunufaika na maji yanayotiririka hovyona kupotelea baharini wakati wa mvua. Mfano, barabara ya Dar es Salaam - Dodoma eneo la Kibaigwa pande zote mbili maji yanatua na wakati mwingine yaliuma, lakini hakuna juhudi za kuyatumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninakukumbusha mradi wa maji wa Nyumba ya Mungu - Mwanga, Same, Mombo, ni lini hasa utamalizika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, bajeti iliyotengwa katika Wizara hii haitoshi, Serikali iongeze fedha katika Wizara hii; pili ni kuhusu maombi ya fedha kwa ajili ya *Muze Group*. Mheshimiwa Naibu Waziri maombi ya mradi huu ni maombi ya kupeleka maji ya mserereko toka chanzo cha Mto Kalumbaleza na mradi huu unatarajiwa kupeleka maji katika vijiji kumi na mbili, kwa nini mradi huu haujatangewa fedha?

Tatu, miradi ya umwagiliaji tumekuwa tukiiombea pesa mfululizo miaka mitano hatujawahi kupewa, tatizo ni nini? Mradi wa umwagiliaji wa Maleza, mradi wa umwagiliaji wa Uzia na mradi wa umwagiliaji wa Msia. Naomba maelezo kwa nini Serikali haitoi pesa katika miradi hiyo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri yafuatayo; Serikali iongeze bajeti kwenye fungu la maendeleo na pesa hii ipo kwenye mafuta, umeme na maji yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya umwagiliaji inakumbana na pingamizi kwa kuwa ujenzi wa miundombinu umejielekeza kujenga mabwawa kuinga maji. Hapa wananchi wanaogopa kupoteza ardhi zao, kwa nini tusitumie mfumo wa visima virefu na *wind wheels* kuweka maji kwenye matanki na kusambaza kwa *gravity* kwa kuwa gharama ni nafuu na eneo linalopotea ni dogo. Mradi kama huu upo kata ya Kanyalla lbada na umepingwa na wananchi kwa sababu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la maji Mjini Geita, hivi sasa Mradi wa Maji wa LV-Watsan unasuasua sana mpaka leo miezi minne imepita, mkandarasi ameshindwa

kumaliza kazi, nashauri mtu huyu afutwe kwenye orodha ya wakandarasi kwa kuwa hana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa maji katika Mji wa Kasamwe, naishauri Serikali kuunganisha mradi mpya wa maji wa fedha za India kwa Mji wa Geita ili maji yake yafike Kasamwa, kwa sababu kwa mujibu wa wataalamu hivi sasa kuna tanki kubwa la maji Buhalanda ambalo lipo kilometa 10 tu kutoka Kasamwa na ambapo maji yatafika kwa *gravity* na kwa kuanzia ziwekwe *DP's* tu kwenye mitaa ili wananchi wapate maji, badala ya sasa kutumia bwawa ambalo gharama yake ni kubwa

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kunipa majibu maji katika Kata za Shiloleli, Bulela, Ihanamilo, Nyanguku, Mgusu na Bung'wangoko yatafika kupitia mradi huu wa fedha za India? Kwa sababu hizi kata ni sehemu ya kata za Mji wa Geita Jimbo la Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuongeza michango yangu baada ya kuchangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linalosumbua katika miradi ya maji inayoendelea kwani imeshindwa kukamilika, miradi ya maji inayoendelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ni minne, hali ya ujenzi hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Isunga hadi Kadashi asilimia 50, kazi kubwa iliyobaki ni ulazaji wa bomba ambapo bomba linalohitajika ni kilometa 22.

(ii) Igunguya hadi Nyanhiga mpaka Igunguya asilimia 95, mradi upo katika majaribio na Nyanhiga amebakiza kulaza bomba kilometa 11.

(iii) Igumangobo asilimia asilimia 75, amebakiza kulaza bomba mita 150 na kukamilisha ujenzi wa tenki.

(iv) Mhande hadi Shirima mpaka Izizimba 'A' asilimia 45 kazi kubwa iliyobaki kutandaza bomba kuu kilometa 40 na mtandao wa bomba vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ni kuwa wakandarasi kutoiamini Serikali kuhusiana na malipo yao kutokana na ucheleweshaji uliojitokeza huko nyuma. Serikali inasema nini katika kujenga imani kwa Wakandarasi ili waweze kufanya kazi kwa haraka na wakandarasi kushindwa kujituma au kuwa wazalendo kwa kufanya kazi kwa kasi na kwa ubora tarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba visima vingapi ni vibovu na viko maeneo gani na sababu ya ubovu, tuna visima 188 vibovu na sababu ya ubovu kunaibiwa kwa pampu, kuharibika kutokana na umri mkubwa na kuishiwa maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na Sera ya Maji ya mwaka 2002, uendeshaji na matengenezo kwa maji vijijini asilimia 100 ni wananchi kupitia Jumuiya za Watumiaji Maji (COWSO) wakati kwa Mamlaka za Maji za Wilaya na Mikoa Serikali inasaidia kutoa ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni imefika wakati Kamati za Maji au Jumuiya za Maji Vijijini kusaidiwa hasa kwa kukarabati visima vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima hivi vibovu viko katika maeneo yafuatayo; Bungulwa (5), Bupamwa (3), Fukalo (4), Hungumalwa (4), Malya (12), Mantare (8), Bungando (2), Igongwa (4), Ilula (4), Iseni (1), Kikubiji (5), Maligisu (3), Malya (13), Mhande (5), Mwabomba (9), Mwagi (7), Mwakilyambiti (7), Ng'hundi (6), Ngudu (6), Nkalalo (2), Nyambiti (11), Sumve (17) na Walla (18).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kata ambazo hazina kabisa huduma ya



maji safi na salama ni kata ya Shilembo ambapo kuna kisima kimoja tu vijiji vyote, vijiji ambavyo havina kabisa huduma ya maji ni Mantare (Mwampuru) na Ngulla (Nyambuyi).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuandaa vizuri hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia majedwali katika kitabu cha hotuba jedwali namba 13 la orodha ya visima vilivyochimbwa hadi mwezi Machi, 2017, sehemu inayoonesha uwezo wa kisima kuna maeneo yameachwa wazi na maeneo mengine yameachwa wazi kwa uzembe. Kwa mfano, kisima namba 204 cha Msijute kilichofadhiliwa na *ESRF* na kuchimbwa na Wakala wa Visima wa Serikali kuna uzembe mkubwa umefanyika. Baada ya kuchimba kisima waliletwa watu wa kupima uwezo wake wakatoa taarifa kwamba hakuna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa *ESRF* wamehitaji wapate taarifa itakayowaelekeza nini kifanyike ili maji yapatikane lakini miezi imepita bila mafanikio, binafsi wakala waliniambia niongeze shilingi milioni tatu ili wachimbe kisima kingine na baadae mwezi wa nne nikaambiwa niongeze shilingi milioni sita ili nichimbiwe kisima kingine. Ajabu ni kwamba watu wa bonde walipokuja wamepima na kuona kwamba maji yapo kwa asilimia 30 ya mita 150 zilizochimba, wamesema kwamba wale waliojaribu kupima uwezo wa kisima walitumia *pump* kubwa ambayo ilikausha maji kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yao ni kwamba zingetumika *pump* zenye uwezo tofauti na pia ilibidi wa-*flash* kisima, ushauri wangu kisima kile ni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Msijute ambao walimuamini Wakala wa Visima wa Serikali. Ni vema iandikwe taarifa ya ukweli na uwazi kwa *ESRF* ili aweze kuchukua hatua za ziada kuwasaidia wananchi wa kijiji cha Msijute wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, chunguzeni visima vyote ambavyo havioneshi uwezo wake mjue sababu na taarifa itolewe kuepusha ubabaishaji wa baadhi ya wachimbaji visima. Fikeni katika maeneo husika mkutane na wachimbaji na Mamlaka za Mabonde na wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mungu kwa kunijalia afya na nguvu za kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kipekee kuipongeza Serikali yangu kwa kazi nzuri inayofanyika kuanzia Rais wetu, Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla. Nampongeza sana Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa sana kwa Taifa letu, maeneo mengi hawana maji safi na salama, pia hata wale wanaopata maji wanayapata kwa umbali mrefu sana zaidi ya kilometa kumi mpaka 20. Kitu ambacho kinarudisha nyuma shughuli za maendeleo na kushusha uchumi wa Taifa na katika hili waathirika wakubwa ni wale walio vijijini ambao ni wakulima zaidi ya asilimia 70 na ndiyo wazalishaji wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Wizara ikiwezekana iongeze pesa kwenye bajeti kwa sababu bajeti hii imeshuka sana kulingana na mahitaji ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jimbo langu hali ni mbaya sana ya upatikanaji wa maji safi na salama, niishukuru sana Serikali kwa miradi ya zamani ya miaka ya 1970 ambayo ilikuwa imechakaa sana. Kazi ya kuboresha miundombinu imeanza katika kata ya Mabila, mradi wa Kilela - Isingiro, Kagenyi, Lukurayo na miradi mingine midogo. Miradi hii ni sehemu ndogo sana ya mahitaji ambayo ikikamilika itasaidia kama asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho la kuwapatia wananchi wa Kyerwa maji, niendeleo kushukuru Serikali kwa mradi mkubwa wa vijiji 57 kwenye kata 15 ambao uko kwenye hatua ya usanifu ambao hatua hii itakamilika mwezi wa Septemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulileta mapendekezo kuomba shilingi bilioni 12 kama kianzio ili tunapomaliza usanifu kazi ianze kuwanusuru wananchi wa Kyerwa na tatizo la upatikanji wa maji safi na salama, pia kuwandolea wananchi usumbufu wa kufuata maji mbali zaidi ya kilometa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kuona kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 mapendekezo yetu hayajakubalika kitu ambacho kitasababisha kusubiri mwaka 2018/2019. Naiomba sana Wizara, niko chini ya miguu yenu na kwa unyenyekevu mkubwa nakuomba Mheshimiwa Waziri uangalie namna yoyote ya kupata pesa ili tunapomaliza usanifu kazi ianze haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuongeza shilingi 100 kwenye mafuta na mimi nashauri Serikali yetu ikubali ili kuwaokoa Watanzania wanaopata mateso makubwa ya ukosefu wa maji safi na salama. Pia umbali wanaoupata kufuata maji mbali na baada ya kukubali ombi hilo na Kyerwa maombi yetu yapokelewe ya kutengewa shilingi bilioni 12 ili kuanza mradi wetu mkubwa wa vijiji vyetu 57 na kata 15, naomba sana Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maombi hayo bado kuna kata zingine ambazo hazijafikiwa na mradi mkubwa wa vijiji 57, niendeleo kuiomba Serikali kututengea pesa ili kuwapatia huduma hii muhimu wapiga kura wangu. Najua Serikali yangu na Mheshimiwa Waziri wangu ni sikivu, maombi yangu yatazingatiwa na kupewa umuhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika aya ya 21 ukurasa wa tisa na 10 ya hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, imeelezwa kwamba hali ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam imeimarika baada ya kukamilika kwa maboresho ya mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Hata hivyo, Wizara izingatie kuwa hali haijaimarika katika maeneo yanayohudumiwa na Ruvu Juu kwa upande wa Jimbo la Kibamba katika kata za Kwembe, Mbezi, Msigani, Saranga na Kibamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kufanya ziara ya haraka ya kikazi yenye kumhusisha Waziri wa Maji, Mbunge, *DAWASA* na *DAWASCO* ili kukagua maeneo yote ya mabomba ya Mchina ambayo nilipowasilisha hoja binafsi tarehe 4 Februari, 2013 Bungeni Serikali iliahidi kwamba baada ya kukamilika kwa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na ujenzi wa bomba maji yangukuwa yanatoka. Aidha, kwa upande wa maeneo katika kata hizo za Kibamba, Kwembe, Mbezi, Msigani na Sarange ambayo hayana mtandao wa usambazaji wa maji, kasi ya kuwaunganishia wananchi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba katika aya ya 135 ukurasa wa 72 na 73, Wizara imetaja maeneo ya Mbezi hadi Kiluvya na maeneo ya Kibamba, Msakuzi, Makabe, Malamba Mawili na Msigani. Upanuzi wa mfumo wa kusambaza maji katika maeneo hayo unasuasua, kadhalika yapo maeneo mengine katika kata hizo hayajatajwa katika orodha hiyo. Hivyo naomba Wizara inipatie orodha ya maeneo yote ambayo hayana mfumo wa kusambaza maji safi katika kata hizo tano na ratiba yenye kuonyesha ni lini maeneo hayo yatasambaziwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ruvu Chini ieleweke kwamba katika Jimbo la Kibamba kata pekee inayopata maji kutoka chanzo hiki ni kata ya Goba, katika aya ya 135 ukurasa wa 73 yanatajwa maeneo ya Kinzudi, Matosa na Mtaa wa Goba. Hata hivyo mtandao wa mabomba ya maji katika maeneo hayo haulingani kabisa na mahitaji. Aidha, ipo mitaa mingine katika kata ya Goba

ambayo haipo katika orodha ya kusambaziwa maji katika mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba kupewa orodha ya maeneo yote ya kata ya Goba yasiyokuwa na mtandao wa mabomba ya maji yenye kuonyesha ratiba ya lini yatawekewa mabomba ya maji. Naomba Wizara inaposhughulikia miradi ya maji ya Ruvu Chini kwa upande wa *DAWASA* na *DAWASCO* itoe kipaumbele maalum kwa kata ya Goba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika aya ya 133 ukurasa 71, Serikali imeeleza kwamba inaendelea kutekeleza mradi wa Bwawa la Kidunda unaogharimu dola za Marekani milioni 215. Hata hivyo, kimsingi hakuna utekelezaji unaoendelea kwa kuwa pamoja na usanifu kukamilika muda mrefu, mpaka sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha. Mradi huu ni wa kutoka wakati wa Mwalimu Nyerere mwaka 1980 na sasa ni wa dharura kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii nyeti na muhimu sana ya Maji na Umwagiliaji. Ni ukweli ulio dhahiri kabisa kwamba Wizara hii ni muhimu sana na ni uti wa mgongo wa Taifa hili na pia ninaunga sana ule msemo wa maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji Mheshimwa *Engineer* Kamwelwe kwa kufanya ziara muhimu kabisa Jimboni kwangu Mikumi na Wilayani kwetu Kilosa kwa ujumla. Mheshimiwa Kamwelwe alipokuwa Jimboni Mikumi alifanya na kuahidi mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha maji cha Sigareti kilichopo kata ya Ruaha, Mheshimiwa Naibu Waziri alituma wataalam wa Wilaya ya Kilosa wakakague chanzo hiki na wataalam walifanya hivyo na kunipa *report* ya kitaalamu kuwa chanzo hiki cha Sigareti ni chanzo cha mserereko chenye maji mengi, safi na salama, kinaweza kutoa

huduma kwa wananchi wa kata ya Ruaha yenye wakazi zaidi ya 30,000 na kata za jirani za Ruhembe na vijiji vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulikadiriwa kufikia kiasi cha pesa cha shilingi bilioni mbili na kidogo na nilipomletea Mheshimiwa Naibu Waziri aliahidi kuwa kiasi hicho cha pesa kitawekwa kwenye bajeti hii ya mwaka 2017/2018. Niliwaambia wananchi wasikivu wa kata ya Ruaha ambao walifurahi sana na kutoa pongezi nyingi kwa Serikali hii kwa kusikia kilio chao cha muda mrefu, lakini cha kusikitisha bajeti ya chanzo hiki muhimu cha maji cha Sigareti haipo kwenye taarifa ya bajeti hii.

Naomba Waziri atimize ahadi yake kwa wananchi wa kata ya Ruaha na kuwawekea au kutenga pesa hizo shilingi bilioni mbili ili mradi huu muhimu wa maji uweze kuanza kujengwa na kuokoa vifo vya akina mama na watoto wa kata ya Ruaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Madibila katika kata ya Mikumi niliwahi kuuliza ni lini Serikali itakarabati miundombinu na *intake* ya chanzo cha maji cha Madibila ambacho kilijengwa mwaka 1975 wakati idadi ya wakazi wa Mikumi ni watu 6000 tu na sasa imepita miaka 40 miundombinu ni ile ile chakavu sana na wakazi wa Mji Mdogo wa Mikumi wamefikia watu 30,000 na zaidi, Naibu Waziri alianiahidi kwenye majibu yake kuwa wanalitambua tatizo hilo na watalifanyia kazi kuanzia mwezi Julai mwaka huu, lakini sijaona pesa zikiwa zinatengwa *specifically* kwa ajili ya chanzo hiki muhimu cha maji cha Madibila kwa wakazi wa Mji Mdogo wa Mikumi. Naomba majibu je, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya mradi huu wa chanzo cha Madibila.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji vya Iyovi na Mto Mholanzi ni wazi Mji wa Mikumi ni mji wa kitalii na unakua kwa kasi sana kwa kupata wageni na watalii mbalimbali kutoka kona zote za dunia. Tatizo sugu la maji linapunguza sana kasi ya wawekezaji wa mahoteli na sekta mbalimbali za kukuza uchumi wakati Mikumi ina vyanzo vingi

sana vya maji kama Mto Iyovi na Mto Mholanzi. Je, ni lini sasa Serikali itavifanyia kazi vyanzo hivi vyenye maji mengi tena ya *gravity* au msereereko vyenye gharama nafuu kabisa kuokoa wananchi wa Mikumi na kukuza mji na uchumi wa wananchi wa Mikumi kama ambavyo wenzetu wa Kanda ya Ziwa walivyotumia vizuri Ziwa Victoria kupunguza tatizo hili sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa maji wa vijiji kumi katika kata ya Mikumi na Kidodi. Mradi wa Maji wa Visima wa *World Bank* kata ya Mikumi bado unasuasua na haujakabidhiwa kwa wananchi kama iliyoahidiwa na Mkandarasi *Malaika Construction*, pamoja na Serikali kumpatia shilingi milioni 208 alizoomba. Pia vituo vya maji 52 vimeanza kuharibika kwa kuwa vilijengwa muda mrefu na tanki la lita 300,000 bado wananchi hawaoni mwanga wa kupata maji safi na salama ingawa majaribio yalifanyika na akinamama na watoto wa Mikumi walifurahi sana kuona maji yanatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kustaajibisha mpaka leo mradi huu haujakabidhiwa kwa wananchi. Tunataka kujua ni lini mkandarasi Malaika atakabidhi mradi huu kama alivyokuahidi wewe na wananchi wa Mji Mdogo wa Mikumi? Pia Mradi wa Msowero uliopo kata ya Kidodo ulikabidhiwa kwa wananchi wa kata ya Kidodo tangu mwaka 2015, lakini cha kushangaza ni kuwa tangu mradi huu umekabidhiwa kwa wananchi maji hayatoki, naomba kauli ya Serikali kuhusu mradi huu muhimu wa Msowero uliopo kata ya Kidodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Lengewaha kata ya Ueling'ombe, tunaomba sana Serikali imlipe pesa mkandarasi wa mradi huu ili arudi *site*, maana hayupo kwa muda mrefu na tunaomba tujue tatizo liko wapi na kama ameshindwa kazi basi afukuzwe na kuvunja naye mkataba, na kama anadai basi alipwe pesa zake ili aendelee na umaliziaji wa mradi huu muhimu kwa wananchi wa Ueling'ombe, ambao wanakunywa maji machafu ya mto huku waki-*share* na wanyama na kusababisha magonjwa

ya mara kwa mara ya mlipuko na kusababisha vifo kwa mama zetu na watoto wa Kata ya Uleling'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu visima, tunaiomba sana Serikali itukumbuke kutuchimbia visima virefu na vifupi hasa kwenye kata za Mhenda, Malolo, Ulaya, Msanze, Kilangali, Mabwerekwere, Tindiga, Ruhembe, Vidunda, Ruaha, Kisanga Zombo, Mikumi, Uleling'ombe na Zombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nimalizie na suala la umwagiliaji, nilishawahi kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji ni lini Serikali itatoa tamko na kutuma wakaguzi wakakague mradi wa umwagiliaji wa Bwawa la Dachi lililopo kwenye kata ya Malolo, ambapo Serikali kupitia ufadhili wa Shirika la Kijapan la JICA ambao walitoa zaidi ya shilingi milioni 600 ambazo zimeliwa na bado makingio ya mchanga unaohatarisha Mto Mwega kujaa mchanga, na kupoteza kabisa nia njema ya wananchi wa Kata ya Malolo wanaoutegemea kwa kilimo cha umwagiliaji vitunguu, mboga mboga na mazao mengine muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, makingio hayo yamejengwa chini ya kiwango, michanga bado inajaa kwenye mto mwega, shilingi milioni 600 zimeliwa na hakuna mtu yeyote anayehoji kuhusu ubadhirifu huu mkubwa sana unaohatarisha maisha ya wananchi wetu wa kata ya Malolo. Naomba Waziri akija kuhitimisha atuambie ni lini atakuja kata ya Malolo akiongozana na mimi ili kusikia kilio kikuu cha wananchi hawa kuhusu Bwawa la Dachi na shida yao ya maji ambayo yanahatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kumalizia Naibu Waziri akijibu swali langu alijibu kuwa mkandarasi wa Bwawa la Kidete lililopo Wilayani Kilosa mkataba wake umesitishwa na *tender* itatangazwa hivi karibuni, nimeona kwenye ukurasa wa 47 wa hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuwa ni moja kati ya mabwawa yatakayojengwa kwenye bajeti hii ya mwaka 2017/2018. Wananchi wa Wilaya ya Kilosa wanataka kujua ni kiasi gani kimetengwa kwenye ujenzi wa bwawa hili muhimu la Kidete ambalo linasababisha mafuriko



ya mara kwa mara Wilayani Kilosa yanaharibu makazi ya watu. Vifo vya wakazi wa Wilaya ya Kilosa na pia mafuriko yanayosababishwa na Bwawa la Kidete yanasababisha uharibifu mkubwa sana, reli yetu ya kati ambayo Serikali inajitahidi kuijenga kwa kiwango cha *standard gauge* na lini ujenzi huu wa Bwawa la Kidete utaaanza. Ahsante.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Maji ni uhai, wanadamu, wanyama, mazao kila kitu kinahitaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi tumekuwa tukilalamikia upatikanaji wa maji katika Jiji letu la Dar es Salaam, tukumbuke Jiji hili ndilo kioo cha nchi yetu, lakini tatizo la maji ni kubwa. Hata baadhi ya maji yanapopatikana siyo salama na safi. Baadhi ya maji yanayotoka yamechanganyika na kinyesi sababu ya miundombinu mibovu na mingine imechakaa, pamoja na Serikali kujitahidi kubadilisha baadhi ya mabomba. Je, ni lini Dar es Salaam watapata maji safi na salama kwa ajili ya kunywa? Tumeshuhudia kipindipindu na magonjwa mengine ya kuhara hayaishi Dar es Salaam sababu inachangiwa zaidi kutokuwa na maji salama na safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji taka, bado mfumo wa maji taka ni tatizo Dar es Salaam hata hapa Dodoma. Kipindi cha mvua tumeshudia ndiyo wakati mashimo ya maji taka yanafurika na kusababisha kwanza mji mzima kunuka, kusababisha kulipuka magonjwa na kadhalika. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua mifumo ya maji taka sababu iliyopo ilikuwa inahudumia watu wachache, kwa sasa Jiji limeongezeka watu wengi zaidi ya milioni nne lakini mfumo ni ule tangu enzi za ukoloni

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Moshi; pamoja na Wilaya hii kuwepo chini ya Mlima Kilimanjaro lakini bado wananchi wanaotoka kata za Mbokomu, *Old Moshi*, Kiboriloni, bado kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa maji. Mradi wa maji vijijini ulikuwepo lakini maji yake yalitoka na siyo zaidi ya miezi sita. Wanaoteseka ni

watoto wa shule badala ya kusoma, wanatumia na walimu kwenda kuteka maji na akina mama wanatembea mbali wanabeba maji vichwani, hii ni kurudisha maendeleo nyuma. Je, mpango wa kuleta maji ya uhakika vijijini utakamilika lini badala ya haya maji ya kisiasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umwagiliaji mpaka sasa wakulima wetu wengi walikuwa wanategemea mvua na hawa wapo zaidi ya asilimia 80. Bado Wizara haijatoa elimu ya kutosha jinsi ya kuvuna maji ya mvua kwa kujenga mabwawa, kujenga mifereji ya kudumu ili waweze kupata maji kwa ajili ya kilimo. Serikali ituletee mikakati na mipango ya kuwawezesha wakulima ili waondokane na kilimo cha kutegemea mvua na kilimo hiki ni cha msimu lini waanze kilimo cha umwagiliaji ambacho kitakuwepo misimu yote? Bila hivyo viwanda tunavyotangaza vya usindikaji vitafanya kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Moshi Mabogini, Wajapani walianzisha kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha mpunga walijenga mpaka miundombinu ya maji na kilimo kule kiliendelea vizuri sana, lakini tangu Wajapani waondoke kilimo kile ni kama kimekufa. Wizara imeshachunguza ni kwa nini maji yale yamepungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji; miaka ya 1960 na 1970 wananchi walielewa maana ya utunzaji wa vyanzo vya maji. Mfano, Mkoani Kilimanjaro zao la kahawa lilishamiri sana kwa kutegemea umwagiliaji na kutumia mifereji ya asili. Walipanda miti na walivitunza vyanzo vya maji, lakini kwa wakati huu vyanzo vingi vimekauka. Miti inakatwa ovyo, wananchi wanalima pembeni mwa mito na Serikali inaona makosa yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kurudisha wanafunzi kuwa na vitalu vya miti. Viongozi wa vijiji wahakikishe miti inapandwa na hawalimi kando kando ya mito na kusimamia kwa nguvu zote vyanzo vya maji vifufuliwe

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali naomba niishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali inazochukua kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa maji nchini. Kimsingi naunga mkono mipango ya Serikali kupitia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi naomba kuwasilisha maoni kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, *scheme* za umwagiliaji kutokuwepo Shinyanga; pamoja na ukweli kuwa Shinyanga ni kambi la njaa wakati mvua hunyesha na mabonde yanayofaa kwa umwagiliaji yapo, lakini cha ajabu ni kuwa katika mipango ya Serikali hakuna *scheme* hata moja katika bajeti. Jedwali Namba Nane, Shinyanga haipo kabisa, naomba maeneo yafuatayo yaingie katika mipango ya Serikali:-

- (i) *Scheme* Bonde la Chela;
- (ii) *Scheme* Bonde la Bumva; na
- (iii) *Scheme* Mabonde ya Kashishi na Kabondo.

Pili, bili za umeme na ruzuku ya uendeshaji *KASHWASA*; kwa zaidi ya wiki mbili sasa Kahama na Shinyanga hakuna maji kwa sababu *KASHWASA* inadaiwa na *TANESCO* na hivyo umeme kukatwa. Naomba utaratibu wa utoaji ruzuku *KASHWASA* uangaliwe upya ili huduma za maji zisikosekane kwa wananchi wa Kahama na Shinyanga kwa sababu za Kiserikali wakati wateja wanalipa bili zao vema

Tatu, mradi wa vijiji 100 vilivyoko pembezoni mwa Bonde la lthelele - Kahama na Shinyanga ahadi ni ya muda mrefu tangu mwaka 2013 lakini kasi ya utekelezaji ni ndogo. Naomba mwaka huu angalau katika Jimbo la Msalala vijiji vya Mwakuzuka, Kabondo, Matinje, Izuga, Busangi, Nyamigege, Vula, Ntundu, Buchambaga, Mwaningi, Bubungu, Ntobo na Mwankima vipatiwe maji

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru kama maeneo haya yatazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kunipa afya na nguvu kuwatumikia wananchi Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na maji mengi sana kutoka vyanzo mbalimbali kama maji juu ya ardhi, maji chini ya ardhi na maji ya mvua yanayosababisha mafuriko mara kwa mara. Hata hivyo, kila mara Tanzania imekuwa inakabiliwa na uhaba wa maji safi na salama katika maeneo mengi mjini na vijijini. Uhaba wa mvua unaosababisha ukame na kusababisha njaa na adha kubwa ya kiuchumi. Mfano, wanyama kufa na kukosekana kwa mazao, vilevile nchi imekuwa mhangamkuwa wa mvua kubwa inayosababisha maafa ya mafuriko, uharibifu wa mazao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 53 ya uhuru pamoja na wataalam waliobobea katika taaluma ya maji na mipango, Serikali imeshindwaje ku-*manage* suala la maji ili kupunguza kero na umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Serikali haisimamii kwa Sheria ya Uvunaji wa Maji ya Mvua na Sheria ya Ujenzi irekebishwe kujumuisha miundombinu ya kuvuna maji kwenye majengo mbalimbali. Kwa nini mabwawa makubwa ya kukinga na kutunza maji kwenye maeneo ambayo kila mara kuna mafuriko na ya katumika kwa ajili ya kilimo, mazao na mboga mboga za muda mfupi ili kuinua uchumi wa wananchi na kupunguza umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini maeneo yenye maji chini ya ardhi wananchi wasichimbiwe visima ili kuwanusuru na kero ya maji? Katika hotuba, maeneo yenye maji chini ya ardhi yameainishwa, lakini hakuna popote fedha

imetengwa kwa ajili ya kuchimba visima vichache kwa vipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu kwamba Wizara ijipange kukusanya/kuvuna maji mengi yanayopotea na kwenda baharini. Nchi ya *Israe*/ni mahali pazuri pa kujifunza, maji ni almasi, hakuna tone linalopotea. Hapa kwetu tuna maji mengi lakini tunafanya mzaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002, nchi yetu ina eneo la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mkoa wa Songwe una vyanzo vingi vya maji ambavyo vingeweza kutumika vizuri, vingeweza kusaidia huduma ya maji pamoja na kilimo cha umwagiliaji ambacho kinaweza kulisha nchi nzima. Ushauri wangu kwa Serikali, Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Kilimo vikae pamoja na kuona ni namna gani wanaweza kutumia vyanzo vya maji ili kuboresha kilimo cha umwagiliaji kwa mkoa mpya wa Songwe

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango shirikishi wa maji shirikishi katika Mto Momba na Songwe unaweza kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na kutoa ajira kwa makundi ya vijana na akina mama ambao wengi wanategemea kilimo. Wizara ishirikiane na sekta binafsi kukamilisha miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uharibifu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji; kumekuwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya maji hasa maeneo ya vijijini. Mfano, maeneo mengi ambayo yamewekwa mabomba ya maji ya kuchota kwa ujumla, wananchi wamekuwa wakiharibu mabomba hayo kwa kuwa hawana uchungu na miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri uwekwe utaratibu wa kuchangia miundombinu ya maji ili wananchi watambue thamani ya miundombinu ya maji na kuithamini. Hii itasaidia ukarabati wa miundombinu hiyo bila kutegemea ufadhili pindi miundombinu hiyo ikiharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la upotevu wa maji hasa kwenye mashamba makubwa ya mpunga na mfano mzuri ni Bonde la Usangu - Mbarali. Miundombinu ya umwagiliaji ni ya zamani tangu kukiwa na mashamba machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za haraka zisipochukuliwa kudhibiti kilimo holela cha umwagiliaji katika Bonde la Usangu kuna uwezekano mkubwa wa uzalishaji wa nishati ya umeme katika Bwawa la Mtera na Kidatu ukapotea kwa kiwango kikubwa kutokana na upotevu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia haki za binadamu ziheshimiwe, mfano; haki ya kupata elimu, afya, maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa maji safi na salama vijijini bado ni changamoto kutokana na wananchi wengi kupata maji yasiyo salama. Uharibifu wa mazingira ni hatari sana kwa maisha ya binadamu kwa asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania wanatumia misitu kama malighafi kwa shughuli za uzalishaji na huduma pamoja na kuwa ni fursa ya ajira kwa watu wengi. Uharibifu wa mazingira ni chanzo cha mafuriko na ukame wa kutisha

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira na Wizara ya Kilimo kuhakikisha utoaji wa elimu juu ya utunzaji wa mazingira unapewa kipaumbele na ikiwezekana kuwepo na faini zinazotozwa kwa watumiaji wabaya wa maji na vyanzo vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maji ni afya, uhai na maendeleo, ninashauri Wizara ya Maji kwa kushirikiana

na Wizara zote ihakikishe kuwa majengo yote ya taasisi mbalimbali yawe na michoro itakayoonesha utunzaji wa maji ya mvua ili kusaidia wakati ambao kuna upungufu wa maji. Mfano katika shule, hospitali, ofisi, hoteli na shughuli zote za kilimo cha umwagiliaji kuwekewa mifumo ya kutumia maji kidogo na kuzuia upotevu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kushauri Wizara iendeleo kutembelea na kutoa elimu kwenye maeneo yenye vyanzo vya maji hasa kusisitiza suala la mita 60 kutoka vyanzo vya maji. Kuendelea kutumia mila na desturi zinazosaidia utunzaji wa maeneo yenye vyanzo vya maji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumemaliza uchangiaji katika Wizara hii. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Luhaga Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Isack Kamwelwe, Naibu Waziri wa Maji, atamalizia Mheshimiwa *Engineer*. Gerson Lwenge ambaye ni Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. Ninazo hoja chache ambazo nataka kuchangia. Moja, ni ile hoja ya...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, una dakika 10.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka kuchangia moja ya hoja ya kemikali zenye sumu zinazotumika mashambani ambazo zinazagaa kwenye mazingira na kuathiri vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla. Hoja hii iliulizwa na Waheshimiwa Wabunge katika michango yao na Mheshimiwa Vullu ndio aliuliza. Ni kweli kwamba kwanza tunazo taasisi nyingi sana ambazo zinasimamia kemikali hapa nchini; uingizaji, usambazaji, uzalishaji na utumiaji wa kemikali hapa nchini. Taasisi zote hizo kwa pamoja kila moja inalo eneo lake la kusimamia. Sasa eneo hili la kemikali za mashamba linasimamiwa na *TPRI* na *NEMC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema hapa, tutakachokifanya kule ambako Mheshimiwa anakulalamikia ni kwamba hizi sumu zimekuwa na shida kubwa na zinaathiri wananchi, tutawatuma *TPRI* pamoja na *NEMC* waende wakafanye kazi hiyo ili kujua hatua sahihi za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa maana ya kemikali nchini, tumegundua pia kwamba kulikuwa pia na usimamizi dhaifu kule nyuma. Tumeimarisha mfumo mzima wa kuhakikisha kwamba kemikali hapa nchini zinasimamiwa vizuri ili zisiweze kuleta athari kwa wananchi. Moja ya hatua kubwa ambayo tumeichukua ni kuanza maandalizi ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na *incinerator* kwa ajili ya kuteketeza mabakio ya vifungashio vya hizo kemikali lakini pamoja na kemikali ambazo zimesha-*expire*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana juu ya Jiji la Dar es Salaam kwamba linazidi kuongezeka ukubwa, watu wanazidi kuongezeka na shughuli za kiuchumi zinazidi kuongezeka, lakini miundombinu ya majitaka haiongezeki. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwa muda mrefu Jiji la Dar es Salaam ni asilimia 10 tu ya miundombinu ya majitaka. Miundombinu ya majisafi imekuwa ikiendelea kujengwa lakini miundombinu ya majitaka ilikuwa ni asilimia 10 tu toka miaka ya 1970 na kusababisha madhara makubwa sana ya kutapakaa kwa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechukua hatua kubwa na mkisoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 74, ndiyo utaona hatua tulizozichukua kupitia Shirika la Serikali za *DAWASA* ambapo leo tunazungumzia zaidi ya shilingi bilioni 342 ambazo zimetolewa na Serikali ya Korea pamoja na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuhakikisha kuwa tunajenga miundombinu ya kuimarisha Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *DAWASA* hiyo hiyo, kuna *commitment* kubwa ya fedha nyingine za kutoka *DANIDA* pamoja na *IFD* kwa maana ya Serikali ya Ufaransa



ambayo itakuwa na zaidi ya karibu shilingi bilioni 914. Katika hii Serikali ya Awamu wa Tano tunaenda kumaliza kabisa tatizo la majitaka ambalo linazungumziwa na Waheshimiwa Wabunge katika Jiji la Dar es Salaam. Nami nawapongeza DAWASA kwa kazi nzuri hiyo waliyoifanya ambapo ujenzi unaanza mwaka huu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaishia hapo, suala la kutoa vibali kwa ajili ya majengo makubwa pamoja na shughuli nyingine ambazo zinapelekea majitaka kutapaka, tutazidhibiti kwa karibu zaidi ili kuhakikisha kwamba utapakaaji huo wa majitaka hauwezi kutokea tena. Kwa kwa mipango hii tuliyonayo tu hii ya hivi karibuni kwa maana ya kupitia DAWASA ni kwamba miundombinu hii ikijengwa, asilimia 10 mpaka asilimia 30 tutakuwa tumefikia katika uondoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuishii hapo tu, hata ukiangalia pia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alizungumza kuhusu miundombinu ambayo imejengwa na miradi mbalimbali katika Majiji saba pamoja na Halmashauri 18, yote hayo ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti utapakaaji wa majitaka na hivyo tunaongeza ubora wa maji yetu tunapouepusha na hizi taka ambazo zinazagaa kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tutakalohakikisha kabisa ni kwamba hakuna namna yoyote ambayo watu wataendelea kuchafua maji yetu ambayo watu wataendelea kuharibu maji kwa namna yoyote au kwa shughuli zozote zile za kiuchumi ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo Waheshimiwa Wabunge walilizungumza ni kwamba Serikali kuchukua hatua gani katika suala la vyanzo vya maji? Katika suala la vyanzo vya maji, kuhusu kuvilinda vyanzo hivyo pamoja na madakio yake, sheria mbili zote tunazo; Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009 pamoja na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, zote hizi zinatoa nafasi nzuri sana ya kusimamia hivi vyanzo vya

maji. Kwa hiyo, la kwanza kabisa ni kuhakikisha kwamba sheria hizi tunazisimamia vizuri ili tuhakikishe kwamba maji yetu yako salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, lazima tuvilinde vyanzo hivyo vya maji na Serikali kwa kuanzia tumehakikisha kwamba *TFS* imeenda kila Wilaya. Kwa sasa hivi *TFS* iko kila Wilaya na tunahakikisha kwamba wanachangia angalau miche 150,000 mpaka 500,000 kwa kila Halmashauri na kwa kila Wilaya. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, waoneni *TFS* kule kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mnapeleka msukumo mkubwa katika upandaji wa miti hasa katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kulinda vyanzo hivyo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la mabadiliko ya tabianchi. Suala la mabadiliko ya tabianchi ni tatizo kubwa sana hapa nchini sasa. Ni takriban zaidi ya shilingi bilioni 180 Taifa hili linapata hasara kwa mwaka kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Sasa tuamue kuchukua hatua. Tumeingia mikataba na dunia sasa hivi inahangaika makubaliano na mkataba wa Paris tumekubaliana kwamba tusiruhusu gesi joto iongezeke zaidi ya nyuzijoto mbili na kwa sasa hivi ongezeko la nyuzijoto limefikia 0.85.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati wetu sasa ni lazima tukubaliane kama Taifa kuhakikisha kwamba tunafanya kwa nguvu zetu zote; moja ni kupanda miti kama wendawazimu katika Taifa hili ili kuweza kumudu haya madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhakikisha kwamba tunabuni miradi mizuri ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi sasa. Kama sasa hivi inavyoripotiwa mvua nyingi, maporomoko, mafuriko, wananchi wana matatizo makubwa. Kwa hiyo, sasa kama Taifa, tuamue kuhakikisha kwamba njia bora zitakazotuwezesha kwa ajili ya kuondosha hili tatizo la mabadiliko ya tabianchi tuweze kulihimili, ni kuhakikisha kwamba miradi hiyo tunayoibuni ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi tunaifanya kwa nguvu zetu zote. Sasa hivi sekta zote za kiuchumi zimeathirika.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunachopaswa kufanya ni kuhakikisha kwamba tunao mkakati wa mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2012, kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumza hapa; huu mkakati tumeandaa toka mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona ni vyema basi, tutaomba kwa nafasi yako ikiwezekana tuendeshe Semina na Wabunge ili tuweze kuwasilisha mkakati wa mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2012 mbele ya Bunge hili. Vile vile tuweze kuwasilisha hali ya mazingira ya Taifa hili ya mwaka 2014. Pia tuweze kuwasilisha mkakati wa kuhifadhi mazingira na ardhi na vyanzo vya maji ya mwaka 2006 pamoja na mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari ukanda wa Pwani; maziwa, mito na mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo, nadhani sasa tutakuwa tumepata mwanzo mzuri wa kwenda pamoja na Bunge hili katika kushughulikia mambo haya ambayo ni makubwa na kuweka mipango ya pamoja ambayo itatuhakikishia kwamba tunatoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer Isack Kamwelwe. (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kujalia amani nchi yetu na kutuwezesha Wabunge wote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais, *Champion* wa Maji kwa kuendelea kuniamini na kuamini wafanyakazi wa Wizara ya Maji ili tuweze kutatua tatizo la maji kwa wananchi wa Tanzania. Namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu,

Mheshimiwa Rais alimteua Mama na suala la maji ni la mama, kwa hiyo anatusimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuendelea kusimamia vizuri shughuli za Bunge na tunaendelea vizuri kwa amani kabisa bila fujo ya aina yoyote. Namshukuru Mheshimiwa Spika, nawe Mheshimiwa Naibu Spika na leo ndio umekalia kiti hicho kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wenu, kwa miongozo yenu na kwa jinsi mnavyotombea, lakini jinsi ambavyo mnaendelea kushirikiana nasi ili azma hii ya kuondoa tatizo la maji katika nchi yetu liweze kufikiwa bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa wananchi wote nchini hususan wananchi wa Arusha, kwa msiba mkubwa wa ajali ya gari uliogharimu maisha ya wanafunzi, Walimu, dereva na shule, msiba uliotutokea mwezi huu, msiba mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika sana kwa sababu barabara ile nimeisimamia mwenyewe kutoka Makuyuni mpaka Ngorongoro. Tunaomba roho za vijana hawa na hawa watu wazima wote Mungu aziweke mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Lwenge, amenipa ushirikiano mkubwa sana, ameniongoza ndiyo maana hata nimeweza kufahamu mambo mengi kwa muda mfupi. Namshukuru sana Mheshimiwa Lwenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Katavi kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa mimi Mbunge wao, unaosaidia kufanikisha shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo letu,

naendelea kuwaahidi kwamba nitawatumikia kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia na kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naishukuru familia yangu sana kwa jinsi inavyonishauri na jinsi inavyonipa ushirikiano ikiongozwa na mke wangu ambaye ni Mwalimu Bora Jeremiah Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda kuwa ni mdogo, nianze kuunga mkono hoja au shughuli yetu hii ya leo na niombe Waheshimiwa Wabunge mpitishie ili tukafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea michango mingi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, michango ambayo kwa kweli inatutetea ili tuweze kuhakikisha kwamba tunatimiza kuwapatia wananchi wa Tanzania majisafi na salama lakini pia tuweze kuboresha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza mchango wangu kwa kilimo cha umwagiliaji. Nchi yetu mwaka 1990 ilifanyika *study* ambayo ilibaini kwamba tuna hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini ambazo zimeendelezwa ni hekta 461,000. Baada ya kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, nashukuru maeneo niliyofanya ziara; nimekwenda kuona jinsi gani hili eneo dogo ambalo limeendelezwa jinsi linavyofanya kazi na nimebaini upungufu uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea eneo la Mang'ola, nimekwenda kuona kilimo pale Wilaya ya Karatu, wanalima mara tatu. Hekta moja inatoa kuanzia tani tano mpaka tani kumi lakini hekta moja hiyo hiyo inalimwa mara tatu. Ni maeneo machache sana ambayo yameshafikia hatua hiyo ya kilimo kwamba hekta moja inaweza ikalimwa mara tatu. Maeneo mengi yanalimwa mara moja na ni kipindi cha mvua tu; kipindi cha kiangazi hatuwezi kulima kwa sababu hakuna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Serikali kwa sasa imeweka Mhandisi Mshauri ambaye anapitia maeneo yote ili kubaini upungufu uliopo ni kwa nini hatuwezi kulima mara tatu ili tuweze kuondokana na tatizo la njaa katika nchi yetu. Upungufu huo ukishapatikana utainishwa na malengo yetu ya kuhakikisha kwamba tunaandaa hekta nyingine milioni moja katika huu muda wa miaka mitano, nina hakika kwamba yatafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuhakikisha tunalima mara mbili hadi mara tatu, kwa sababu hata hizo hekta chache ambazo nazo hazitumiwi kwa *efficiency* inayotakiwa, lakini bado zina uwezo wa kuchangia chakula kwa zaidi ya asilimia 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ndiyo uti wa mgongo wetu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeelekeza kwamba nchi yetu inakuwa ya viwanda na viwanda hivyo vitatumia rasilimali ya kutoka mashambani ili tuweze kunyanyua uchumi wa wananchi wetu twende kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutahakikisha kawamba kilimo hiki cha umwagiliaji tunakisimamia ipasavyo. Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge mlipitisha tume, katika huu muda mfupi ambao nimekaa nao, nimebaini upungufu uliopo. Upungufu uliopo, ni kweli kama mnavyolalamika Waheshimiwa Wabunge miradi mingi ambayo tulipata hela za wafadhili hajajengwa katika ile hali ambayo tulikuwa tunaitarajia. Kila ukiuliza, ukienda kwenye Halmashauri, Halmashauri wanakwambia ni matatizo ya Tume; ukiongea na watu wa Tume, wanakwambia ni matatizo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongea na Waziri wangu kwamba hiyo miradi iliyokuwa inaendelea iendele, lakini miradi mipya yote itakayokuja, tunataka tuone mtu mmoja anaitekeleza na sio mwingine, itakuwa ni Tume ya Umwagiliaji, ili kama kuna upungufu katika ile tume, Waheshimiwa Wabunge tuweze kuurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata michango mingi, Mheshimiwa Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini ameongea kitu cha msingi sana, kwamba Halmashauri yake ina matatizo ya Wahandisi, ina matatizo ya wataalam wa manunuzi. Ni kweli, lakini nashukuru bajeti ya mwaka 2016, mliagiza Wizara ya Maji na umwagiliaji kwamba mnataka tuunde Wakala wa Maji Vijijini. Mheshimiwa Waziri atalielezea vizuri, niwahakikishie kwamba tumeshaanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hata mimi mwenyewe baada ya kuteuliwa katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa sababu nimetoka kwenye Wakala wa *TANROAD* niliona ili tuweze kwenda hakuna namna nyingine, ni lazima tuunde wakala ujitegemee, ufanye kazi kama ambavyo *TANROAD* imekuwa inafanya, ufanye kazi kama ambavyo *REA* inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mwalongo tatizo hilo alilionalo la wataalam wa manunuzi litakwisha baada ya sisi kuwa na Wakala wa Maji Vijijini. *TANROAD* imefanikiwa kwa sababu wataalam wa manunuzi ndani ya *TANROAD* ni Wahandisi hao hao wanaojenga barabara, ndiyo maana mambo yanakwenda vizuri; tunaelekea huko Waheshimiwa Wabunge. Sasa hivi inaandaliwa na tutakapoileta hapa, tutawaomba Waheshimiwa muipitie, mtushauri na muipitishie ili tuanze utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Musukuma katika mchango wake, nilikuwa nafikiri nami ataniuliza *what is your weakness?* Alisema kwamba miradi hii, bajeti hii hatuwezi kuitekeleza kwa mwaka mmoja.

Waheshimiwa Wabunge tumejipa miaka mitano, tumeanza na bajeti hii tumeitendea haki, tumeingia mikataba, tutatekeleza. Hebu tupimeni baada ya miaka mitano mtaona tutafanya nini? Huu mwaka mmoja tumejitahidi, tumeelewa tunatakiwa kufanya nini. Kwa hiyo, tupeni muda tuifanyie kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera. Waheshimiwa Wabunge tayari visima 17 vimeshakamilika na niwaambie tu kwamba visima vitatu bado, lakini vinakamilika mwezi Juni, 2017 maana yake ni mwezi ujao. Visima hivi vikikamilika, visima vya maeneo ya Mpera vitahudumia wakazi wa maeneo ya Gongolamboto, Chanika, Luzando, Pugu, Mpera, Chamazi, Kidunda, Ukonga, Kinyerezi na Uwanja wa Ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima vya maeneo ya Kimbiji vitahudumia wakazi wa maeneo ya Temeke, Kisarawe, kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Tandika, Keko na Chang'ombe. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuweze kuweka miundombinu ya usambazaji.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mtuamini, tunaifanya hii kazi ili tuhakikishe wananchi wote wa Dar es Salaam na Pwani wanakuwa na majisafi na salama kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ignas Malocha, Mbunge wa Kwela. Amesema kwamba tumekuwa tukiomba pesa mfululizo kwa miaka mitano, hatujawahi kupewa. Tatizo ni nini? Anaelekeza kwenye miradi ya Maleza, Izia na Mfia. Mheshimiwa tutaweka fedha, tumeanza. Kama nilivyosema, utekelezaji wetu unakwenda miaka mitano, nimhakikishie wananchi wake watayaona sasa matokeo kwamba tunatekeleza maeneo yote haya aliyoyahitaji yakiwemo pamoja na maeneo ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe amesema mradi wa umwagiliaji wa Mwamapuri kwamba haujatengewa fedha katika bajeti ya mwaka huu; anaomba mradi huo utafutiwe fedha. Skimu ya umwagiliaji ya Mwamapuri ipo Halmashauri ya Mpimbwe, Wilaya ya Mlele Mkoa wa Katavi. Skimu hii ina zaidi ya hekta 13,000 zinazofaa kwa umwagiliaji.



Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, tayari upembuzi yakinifu umeshakamilika na tayari tumeshapata gharama, tunahitaji shilingi billioni 15 ili tuweze kuikamilisha hiyo skimu ikiwa ni pamoja na kujenga Bwawa la Ilanguku ambalo litatunza maji ili tuhakikishe kwamba skimu hiyo inafanya kazi mwaka mzima isifanye kazi wakati wa mvua tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele ameuliza, katika nyakati hizi mbaya za mabadiliko ya tabianchi, licha ya kwamba sasa maeneo yetu bado ya misitu na miti kiasi, lakini suala la uharibifu wa mazingira litasababisha ukame utakaosababisha uhaba wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mpina ameeleza vizuri sana nini kinafanyika, sheria tunazo, lakini kikubwa Mheshimiwa Masele sisi ni Madiwani, lazima tukae na wananchi wetu, tuongee nao, tubadilisha tabia sisi wenyewe. Hatuwezi kuishi kwa sheria tu, lazima tuwe na tabia ya kufahamishana tuelewe kwamba misitu ni uhai na uhai ule siyo wa misitu wala siyo wa wanyama tu, ni pamoja na sisi binadamu. Tukielimishana, basi suala hili la mabadiliko ya tabianchi halitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Wabunge wengi wamelalamika, miradi mingi ya maji tumetekeleza, lakini haifanyi kazi. Ukienda kuangalia, pamoja na matatizo yaliyokuwepo kwamba labda imejengwa vibaya, labda usanifu ulikuwa mbaya, lakini maeneo mengi ni kwamba vile vyanzo vilivyokuwa vimetarajiwa vimekauka. Sasa kama vimekauka, maji ya kuingiza kwenye bomba utayapata wapi? Haiwezekani. Tatizo hili sisi wenyewe, ndugu zangu tuhakikishe kwamba tunasimamia, tunaongea na wananchi wetu kuhakikisha kwamba tunadhibiti uharibifu wa misitu kwa sababu misitu ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la kwamba mradi kutumia hela nyingi. Ukienda kuuliza, unaambiwa hii *design* iliharibiwa

na *Consultant*. Mikataba iko wazi! Iko *design liability* ya *Consultant*. Kama *Consultant* ameharibu na ikathibitishwa kwamba ameharibu, lazima anailipia. Hizo fedha za kujenga huo mradi tutazipata kutoka kwenye *insurance* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko michango mingi sana ya Waheshimiwa Wabunge ambayo hatuwezi kumaliza kujibu yote, lakini tutahakikisha kwamba kwa muda mfupi michango yote hii tutaiandika na kuhakikisha kwamba tunawapatia Waheshimiwa Wabunge kabla ya kumaliza hili Bunge ili kila mtu awe na nakala na aone mchango wake na majibu ambayo tumeyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, maji yasiyotibiwa, malengo yetu na ndiyo Sera yetu kuhakikisha kwamba maji yote ya matumizi ya binadamu yanatibiwa ili mtu aweze kunywa maji yaliyo safi na salama. *Concept* hii tumeiona, Waheshimiwa Wabunge mmechangia, tukinywa maji yaliyo safi na salama tunapunguza hata kwenda hospitali na gharama za kununua madawa zitapungua. Hilo ndilo lengo letu. Sisi Wizara ya Maji hatupendi tuwe sababu ya kumaliza fedha za nchi hii kwa Serikali kununua madawa mengi kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Kapufi amezungumzia maji ya Ikorongo. Tayari tumeshasaini mkataba mmoja na wa pili utasainiwa ili tuhakikishe kwamba tunaongeza kiwango cha maji kufikia lita milioni 10.2 zinazohitajika katika Mkoa wa Katavi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Munde, Mbunge wa Tabora, tunakushukuru sana kwa pongezi. Tumesaini mikataba; mkataba ule ni wa zaidi ya shilingi bilioni 600, tunasimamia utekelezaji. Tumejipanga kuhakikisha kwamba unakamilika katika muda uliotarajiwa ili tuhakikishe tunamaliza yale matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa mama yangu Mheshimiwa Sitta amelalamikia kuhusu mradi

tunaotoa maji Malagarasi kuleta Tabora kwamba utachukua muda mrefu. Tutahakikisha kwamba katika huo muda tunaosubiri ili tuweze kupata fedha kujenga huo mradi ambao utachukua miaka mingi, tutahakikisha kwamba tunafanya hatua za dharura ili wananchi wa Kaliua, Urambo waweze kupata maji yaliyo safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hapa nimeshapigiwa kengele tayari, nimalizie kwa kuunga mkono hoja, lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kila bajeti inapokamilika, tunawapatia vitabu. Katika mizunguko yangu ambayo nimekwenda huko kwenye Halmashauri, unakutana na Mkurugenzi anasema yeye haelewi kama ana bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kabisa, kabisa mama yangu. nimeyaona haya na siyo Halmashauri moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge, baada ya leo, kesho mpigie Mkurugenzi wako, basi msomee hata kama hukumpa kitabu, kwamba Wizara ya Maji na Umwagiliaji una shilingi kadhaa ili waweze kujipanga. Zipo, lakini hawaangalii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Tunakushukuru sana, muda umekwisha. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer* Gerson Lwenge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani za dhiti kwa Bunge lako kujadili hoja hii kwa huo muda wa siku tatu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia Wizara hii. Wabunge wapatao 193, zaidi ya nusu ya Wabunge waliopo hapa wamechangia kwa kuandika na wengine wameongea hapa. Walioweza kuchangia kwa maandishi wako Wabunge 102 na walioweza kuongea hapa ni Wabunge 91. Nawashukuru sana. Ushauri wenu wote mlioutoa, Wizara yangu itauzingatia katika utekelezaji. Naomba niwahakikishie, haya maandishi na majibu tutayatoa kabla

ya mwisho wa Bunge hili. Kwa hiyo, kila mmoja atakwenda Jimboni kwake akiwa na majibu ya hoja zake alizokuwa amezitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza habari ya kugawana maji yaliyopo. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, rasilimali za maji tulizonazo nchini ni kilometa za ujazo 96.27 ambapo tukigawana sisi kwa *population* ya nchi kila mmoja anaweza akatumia maji ya ujazo 1,800, lakini tumefanya utafiti na kufuatilia, maji haya tunategemea zaidi mvua. Hali ya tabianchi kama mnavyoona imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka, kwa hiyo, hata rasilimali za maji zinapungua. Sasa sisi kama Serikali ni lazima tuwe na mikakati ya kuhakikisha tunaongeza rasilimali za maji nchini kulingana na mahitaji ili tuweze kuwagawia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tuchukue hatua mbalimbali. Pamoja na hatua hizo tunazozichukua, Serikali ina mpango maalum wa kutunza vyanzo vya maji; kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kuhakikisha vyanzo vinabainishwa, vinawekewa mipaka; tunatengeneza ramani pamoja na kuandaa taratibu za fidia kwa sababu baadhi ya watu tutawaondoa maeneo yale ambayo yana vyanzo vya maji na maeneo oevu. Hili naomba sana Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba lazima tuchukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuwa na mipango hii, tunaomba tutoe wito kwa Watanzania wote, tusiendeleo kulia kwamba maji hakuna na tuna miradi mingi ambayo imejengwa kwa fedha nyingi za Serikali, leo haifanyi kazi. Haifanyi kazi kwa sababu vyanzo vile vilivyoainishwa, leo havitoi maji. Kwa hiyo, sasa ni lazima sisi tuchukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea Mkoa mmoja, naweza nikasema Mkoa wa Rukwa nikakuta kuna chanzo ambacho kilikuwa kinatoa maji kwa vijiji kama vinne, lakini chanzo kile kwa sababu watu wamekivamia, ndiyo eneo wameweka la ufugaji ng'ombe, kwa hiyo, maji hakuna. Leo hawapati maji! Inabidi tuanze kutafuta tena njia nyingine

ambazo ni gharama zaidi kwa Taifa ili kuwapelekea wananchi wale maji wakati maji yalikuwepo. Kwa hiyo, ni lazima tuchukue hatua kwamba wananchi washiriki katika kutunza na kulinda vyanzo vya maji lakini pia tutoe elimu ya kutosha, wananchi waache kulima na kufuga katika maeneo ndani ya mita 60 ambayo tumeainisha ndiyo vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwahamasisha wananchi kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua, hiyo itaongeza rasilimali ya maji kama mlivyochangia Wabunge wengi. Tumekuwa tunapata mvua, lakini maji yote yanakwenda baharini. Sasa tunaanza kuchukua hatua kwa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na kwenye Taasisi zetu, kwenye shule, zahanati; hakuna sababu ya kuwa huna maji ya kuwahudumia wagonjwa wakati tunaweza tukavuna maji ya mvua kwenye paa la zahanati. Tumetoa mwongozo kwa Halmashauri zetu zote nchini sasa tuanze kuchukua hatua. Kibidi tutunge Sheria ndogo ndogo za kudhibiti watu ambao hawatataka kufanya suala hili la uvunaji wa maji ya mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za muda mrefu Serikali imepanga kujenga mabwawa ya kimkakati, likiwepo Bwawa la Farkwa, Ndembela na Kidunda ili kuweza kuongeza rasilimali za maji. Pia tumetoa mwongozo kwa Halmashauri zetu kwamba tuwe na mkakati kwa kutumia mapato ya ndani tujiwekee ratiba wa kujenga bwawa moja kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kitu kinachowezekana kwa mabwawa madogo madogo; tutaondoa tatizo la wafugaji wetu kuwa wanazunguka nchi nzima tatizo kubwa wanatafuta maji kwa ajili ya mifugo. Tukiwajengea mabwawa kwenye maeneo yao, migogoro ya wafugaji na wakulima itapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wabunge wengi wamezungumza habari ya mifumo endelevu ya kuweza

kuendesha miradi yetu ya maji katika maeneo ya vijijini. Wizara inaendelea na uandaaji wa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa kutumia ofisi zetu za mabonde kama ya Rufiji, Ziwa Rukwa, Ruvuma na Pwani ya Kusini; Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na bonde la kati. Sasa hivi tunaandaa taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuweza kuajiri wataalam watakaosaidia mabonde haya katika suala hili la mifumo endelevu ya kusimamia rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto za uendelevu za huduma ya maji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri inaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu. Sasa hivi tunazungumza habari ya wastani wa upatikanaji wa maji 72.15%, lakini Kambi ya Upinzani wao badala ya kusikiliza takwimu za Serikali wanakwenda TWaweza. Sasa unamwamini TWaweza kuliko Serikali!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, Waheshimiwa Wabunge, takwimu za upatikanaji wa maji zinaendana na uwingi wa watu wanaopata maji, siyo kwa wingi wa vijiji. Maana mtu anasema nina vijiji 100; vinavyopata maji viko 30. Kwa hiyo, anasema wastani ni hivyo. Haiendani hivyo! Tunaangalia wingi wa watu wanaopata maji kulingana na Sera yetu ndani ya umbali wa mita 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kituo cha kuchotea maji tumeweka wastani wa watu 250. Kwa hiyo, kwa namna hiyo ndiyo tumetengeza takwimu, lakini bado tunaweza tukaboresha zaidi suala hili la upatikanaji maji, lakini usitumie TWaweza, kwa sababu TWaweza anaweza akamwuliza mtu kwa kupiga simu. Huwezi kufanya utafiti kwa kupiga simu. Sisi tunazo *data*. Nakubali kweli kuna miradi mingi ambayo ilikuwa inafanya kazi, leo ina changamoto kwamba maji hayatoki, lakini ni jambo la kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, tumeshatoa mpango sasa wa kukarabati

miradi yote ambayo haitoi maji. *Payment by result*, Serikali ya Uingereza imeweka fedha zaidi ya shilingi bilioni 200 na kitu kwa miaka mitatu kusaidia Halmashauri zetu kufufua miradi yote ambayo imekufa (ambayo haifanyi kazi). Kwa hiyo, mpango huu ni mzuri na nina hakika kwamba tukifufua miradi yote ya zamani tutakwenda vizuri na tutakwenda kweye *data* hizi ambazo tunazitungumza leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaahidi wananchi wetu kwamba ndani ya miaka mitano, ikifika mwaka 2020 Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha upatikanaji wa maji unafika asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini. Ndugu zangu huu ni mwaka wa kwanza wa Bajeti, ndiyo tumemaliza. Tunaandaa sasa mwaka wa pili. Kwa hiyo, hatuwezi kufikia asilimia 85 katika bajeti ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa kwanza tulipanga bajeti ya shilingi bilioni 915 kwenye maendeleo, lakini sasa kuna hatua mbili; kwanza unafanya manunuzi halafu unakwenda kwenye utekelezaji...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumwache mtoa hoja azungumze. Mkiendelea kumwongelesha hapo mbele, hatutafika mwisho, maana sasa kila mtu ana swali lake. Mheshimiwa Bobali usimzungumzishe mtoa hoja. Anazungumza hoja ambazo mlishachangia Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, tafadhali, tuwe na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lwenge.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kumekuwa na hoja watu wanasema kwamba pesa zilizopangwa mwaka huu ni kidogo. Mimi nasema siyo suala la kusema kidogo, suala kubwa ni fedha kupatikana. Kwa hiyo, bajeti yetu ya mwaka huu ya shilingi bilioni 913, sisi kama Wizara tumeshafanya manunuzi. Fedha zilizotolewa zaidi ya shilingi bilioni 10 ambazo ni asilimia 19, ni zile ambazo tayari tumelipa *certificates* kwamba fedha hii

inakwenda kulipa kazi iliyofanyika. Fedha ambazo tayari tumeajiri Wakandarasi na tumeshasaini mikataba zaidi ya fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi tunakwenda kwa utekelezaji wa hiyo shilingi bilioni 915 na Serikali kwa *commitment* hiyo ni kwamba mpaka ikifika Juni; kwa sababu hii *status* ilikuwa ni mwezi wa Tatu; kuna mwezi wa Nne, wa Tano na wa Sita. Kwa hiyo fedha itatolewa na Serikali kama ilivyokuwa imepanga. Kwa hiyo, hakuna haja ya kuwa na wasiwasi wa hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya hilo, kuna hizi dola milioni 500 za kutoka Serikali ya India. Katika utaratibu wa upangaji wa bajeti, wakati mnaandaa zile *ceiling*, mara nyingi huwezi ukaiweka kwenye vitabu vya Hazina fedha ambayo bado hujasaini ule mkataba wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ambayo naomba niitoe ambayo tayari Kamati ya Madeni na Mikopo imeshaidhinisha fedha hii, kwa hiyo, fedha hii itakuja kupatikana katika mwaka wa fedha huu wa 2017/2018. Kwa hiyo, fedha ya Bajeti ya Wizara ya Maji itaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kikubwa ambacho naomba na ambacho ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge nimeona, kwa kweli kila mmoja amekuwa analia na Jimbo lake. Naomba sana, tatizo kubwa tulilokuwa nalo ni utekelezaji ndani ya Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeleka fedha za Mfuko wa Maji katika Halmashauri mbalimbali lakini mpaka leo kuna Halmashauri fedha zipo lakini hakuna walichokifanya. Sasa ndiyo maana tunafikiria kwamba ili tuweze kujenga miradi hii ya maji, lazima tuanzishe Mfumo wa Wakala wa Maji Vijijini ili tuwe na *standard* inayofanana katika utekelezaji. Kwa sababu mpaka leo yuko Mkurugenzi hajafanya manunuzi, anasubiri apelekewe fedha na tumetoa mwongozo.



Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, tumewapa nakala za mwongozo kwamba hatutapeleka fedha, bajeti yetu ni *cash budget*. Tunapeleka fedha mahali ambapo kuna utekelezaji na ndiyo maana kumekuwa na hata uwiano wa mgao. Tumepeleka fedha, unaweza ukakuta mahali pengine zimekwenda fedha nyingi kwa sababu wana mradi, lakini sehemu nyingine utapeleka fedha nyingi mradi hawana, hawataki kubadilika wanataka kufanya kazi kimazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge, tusaiane katika kusimamia Halmashauri zetu ili tuendane na kasi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Ningeweza kusema maji hoyee, lakini ndiyo hali halisi kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kabisa kuondoa tatizo hili la maji kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Mkutano wa Kimataifa ambayo tunasema lengo la sita la maendeleo endelevu wanataka kwamba tukifika mwaka 2030 tuhakikishe wananchi wetu wanaoishi vijijini na wanaokaa mijini wanapata maji kwa asilimia 100. Nataka niwahakikishie Bunge hili kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Tano itahakikisha tunafikisha lengo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja ya kuboresha Mfuko wa Maji na hoja hii imetolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Maji na Mifugo. Ni hoja nzuri na ilishatolewa hata kipindi kilichotangulia, lakini kulingana na Kanuni zetu, hatuwezi tukaamua humu ndani. Tutapeleka kwenye Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kile kipindi cha siku saba, tutafanya mashauriano na kuona namna gani

pendekezo la Wabunge la Kamati ya Bunge pamoja na Wabunge wengi wameunga mkono. Tutaona namna gani jambo hili linaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mchango wa Mheshimiwa Kitwanga. Amechangia hapa kwa hisia kubwa kuonesha kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijafanya chochote kwa Wilaya ya Misungwi. Sasa nataka nimwulize Mheshimiwa Kitwanga kama yupo, labda yale maneno anasema ni ya kwake au ya wananchi; kwa sababu wananchi nitawaambia nini kimefanyika Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumesaini mikataba, Mkurugenzi wake na Mwenyekiti wa Halmashauri alikuwepo, tunasaini mikataba hadharani ya kupeleka maji ya Ziwa Victoria Wilaya ya Misungwi, kwa fedha nyingi, zaidi ya shilingi bilioni 38.5, zinakwenda Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anaposema anakwenda kuhamasisha wananchi wakabomoe huo mtambo wa lhelele, maana yake analeta uasi au anataka asithamini kazi iliyofanywa na chama chake? Basi ajitoe kwenye chama! Eeh!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali imepeleka fedha, sasa leo maendeleo ambayo yameshafanyika ni lazima tuwahamasishe wananchi wetu. Kitu cha kwanza tuwahamasishe wananchi wetu kutunza miundombinu ambayo tayari tumeshafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani ukasema miundombinu ambayo tumefanikiwa tukabomoe. Ukichukulia umeme kwa mfano, unatoka kijiji kimoja unaruka vitatu unakwenda cha nne, sijasikia mahali wanang'oa nguzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimwambie Serikali inaendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwepo Misungwi na Usagara. Kwa upande wa Usagara, watapata maji yata kayosukumwa kutoka eneo la Nyashishi hadi kilima cha Usagara ambapo watazalisha maji kiasi cha lita milioni tatu. Hadi sasa usanifu wa awali unaojumuisha Buswelu umefanyika. Kwa hiyo, kazi hii itafanywa kwenye mwaka huu wa fedha, tumeshaweka fedha. Sasa akisema haungi mkono maana yake hii fedha shilingi bilioni 4.46 tupeleke Wilaya nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mji wa Misungwi, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza tayari imesaini mkataba na mkandarasi wenye thamani hiyo ya shilingi bilioni 38 kwa ajili ya kupeleka maji katika Mji wake wa Misungwi. Tumepata ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo Ufaransa. Sasa leo ukisikia mtu wa Misungwi anasema kwamba kwa kweli haithamini kazi ya Serikali ni kitu kinachosikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Misungwi, awamu ya kwanza ya mradi Serikali itajenga miundombinu ya maji kutoka Kijiji cha Mbarika kwenda Misasi kupitia Vijiji vya Lutaletale, Bugisha, Naya, Ikula, Sumbungu, Makale, Kasororo, Misha na Nabwawa. Kwa hiyo, miundombinu hii tayari imekamili kwa fedha ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Vilevile zaidi ya shilingi bilioni 3.5 imepangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine katika Wilaya ya Misungwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kwa hisia sana kuhusu hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo yao. Naomba Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wao waunge mkono juhudi za Serikali katika kutatua changamoto za upatikanaji wa maji nchini. Katika maeneo mengi nchini, miradi ya maji na umwagiliaji imeendelea kutekelezwa na ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji kama ilivyoenezwa katika hotuba yangu. Miundombinu iliyokamilika kujengwa ni mojawapo

ya mafanikio ya Serikali na inabidi tushirikiane kuhakikisha inatunzwa ili wananchi waendeleo kupata huduma inayokusudiwa na kwa ubora unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema sikutarajia sana kauli hii itoke kwa Mheshimiwa Kitwanga, mtu aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya mgawanyo wa fedha usiokuwa na uwiano sawa kwenye Halmashauri. Kama nilivyoeleza hapo mwanzo, ni kweli hatujagawa sawasawa kwa sababu ya kasi ya utekelezaji kutofautiana. Kwa hiyo, suala hili tunalifanyia kazi lakini tumetembelea kila Halmashauri na kuwaelekeza mahali ambapo kuna matatizo ya wataalam tunatumia Mamlaka za Mikoa au Kanda kusaidia kuwaelekeza namna ya kufanya manunuzi na kuweza kusimamia miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu fedha za USD milioni 503. Kama nilivyosema, wakati tunafanya *celling* fedha hii tunaitarajia kwamba itasainiwa kabla ya mwisho wa mwaka huu. Kwa hiyo, bajeti yetu ya maji itaruka toka shilingi bilioni 600 na itakwenda zaidi ya shilingi trilioni 1. Kwa sababu hii fedha ya USD milioni 503 tayari imeshaidhinishwa na Kamati ya Madeni na Mikopo. Tunatarajia mkataba utasainiwa kabla ya Juni kwa sababu Kamati ya Mikopo imeshaidhinisha na itakuja kuonekana kwenye bajeti ya 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee hoja moja ya Kambi ya Upinzani kuhusu tenda ya miradi ya Ziwa Victoria kwenda Tabora na Nzega. Mwasilishaji wa hoja hii ya Kambi ya Upinzani anasema kulikuwa na harufu ya rushwa. Nataka kwanza nimhakikishie harufu ya rushwa labda iko upande wake kwa sababu katika taratibu za manunuzi za tenda wakati mkiwa kwenye mchakato kuna *stage* fulani mkifika mnataka sasa kupata aliyeshinda huwa kunatolewa muda

wa kutosha kwamba kuna mtu mwenye malalamiko anatakiwa apelekwe kwenye mamlaka za *PPRA* na *PPA*. Waziri wa Maji hawezi kuingilia kwenye mchakato ya tenda, hii hairuhusiwi na pia hairuhusiwi kwenda kwenye magazeti. Mchakato huu uliandikwa hata kwenye magazeti mtu analalamika anakwenda kwenye magazeti, sasa leo wanawatumia Wabunge kulalamika, hiki kitu hakikubaliki. Ni lazima twende kwenye kanuni na taratibu za manunuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, manunuzi yamekwenda vizuri na tumepata wakandarasi wazuri na kila hatua tulioifanya tunawasiliana na mwenye fedha *Exim Bank*. Kama kuna kampuni imeonekana imetumia rushwa kule India haruhusiwi kupata kazi ile, kwa hiyo sisi tunapeleka kwake. Kama kungekuwa kuna jambo ambalo halikubaliki na Serikali ya India wangesema, Serikali ya India wametoa *No Objection* kwamba endeleeni. Sasa ndugu yangu wa Kambi ya Upinzani yeye hili analitoa wapi? Sasa mkandarasi ameshapatikana, tayari tumeshasaini mkataba na anakwenda kuanza kufanya kazi. Namshauri aunge mkono fedha zile zifanye kazi ili kuleta maendeleo kwa wananchi waliokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee kidogo kuhusu masuala ya azma ya Serikali kuboresha huduma ya maji safi kwa Jiji la Dar es Salaam. Kama tulivyosema tumeshaongeza uzalishaji kutoka lita milioni 300 kwa siku sasa tumefikia lita milioni 504 kwa siku. Mheshimiwa Mnyika maeneo mengi aliyosema ya mabomba ya Mchina leo yana maji. Ninayo taarifa ya leo kwamba maji yanatoka. Tatizo lililopo mabomba ya Mchina yamekaa muda mrefu hayakuwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna watu sehemu zingine waliamua kutoboa na tatizo tullionalo sasa ni umwagikaji ovyo wa maji katika mabomba haya lakini kazi hiyo ndiyo tunayoishughulikia ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu katika maeneo yale ambayo hayakuwa na mtandao. Kuna mkandarasi ameshaanza kufanya kazi

Changanyikeni kwenda mpaka Bagamoyo kuongeza mtandao. Pia tumepata fedha kutoka Benki ya Dunia nao watajenga mtandao maeneo mengine. Kwa hiyo, tunaendelea kutafuta fedha na kwenye bajeti hii tumeweka fedha za kujenga mitandao katika maeneo yale ambayo hayana mtandao. Kwa hiyo, maji yapo mengi na ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika maji yanayotokana na visima vya Kimbiji na Mpera tunategemea kupata lita milioni 260. Katika mwaka huu wa fedha tunategemea tujenge sasa mtandao wa bomba la kuleta maji maeneo ya Kigamboni na maeneo mengine yote ambayo hayana maji kwa upande ule. Kwa hiyo, Serikali inafanyia kazi suala hili na hayo matatizo madogo madogo ya kuvuja na kadhalika ndiyo kazi inabidi tuifanye. Ndiyo maana sasa hivi tunataka tuimarisha sana Shirika la *DAWASCO* kwa ajili ya kupeleka maji kwa wananchi. Kwa sababu *DAWASCO* kwa utaratibu uliokuwepo anakwenda kushughulikia kuwasha mitambo sisi hatutaki afanye kazi hiyo. Tunataka tufanye maboresho, yeye ashughulike na wateja moja kwa moja, aende kwa Mheshimiwa Mnyika ili tupeleke maji haya kwa wateja wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa, wananchi waliounganishiwa maji kwa Dar es Salaam hawazidi 300,000 tunataka sasa wafike 1,000,000 ili waweze kuchangia gharama za uendeshaji. Nimeshawaambia hiyo ndiyo kazi ya kufanya tupate wananchi wengi waliounganishwa na maji safi. Pia tuna miradi ya majitaka, mfumo wa majitaka kwa Dar es Salaam kwa muda mrefu ulishakuwa hakuna na wananchi chini ya asilimia 20 ndiyo ambao wameunganishwa na maji taka. Tumepata fedha toka Korea Kusini pamoja na Benki ya Dunia tunakwenda kujenga mitambo ya kisasa ya kusafisha maji taka kwa ajili ya Jiji letu la Dar es Salaam. Kwa hiyo, ndugu zangu tumeahidi na tunatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimwambie Mheshimiwa Mnyika na Wabunge wengine wa Dar es Salaam maeneo ambayo sasa maji yanapatika. Ukichukulia kwa

mfano Temeke, maeneo ya Kurasini Beach, Baraza la Maaskofu, Mtoni, Sabasaba, Mtoni kwa Kabuma, Temeke Wiles, Temeke *Quarter*, Temeke Sokota, Temeke *Veterinary*, Temeke Sandali, Temeke Mwembe Yanga, St. Mary's Mbagala, *VETA* na Rangi Tatu. Haya maeneo yalikuwa hayana maji lakini sasa yana maji. Ukija kwa Kimara, Stop Over kwa Koleza, Kimara Bakery, Kimara Polisi, Michungwani, Mbezi Igubilo, Kimara, *TANESCO*, Kimara B Bonyokwa, leo maeneo haya yanapata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija sehemu za Ilala, maeneo ya Buguruni Mnyamani, Buguruni Sokoni, Buguruni Rosana, Buguruni Y2K, Sharifu Shamba Bondeni, Kipata Kariakoo, Uhuru kuanzia *round about* to Lumumba, Ilala Bungoni, Mtaa wa Mafuriko, Amani Kariakoo leo wanapata maji maeneo yote yalikuwa hayana maji. Ni kazi kubwa inafanyika ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika. Eneo la Tabata Mbuyuni, Ogongombelwa, Kilumi Chang'ombe, Banebane, Vigunguti Darajani, Segerea, Tutundu, Makaburi Mwasaka, Vigunguti, Kwamnyamani, Maji Chumvi Kasukuru, Msamvu Street, Kibangu Ubungo, Segerea kwa Bibi, Kisukuru Chumba Kimoja na Kibangu Unovo leo wanapata maji. Kwa hiyo, kazi kubwa tumeshafanya kwa kuboresha huduma ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam. Ni lazima tuthamini kazi ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa msukumo mkubwa anaoutoa kuondoa kero hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema maeneo yale mengine ya pembezoni haya sasa tunaendelea na utaratibu wa kuongeza mtandao. Naamini tutafanikisha kwa sababu maji yapo. Tuna tatizo la upotevu wa maji na ndiyo maana tunasema *DAWASCO* sasa tunataka *a-concentrate* na *distribution* pamoja na kudhibiti upotevu wa maji, tuachane naye na kwenda kuwasha mitambo kila siku kule Ruvu Chini, Ruvu Juu kazi hiyo itafanywa na watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna muda basi nafikiri naweza nikaongezea baadhi ya hoja, kuna Mradi wa maji Kishapu. Hii ilikuwa hoja ya Kamati ya Bunge, kazi ya

usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji katika Mji wa Kishapu imekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumziwa mambo mengi lakini kama nilivyosema tutajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya...

**MBUNGE FULANI:** Bado umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, habari ya umwagiliaji Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea kwa kirefu sana. Miradi hii ilikuwa inashughulikiwa katika Programu ya Maendeleo ya Kilimo. Sasa sisi Wizara ya Maji kazi yetu kubwa ni kushughulika na ujenzi wa miundombinu na miundombinu mingi iliyokuwa imejengwa ni kweli tumekuta ipo hovyoy. Awamu hii inabidi tuanze pale walipoanzia wenzetu tuweze kurekebisha na tumeanza kuainisha maeneo ambayo yanatakiwa yarekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimepitia miradi mingi na Naibu Waziri amepitia miradi mingi. Kazi yetu mwaka huu wa fedha wa bajeti tulisema tuirekebishe miradi ile ambayo iko tayari inafanya kazi kabla ya kujenga miradi mipya lakini pia kufanya usanifu wa miradi mipya ambayo inaendana na ujenzi wa mabwawa. Hii ni kazi ambayo tutaendelea nayo katika bajeti hii na tumeweka maeneo mengi kwenye bajeti ukisoma hotuba utaona maeneo mengi tumelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa ufupi ni kwamba hapa kwenye umwagiliaji tunahitaji uwekezaji zaidi kama Taifa. Mwaka wa kwanza hatukuweza kuweka uwekezaji wa kutosha, mwaka wa pili hatujaweza kuweka pia uwekezaji wa kutosha lakini nina imani mwaka utakaofuata tutaweka uwekezaji wa kutosha wa kujenga miundombinu ili tujiondoe kwenye tabu hii ya kuwa na njaa kila mwaka. Najua katika hizi hekta milioni 29 ambazo zinafaa kwa umwagiliaji tukiziendeleza hatutakuwa na tatizo la



chakula. Pia tutaelekeza na aina ya mazao ya kulima ili kusudi kwa sababu wengi wanafikiri kuondoa njaa ni kulima mahindi tu na mpunga...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Lakini tunaweza kulima mahindi tukamwagilia. Kwa hiyo, nadhani sasa kama Taifa tuweke rasilimali na wanaoweza kuweka rasilimali ni Wabunge mnaoidhinisha bajeti.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri zungumza na mimi maana hawa wa upande wa kushoto huwa hawamalizi kuzungumza hata waliokuja kwa kuchelewa ambao hawajamsikia Mheshimiwa Naibu Waziri na wenyewe wanakuuliza tena maswali. Mheshimiwa Waziri maliza hoja yako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwa kirefu sana masuala ya umwagiliaji. Nami nakubaliana naye kabisa na namuunga mkono amesema vizuri sisi Wabunge ndiyo tunaopanga bajeti sasa tuwekeze zaidi kwenye umwagiliaji kwa ajili ya kujiondoa katika tatizo la chakula maana ndiyo kitu cha msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni yenu na mapendekezo mliyotoa. Niwahakikishie msiwe na wasiwasi, Wizara ya Maji ina bajeti ya kutosha ya kutekeleza miradi tuliyopanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba sasa nitoe hoja kwamba Bunge lako lilingie kwenye Kamati ya Matumizi na kuweza kuidhinisha bajeti hii ili twende kutekeleza tuliyojipangia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Watanzania wetu wanapata maji safi na salama na pia wanaendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono tutaendelea na utaratibu unaofuata, Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

Kif.1001–*Administration and*

*HR Management.....Sh.3,015,391,976/=*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, nimeletewa orodha hapa na vyama vilivyoko Bungeni na tutaanza na Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya awali na nataka niseme kutoka mwanzo kwa kujua matatizo ya maji kwamba Waziri asiponipa maelezo ya kutosheleza nitatoa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ni kubwa sana katika nchi hii kama Waheshimiwa Wabunge wote walivyolielezea hapa na kama Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilivyobainisha matatizo ambayo yanawasibu wananchi wa Tanzania. Hakuna suala ambalo ni tatizo kwa wananchi kama ilivyo maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumeona na tumeshuhudia kwamba bajeti ya mwaka huu ni shilingi bilioni 600 na ukilinganisha na ile ya mwaka jana shilingi bilioni 900 imepungua. Kamati ikaomba kwamba kama ilivyoomba mwaka jana kwamba Serikali iweze kutoza kuongeza tozo kwa kila lita ya dizeli na petroli Sh.50 ili ifike Sh.100. Nataka kujua kama Wizara na Serikali kwa ujumla wamefanya kazi na kama watatupa majibu kwamba tozo hii itaongezwa kwa sababu itakavyotozwa inaweza ikaongezeka shilingi bilioni 300 na hivyo kukaribia ama kupita bajeti ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, sitaridhika kwa kweli na naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu anayependa nchi hii na anayependa wananchi wake anajua matatizo ya Watanzania na akaamua kutua ndoo kutoka kwenye kichwa cha mama ili wasiwe na matatizo ya kwenda kilometa nyingi kutafuta maji. Naombeni sana Waheshimiwa Wabunge kama hatutapata majibu ya kutosheleza mniunge mkono na tunaishauri Serikali...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu utapewa nafasi tena akishajibu mtoa hoja ili ndiyo uendelee na hayo maelezo ya ziada.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nahitimisha hoja yangu kwamba Kamati ya Bunge imeibua hoja hii ya kuweza kuboresha Mfuko wa Maji. Hata hivyo, kulingana na taratibu zetu za Kanuni, siwezi kuwa na jibu la kutoa sasa, kwamba nasema ndiyo au hapana, kwa sababu ni lazima jambo hili ambalo litabidi lihusishe mambo ya kodi lipelekwe kwenye Kamati ya Bajeti katika ule muda wa siku saba ambapo huwa

tunafanya mashauriano. Kwa hiyo, nafikiri suala lipelekwe kwenye Kamati ya Bajeti halafu wataona namna gani wanaweza wakaboresha Mfuko wa Maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kwell sijaridhika na jibu la Mheshimiwa Waziri na naomba nitoe shilingi, kwa sababu nimeeleza kwamba hili halijaanza kwenye Bunge hili, tuliambia Serikali kupitia Kamati ya Bajeti kwamba Sh.50 ziongezwe. Kwanza tuliona kwenye kitabu hiki cha Waziri kwamba kuna fedha ambazo zitatumika kuboresha maji kwenye miji 17 lakini hela hii haionekani kwenye kitabu cha *Vote*. Sasa haya ni mambo ambayo yanataka atupe uhakika. Ndiyo maana natoa shilingi ninaomba kutoa hoja, naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sawa, hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa sasa naomba tukae ili niwaone wanaotaka kuchangia hoja.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kwanza, kuna utaratibu kikanuni, unaunga kwanza mkono hoja halafu unasimama. Kama wote mmeunga mkono na wote mnataka kuchangia pia ni sawa ila lazima hoja iungwe kwanza mkono, tumalize hilo zoezi halafu ndiyo tuanze wengine. Haya, wanaotaka kuchangia hoja, Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa Bashe.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kwandikwa hayupo yupo Mheshimiwa Doto.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Keissy.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *CUF* hujachukua hata mmoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo. Pia atachangia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Mheshimiwa Sakaya. Sasa tuna wachangiaji saba watatosha kwa hii hoja ya kwanza. Majina yako mengi tu hapa ya watoa shilingi, kwa hiyo, tutajitahidi kwenda kwenye hao wengine.

Mheshimiwa Haonga naomba ukae, upo kwenye nini, kama chama chako kimekuleta utakuwepo, kama hakijakuleta huwezi kuwepo.

**MBUNGE FULANI:** Kwenye hoja hii.

**NAIBU SPIKA:** Kwenye hoja hii tayari wameshachaguliwa watu saba. Mheshimiwa Mbunge naomba ukae. Tutaanza na Mheshimiwa Selasini atafuata Mheshimiwa Paresso.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme mapema kabisa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mama Dkt. Nagu. Naiunga mkono kwa sababu ya dhamira ya Mheshimiwa Rais. Rais alipokuwa anawaahidi Watanzania wanaamini hakuwa anawadanganya. Bajeti ya mwaka jana ilikuwa shilingi bilioni 900 ikaenda shilingi bilioni 600. Kama bajeti ya mwaka jana haikuweza kufanya kitu *obviously* hii ya sasa hivi haiwezi kufanya chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo mwaka jana zilikuwa shilingi bilioni 150 lakini zilitoka shilingi bilioni 92 tu maana yake dhamira haipo kwenye Mfuko wa Maji. Kwa hiyo, kama kweli tunataka kuwasaidia Watanzania, niwaambie wenzangu pamoja na kwamba mmesema maji ni uhai ngoja niwaambie lingine, maji ni siasa katika nchi hii. Hakuna jimbo katika nchi hii ambalo halina tatizo la maji na wapiga kura ni akinamama na naongea hivi wale wa kwangu wa Rombo wananisikiliza hawana maji. Kwa hiyo, naomba sana sana tukubaliane na hiyo tozo iwe Sh.100 ili kweli dhamira ya Rais ya kuwatua akinamama ndoo kichwani iweze kufikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika kabisa hili jambo la maji lisifanyiwe mzaha. Siyo katika suala la tozo kuongeza hiyo Sh.50 tu, tutafute na *avenue* nyingine ili huu mfuko uweze kutuna tumalize hii shida ya maji. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niunge mkono hoja hii ambayo imeletwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ambaye hafahamu umuhimu wa maji. Umuhimu wa maji unajulikana, kukiwa na upatikanaji wa maji wa uhakika tunasaidia wananchi wetu, tunasaidia Taifa na tunasaidia wanawake kwa kiwango kikubwa sana. Wanaoathirika kwa kiwango kikubwa na ukosefu wa maji ni wanawake. Tunavyoongea hadi hivi sasa ni asilimia 19 tu ya fedha za maendeleo kwenye Wizara hii ya Maji ndiyo imeweza kutekelezwa katika bajeti hii ambayo tumeimalizia, ni fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya kuongeza hiyo tozo kutoka Sh.50 mpaka Sh.100 na ziende kwenye Mfuko wa Maji. Fedha hizi zinaenda kuwa *ring-fenced*, hazitaweza kuguswa, zitaenda kutekeleza moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo ya maji na tutahakikisha akinamama na wananchi wetu wanapata maji kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola atafuatiwa na Mheshimiwa Kwandikwa.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waziri kwenye ukurasa wa 30 alimtaja Mheshimiwa Rais kwamba ni *champion* wa maji katika Bara la Afrika sio Tanzania tu, hatutaki kumwangusha Mheshimiwa

Rais katika *championship* yake ya kuwapatia akinamama maji. Waheshimiwa Wabunge, akinamama ni tofauti na wafanyakazi ambao wana vyama vya wafanyakazi, hawana *TUCTA*, *CHODAW*, *RAAW*, hawana *TIPAU* sisi Bunge hili ndiyo *TUCTA* ya akinamama hapa nchini, lazima tuwe na huruma kwa hawa akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa zilizotajwa kwenye kitabu humu zinaenda kupeleka maji kwenye miji sasa kule vijijini ambako akinamama ndio wengi wanateseka lazima tozo hii ya Sh.50 iongezuke. Namunga mkono Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kwamba Serikali ituambie, sisi kama Bunge tumeona mahali pa kupata fedha za kuwasaidia akinamama maji ni kwenye tozo, sasa Mheshimiwa Waziri atuambie yeye ana eneo lingine ambalo litatupatia fedha? Kama eneo hilo analo sisi hatuna matatizo tutaacha hiyo tozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima akinamama hawa tuwatue ndoo kichwani na hata ukiangalia kwenye kitabu chake huku mwishoni Mheshimiwa Waziri Mkuu amemtua mama ndoo ya maji. Lazima tumuunge mkono Waziri Mkuu aendelee kuwatua ndoo akinamama ambao kwenye vitabu hivi wameoneka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kwandikwa atafuatia na Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Sakaya ajiandae.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Naunga mkono kwa sababu inaonesha historia inajirudia kwamba hatujaweka kipaumbele inavyostahili kwenye hii sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wanateseka, kwenye maeneo yetu imekuwa migogoro mikubwa sana kwa sababu wanatumia muda mrefu kwa ajili ya kutafuta maji. Tunahitaji kuelekea kwenye uchumi wa kati, tunataka tujenge

viwanda, tunataka kupunguza umaskini, hatuwezi kwenda kwenye uchumi wa kati tukiwa na shida kubwa ya maji kama hali ilivyo sasa. Kwa hiyo, naunga mkono kwamba tozo iongezeke tuweze kuujenga vizuri huu Mfuko wa Maji ili suala la maji lishughulikiwe vilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Sakaya na Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi niunge mkono hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maji Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Niseme tu kitu kimoja Waheshimiwa Wabunge, uchaguzi na ahadi tulizotoa kwa wananchi namba moja ilikuwa maji na suala la maji ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwenye jukumu la kutupa *commitment* hii ni Waziri wa Fedha, kwa sababu Waziri wa Maji amesema ataenda kushauriana na ataenda kushauriana na itaenda kwenye Kamati ya Bajeti, mwenye kugawa fedha ni Waziri wa Fedha, anayetakiwa kuleta tozo hii kwenye *Finance Bill* ni Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, ningeshukuru Waziri wa Fedha angetoa hii *commitment* kwamba wanalichukua hili jambo kwa sababu kumweka msalabani injinia ni kumwonea, analichua hili jambo wanatuletea kwenye *Finance Bill*, hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri jambo la pili kama chanzo, Watanzania wenye mita za maji ni laki tano na elfu themanini na nane. Tukiweka tozo ndogo ya angalau Sh.2,000 katika bili mwisho wa mwezi kwa mwaka tutapata shilingi bilioni 12 ambazo zitasaidia kuweka kwenye Mfuko wa Maji na kuwa chanzo *reliable* kwa ajili ya kusukuma maendeleo na sekta hii ya maji.



**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa tutamsikia Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Nagu, ni hoja ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hapa alisema kwamba Waheshimiwa Wabunge tusiwe na wasiwasi kwa sababu Serikali ina mpango mpaka mwaka 2020 asilimia 85 ya Watanzania waweze kupata maji lakini siyo kwa mwendo tunaoenda nao. Ni lazima tuwe na chanzo cha uhakika kama iliyokuwa *REA*. Leo tunazungumza angalau *REA* tunaona mambo yanakwenda kwa sababu ni *ring-fenced*. Kwa hiyo, tunaomba, yale yaliyofanyika kwenye Wizara ya Nishati na Madini tuhakikishe tuna chanzo cha uhakika tuende huko tunakokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tunakotoka, wananchi wetu wanavyoteseka tunajua, ndio maana Mbunge akisimama hapa anatamani kulia kwa sababu tunajua tunakotoka. Tunaomba hiyo tozo ambayo Kamati ime-*propose* kuanzia kwenye vikao vya Kamati iongezwe kwa ajili ya Mfuko wa Maji ili tuwe na uhakika wa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa hili wote tuwe wamoja, lazima Serikali iongeze tozo hiyo, kama ni *commitment* itoke hapa leo na siyo baada ya siku saba. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Ghasia atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii haitolewi leo kwa mara ya kwanza. Hoja hii ilitolewa katika bajeti iliyopita kwamba tuongeze tozo kutoka Sh.50 kwenda Sh.100 na ililetwa kwenye Kamati ya Bajeti, Serikali ikaomba ipewe muda wafanyie kazi na sasa hivi ni mwaka mzima. Tulitegemea leo hapa tunavyokuja Serikali iwe imemaliza kazi ambayo ilikuwa inafanya na itupe majibu. Naibu Waziri wa Fedha yupo, napenda atuambie hapa ni nini kilichofanyika katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu hata zile pesa zilizotoka zote zimeenda kutekeleza miradi ya maji mijini. Tunaomba mfuko huu useme asilimia 70 iende vijijini na 30 iende mijini, kwa sababu shida ya maji vijijini ni kubwa zaidi kuliko mijini. Mijini wanataka kufika asilimia 90, vijijini tuko bado asilimia 65. Hivi aliyeko asilimia 65 badala ya kumwongezea *speed* bado unataka awe chini ya yule wa mijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hoja inayozungumzwa ni nzito na kubwa na siyo mara ya kwanza. Nataka niseme tu, ulinganishaji wa bajeti kwa kuangalia tarakimu inaweza ikawa si jambo la maana sana lakini kubwa kama alivyosema Waziri mwenye sekta kwamba jamani kama fedha zinapatikana hatua itapigwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukienda kwenye fedha ya *development* peke yake kwenye sekta ya maji ni shilingi bilioni 623.6, kwenye umwagiliaji shilingi bilioni 20 lakini kwenye sekta ya maji hiyo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepelekwa shilingi bilioni 70.1 ukiondoa za *supervision, monitoring* ukijumlisha hapa unapata kiwango kizuri tu, kubwa hapa ni kama fedha zitapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Waziri anasema jamani kwa sababu tuna Kanuni ya 105 ya kwenda kwenye Kamati ya Bajeti wakati zile *tax measure* zitakapokuwa zinatolewa na kujadiliwa pale tunaweza kujadiliana. Kusema hapa sasa hivi Serikali ifanye *commitment, commitment* pekee tu ni ya kurudi kwenda kwenye Kamati kujadiliana wakati tunazona sasa *tax measures* na kila kitu unakiona pale lakini kwa hapa ndani *that commitment* itakuwa ni *commitment* hewa, kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshauri Waheshimiwa Wabunge *with due respect* kwamba tukubaliane kwamba tuna hatua nyingine katika kumaliza hii bajeti kama alivyosema Waziri mwenye sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, napenda kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali hakuna anayekataa kwamba maji ni muhimu na ndiyo maana yamepewa kipaumbele sana hata kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kwamba maji ni siasa kama alivyosema Mheshimiwa Selasini lakini kama alivyosema Mheshimiwa Simbachawene kwamba hiki kinachopendekezwa, nashukuru kwa mapendekezo lakini tusiwahishe shughuli, siku yenyewe ikifika Serikali itakuja hapa tutaleta na hiki tunachokijadili tutaweza kukijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kusema kwamba alichosema Mwenyekiti wa Kamati, ukurasa wa 173

mchanganuo wa fedha hizi kwenda katika miradi 17, shilingi milioni 503 dola za Marekani pesa hii haikuingizwa kwenye bajeti, kwa hiyo, kwenye bajeti ya Wizara ya Maji pesa hii haionekani. Hata hivyo, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Madeni imekaa juzi na sasa hivi tuko katika hatua nzuri ya pesa hizi kupatikana. Napenda pia kuliambia Bunge lako kwamba pesa hii itakapopatikana na kama ambavyo amesema Waziri wa Maji, kwamba miradi ya maji haitekelezwi yote kwa mwaka mmoja, inatekelezwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokifanya pesa hii itapatikana ndani ya mwaka huu wa 2017/2018 na tutakaa pamoja, Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji, tutafanya uchambuzi ni miradi ipi ianze mwaka 2017/2018. Waheshimiwa Wabunge, yawezekana kabisa hata hiki mnachokiomba kikawa kidogo tutakapokuwa tumefanya uchambuzi na Wizara ya Maji na kwa pamoja tutaweza kuzidi hata zile shilingi bilioni 900 ambazo zimetoka ndani ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema Waheshimiwa Wabunge wanachokipendekeza sikatai lakini sitaki kukisemea, sitaki kuiwahisha shughuli, lakini pesa zipo kwa ajili ya Wizara ya Maji. Nimwombe sana Mwenyekiti wa Kamati tumemsikia kama Serikali, atupe nafasi ili tuweze kulifanyia kazi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge kusema kwamba, katika bajeti hii ambayo imesomwa na Serikali kwenye Bunge lako Tukufu hoja ya maji na hasa maji vijijini kwa kweli ni hoja ambayo imezungumzwa kwa mapana yake na kuonesha umuhimu wa hoja ya maji na hasa vijijini kwa kiasi kikubwa. Sasa tunapokwenda kuhitimisha hoja hii ni lazima tutazame namna nzuri ambayo inaweza ikatupa kwanza nafasi ya

kutosha ya majadiliano kati yetu sisi kama Serikali na Bunge na kwa kuzingatia kanuni zetu ambazo zinatungoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali, tunaamini kabisa kwa sababu ya mawazo na michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, imezungumzwa hapa Sh.50/= lakini umewasikia Waheshimiwa Wabunge wengine kama Mheshimiwa Bashe na wengine, wamejaribu pia kuongeza vyanzo vingine ambavyo vingeweza kufanya kazi hii nzuri. Katika Kikao hiki hapa kuweza sasa kujua chanzo gani kinaweza kuwa ni chanzo muafaka hasa katika kushughulikia suala hili si kipindi muafaka ambacho tunaweza tukamaliza haya yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tuko tayari kufanya majadiliano ya kina na kupokea ushauri huo wote. Kwa sababu Waziri wa Fedha na *Budget Committee* wanayo nafasi nzuri sasa katika kipindi cha kikanuni kilichowekwa, basi naomba sana nimwombe Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu aone umuhimu wa jambo hili kama alivyolileta kwa niaba ya Kamati na sisi Serikali tulivyolichukulia, turudi kwenye Kanuni inavyotuelekeza tukakae pamoja na Wabunge wenye ushauri wa namna moja ama nyingine waje kwenye Kamati ya Bajeti, kwa pamoja tupate suluhu na mwisho wa siku lengo letu sisi Wabunge la kuwawakilisha wananchi na hasa wa vijijini kupata maji liweze kutekelezeka. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mwenyekiti aridhie jambo hili ili likafanyiwe kazi vya kutosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri una nyongeza hapo?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILAJI:** Hapana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu, mtoa hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena kunipa fursa hii na naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kutambua matatizo ya akinamama, kutambua matatizo ya wananchi

na kutambua jinsi maendeleo ya Taifa hili yasivyoenda mbele kwa sababu ya kukosa maji. Nawashukuru sana kwa sababu tumejenga hoja kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nishukuru na niseme kwamba, nimefarijika na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Fedha. Nataka kusema hivi Waheshimiwa Wabunge, fedha za mfuko hizi kidogo za Sh.50/= kwa kila lita ndizo ambazo zimetumika kutekeleza miradi ya mwaka huu. Asilimia 52 ya fedha ambazo zimetolewa ni za huo mfuko. Kwa hiyo, tujue kwamba, mfuko huu ndiyo uhakika wa kuweza kutekeleza miradi ya maji na kuondoa matatizo ya maji katika nchi hii. Kama kutakuwa na vyanzo vingine tutakuwa tumefanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilikuwa Waziri kwa muda mrefu, nafahamu kwamba pengine majibu hayawezi yakatokea hapa kwa sababu ni mambo ya kisheria, hatuna sababu ya kutokuamini Serikali yetu. Naiamini sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli, naomba Waheshimiwa Wabunge tuamini na ikitokea wakati wa *Finance Bill* hili jambo halijafanyika bado tuna muda. Naomba leo tumpitishie Mheshimiwa Waziri wa Maji na mimi narudisha shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana, kila mmoja ametimiza wajibu wake hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Kwa hiyo, shilingi imerudi na tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Hili nitakalolisema pengine wengine wanaweza wasilielewe vizuri, lakini watu wanaotokea Iringa, Mafinga, Mufindi na Njombe wanaweza kulielewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na suala la kulinda vyanzo vya maji kwa sababu maji ni uhai. Hata

hivyo, hii tafsiri ya mita 60 kutoka kinachoitwa ama vyanzo vya maji ama mito ama mabonde imekuwa ikitafsiriwa katika namna ambayo utekelezaji wake unaleta madhara kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sisi kule kwetu Mafinga, Mufindi na Iringa tuna kilimo tunaita Kilimo cha Kulima Vinyunguni, ni kilimo cha mabondeni, lakini mabonde yale si mabonde ambayo ni chanzo cha maji, si mabonde ambayo yanaweza kuhatarisha uwepo wa maji. Ndiyo maana toka mababu na mabibi zetu wamekuwa wakilima na bado Iringa imekuwa ni chanzo kikubwa cha maji ndiyo maana tunazalisha maji kupitia Bwawa la Kihansi na Bwawa la Mwenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wamewekewa nyumba 'X' kwa sababu wako ndani ya kinachoitwa mita 60. Kwa hiyo, naomba tafsiri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ya hiyo mita 60 ili iweze kueleweka na izingatie hali halisi ya maeneo husika vinginevyo na mimi nitashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kama nchi tufike mahali katika suala la utunzaji wa vyanzo vya maji lazima tuzingatie sheria tuliyojiwekea wenyewe. Sheria hii ya mita 60 imetungwa na Bunge hili sasa tunapokwenda kwenye utekelezaji Wabunge wengine wanataka tusifuata sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefanyika utafiti kuona kwamba watu wanapolima ndani ya mita 60, kwanza kilimo kingi wanatumia dawa na dawa hizi zinakwenda kwenye maji ambayo wananchi wetu wanakunywa, kuna *multiplying*

*effect*, madhara makubwa. Kwa hiyo, naomba sana kama Taifa tukubaliane hilo. Najua litawaumiza hawa ndugu zangu Wahehe wanalima vinyungu na Wabena wanalima vinyungu na huko ndiko kwenye vyanzo vingi vya maji ambapo maeneo mengi tunavitegemea. Sisi tutaangalia namna ya kuwapa shughuli nyingine mbadala badala ya kulima vinyungu, hili ndilo jukumu ambalo tunaweza tukalifanya. Kwa hiyo, mita 60 lazima tuzingatie kwa sababu ndio sheria iliyofanyiwa utafiti kwamba kwa kulima nje ya mita 60 madhara yake ni kidogo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Chumi ameridhika. (*Kicheko*)

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Bado Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaposema watatupa shughuli nyingine na ukienda kwenye bajeti ya umwagiliaji unakuta kuna shilingi bilioni 20 tu kati ya hizo shilingi bilioni 600 hiyo shughuli nyingine itawezekanaje. Hata hivyo, lingine ninalosema hizo mita 60 tafsiri yake ndiyo tatizo. Maeneo mengine siyo chanzo cha maji na Mheshimiwa Waziri bahati nzuri anafahamu jambo hili kwa sababu ametoka kwenye vinyungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kilio changu unapokwenda unawawekea watu 'X' kwenye nyumba zao unawaambia baada ya siku 90 muondoke, *simply because* ya hizo mita 60 ambazo maeneo waliyopo sio vyanzo vya maji wala sio mito na wamekuwa wanafanya shughuli hizi miaka yote, hakuna kukauka kwa maji. Ndiyo maana nikasema naomba Waheshimiwa Wabunge mnisaidie, natoa hoja, tuweze kujadili jambo hili, ni nini hatima ya watu hawa? Kwa sababu tafsiri ya mita 60 yaani *it is completely confusion*. Leo hii mtu kahangaika kajenga kanyumba kake unamwekea 'X'? Tafadhali Waheshimiwa Wabunge na *especially* mnaotoka maeneo hayo mnajua kilimo cha



vinyungu ni mbadala hasa wakati wa njaa na wakati mvua ikiwa haba, naomba mniunge mkono, natoa hoja tujadili.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono. (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Tumeunga, tupo huku.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Watakachangia ni Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Mwamoto...

**MBUNGE FULANI:** Angalia na huku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa nina macho ya kuona, kwa hiyo, wakati mwingine utulivu ni muhimu Waheshimiwa, sasa kila mtu akitaja jina lake tutasikilizana kweli humu ndani? Haiwezekani! Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Mtulia na Mheshimiwa Mpina. Tunaanza na Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Niseme tu wazi kwamba, mtoa hoja siyo kwamba anataka kukatalia shilingi lakini anataka kuelewa maana ya mita 60. Ukweli ni kwamba, kuna upendeleo wa wazi katika mambo ya vijijini kuliko mijini, mita 60 zinazozungumzwa ni mambo ya mazingira, ni *Environment Act*, kwa nini maeneo ya vijijini mita 60 zinasisitizwa lakini maeneo ya mjini watu wanafanya kazi? Ndiyo hoja ambayo iko hapa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mita 200 na mita 60 katika masuala ya mazingira. Mimi na-*declare interest* kwamba nimesoma mazingira, mazingira hayajafanya mwanadamu aathirike au mimea iathirike, wote tunategemeana kati ya mimea na binadamu. Pale ambapo unaona kuna umuhimu wa binadamu kuishi wanaishi, huwezi kusema mita 60 wakati unaona watu maslahi yao yako pale. Sasa ni kwa nini vijijini mita 60 zinatumiwa zaidi lakini mjini hazitumiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuunge hoja hii ili watu waende waangalie kwenye eneo la mtoa hoja kama kuna umuhimu wa kwenda kulinda maslahi ya binadamu kuliko mimea iliyopo au mambo ya *environment* yaliyopo waseme, lakini sio kulisitiza kwamba mita 60 isitumike. Mita 60 itumike pale ambapo mnaona kwamba kuna umuhimu wa binadamu na mimea. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kuunga hoja hii mkono. Tunapozungumzia mita 60 kwenye vyanzo vya maji, hilo halina ubishi na tunakubaliana nalo lakini kule ambako mto unaendelea, kuna maeneo hasa katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe ni milima na milimani ni sehemu ya hifadhi hairuhusiwi kulima, sehemu inayobaki ya kulima ni sehemu ya mabondeni. Sasa ukizuia mabondeni, ukazuia na milimani, wananchi watalima wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ni la muhimu sana. Sisi tunachosema kwenye vyanzo vya maji mita 60 ziheshimiwe lakini huku ambako mto unaendelea wananchi waruhusiwe isiwe mita 60, zipunguzwe ili waweze kuzalisha. Naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hoja hii na naunga mkono maneno ya Mheshimiwa Chumi. Suala hili nimeuliza mara nne, mara tano, lakini sijajibiwa vizuri, ni kwamba nia ya Serikali ni nzuri lakini kabla haijatungwa sheria hii ilipaswa kuwa tumeweka mkakati kitu gani mbadala kifanyike. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri leo angekuja na dhana kwamba wanaimarisha umwagiliaji kwa kutumia mifereji lakini suala la kuzuia linatupa matatizo. Nahisi kwamba wananchi wa maeneo ambayo wamekumbwa na hili jambo hawakushirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba suala hili litakuwa ni gumu na wananchi kule hawaelewi kitu gani kinaendelea. Kama ni sheria iangaliwe upya na wahusika, kwa maana ya watu wa Iringa, Mbeya, Kilolo na sehemu nyingine washirikishwe ili mambo yakae vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chumi endelea kushikilia shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono kabisa hoja ya Mbunge ili watupe ufafanuzi wa sheria. Kwa mfano, Wilaya ya Kilombero kila baada ya kilometa mbili mto au kijito, kilometa mbili mto au kijito, yaani kuna vijito haijawahi kutokea duniani lakini kuna mito mikubwa inapita na wananchi wa Kilombero na Jimbo la Mlimba wanaheshimu hiyo mito mikubwa, hatukatai kutunza mazingira, hata mimi ni mdau wa mazingira, lakini vijito na vibwawa vidogo vidogo kote wanaambiwa waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyosema Kamati iko huko, eti wanawaambia watu waondoke yaani kuna taharuki mimi sijawahi kuona duniani. Kwa hiyo, hiyo hoja imefika mahali pake, Waziri mwenye dhamana atupe ufafanuzi, awaambie wananchi kwani kuna taharuki kubwa, hawa watu wa *RUBADA* wako huko ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kweli, hata mimi hii mita 60 nakubaliana kwamba ni suala ambalo haliwezekani. Sisi kwetu, mfano watu wa Dar-es-Salaam tuna mito yetu kama Mto Msimbazi, Mto Ng'ombe, inaitwa mito kwa sababu ya majina tu, lakini si chanzo cha maji wala maji hayatumiki kwa umwagiliaji

lakini mita 60 hii imekuwa tatizo kubwa na bahati mbaya kuna upendeleo mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Jengo la Moi pale Muhimbili na pale kalipokuwa ka-mto mita 60 haitimii. Ukiangalia Jengo la *DARTs* pale Jangwani na ulipokuwa mto mita 60 haitimii. Sasa mimi naona ni mkanganyiko na upendeleo. Hili jambo lazima liwekwe sawa, wananchi wasiyumbishwe kuhusu hii mita 60. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), naongeza nusu saa. Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ambayo anayalalamikia Mheshimiwa yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira, Namba 12 ya mwaka 2009, pamoja na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Bahati nzuri katika mjadala huu wakati tunaendelea, Wabunge wote walilalamika juu ya uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na madakio yake unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Cosato Chumi nimemsikiliza vizuri sana katika hoja yake, inaonekana kwamba ana malalamiko maalum (*special*) tofauti na haya tunayoyazungumza ya mita 60. Kwa sababu wakati mwingine sio mita 60 tu peke yake, mahali pengine tunaamua kulingana na chanzo kile cha maji kutangaza lile eneo kuwa eneo tengefufu, kwa hiyo, inaweza isiwe mita 60 tena inaweza ikawa hata mita 500 kwa ajili ya kulinda kile chanzo cha maji pamoja na madakio yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hoja yake hii anayoizungumza wale walioweka 'X' inawezekana ikawa ni Halmashauri au *NEMC*, sasa badala ya kumchukulia shilingi yake Waziri hapa, nimuahidi kwamba sisi tutaenda tukaangalie maeneo hayo anayoyazungumza Mheshimiwa. Kwa bahati nzuri kwa Sheria hii ya Mazingira, Kifungu kile cha 57, ukisoma ile 57(2) inaturuhusu sisi kuyaondoa yale maeneo

ambayo hayahusiki katika kile anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, nitoe *commitment* kwamba kama Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia mazingira, tutaenda kufuatilia eneo hilo na kuona hasa anachokilalamikia Mheshimiwa na kukishughulikia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Maghembe.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo limeelezwa hapa la vinyungu nalijua kidogo. Suala la mto unapotoka pale kwenye chanzo chake, njiani unavyokwenda kuna maeneo yale ambayo ni chepechepe, maeneo yale ndio *reservoir* maji yanapokusanywa pale halafu yanarekebishwa, yanakwenda mwaka mzima. Sasa haya maeneo ambayo yamezunguka mto yakilimwa mito ile wakati wa kiangazi inakauka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo tunaloeleza hapa kwamba wananchi wanahitaji maji kwa ajili ya umwagiliaji, hasa wakati ule wa kiangazi, lakini pia, tujue kwamba mito yetu matumizi yake 78% ni miradi ile mikubwa ya umwagiliaji ambayo tunaitegemea kama Taifa. Kinachosemwa hapa ni lazima sasa tuanze kufikiria namna ya kuvuna maji katika mito yetu mikubwa na kutengeneza mabwawa ambayo yatatumika wakati wa kiangazi ili mito yetu isipungue maji nyakati zote za mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni mto Wami. Mto Wami wote tukitoka Dar-es-Salaam tukija hapa Dodoma wakati wa kiangazi watoto wanacheza mpira ndani ya *base* ya mto. Wakati wa mvua unakuta maji yanapita lakini wakati wa kiangazi ni eneo la kucheza mpira. Nadhani kwamba sasa umefika wakati lazima tufikirie upya jinsi tunavyotumia maji ya mito yetu na jinsi ambavyo tunatumia maji ambayo yanatokana na mvua na wakati wa mvua yote yanakwenda baharini tunabaki na jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri una hoja. Naona Waziri wa TAMISEMI anataka kujibu vinyungu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, shida kubwa ninayoiona hapa ni tafsiri ya vinyungu na vyanzo vya maji. Kwa sababu ya mazingira mpaka tuelewane wote acha sisi kama Serikali na kama alivyosema Waziri wa Mazingira na wengine wamesema tuichukue kwa sababu hii ni *case to case*. Kwa sababu tafsiri ya chanzo cha maji kwa nchi nzima ni kweli ndipo maji yanakotokea au yanahifadhiwa. Sisi maeneo yanayohifadhi maji yale chepechepe tunaita "litetema au tetema", pale ukisema chanzo cha maji inaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinyungu cha Cosato Chumi kwamba ni mahali ambapo mvua ikinyesha panakuwa pana ubichi, ni sawasawa na kusema ni *irrigation* ya asili na ndiyo imeishi kwa miaka na miaka ukienda kusema leo hii watu wasilime kule hawatakaa wakuelewe. Ikiwa kuna umakini wa kutafsiri chanzo cha maji ni nini maana kinyungu hakizalishi maji ya kwenda popote, ni hayo yaliyoko hapo, hayaendi popote na hakuna namna ya kwenda mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tafsiri inatofautiana kutoka mazingira fulani na mazingira fulani. Alichokisema Naibu Waziri wa Mazingira kwamba hebu tukuchukue hizi *cases* halafu wataenda kuangalia *specific case* ya kwa Chumi na maneno mengine *then* wanaweza wakaja na jawabu. Kusema tuchukue *general formula* pale ya mita 60 itakuwa ni jambo gumu sana kwa baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru mawazo mazuri na mengi ya wengi waliochangia hoja hii. Katika kuhitimisha hoja hii kama

mwenye sera siwezi nikatamka hapa kwamba leo ruksa kulima kilimo cha kiangazi. Kilimo cha vinyungu ni kilimo cha kiangazi kwenye vyanzo vya maji, *bottom line* ni vyanzo vya maji kama hicho siyo chanzo cha maji hicho ni kitu kingine. Kama wanavyosema wengine twende tukatazame hapo mahali penyewe je, ni chanzo au siyo chanzo. Tunachozungumza hapa ni kwamba chanzo cha maji haturuhusu mita 60 kulima kilimo cha kiangazi, ndiyo hoja hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mito mingi imekauka sasa hivi, sasa leo tukitaka kurudi huko haitakuwa sawa, tunataka tutafute jibu la kutiririsha maji kwenye mito. Kazi ambayo tunafikiri kama Serikali sasa tunataka kujenga miundombinu ya umwagililaji endelevu. Kwa hiyo, ni vizuri tukakubaliana kwenye hili. Naomba Mheshimiwa Chumi anirudishie shilingi ili tukajenge miradi ya umwagililaji endelevu kwa wananchi wake wa Mafinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi, baada ya ahadi ya Mawaziri kwamba watakuja waangalie hilo eneo lako nadhani tunaweza sasa kuendelea wa ajili ya kutunza muda maana wameshatoa ahadi ya kuja.

**MHE. COSATO D.CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nawashukuru sana Wabunge wote ambao wameliona jambo hili. Niwe *honest*, hapa narejesha shilingi kwa sababu ya maelezo yaliyoniridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira kwamba tutakwenda tukaangalie tafisri ya mita 60. Wakati huu niiombe Serikali pamoja na Waziri wa TAMISEMI zoezi la kuweka zile 'X' hebu lisitishwe kwa muda kwa sababu lilmeleta taharuki kwa watu. Hilo ni la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, maeneo haya Waziri wa Maji amekiri kwamba ndiyo vyanzo vya maji lakini ukienda kwenye bajeti ndiyo tumepewa kiduchu. Kwa hiyo, wakati ujao Serikali itazame maeneo haya, siku ile nilisema tuko karibu na waridi lazima tunukie kama waridi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, nashukuru sana maelezo ya Serikali kuanzia Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Maji na Waziri wa Mazingira nimwombe twende tukaone hiyo tafsiri ya mita 60 na nashukuru Wabunge wote kwa kuniunga mkono, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Lijualikali.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mwaka 2006 Serikali ilikopa fedha takriban dola milioni 90 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, kwa ajili ya mradi unaoitwa *District Agriculture Sector Investment*. Lengo la hizi fedha ilikuwa ni kujenga skimu za umagiliaji lakini asilimia 80 au 90 za hii fedha zimepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, skimu ya Kisangwa ambayo iko Bunda mradi ulikuwa na thamani ya shilingi milioni 385, mkataba ulisainiwa tarehe 7 Mei, 2012 na ulikuwa ni mradi wa siku 150. Mkandarasi alilipwa shilingi milioni 259 mradi haufanyi kazi mpaka leo. Skimu nyingine ni ya Kakakera iko Misenyi, huu mradi ulikuwa na thamani ya shilingi milioni 497 ulisainiwa tarehe 20 Machi, 2013 ulitakiwa ukamilike ndani ya siku 150, fedha zimeliwa mradi haufanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali iniambie waliofanya huu ubadhirifu walichukuliwa hatua gani? Fedha hizi zimepotea ambazo ni mkopo, fedha hizi kwa nini zimepotea na Serikali mpaka leo haifanya chochote. Wananchi mpaka leo wamekosa huduma hii na Serikali imekaa kimya. Naomba Serikali iniambie na kama majibu yatakuwa ni ya hovyoy, natoa shilingi yangu. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kidogo kanuni zetu zinavyotaka ili tuwe tunakwenda sawasawa. Wakati tunapojadili kwenye Kamati ya Matumizi kifungu kinachohusu mshahara wa Waziri, Kanuni zetu zinataka uongeele jambo linalohusu sera. Sasa ukileta



mikataba mahsusi unataka majibu kwenye hiyo mikataba tunakuwa tunaenda nje kidogo. Nitampa Waziri ajibu lakini siyo lengo la kanuni la kushika mshahara kwenye fungu hili. Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuona umesimama.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Lijualikali kwa kutupa taarifa. Nitaomba hiyo taarifa atupatie ili tuiundie kamati, tukaifanyie *audit* ili tuweze kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zilizopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alikuwepo wakati nahitimisha atakumbuka kwenye majibu yangu nimelizungumza hili kwamba nimepita kwenye miradi na Mkoa wa Morogoro nimepita nimekutana na miradi ambayo iliingiwa mikataba siku za nyuma ina shida kidogo. Kwa hiyo, tutaifanyia kazi tu- *audit* na itakapoonekana kwamba kuna ubadhirifu nina imani hao watu wapo mkondo wa sheria utachukua nafasi yake. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lijualikali, nadhani kwa sababu hiyo taarifa ya hiyo mikataba itabidi ifuatiliwe ili ndiyo tujue watu wamefanyiwa nini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika naomba ukae.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lijualikali nataka nimalize maelezo natakupa nafasi wewe si ndiyo mtoa hoja? Serikali inatoa maelezo kwamba mikataba hiyo uliyoisoma na matatizo yote uliyoyasema Serikali ipo tayari kuchukua hiyo taarifa na kuifanyia kazi. Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Waziri anaposema kwamba alikuwa hajui ndiyo anasikia sasa hivi siyo kweli, hii ipo kwenye taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo imekuwa *tabled* leo, kwa

hiyo, anajua kwa sababu amesoma. Pili, hili suala siyo geni lipo tangu 2006 na linaathiri nchi nzima. Kwa hiyo, naomba nitoe shilingi yangu liwe *debatable*. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, suala hili sitaweza kulitoa lijadiliwe kwa sababu haliko kiseru kama nilivyosema ni suala ambalo linahusu mikataba mahsusi. Kwa hiyo, Wabunge watakuwa wanajadli nini wakati hawajui hiyo mikataba. Kwa hiyo, sitoa hiyo hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tufuate Kanuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, Kanuni inataka suala la sera, naomba ukae.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 103(3) inatoa nafasi kwa Mbunge kuondoa shilingi asiporidhika na jambo lolote, naomba tufuate Kanuni.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Tunaficha huu ufisadi.

**MWENYEKITI:** Huo huo ufisadi lazima uulete ukiwa kwenye sera siyo wa mikataba. Umetuletea mikataba hapa haiko mezani.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mbona kashika shilingi kwa nini isiwe *debated*.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa.

**MHE. JOHN JOHN MNYIKA:** Hii siyo sahihi kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru nami kwa kupata hii nafasi na kwa kweli

nimeshukuru sana Wabunge wote tumeshirikiana kuliona suala la maji ni tatizo na ni janga la kitaifa na hasa ukiangalia vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kuhusu *EWURA*, ukichukua Uganda wanatoa tozo la maji kwenye mafuta pamoja na mazingira asilimia nne, Kenya wanatoa asilimia nne lakini Tanzania wanapeleka asilimia 14. Kutokana na hali ngumu iliyopo sasa na wanawake na watoto wanahangaika kutafuta pesa ili kuweza kukidhi mahitaji ya maji, naomba Waziri atuambie *EWURA* wanapata kiasi gani katika hiyo tozo ya 14% na wanatumia kwa kitu gani ili hela hizi zigawanyike ziende upande wa maji kuwasaidia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda basi Wabunge wenzangu waniunge mkono, Waziri akinipa jibu zuri sina matatizo lakini kama sitapata jibu ambalo nitaridhika naomba tuweze kuchangia hoja hii. Ahsante sana, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Bado Mheshimiwa Lulida naomba ukae. Mheshimiwa Waziri ni nani kati yenu anazungumza sioni ambaye yuko tayari. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kuhusu makusanyo ya *percent* yanayochukuliwa na *EWURA*. *EWURA* ni taasisi ya Serikali, taasisi zote za Serikali zilifunguliwa akaunti Hazina kwamba makusanyo yake ya fedha yanapelekwa Hazina. *EWURA* matumizi yake inatengeneza bajeti inapewa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fedha zote zinazokusanywa na *EWURA* ni pamoja na taasisi zingine za Serikali zote zimefunguliwa akaunti ziko Hazina. Akitaka kupata hiyo taarifa Mheshimiwa Mbunge itabidi basi tupeleke Hazina waweze kutuambia kwamba hiyo hela ni shilingi ngani

inakusanywa na matumizi yake yanapangwa vipi, lakini kwa maana ya *EWURA* kama taasisi ya Serikali fedha zake zote zinapelekwa Hazina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kutokana na pesa wanazozichukua *EWURA* kuwa ni *percent* kubwa sana na hali ya upatikanaji wa maji imekuwa ngumu hasa ukichukulia mikoa ya pembezoni mmojawapo ukiwa Mkoa wa Lindi hata Lindi Mjini maji hakuna. Hizi pesa mpaka sasa hivi inaonekana hata wenyewe Wizara Maji hawajui zinatamikaje. Hivyo, naomba Wabunge wenzangu kwa kuliona hili suala kuwa ni ngumu sana na imekuwa ni janga kwa upatikanaji wa maji vijijini, naomba mniunge mkono na tuweze kuchangia hili suala lililoko mezani, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono, wanatakiwa watu kumi na hawajafika, kwa hiyo hoja haijaungwa mkono.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, sasa wameshaongezeka. Haya, hoja imeungwa mkono wale wanaotaka kuchangia ndiyo wabaki wamesimama. Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Salma Mwasa, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Mwambe, haya Waheshimiwa wametosha hao.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuangalie saa ile pale wote tunaiona. Mheshimiwa Riziki Mngwali.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ni masuala ya sera hapa ndiyo sera yenyewe kwa sababu kama tunatengeneza taasisi hizi, halafu hatuna *control* nazo lakini wao ndiyo tunaambiwa wana *control, at the end of the day* hakuna kinachofanyika. Hivi kweli *issue* ya bei nayo tuundie bodi nzima? Mimi *actually*

nili kuwa nadhani hawa *EWURA* wana-*regulate* upatikanaji wa huduma yenyewe, maji hakuna, bei za maji zinatakiwa za nini? Mafia maji hakuna na maeneo chungu nzima maji hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ituambie hasa hii *EWURA* na hizo pesa wanazokusanya zinasaidia vipi wananchi kupata maji na siyo kuwapangia bei kwa bidhaa ambayo haipo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salma Mwasa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja. Kwanza bei inapagwa na soko, *demand and supply*, hivyo ndivyo tunavyojua kama Wachumi. Sasa kama *demand ipo supply* hakuna unapangaje bei? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu eti ni 14% kwa nini 14%? Mbona tunaona mamlaka za *control* za Uganda na Kenya ni 4%? Hapa mtu kwanza ana-*control* bei halafu akisha-*control* naye ana 14% eti kwa sababu ya kujilipa yeye, mimi hapo sijaelewa kabisa. Kwanza watueleze hiyo bei wanaipangaje na mpaka saa hivi wamefanya jitihada gani za kuongeza maji au umeme katika eneo gani mimi sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nataka niunge mkono jambo hili kwa sababu nakumbuka wakati fulani sikuwa Mbunge lakini sheria zilibainisha wazi kwamba Waziri husika atakapokuja kutoa bajeti yake kwa vyovyote vile lazima kuongelea na taasisi ya mbalimbali zilizoko chini yake. Kimsingi Waziri wa Maji amekuja hajatueleza kinagaubaga majukumu ya *EWURA*. Ukienda vijijini na mijini ni *EWURA* ndiyo wanaopanga gharama za maji tena bila hata kuzingatia vigezo mahsusi katika maeneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunamtaka Waziri atueleze wazi kwamba watu hawa *EWURA* walivyopewa mamlaka makubwa kiasi hiki lakini sehemu kubwa ya pesa wanazozikusanya ni kwa ajili ya kuendesha ofisi. Ni nini sasa faida yao wao kwa umma wa Tanzania kwa ujumla. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naielewa hoja hapa ya Mheshimiwa Mbunge, lakini nafikiri kwa hapa tunapungukiwa takwimu nyingi sana za kulimaliza jambo hili. Kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri pale amezungumza, kwanza kuna hoja ile iliyoulizwa ya mapato yenyewe ya *EWURA* ambayo hapa hatunayo. Vilevile hatuna takwimu yoyote ya kuzungumzia ukubwa wa kiwango hiki cha tozo linalozungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumzia suala la makusanyo tulizungumza vizuri sana kwamba jambo hili litakapokwenda kwenye Kamati haya mambo yote yatapitiwa kwa kina. Kama *EWURA* inatoza fedha nyingi kuliko inavyotakiwa Kamati ya Bajeti wakati inapitia mapendekezo mbalimbali dhidi ya vyanzo vya mapato vya kuongeza kwenye miradi ya maji litapitiwa jambo hili. Kwa sasa hatuna takwim, hakuna anayejua mapato na matumizi ya *EWURA* tutazungumzaje. Nadhani kama tulivyomaliza lile suala la vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuongeza kwenye maji libaki hivyo hivyo Kamati ya Bajeti itatusaidia na kwenye hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitoe taarifa kwamba *EWURA* inachaji asilimia moja sio asilimia 14 kama mtoa hoja alivyosema. Pia majukumu ya *EWURA* tumeleeza kwenye ukurasa wa 92 - 96 wa hotuba yangu. Kwa hiyo, naomba wanaochangia basi wajue kwamba taarifa ya mtoa hoja

sio ya kweli, ni asilimia moja. Hizi fedha zinakusanywa zinapelekwa Hazina, ni maduhuli yanapelekwa Serikalini halafu wao wanaomba matumizi kwa utaratibu ambao Serikali imeweka. Kwa hiyo, siyo kwamba fedha zile wanatumia wao, hapana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa hata Waziri kwamba hajui mapato yanayopatikana kutokana na tozo la *EWURA*. Ina maana amekaa pale kutuambia kiasi gani wanapata *EWURA* ameshindwa maana hii ni Wizara yake, ilibidi aingie kwenye kifungu aangalie *EWURA* inapata kiasi gani ili na sisi tujue hapa. Pamoja na kuwa utasema mimi takwimu zangu sio sahihi lakini kutokana na taarifa nilizonazo kuwa *EWURA* wanachukua tozo kubwa na vilevile Waziri awe anajua kiasi cha pesa kinachopatikana. Pesa za mafuta sina tatizo lakini hizi za maji zitolewe zipelekwe katika masuala ya maji ambayo sasa hivi ni muhimu sana. *EWURA* anachukua hela za mazingira, za mafuta na hizi za maji kwa nini anapewa? Pesa za maji ziende katika fungu la maji na sisi watu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara ambao tuko nyuma katika suala zima la upatikanaji wa maji tuweze kufaidika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Basi amekurudishia shilingi nadhani, huyu ni mtu muungwana sana. Nadhani tuendelee na mchangiaji wa mwisho kwenye hoja hii ni Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami kabla sijaongea naomba kusema kwamba nakusudia kutoa shilingi kama Mheshimiwa Waziri hatatoa ufafanuzi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezungumzwa suala la Mfuko wa Maji. Sote tunatambua kwamba Mfuko wa Maji upo, wengine tumetetea kwamba iongezwe kutoka Sh.50 kwenda Sh.100, ni sawa lakini sheria ile bado haitenganishi na wengine wamesema kwamba vijijini iende asilimia ngapi na mjini iende asilimia ngapi. Hapa tunavyoongea vijijini ndiko

wanakopata shida, ni kilio. Mimi nataka nisema kwamba suala la maji siyo siasa peke yake tena siasa tungeweka pembeni nasema suala la maji ni janga yaani hili ni janga kabisa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anipe ufafanuzi atakuwa tayari kuleta sheria hapa ili tuje tuweke Wakala wa Maji Vijijini kama ilivyo Wakala wa Umeme Vijijini (REA) ili asilimia zile zitakazotengwa ziende moja kwa moja vijijini? Naomba maelezo na asiponieleza vizuri nitatoa shilingi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Mheshimiwa anirudishie shilingi kwa sababu kwenye hitimisho langu nimesema Serikali imekubali ushauri wa kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini, hilo ndilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika suala hili la Mfuko wa Maji na tunataka hii fedha za Mfuko wa Maji isimamiwe na wakala huyu ili kuhakikisha kwamba miradi yetu ya maji huko vijijini inasimamiwa katika viwango vinvavyokubalika, vinakuwa vinafanana Halmashauri moja mpaka nyingine. Kwa utaratibu ambao upo sasa unakuta kila Halmashauri inafanya kivyake, manunuzi kivyake na wengine wanakaa mwaka mzima hawamalizi manunuzi. Sasa ndiyo maana tunataka tuanzishe wakala ili kusudi wasimamie vizuri Mfuko wa Maji uweze kuleta matokeo ya haraka ambayo Watanzania wanayataka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata kwa majibu hayo ya Waziri kwamba wakala anaanzishwa, bado una neno?



**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natangaza kutoa shilingi kwamba, nilimwelewa sana Rais wangu, nilimwelewa sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale alipokuwa akiomba kura aligundua shida za maji kwa wananchi hasa vijijini. Akasema Waziri nitakayemteua akienda mahali akakuta hakuna maji Waziri huyo atageuka kuwa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa ameleta bajeti hapa bado anatuambia anakusudia kuanzisha wakala. Kwa nini hakuanzisha mpaka tuseme? Naomba aseme hapa jamani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata, muda wetu wa kikanuni umekwisha sasa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kanuni yetu ya 104 inaanza kazi sasa. Kwa hiyo, shukrani kwa wote mliounga mkono hoja, lakini Waziri ameshatoa maelezo kwamba wakala utanzishwa.

**MBUNGE FULANI:** Lini?

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunaendelea na utaratibu ambao tumewekewa kwenye Kanuni ya 104(2). Katibu.

#### **Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

Kif. 1001 – Administration and HR Management .....	Sh.3,015,391,976/=
Kif. 1002 – Finance and Accounts .....	Sh.1,206,294,000/=
Kif. 1003 – Policy and Planning .....	Sh.3,499,468,129/=
Kif. 1004 – Government Communication Unit.....	Sh.222,807,000/=
Kif. 1005 – Legal Service Unit.....	Sh.235,842,000/=
Kif. 1006 – Procurement Mgt. Unit .....	Sh.609,816,000/=

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kif. 1007 – <i>Management Information System</i> .....	Sh.245,499,000/=
Kif. 1008 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.290,560,000/=
=	
Kif. 2001 – <i>Water Resources</i> .....	Sh.6,399,936,800/=
Kif. 2002 – <i>Central Stores</i> .....	Sh.151,958,000/=
Kif. 2003 – <i>Water Laboratory</i> .....	Sh.2,238,080,800/=
Kif. 3001 – <i>Urban Water Supply and Sanitation</i> .....	Sh.3,158,055,000/=
Kif. 4001 – <i>Rural Water Supply</i> .....	Sh.1,509,066,000/=
Kif. 4002 – <i>Water Sector Program Coordination Unit</i> .....	Sh.120,000,000/=
Kif. 5001 – <i>Water Development and Management Inst</i> .....	Sh.0/=
Kif. 6001 – <i>Drilling and Dam Construction Agency</i> .....	Sh.1,554,685,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 5 – Tume ya Taifa ya Umwagilaji**

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Mgt</i> .....	Sh.866,384,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> .....	Sh.137,477,000/=
Kif. 1003 – <i>Planning Monitoring and Evaluation</i> .....	Sh.129,827,000/=
Kif. 1004 – <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh.38,352,000/=
Kif. 1005 – <i>Procurement Mgt Unit</i> .....	Sh.71,761,000/=
Kif. 1006 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.49,643,000/=
Kif. 1007 – <i>Information Communication Technology</i> .....	Sh.40,969,000/=
Kif. 1008 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh.45,186,000/=
Kif. 1009 – <i>Environmental and Social Management</i> .....	Sh.127,217,000/=
Kif. 2001 – <i>Irrigation Planning Design and Private</i> .....	Sh.787,242,000/=
Kif. 2002 – <i>Irrigation Infrastructure Development</i> .....	Sh.434,424,000/=

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kif. 2003 – <i>Irrigation Research and Technology Promo</i> .....	Sh.305,641,000/=
Kif. 2004 – <i>Irrigation Operation and Support Service</i> .....	Sh.563,326,000/=
Kif. 2005 – <i>Irrigation Compliance and Quality Insurance</i> .....	Sh.458,032,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 5 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kif. 1003 – <i>Planning Monitoring and Evaluation</i> .....	Sh.704,800,000/=
Kif. 1007 – <i>Information Communication Technology</i> .....	Sh. 0/=
Kif. 1009 – <i>Environmental and Social Management</i> .....	Sh.200,000,000/=
Kif. 2001 – <i>Irrigation Planning Design and Private</i> .....	Sh.8,615,947,000/=
Kif. 2002 – <i>Irrigation Infrastructure Development</i> .....	Sh.10,047,665,150/=
Kif. 2003 – <i>Irrigation Research and Technology Promo</i> .....	Sh.200,000,000/=
Kif. 2004 – <i>Irrigation Operations and Support Service</i> .....	Sh.235,000,000/=
Kif. 2005 – <i>Irrigation Compliance and Quality Insurance</i> .....	Sh.100,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Mgt</i> ...	Sh.11,347,590,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> .....	Sh.14,741,798,000/=
Kif. 2001 – <i>Water Resources</i> .....	Sh.52,180,000,000/=
Kif. 2003 – <i>Water Laboratory</i> .....	Sh.8,927,360,000/=

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kif. 3001 – *Urban Water Supply  
and Sanitation* ..... Sh.273,000,000,000/=

Kif. 4001 – *Rural Water Supply* ..... Sh.263,410,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi imekamaliza kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 -  
Wizara ya Maji na Umwagiliaji yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa bajeti aliyoleta ambayo inaonesha uhalisia. Nimtakie kheri katika utekelezaji na Bunge tunaamini matumizi haya ambayo

yamepitishwa yataweza kuleta majibu kwa matatizo ya wananchi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyataja humu ndani kwa uzito sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 105 liko jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza sana hapa ndani na hata wakati wa Kamati ya Matumizi. Sasa fasili ya (1) inazungumzia hoja ambazo zitakuwa zimejitokeza wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara husika na hoja hizo siyo zote lakini baadhi ya hoja hizo zinaweza kupelekwa kwenye majadiliano na Kamati ya Bajeti. Kwa maana ya kwamba Serikali itachukua mawazo ya hawa Wabunge na kwenda kujadiliana na Kamati ya Bajeti kwa sababu Kamati ya Bajeti inafanya kazi kwa niaba ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuagiza hoja kuhusu ongezeko la Sh.50 kwenye lita ya mafuta ya petroli na mafuta ya dizeli, ikaungane na hoja zingine ambazo zimeshapelekwa na Bunge hili kwenye Kamati ya Bajeti ili jambo hili likaangaliwe kwa umakini, maana Kamati ya Bajeti itaweza kupata kwa upana ni mambo mangapi ambayo Bunge limeagiza. Wakati Serikali inatayarisha Sheria ya Fedha basi iweze kuyaangalia haya mambo kwa pamoja na naamini tutapa fursa ya kujua Serikali imejipanga vipi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, siku ya Jumamosi, tarehe 13 Mei, 2017, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.12 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,  
Tarehe 13 Mei 2017, Saa Tatu Asubuhi)*